

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Ishirini na Mbili - Tarehe 11 Julai, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 210

Muundo wa Utumishi wa Watendaji wa Kata na Vijiji

MHE. ANATORY K. CHOYA (k.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI) aliuliza:-

Kwa kuwa Muundo wa Utumishi wa Watendaji wa Kata na Vijiji ulitengenezwa mwaka 1993 na kwamba sasa umepitwa na wakati na kuleta ugumu katika kupandisha vyeo na kuajiri upya Watendaji wa Kata na Vijiji:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

(b) Kwa kuwa sasa hivi tunao watu wengi wasomi hata waliomaliza Vyuo Vikuu wanaoomba kazi hizo, je, Serikali itakuwa tayari kutoa muundo mpya sasa?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kupitia miundo yote ambayo imepitwa na wakati ikiwemo muundo wa wapiga *type*, Makatibu Mahsusni na Waandishi Waendesha Ofisi uliotolewa tarehe 29 Agosti, 1991 na 1993?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa muundo wa utumishi wa Watendaji wa Kata na Vijiji umepitwa na wakati. Aidha, muundo huo umekuwa unakumbwa na mabadiliko mengi na hivyo kuleta ugumu katika

kupandisha vyeo na kuajiri upya Maafisa Watendaji Kata na Vijiji. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi imekwishaandaa miundo mipya ya ajira za Maafisa hawa inayozingatia dosari zilizopo na mahitaji ya sasa ya wataalam. Miundo hii imekwishapitishwa na Baraza la Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa mwanzoni mwa mwaka huu wa 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli katika soko kuna wasomi wa ngazi zote wanaoomba kazi za Uafisa Mtendaji wa Kijiji na Kata. Kama nilivyosema katika jibu la kwanza, kwa kuzingatia mahitaji halisi ya sasa, Ofisi yangu imekwishakamilisha kuandaa na kupitisha miundo mipya ya Maafisa Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa itakayoweza kuwapata wasomi waliopo katika soko. Tunashauri Waheshimiwa Wabunge tusaiane kuwahamasisha wasomi hawa walioko katika Majimbo yetu ili waweze kuomba nafasi hizo muda utakapowadia.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekuwa daima ikiboresha miundo ya watumishi wake hali inaporuhusu. TUMITAA imekwishafanya mapitio ya miundo mbalimbali ya watumishi katika Serikali za Mitaa ipatayo 50 ambapo kada za watumishi waliotajwa na Mheshimiwa Mbunge pia imepitiwa. Hivi sasa imepelekwa kwa Mpiga Chapa na baada ya hapo itasambazwa na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2003/2004.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa kazi hii ya Utendaji wa Kata au Utendaji wa Kijiji inahitaji taaluma kama zilivyo kazi nyingine zenye taaluma. Lakini kwa bahati mbaya sana hakuna vyuo ambavyo vinafundisha kazi ya Watendaji wa Kijiji au wa Kata; na kwa kuwa sasa hivi Serikali imekwishaondoa kazi ya kukusanya kodi hivyo wanashiriki katika ulinzi wa amani na kuleta maendeleo; je, Wizara ipo tayari kutayarisha vyuo ili kuweza kuwatayarisha Watendaji wa Kata na Vijiji waweze kwenda sambamba na maendeleo na ulinzi wa amani kama sera inavyotakiwa? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, vyuo kwa ajili ya kuwasaidia Watendaji wa Kata na Vijiji kuweza kuboresha elimu yao tunavyo. Kipo Chuo cha Hombolo ambacho ni mahsusi kwa ajili ya shughuli za Serikali za Mitaa na kwa sasa kimekwishaanza kutumika katika mafunzo ya awali kwa ajili ya Watendaji wa Kata. Lakini vile vile kipo pia Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ambacho kipo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ambacho nacho ni chuo kinachotoa mafunzo mazuri tu kwa ajili ya ngazi kama hizi wa Watendaji katika kuwawezesha kuweza kufanya kazi zao vizuri.

Kwa hiyo, tutakachofanya ni kuendeleza hizi juhudi zilizopo hivi sasa na kama hapana budi tutatumia hata vyuo vingine vya maendeleo ya jamii vilivyoko katika Mikoa ili kuweza kuboresha hali hiyo. *(Makofi)*

MHE. MARIAM SALUM MFAKI: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa niulize kwamba, sasa hivi Serikali imekubali kuwalipa Watendaji wa Kata na Vijiji; je, Serikali imeandaa muundo ambao utasaidia kuonyesha utaratibu wa upandishaji vyeo kwa wakati unaokuja?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika maelezo ya msingi hapa kwamba miundo kwa ajili ya Watendaji wa Kata na Vijiji tayari imekwishaandaliwa na imekwishakamilishwa, hivi sasa tumeshaipeleka kwa Mchapaji wa Serikali, nadhani ikiishatoka tutafanya jitihada pengine kuisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge ili muweze kupata fursa vile vile ya kuona kilichowekwa katika miundo hiyo ni kitu gani.

Na. 211

Huduma na Mishahara ya Walimu

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (k.n.y. MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA) aliuliza:-

Kwa kuwa Walimu ni muhimu kama watumishi wengine katika jamii inayojua maana ya maendeleo:-

(a) Je, ni kwa nini mishahara ya walimu imeendelea kuwa midogo, inacheleweshwa kulipwa na kila wakati walimu hulazimika kulipwa mishahara yao kwa kujipanga mstari kama watoto?

(b) Je, ni kwa nini walimu hawapewi huduma ya usafiri wa mazishi wanapofiwa na ndugu zao wa karibu kama vile mume, mke na watoto kama ilivyo kwa watumishi wengine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa walimu ni muhimu kama watumishi wengine katika jamii yoyote ile inayojua maana ya maendeleo. Hivyo wote wanapaswa kushughulikiwa sawa na Serikali.

Kuhusu tatizo la mishahara ya walimu kuwa midogo, ni suala linalowakabili watumishi wote wa Serikali na sio walimu peke yao. Mishahara ya walimu kama ilivyo mishahara ya watumishi wengine hupangwa na Serikali na hutangazwa kupitia Waraka wa Serikali wa mwaka husika. Karibu kila mwaka mishahara ya watumishi ikiwemo ya

walimu imekuwa ikiboreshwa kulingana na uwezo wa Serikali na itaendelea kuboreshwa kadri hali itakavyozidi kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya mishahara kwa walimu. Tamko la Mheshimiwa Rais la kulipa mishahara ya watumishi wote ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi kwa sehemu kubwa kabisa linazingatiwa na mamlaka za Halmashauri zetu hapa nchini. Walimu katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge tunapenda kumthibitishia kwamba wamekuwa wanalipwa mishahara yao kwa kuzingatia tamko hilo kila wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu kujipanga katika mstari wakati wa kupokea mishahara, utaratibu huu ni wa kawaida na hutumika kwa watumishi wote wanaopokelea mishahara yao Maofisini ili kurahisisha ulipaji, kupunguza msongamano na fujo.

Aidha, utaratibu huu hutumika pia sehemu nyingine kama vile maeneo ya huduma za afya, Mabenki na hata wakati wa kupiga kura. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, yenyewe inao utaratibu mzuri zaidi kwani wametenga maeneo matatu kwa ajili ya kulipia mishahara. Maeneo hayo ni Kibara, Nyamuswa na Makao Makuu ya Halmashauri. Utaratibu huu umesaidia sana kupunguza msongamano katika eneo moja.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu, Kanuni Na. 72, mwalimu anapopata maafa yeye mwenyewe atahudumiwa kama ilivyo kwa watumishi wengine wa Serikali. Huduma anazotakiwa kupewa kwa mujibu wa kanuni hizo ni jenzea, sanda, mashada na kusafirisha mwili wa marehemu nyumbani kwake.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa huduma hii, Halmashauri za Wilaya ambazo kieneo ni kubwa na bado zina miundombinu duni, huduma hizi hazitolewi kwa ufanisi kama zinavyotolewa katika Halmashauri za Miji. Iwapo mwalimu atafiwa mzazi, mwenzake au mtoto kwa utaratibu ulivyo sasa hapati huduma hizo au hastahili kupata huduma hizo ingawa mara nyingi Wahasibu wamekuwa wakitumia ubinadamu kutoa huduma mbalimbali.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa walimu katika utumishi wa Serikali ndio wengi; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa mikopo kwa vikundi vya wakulima, vijana na wetu wengine; je, Serikali kuanzia sasa iko tayari kuweka programu ya kuwakopesha walimu kwa kuwa mishahara yao inapita kwenye *payroll* na inaweza kuwajua huko waliko kwa kupitia Benki ya *NMB*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kama Serikali inaona kuwa wazo hili inaweza ikalichukua, iko tayari kuanzia sasa kulifanyia kazi ili ifikapo mwaka 2004/2005 iweze kuweka utaratibu, walimu waweze kukopa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kularifu Bunge lako Tukufu kwamba walimu kama watumishi wengine wanastahili vile vile kupewa mikopo katika Halmashauri zao kulingana na uwezo wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nami ninayo mifano ya baadhi ya Halmashauri ambao wamefanya juhudi za kukopesha baiskeli kwa walimu wao na wameendelea kuwakata bila tatizo lolote.

Kwa hiyo, ni suala tu kwa kweli la kuendeleza pengine na kupanua elimu hii kwa Halmashauri zote ili waweze kila watakapoweza kutoa mikopo. Kwa hiyo, suala la utaratibu lipo, nadhani ni suala la uwezo tu katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa walimu wanafanya kazi masaa zaidi ya kawaida ya saa zile za kazi; je, Serikali ina mpango wa kuwalipa malipo ya kazi ya saa za ziada? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, masuala ya kulipana posho kwa ajili ya saa za ziada ni utaratibu ambao unawekwa na Serikali na katika maeneo mbalimbali upo na unatumika vizuri.

Kwa hiyo, tunachoweza kusema tu ni kwamba kikwazo kikubwa kwa sasa nadhani ni kutokana na idadi kubwa ya walimu. Inawezekana suala hili ni suala ambalo linahitaji kutazamwa ili tuone kama utekelezaji wake unawezekana.

Na. 212

Mahitaji ya Umeme

MHE. LEKULE M. LAIZER (k.n.y. MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN) aliuliza:-

Kwa kuwa miongoni mwa sababu za kugawa Mikoa na Wilaya ni kupeleka huduma karibu na wananchi; na kwa kuwa Mkoa wa Arusha umegawanywa kwenye Mikoa miwili lakini Loliondo ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro ndiyo pekee kwenye Mkoa wa Arusha isiyo na umeme ambao ni kichocheo cha maendeleo:-

(a) Je, ni lini Makao hayo Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro - Loliondo yatapatiwa umeme?

(b) Kama uwezekano wa kupatiwa umeme toka Gridi ya Taifa bado ni mdogo kwa sasa; je, wanaweza kupatiwa Kangavuke la kutumia *diesel* ili waweze kupata umeme wakati wakisubiri kuunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuupatia umeme Mji wa Loliondo katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2005. Makadirio ya gharama ya kupeleka umeme yanafikia shilingi bilioni 3.3. Pamoja na kuwepo na njia mbalimbali yaani *options* za kuupatia Mji wa Loliondo umeme, mradi utakaotekelezwa ni ule unaotokana na kukidhi matakwa ya mazingira, mahitaji ya umeme na vigezo vingine muhimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na *TANESCO*, wanaendelea kutafuta fedha ama za humu ndani au za wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali katika kujibu sehemu ya kwanza, uwekaji wa Kangavuke au jereneta la *diesel* ni njia mojawapo ya kuupatia umeme Mji wa Loliondo. Kama nilivyosema njia yoyote itakayoonekana inafaa itahitaji fedha na njia yenye gharama ndogo au gharama nafuu itaangaliwa zaidi kuona kama inakidhi vigezo vingine vyote muhimu ili kuupatia umeme Mji wa Loliondo.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Miji mingi iliyoko pembezoni au Wilaya zilizoko pembezoni hazina umeme; na kwa kuwa kuna umeme nchi jirani kwa mfano Masai - Mara iliyoko karibu na Loliondo; je, Serikali haiwezi kuomba na kuleta umeme kutoka Masai - Mara mpaka Loliondo?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Mji wa Namanga uko mpakani mwa nchi yetu na Kenya; na kwa kuwa wakati wa kampeni mwaka 1995 Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi kwamba umeme utaletwa Namanga na mwaka 1997 alipokwenda Namanga ukarudia tena kusema kwamba umeme lazima ufike Namanga; na Waheshimiwa Mawaziri wote waliopitia katika Wizara hii nao wameahidi hivyo hivyo; je, hiyo ahadi yao itatekelezwa lini? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa niseme waziwazi hapa kwamba wakati mwingine kutokana na mahitaji makubwa sana ya umeme nchini, kazi inayofanyika inawezekana isionekane sana. Lakini napenda niseme kwamba, kwa mfano katika mwaka 2000 Wilaya ambazo Makao Makuu yake yalikuwa hayajafikiwa na umeme kwa takwimu zilikuwa ni Wilaya 14, kati ya mwaka 2000 hadi sasa Wilaya nane tayari ama nyingine zimekwishapata umeme au zipo katika mpango wa kupata umeme ikiwemo hata Wilaya kama kwa watani zangu Wasukuma, kama Urambo na Kaliua kwa akina Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Serengeti, Ukerewe anakotoka Mheshimiwa Spika na kwa Mheshimiwa Balozzi Getrude Mongella na kadhalika.

Kwa hiyo, kazi kubwa inafanyika. Hakuna dhamira ya kusema kwamba Wilaya zilizoko pembezoni zisipate umeme, kazi kubwa inafanyika lakini tunafahamu kwamba mahitaji pia ni makubwa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge kwamba tupate umeme kutoka Kenya. Ningependa kusema kwamba Kenya nao pia wana uhaba wa umeme na hivi sasa wamo katika majadiliano na Tanzania ili kuhakikisha ya kwamba tuwasaidie umeme na kuunganisha umeme baina ya Tanzania na Kenya na pia kuunganisha umeme pamoja na Zambia na nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Namanga. Napenda niseme kwamba ahadi imetolewa, ahadi hii kama zilivyo ahadi nyingine zinafanyiwa kazi. Kuchelewa kwa ahadi hii kwa kweli kunatokana na ukweli kwamba miradi ya kusambazwa umeme ina gharama kubwa na wakati mwingine kama nilivyoeleza katika kujibu swali la Loliondo, fedha zinakuwa bado hazijapatikana. Lakini napenda nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunathamini sana umuhimu wa kupeleka umeme pale Namanga na kwamba mara fedha zitakapopatikana basi umeme huu utafikishwa Namanga.

213

Mahitaji ya Umeme Kata ya Mgandu

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (k.n.y. MHE. ISMAIL J. R. IWWATTA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Uongozi wa *TANESCO* katika ngazi ya Mkoa na Wilaya wameshapelekewa maombi ya wananchi wa Kata ya Mgandu ya kupatiwa umeme; na kwa kuwa Uongozi huo umekwenda Mgandu kwa zaidi ya mara mbili kwa ajili ya kufanya uchunguzi ili kuona kama kiuchumi eneo hilo linakidhi haja ya kupelekewa umeme na kuridhika kwamba inafaa:-

Je, ni lini sasa wananchi wa Kata hiyo watapelekewa umeme kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kimaendeleo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mgandu iko umbali wa kilometa 65 kutoka Itigi sehemu ambayo umeme unapatikana kwa hivi sasa. Tathmini ya awali ambayo imefanywa na uongozi na Shirika la Umeme nchini yaani *TANESCO* katika Mkoa wa Singida, inaonyesha kuwa mradi huu unakisiwa kugharimu shilingi za Kitanzania bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali lingine lililopita hapa, ni kwamba mradi kama huu utatekelezwa tu pale ambapo fedha zimepatikana. Hadi sasa fedha hazijapatikana na hapo fedha zitakapopatikana tutaushughulikia mradi huu.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa niaba ya Mheshimiwa Ismail Iwavtta, naomba kuwaombea dua Mwenyezi Mungu ajalie ili hizi fedha shilingi bilioni 1.2 ziweze kupatikana ili Kata ya Mgandu waweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa Kata ya Mgandu gharama yake ni shilingi bilioni 1.2; lakini kwa tathmini iliyofanyika mwaka 1997 katika Kijiji cha Chemchem Wilaya ya Mafia ilibainika kwamba ni shilingi milioni 48 tu, naamini juu ya gharama zetu za shilingi kushuka sasa hivi haiwezi kuzidi shilingi milioni 60; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kata ya Miburani, Kijiji cha Chemchem Wilaya ya Mafia ili wananchi hao nao waweze kufanikisha kuingia katika karne ya kisasa? *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Aah!! Swali la umeme wa Mafia liletwe kipekee, hilo ni jipya. *(Kicheko)*

Na. 214

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA (k.n.y. MHE. BAKARI M. MBONDE)
aliuliza:-

(a) Je, ni mafanikio gani yamepatikana hadi sasa kutokana na kuanzishwa na kutekelezwa kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya nchini?

(b) Je, ni matatizo gani yamejitokeza katika kutekeleza majukumu ya mfuko huo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna mafanikio kadhaa yaliyopatikana kwa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, wanachama wengi hasa wenye kipato cha chini wamekuwa na uhakika zaidi wa kupata matibabu bila hata kuwa na fedha mfukoni kwenye vituo vya umma na vile vya mashirika ya kujitolea na vituo binafsi.

Pili, kwa kuwa vituo vya kutolea huduma visivyo vya Serikali na vile vya Serikali vimehusishwa, kumejitokeza ushindani mkubwa wa utoaji huduma, jambo linalopelekea kuboreka kwa huduma, tatu, kuwepo kwa Mfuko huu kumepelekea kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwa vituo vitoavyo matibabu ili kuhakiki ubora wa huduma zinazotolewa na nne, kuongeza na kuboresha mafao ya wanachama kwa kuongeza idadi

ya vipimo toka 9 hadi 15 kikiwemo kile cha *Ultra Sound* na kuongeza aina ya gharama za upasuaji ukiwemo ule unaofanywa na Madaktari Bingwa ambao hapo awali haukuwemo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio tuliyoyapata pia kumekuwa na matatizo yafuatayo:-

Ugeni wa dhana ya Mifuko ya Bima za Afya kulifanya wafanyakazi wengi wawe na shaka nao, uhaba wa dawa na vifaa kutokana na Bajeti isiyotosheleza, wanachama kutojaza fomu za uanachama na kuwasilisha picha kwa wakati ili kutengenezewa vitambulisho ambavyo vingeondoa kero ya matumizi ya hati za matibabu na baadhi ya vyama vya wafanyakazi kutoelewa vizuri faida ya Mfuko huu na hivyo kuwafanya wanachama wao kuwa na mashaka nao.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Bakari Mbonde, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya hospitali zilizoteuliwa huwa wanashindwa kuwahudumia wateja wao wakisema kuwa pesa hazijapelekwa kwa mfano hospitali moja iliyokuwepo Lugoba na hata Bagamoyo Mjini huwa imetokea hivyo; je, inapotokea hivyo tunawashauri nini wale wagonjwa ambao ni wateja wa bima na zile hospitali ambazo zimeteuliwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuna mkataba unaowekwa baina ya vituo vinavyotoa huduma na Mfuko wa Bima ya Afya. Katika mkataba huo imeelezwa wazi kabisa kwamba, kipindi cha kutoka madai yanapelekwa mpaka madai yanapolipwa lazima uwe muda maalum. Ndani ya muda huo kama muda haujapita basi kituo hakina haki ya kudai lakini kama muda umeishapita, basi bila shaka kituo kinaweza kuvunja mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kweli kuna tatizo kama hilo, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuone jinsi gani tunaweza kusaidia katika suala kama hilo.

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wateja wengi wa Mfuko wa Bima ya Afya ni walimu wanaokaa maeneo ya Vijijini; na kwa kuwa walimu hao hutumia zahanati zilizo Vijijini; ni kwa nini basi Mfuko wa Bima ya Afya unakwenda kwa mwendo wa konokono kutambua zahanati ili walimu wanaoishi Vijijini waweze kuhudumiwa na zahanati hizo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ieleweke kwamba zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za Mikoa na hospitali za Rufaa zote za Serikali zimo ndani ya utaratibu wa Mfuko wa Bima ya Afya. Kwa hiyo, kama tunazungumza suala la kusajili hospitali mpya, ni zile tu za mashirika ya dini na binafsi,

jambo ambalo linafanyika kwa kasi nzuri na takwimu tutazitoa wakati wa Bajeti yetu.
(Makofi)

Na. 215

Fedha kwa Ajili ya Huduma za Afya Nchini

MHE. DR. AARON D. CHIDUO aliuliza:-

Kwa kuwa kuna utata au kutoeleweka sawa sawa juu ya kiasi cha fedha kinachotolewa kwa ajili ya huduma za afya nchini na jinsi zinavyogawanywa:-

(a) Je, huduma za afya nchini zimepata kiasi gani cha fedha kutoka kwenye Bajeti ya mwaka 2000/2001, 2001/2002 na 2002/2003?

(b) Je, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zimepata fedha kiasi gani kila moja na kiasi kilichotolewa kwa Serikali za Mitaa ni asilimia ngapi katika vipindi hivyo?

(c) Je, ni kiasi gani katika mgao huo kimetumika kwa huduma za tiba, kinga, mafunzo na utawala katika vipindi hivyo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bajeti kwa huduma za afya kati ya mwaka 2000 hadi 2003 ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka	Kiasi
2000 - 2001	100.7 bilioni
2001 - 2002	142.1 bilioni
2002 - 2003	172.3 bilioni

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote hiki mgao kati ya Serikali Kuu (Wizara ya Afya) na ile ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka	Wizara ya Afya	TAMISEMI
2000 - 2001	62.7 bilioni (62.3%)	37.9 bilioni (37.6%)
2001 - 2002	89.9 bilioni (63.2%)	52.2 bilioni (36.7%)
2002 - 2003	109.2 bilioni (63.3%)	63.2 bilioni (36.7%)

(c) Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka	Kinga	Tiba	Mafunzo	Utawala
2000 - 2001	53%	30%	8%	9.0%

2001 - 2002	50%	33%	8%	9.0%
2002 - 2003	51%	34%	9%	6.0%

Na. 216

**Matengenezo ya Barabara ya Kutoka Korogwe - Mabondeni
na Daraja la Songea**

MHE. MUSA A. LUPATU (k.n.y. MHE. JOEL N. BENDERA) aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Korogwe - Kwamndolwa - Kerenge - Magoma - Mashewa Mtoni - Bombo - Daluni - Maramba hadi Mabokweni ndiyo uti wa mgongo na tegemeo la mawasiliano ya barabara kwa wananchi waishio kwenye Kata zaidi ya kumi katika Jimbo la Korogwe na Mkinga; na kwa kuwa kwa kipindi kirefu nimekuwa nikiishauri *TANROAD* Tanga juu ya kushughulikia maeneo korofi kwenye barabara hiyo kwa kuweka changarawe ili iweze kupitika kwa nyakati zote; na kwa kuwa mimi na Mhandisi wa Mkoa wa Tanga wa *TANROADS* pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Vijiji vilivyo kandokando ya barabara hiyo tulikwenda kuangalia maeneo korofi ya barabara hiyo na kukubaliana kuwa yafanyike matengenezo ya changarawe lakini cha kushangaza ni kwamba barabara ya Korogwe - Bombo na ile ya Korogwe - Kwagunda - Mnyuzi hadi Maguzoni zimechongwa na greda bila kuwekewa changarawe matokeo yake ni kwamba hata ile changarawe ya zamani imeondolewa na kuzifanya barabara hizo kutopitika kabisa:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizomfanya Mkandarasi aliyepewa kazi ya kutengeneza barabara hiyo ashindwe kuheshimu makubaliano baina ya Mhandisi wa Mkoa, Mbunge na Uongozi wa Serikali ya Kijiji?

(b) Je, Serikali ipo tayari kumtaka Mhandisi aliyetengeneza barabara hiyo aweke changarawe kwenye maeneo korofi kama inavyotengenezwa sasa eneo la Foroforo na atafanya hivyo lini?

(c) Je, Serikali ina mipango gani ya kulitengeneza daraja la Songea ambalo kwa muda mrefu limekuwa likibomoka kutokana na mvua kubwa ili lisije kuleta maafa na kusababisha kukosekana kwa mawasiliano kwenye barabara hiyo muhimu inayotegemewa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita mwaka 2002/2003 barabara ya Korogwe - Bombomtoni inayopita katika Vijiji vya Kerenge, Magoma na Mashewa yenye urefu wa kilomita 63 ilipangiwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida

kwa Bajeti ya shilingi milioni 15 na ukarabati katika maeneo ya Foroforo kwa Bajeti ya shilingi milioni 100.

Barabara ya Bombomtoni hadi Mabokweni yenye urefu wa kilometa 62.46 ilipangiwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida kwa Bajeti ya shilingi milioni 16.59 na barabara ya Korogwe - Maguzoni yenye urefu wa kilometa 28.8 ilipangiwa kufanyiwa matengenezo ya kawaida kwa Bajeti ya shilingi milioni 12.28. Fedha hizi zilizopangwa zote zilitolewa na matengenezo yaliyopangwa yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi aliyepewa kazi za matengenezo ya kawaida katika barabara ya Korogwe - Bombomtoni na Korogwe - Maguzoni alifanyakazi kulingana na mkataba aliopewa na Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Tanga. Aidha, hapakuwa na makubaliano mengine ya nje ya Mkataba kati ya Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga na Mheshimiwa Mbunge wala viongozi wa Serikali ...*(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Makofi hayo yanaashiria kwamba kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni amerejea kutoka safari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea na majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba nirudie *paragraph* hii.

SPIKA: Sawa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, Mkandarasi aliyepewa kazi za matengenezo ya kawaida katika barabara ya Korogwe - Bombomtoni na Korogwe - Maguzoni alifanya kazi kulingana na mkataba aliopewa na Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Tanga. Aidha, hapakuwa na makubaliano mengine ya nje ya Mkataba kati ya Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga na Mheshimiwa Mbunge wala viongozi wa Serikali za vijiji kuhusiana na matengenezo ya barabara hii.

Mkandarasi alimaliza kazi kulingana na mkataba wake ikiwa ni pamoja na marekebisho aliyotakiwa kufanya. Kazi hii ilifanywa na Mkandarasi *M/s City Interbuild* kwa gharama ya shilingi milioni 22.692. Aidha, sehemu zote zilizofanyiwa kazi zinapitika vizuri bila matatizo yoyote.

(b) Mheshimiwa Spika, si rahisi kumtaka Mkandarasi aliyefanya kazi hii kuweka changarawe katika maeneo korofi kwa sababu Mkandarasi alikwishafanya kazi yake kulingana na mkataba aliopewa. Kazi aliyofanya Mkandarasi huyu *M/s City Interbuild* ni ya matengenezo ya kawaida, wakati ile inayofanywa katika eneo la Foroforo ni ukarabati.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la daraja la Mto Songea katika barabara ya Korogwe - Bombomtoni kwa kuwepo makalvati yasiyokidhi haja kwani wakati wa mvua huwa yanazibwa na magogo na takataka zinazoletwa na maji ya mvua kutoka milimani. Hii husababisha barabara kukatika karibu kila mwaka katika eneo hilo.

Serikali bado inatafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kulijenga Daraja la Songea hivyo kuondokana na ubomokaji wa makalvati yaliyopo.

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu ... *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Makofi hayo yanamshangilia Mheshimiwa Waziri Edgar Maokola-Majogo, aliyepata matatizo huko India. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Musa Lupatu, endelea na swali lako.

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mara nyingi barabara hizi zinapotengenezwa kama zilikuwa kwenye kiwango cha changarawe na inapopita *grader* mara nyingi kwa sababu ya fedha ndogo zinazotengwa, Makandarasi hawawezi kurudishia changarawe je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kuhakikisha kwamba barabara ambazo zilikuwa za changarawe zinapopigwa *grader* zinarudishiwa tena changarawe?

(b) Kwa kuwa mara nyingine Makandarasi wanaopewa matengenezo ya barabara hawana uwezo wa kutosha je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba kila Mkandarasi anayepewa barabara ni yule tu mwenye uwezo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba mara nyingine Makandarasi wanapopata kazi ya kutengeneza barabara huwa wanapewa kazi katika barabara zenye changarawe lakini kwa kawaida barabara yenye changarawe iliyoshindiliwa hupewa kazi ya kukarabati mashimo sehemu korofi sio tena kupiga *grader* barabara nzima. Kwa hiyo, kuondoa hizo changarawe na kuacha udongo atakuwa anafanya kinyume cha kazi ya barabara. Lakini pale inapotokea na sisi tukaarifiwa huchukua hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makandarasi wasiokuwa na uwezo. Tatizo hili la Makandarasi wasiokuwa na uwezo likifika mikononi mwetu mara moja sisi huwa tunatuma Mwenyekiti wa Bodi ya Makandarasi aende akachunguze. Anapotuletea taarifa kwamba Mkandarasi huyu kwa kweli hana uwezo basi na sisi huwa tunamwambia Mwenyekiti amfute mara moja katika Bodi hiyo. Kwa hiyo, huwa tunachukua hatua nyingi sana na ushahidi mmeona taarifa ya Bodi imewafuta Makandarasi maelfu kwa maelfu kwa sababu ya taarifa tu. Kama hatupati taarifa basi tunajua kwamba amekubalika.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya kutoka Maramba - Galuni - Korogwe ina hali mbaya sana na barabara hiyo ni moja ya uti wa mgongo wa uchumi katika maeneo hayo. Tatizo la barabara hiyo ni kwamba wanapomwaga kifusi huwa haishindiliwi kwa *compactor* ili idumu kwa muda mrefu. Je, Serikali itachukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba utengenezaji wa barabara hiyo unakuwa kwa utaratibu huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara ya Maramba - Galuni najua kweli ni barabara ambayo ni tífutifu na mara nyingi husumbua. Lakini kutengeneza barabara ile kwa kushindilia inategemea na uwezo wa pesa ambao Serikali inao. Kama tukipata pesa za kutosha tutafanya hivyo lakini tusipopata pesa za kutosha Waheshimiwa Wabunge itabidi mkubali pale tunapoleta pesa na kusema itatengenezwa kilomita mbili mara nyingi hamtaki mnamwambia *Regional Manager* hebu piga *grader* barabara yote na kwa pesa hiyo kidogo akipiga *grader* barabara yote hakuna kushindilia. Lakini tutajitahidi tukipata pesa naifahamu barabara hiyo tutaishughulikia.

Na. 217

Kasi ya Juu Inayoruhusiwa Kwenye Barabara zetu

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO (k.n.y. MHE. DR. JAMES A. MSEKELA) aliuliza:-

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu aliipendelea Tanzania kijiografia kwa kuipa nafasi ya kuwa muhimili wa uchukuzi (*A Maritime Nation*) kwa eneo la Maziwa Makuu ambapo hatuna budi kuitumia kikamilifu asili hiyo; na kwa kuwa katika utandawazi kuna *option* moja tu ya kushindana kibiashara ambapo shahaba kubwa ni kujenga barabara kuu (*highways*) za viwango vya juu kama vile Dar es Salaam - Morogoro - Tunduma, Chalinze - Arusha - Namanga na kadhalika na kwa kuwa kupandisha kasi ya juu inayoruhusiwa (*highest allowable speed*) kwa magari katika *highways* hizo ni mojawapo ya malengo ya kujenga barabara za viwango hivyo na kwa kuwa Serikali inafanya vizuri kuendelea kuruhusu kuingizwa nchini magari makubwa na madogo yaliyo madhubuti, yenye viwango vya teknolojia za kisasa na yenye uwezo wa kwenda kwa kasi zaidi lakini kwa usalama kuliko awali.

Je, ni lini Serikali itapandisha rasmi kasi ya juu inayoruhusiwa katika barabara zetu kuu zenye viwango vya juu nilivyovitaja?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Kijiografia Tanzania inayo nafasi ya kuwa muhimili wa uchukuzi kwa mizigo itokayo na kuingia katika nchi za eneo la Maziwa Makuu hasa Malawi, Zambia, Demokrasia ya Kongo, Burundi na Rwanda. Mpaka sasa mizigo mingi ya nchi hizo hupitia katika nchi yetu. Ili kuhakikisha usafirishaji wa mizigo hiyo unafanyika bila ya

matatizo makubwa katika barabara zetu, Serikali kwa kutumia misaada na mikopo kutoka kwa wafadhili na pia fedha za hapa nchini imekuwa ikijitahidi kujenga, kukarabati na kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara zetu. Kwa kuwa ujenzi wa barabara mpya huhitaji fedha nyingi kuliko ukarabati wa barabara za zamani na nchi yetu ni maskini, ukarabati umekuwa ukifanywa kupitia kwenye barabara za zamani isipokuwa tu pale panapokuwa na ulazima sana wa kubadilisha mwelekeo (*alignment*) ili kupunguza gharama.

Kwa hiyo, ukarabati umekuwa ukilenga zaidi kuimarisha tabaka za barabara na madaraja yake ili kuwezesha magari kupita bila kukwama kwa urahisi bila kuhusisha mabadiliko makubwa katika *alignment* ambayo huhusisha kukwepa au kukata milima, kubadilisha vipimo vya kona, kukwepa makazi ya watu, kujenga *fly-over* na kadhalika vitu ambavyo vinatawala kuongeza kasi ya magari.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kupandisha rasmi kasi ya juu inayoruhusiwa katika barabara zetu kwani barabara zetu zote zikiwemo alizotaja Mheshimiwa Mbunge zinahitaji marekebisho makubwa ya *alignment* kabla ya kuruhusu magari kutembea kwa kasi zaidi. Kuruhusu bila kufanya marekebisho hayo kutaongeza ajali katika barabara zetu.

Kwa hiyo, marekebisho ya kasi ya juu yatafanywa baada ya uchumi wa nchi kuwa mzuri na kuzifanyia marekebisho muhimu na ya lazima barabara zetu. Aidha, kwa barabara mpya zinazojengwa kufikia kiwango cha lami kwa mara ya kwanza, viwango vya kasi ya juu ya magari itabaki kuwa kama ya barabara zilizopo za lami kutokana na sababu nilizoielezea hapo juu kwamba kuongeza kasi ya juu kunaambatana na gharama kubwa za ujenzi kwani hata upana na barabara inabidi uongezeke.

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa alama za mabango zinazoonyesha viwango vya kasi barabarani zinaibiwa sana, je, Wizara ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mabango hayo hayaibiwi?

(b) Kwa kuwa askari wachache wa *Traffic*, nasisitiza wachache wamekuwa na tabia ya kupanga mitego ya kuwasimamisha madreva kwenye kona na vichakani jambo ambalo huweza kusababisha ajali, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuwasiliana na Wizara husika ili utaratibu huu ukomeshwe?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mabango ya alama za barabarani, ni kweli kabisa alama za barabarani nyingi huwa zinapotea na kung'olewa na baadhi ya watu ambao ni wezi lakini jukumu hili sio la Wizara ya Ujenzi tu ni jukumu la Watanzania wote. Kwa hiyo, napenda kutumia Bunge hili kuwaarifu Watanzania wote

wawe na wajibu wa kuhakikisha kwamba alama za barabara hazing'olewi kwa sababu ni kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu trafiki kwamba wanasimamisha magari kwenye kona, ni kwamba Polisi wakiwemo *Traffic* wana wajibu wa kusimamisha gari lolote ambalo linavunja sheria za barabarani za mwaka 1973 mahali popote pawe kwenye kona, barabarani, kwenye mteremko na mahali pengine pote. Kwa hiyo, nafikiri huo ni wajibu wao kuwashika wanaokiuka taratibu za barabarani lakini kama kuna mahali ambapo *Traffic* amefanya makosa bado tutaedelea kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha tatizo hilo linaondoka.

Na. 218

Bodi za Shule za Sekondari za Kutwa

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi katika Jimbo la Bumbuli wameitikia wito wa kujenga Shule za Sekondari za Kutwa kwa nguvu zao huko Tamota, Mgwashi na Vuga na wanaendelea na ujenzi hadi kukamilisha majengo yote:-

(a) Je, Serikali inashauriwa na chombo gani katika kuteua Bodi za kuongoza shule hizo na je, Mkuu wa Wilaya ya Lushoto ambaye ni kiungo wa maendeleo katika Wilaya hiyo ameshirikishwa kwa kiwango gani katika uteuzi wa bodi za Shule hizo tatu?

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kutoa mwongozo unaopambanua majukumu ya Bodi inazoteua za kuongoza shule na zile zilizoteuliwa na wananchi za kusimamia ujenzi wa shule?

(c) Je, wananchi wanaojenga shule hizo wanayo haki ya kujua matumizi ya michango wanayotoa wanafunzi wanaoingia katika shule hizo?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bodi za Shule ni suala la kisheria kama linavyoainishwa katika Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 iliyopitishwa na Bunge hili. Sheria hiyo imempa uwezo Waziri wa Elimu katika Kifungu Na.38 kutunga sheria ndogo ziiwazo Kanuni (*Regulations*) kuhusu uteuzi wa Bodi za Shule na madaraka yake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ndogo iitwayo *The Grand Aided Community School Board (Establishment Order)* ya mwaka 2002, uteuzi wa Bodi ya Shule ya Shule za Sekondari umekasimiwa kwa Mkuu wa Mkoa ambaye anategemewa amshirikishe Mkuu wa Wilaya ya Shule husika kupendekeza majina.

(b) Mheshimiwa Spika, majukumu ya Bodi za Shule yamefafanuliwa katika Kanuni husika na majukumu ya Kamati za Shule zinazoteuliwa na wananchi kusimamia ujenzi wa shule, huelezwa bayana wakati wa uteuzi wa Kamati hizo. Kwa kuwa majukumu ya Bodi ya Shule yamo katika Kanuni iliyoziunda, kinachohitajika ni kila chombo kuzingatia majukumu yake na kuendesha mambo kwa ushirikiano na nia njema.

(c) Mheshimiwa Spika, michango inayochangwa katika Shule za Sekondari inaidhinishwa na Bodi ya Shule ambayo inawakilisha pia waliohusika na uanzishaji wa shule hiyo ili kuendelea kuyajua mambo yote ya Shule hiyo. Hata hivyo fedha za Serikali zinazotolewa au karo za shule, huwekewa utaratibu wake wa matumizi na utoaji hesabu. Kwa hiyo, wananchi, wanaojenga shule hizo wanayo haki ya kujua na wanashirikishwa ili kuyajua mapato na matumizi ya fedha zote katika shule.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Wakuu wa Shule ni Mameneja, je, Wakuu wa shule hizi tatu wamepatiwa mafunzo ya *management* ya shule za namna hiyo na kama bado ni lini watapatiwa mafunzo hayo?

(b) Kwa kuwa shule hizi tatu ziko katika vijiji ambavyo vina mazingira magumu ya usafiri je, Wizara ina mpango wa kuwatafutia usafiri kwa mfano wa pikipiki ili waweze kufanya kazi zao za *management* vizuri zaidi?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, suala la Wakuu wa Shule kupatiwa mafunzo, jambo hili Wizara yangu imeliangalia upya na tumeona kwamba ipo haja ya kuanzisha utaratibu wa mafunzo.

Kama Mheshimiwa Wabunge watakumbuka katika hotuba ya bajeti nimesema kwamba Chuo cha *ADEM* cha Bagamoyo wamekwishatayarisha *syllabus* ya mafunzo hayo na tutakuwa tunahakikisha kwamba kila anayechaguliwa kushika nafasi ya *Headmaster* anapitia kwenye mafunzo hayo kama vile tunavyofanya kwa Wakaguzi.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba sasa hivi kuna upungufu wa baadhi ya Wakuu wa Shule wameteuliwa tu kwa kutegemea kwamba wanajua namna ya kuwa Wakuu wa Shule. Kwa hiyo, utaratibu huu mpya wale ambao hawajapitia mafunzo ya *School Management* watakwenda kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili la mazingira magumu katika shule hizo tatu kama ambavyo nilitoa maelezo katika Bunge hili tukiwa katika hatua ya Kamati kwamba suala la magari kwa ajili ya shule za Serikali tutaliingiza katika mpango wa MMES.

Sasa hivi shule zilizokabidhiwa Serikalini zilizojengwa na wananchi zimekuwa nyingi na hatujazikamilisha kuzipatia magari. Lakini katika mpango ule wa MMES gari ni *standard equipment* yaani ni kitu kinachohitajika katika kila shule ya Sekondari. Kwa hiyo, ndani ya mpango ule tutaondoa mapungufu haya.

Na. 219

Uchangishaji Wanafunzi Mashuleni

MHE. SEMINDU K. PAWA aliuliza:-

Kwa kuwa Waraka Na.7 wa Wizara ya Elimu na Utamaduni unapiga marufuku michango ya fedha taslimu zinazotowza kwa wazazi na wanafunzi peke yao:-

(a) Je, shule inaruhusiwa kuchangisha wanafunzi vifaa vya michezo, kuchangia mitihani ya wiki kwa shilingi 1,000/= hadi shilingi 1,500/= kwa wiki kiasi ambacho ni kikubwa kuliko ada ya *UPE* iliyofutwa?

(b) Je, iwapo ipo shule inachangisha baadhi ya wanafunzi, Wizara inatoa tamko gani kwa shule hizo juu ya fedha zilizochangwa?

(c) Kama orodha ya baadhi ya shule zinazofanya hivyo ikitolewa hapa Bungeni, je, Serikali itachukua hatua gani?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kwanza, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa Waraka wa Elimu Na.7 wa mwaka 2002 umekataza kabisa michango ya wazazi wa Shule za Msingi peke yao. Baada ya kukubaliana na ukweli huo, majibu ya sehemu (a) (b) na (c) ya swali lake ni kama ifuatavyo:-

(a) Shule hairuhusiwi kuchangisha wanafunzi kwa ajili ya vifaa vya michezo na mitihani ya wiki shilingi 1,000/= hadi shilingi 1,500/= kwa sababu mahitaji hayo yamepangiwa fedha katika ruzuku ya uendeshaji ya dola 10 sawa na shilingi 10,000 kwa mwanafunzi kama nilivyofafanua katika kauli ya Serikali niliyoitoa ndani ya Bunge hili tarrahe 8 Novemba, 2001.

Aidha, katika nyongeza (a) na (c) ya hotuba ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 tumeonyesha mafungu yote yaliyotolewa kwa Halmashauri kama ruzuku za maendeleo, uendeshaji na uwezesaji pamoja na fungu lililopangwa kwa ajili ya michezo kwa kila Halmashauri.

(b) Kama ipo shule iliyochangisha wanafunzi au wazazi wa wanafunzi naomba nipewe taarifa ili hatua ya kinidhamu ichukuliwe dhidi ya walioendesha na kuipokea michango hiyo iliyokatazwa na Serikali. (*Makofi*)

(c) Serikali itachukua hatua kama nilivyoeleza katika sehemu (b) ya swali.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Waraka Na.7 wa mwaka 2002 haubagui lakini baadhi ya Walimu katika Shule za Msingi, orodha ataipata siku za hivi karibuni wanabagua, je, yuko tayari kupokea barua mbalimbali kutoka kwa wananchi wanaonisikia sasa hivi kwa kutumia anuani namba 941, Dodoma ili ziwahi, wapeleke barua bila stempu nitazigharimia mimi kwa kutumia jina la Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, ili azipokee, yuko tayari kuzipokea barua hizo kutoka Tanzania nzima, kutoka kwa wananchi ambao wanachangishwa? *(Kicheko/Makofi)*

SPIKA: Polepole, Waziri anaandika. *(Kicheko)*

MHE. SEMINDU K. PAWA: Aah, hajasikia. Je, Watanzania ambao wanachangishwa wanaweza kuandika barua kwa anuani namba 941, Dodoma kwa Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, hata kama hawana stempu mimi nitazigharimia walete hapa katika kipindi hiki atakubali kuzipokea? Hiyo ni a.

(b) Kwa kuwa Waraka haubagui lakini baadhi ya Walimu wanabagua na kwa kuwa fedha zilitolewa lakini wananchi walichangishwa je, watarudishiwa fedha zile ambazo wamechangishwa?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, niko tayari kupokea malalamiko hayo lakini ni vizuri zaidi kama yatapitia kwa Mheshimiwa Mbunge akayapa uzito kuliko ikija barua moja moja na tukipata taarifa tutachukua hatua husika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio rahisi kusema hela zitarudishwa ni vizuri kama yako malalamiko tuone mazingira halisi, nini kilikuwepo hata ikaamuliwa hivyo. Lakini napenda nichukue nafasi hii kusema tena kwa mara nyingi kwamba suala hili la kukataza michango ya kulipwa na wazazi ni suala lenye nia njema kwa sababu lilikuwa linaongeza kasi ya wanafunzi kuacha shule.

Mheshimiwa Spika, tulifikia asilimia 6.6 ya wanafunzi kuacha shule kwa mwaka na ukijumlisha kwa miaka sita unatakiwa uchukuwe hiyo asilimia 6.6 uzidishe mara miaka sita na ndio maana Kitaifa katika kila watoto 100 waliokuwa wanaanza darasa la kwanza walikuwa wanamaliza watoto sita tu darasa la saba. Kwa hiyo, tulikuwa na ugonjwa ambao tiba yake ilikuwa ni kufuta ada na michango. Kwa hiyo, naomba tusaaidiane.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Waraka Na.7 na Nyaraka nyingine zilizotolewa hivi karibuni zinatokana na Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 na kwa vile sheria hiyo

haikudhamiria wala haikuwa na madhumuni au malengo ya yote yanayotokea sasa katika sekta ya elimu na namthibitishia hili Waziri kwa sababu nilihusika katika kuandika sheria hiyo wakati huo, sasa Waziri haoni wakati umefika wa kutunga Sheria mpya ya Elimu ya mwaka 2004 na kuendelea?

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimtambue kwamba yeye ni bingwa katika masuala haya ya sheria kwa hiyo, anapouliza swali hili lina hoja ya uzito wa kisheria. Mimi kama Waziri naheshimu sana kwamba limetolewa na mtu mwenye uzito huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane naye kabisa kwamba sasa hivi Sheria ya Elimu kwanza ina viraka vingi, mabadiliko yaliyofanywa hapa na pale kuanzia mwaka 1978 na tumegundua kwamba kuna haja ya kuitazama upya. Katika nchi yetu kumekuwa na mabadiliko mengi yanayoendelea pamoja na mageuzi ya Halmashauri za Wilaya ambapo Halmashauri hizi ndizo zinasimamia Shule za Msingi. Kwa hiyo, mabadiliko yote haya Serikali imeshaamua kuyatazama upya na kuitazama upya Sheria ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba rasimu ya kwanza ya Sheria mpya ya Elimu iliyokwishaandaliwa na wataalam wote nimekabidhiwa juma lililopita ili niweze kuiangalie kama imeingiza mambo yote na natarajia kuishirikisha Kamati husika ya Bunge tushirikiane kuitazama kwa pamoja ili hatimaye tuweze kuleta Sheria mpya ya Elimu hapa Bungeni. Siwezi kujua lini, itategemea na ratiba ya kazi zetu za hapa Bungeni.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha kabla ya muda wake kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine. Matangazo ya leo, kuna kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti, anaomba kikao hicho kifanyike kuanzia kipindi hiki baada ya maswali chumba namba 58.

Kikao cha Wabunge Wanawake wote *(TWPG)* Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Janeth Mashele, anawaomba Wabunge wanawake wote leo tarehe 11 Julai, 2003 saa 7.00 mchana wakutane katika chumba namba 81, ghorofa la pili.

Tangazo la semina ya kesho, tutakuwa na semina kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambao unasimamiwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni kuanzia saa 3.00 asubuhi kama kawaida. *(Makofi)*

Tangazo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, mtakumbuka mapema mwezi huu niliwaandikia barua Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Afya imepanga wataalam wa kuwezesha kupima afya za Wabunge hapa hapa katika maeneo ya Bunge.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya anasema wataalam kutoka Wizarani waliokuja kufanya *Prostate Cancer Screening* kwa Wabunge wameomba wapate nafasi ya kuzungumza na Wabunge wote kwa pamoja ili kuwaelezea kuhusu kipimo chenyewe. Wanasema itakuwa vigumu kuongea na Mbunge mmoja mmoja.

Sasa tufanye hivi, nafikiri baada ya kuahirisha shughuli za Bunge asubuhi hii, nadhani itakuwa mapema kabla ya saa 7.00 mchana basi wale Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kupima mambo haya wakae humu ndani ili wataalam waje kuwaelimisha. *(Kicheko)*

Mwisho wa matangazo, Katibu tunaendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

(Majadiliano yanaendelea)

MOHAMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nikiwa msemaji wa mwanzo.

SPIKA: Ngoja kidogo tutulizane ndiyo uanze. Sasa unaweza kuendelea.

MHE. MOHAMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Spika, nasema nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili na mimi nichangie kidogo katika Wizara hii muhimu sana ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naanza kwa kusema kwamba sina sababu ya kutokuunga mkono hoja hii, kwa hiyo, naanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara mama. Ni Wizara ambayo inasimamia amani na utulivu katika nchi. Nadhani Waheshimiwa wenzangu watakubaliana na mimi kwamba bila ya amani na utulivu hatuwezi kuwa na maendeleo.

Kwa hiyo, maendeleo ya nchi kwa ujumla kwa kiasi kikubwa sana pamoja na kwamba yanategemea raia wenyewe lakini pia kwa msaada mkubwa sana wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii watu walio na jukumu kubwa sana la kuimarisha hiyo amani na utulivu wenyewe ni hawa wenzetu wa Jeshi la Polisi. Sasa mimi nataka niseme tu kwamba kwa uzito wa kazi waliyonayo ukilinganisha kazi yao na vikosi vingine vya ulinzi kama vile Jeshi la Wananchi, Usalama wa Taifa na wao kwa kweli hawa inaonekana kwamba kazi yao hailingani kabisa na mapato yao.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri afikirie zaidi pamoja na kwamba Bajeti yake imeonyesha kwamba mishahara yao itaongezwa lakini sijui ni kwa kima gani. Lakini nasema kwamba kwa uzito wa kazi yao hawa wanapaswa kupata mishahara mikubwa na marupurupu vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara ya Mambo ya Ndani na ndani kuna mambo mengi, hapa kuna majambazi, kuna wezi wa kawaida, kuna vibaka, kuna watu wa

madawa ya kulevya, kuna wakwepa kodi ili mradi kuna wahalifu wengi na wa aina nyingi na hao wote kwa kweli wanaotegemewa kuwadhiti ni askari Polisi.

Sasa ili waweze kufanya vizuri kazi zao nasisitiza kwamba maslahi yao yawe yanaangaliwa mara kwa mara. Pale Chakechake tunaishi nao, kwa kweli ukilinganisha maisha yao na maisha ya vikosi vingine vya ulinzi hivyo nilivyovitaja kuna tofauti kubwa. Pale Chakechake mimi sijapata kumwona askari Polisi hata mmoja aliyefanikiwa kujenga nyumba ya maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawafahamu watu wengi ambao wanafanya kazi katika kikosi hiki cha Usalama wa Taifa wamejenga majumba ya fahari kabisa. Pia nawafahamu baadhi ya Wanajeshi wamejenga majumba ya fahari kabisa, lakini askari Polisi kwa kweli ni kikosi kinachoonekana kwamba maisha yao yapo hoi bin taaban. Kwa hiyo, naomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla iwafikirie sana hawa askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu suala la *passport*. Waheshimiwa wenzangu akiwemo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, alilizungumzia sana hili suala la *passport*. Lakini mimi nasema kwamba sioni sababu kwa nini *passport* au hati ya kusafiria impe shida sana mwananchi kuipata. Kumnyima mwananchi au kusababisha usumbufu kwa mwananchi kupata *passport* kwanza kabisa ni kwenda kinyume na wito wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu katuhimiza waja wake katika *Qur-an* Tukufu kwa kuisifu hii ardhi yake, yaani hii dunia yake, kwamba ni kubwa sana na ni pana sana na ametuagiza sisi waja wake tutembe katika hii dunia ili tupate fursa pana zaidi ya kujitafutia riziki. Kisichokuwepo Tanzania, Kenya kipo, kisichokuwepo Kenya, Uganda kipo. Sasa unaposababisha usumbufu wa mtu kupata *passport* unamnyima fursa ya kutembea kwenda huko. Kwa hiyo, ni vizuri kwa kweli tatizo hili lingeondoka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hii inakiuka hata Katiba yetu ya nchi. Katiba yetu ya nchi Ibara ya 17(1) ukurasa wa 18 inasema: “Kila raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote kutoka nje ya nchi na kuingia na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hapa kwanza, tunakwenda kinyume na agizo la Mwenyezi Mungu lakini pia tunakiuka Katiba yetu wenyewe. Lakini tatu, inasema kwamba ikiwa kitendo cha kumpatia raia *passport* kitasababisha usumbufu basi hatimaye kinaweza kikasababisha rushwa. Kwa sababu Waswahili wanasema penye udhia penyeza rupia. Sasa mtu akiwa amehangaika miezi nenda rudi, anatafuta *passport* akifika anaambiwa njoo kesho au keshokutwa au mwakani, atauliza kwani kuna tatizo gani? Anaweza akaambiwa chai. Kwa hiyo, anaweza kutoa chai. Kwa hiyo, ili kuondoa pia nafasi ya rushwa ni afadhali Serikali ikabadilisha kidogo hii *quality* ya mambo ya *passport* ikaifanya rahisi zaidi kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, sijui kuna nini kwa sababu mimi nakumbuka kwa mfano pale kwetu Pemba katika Mkoa wa Kusini wananchi walikuwa wakipata *passport* pale pale, *process* zote zilikuwa zinaishia pale pale, mtu anapatiwa fomu pale pale na Afisa

Uhamiaji wa Mkoa. Lakini sasa hivi jambo hili limebadilika, hawapati tena *passport* pale Pemba mpaka wavuke au Idara ya Uhamiaji mpaka ihame, makaratasi iyapeleke Unguja baadaye ndiyo mtu anaweza akaletewa *passport* jambo ambalo kwa kweli kama nilivyosema linasababisha usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kuliangalia hili ili usumbufu huu kwa wananchi uondoke.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuhusu hili la *passport*, nilisema kwamba Mwenyezi Mungu ametwambia tutembe. Mimi nadhani Serikali ingebadilisha hasa sera ya *passport* kwa sababu tumejifunza sisi kule kwetu. Vijana wengi kwa kweli waliojitahidi mpaka wakapata hizi *passport* wakatoka nje ya nchi wameondokana na umaskini. Wamekwenda kule wanafanyakazi, wanapata fedha nyingi na matokeo yake fedha hizo wanazisafirisha mpaka hapa kwetu, mwenyewe yupo Ulaya lakini hapa analeta fedha kwa jamaa zake kwa ajili ya kujengewa nyumba nzuri na anaikuta ipo tayari au jamaa zake wameshaanza kuishi wakati yeye mwenyewe bado akiwa uhamishoni. Kwa hiyo, nadhani mimi hili suala la kubinyabinya huu uhuru wa kuwapa watu *passport* pia linaweza kuwa moja kati ya sababu za kuimarisha umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu ajira hii ya Polisi. Jana ilizungumzwa hapa katika kambi mbalimbali za fikra. Wengine wakasema kwamba kusiwe na ubaguzi katika kuajiri Polisi, wengine wakasema kwamba nafasi hii wapewe zaidi wazalendo. Kusema ukweli hili neno uzalendo mimi linanipa mashaka kidogo kwa sababu sheria namba tano kama tofauti maana yake uzalendo msingi wake ni Chama. Sheria Na. 5 inasema kwamba: “Moja kati ya sharti la usajili wa Chama cha Siasa ni kwamba Chama chochote kile, mtu yeyote hawezi kuruhusiwa kuunda Chama kama si mzalendo.” Hakuna mtu yeyote wa nje aliyekuwa si Mtanzania halisi anayeweza kuruhusiwa kuunda Chama cha Siasa ndani ya nchi hii.

Kwa hiyo, mimi naamini kwamba Vyama vyote hivi ni vya Wazalendo. Sasa unaposema kwamba labda *CUF* au *CHADEMA* au nani asiingizwe katika Polisi kwa sababu yeye si mzalendo kwa kweli mimi lugha hii siifahamu. Kwa hiyo, mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri na nina hakika kwa jinsi ninavyomfahamu hili la kwamba wengine kwa sababu ya Vyama vyao tu siyo wazalendo hatokubaliana nalo na natumaini kwamba kuanzia sasa Waziri wa Jeshi la Polisi atawaingiza watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi nataka niseme kwamba ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwamba kule kwetu kuna manung'uniko ya hapa na pale kwamba hata hao ambao ni wazalendo basi pia inaonekana kuna wazalendo zaidi kutoka sehemu nyingine ndiyo wanaopata nafasi. Kama alivyosema ni kwamba kuna fununu kwamba maofisa fulani wa Polisi husafirisha jamaa zao kutoka sehemu mbalimbali wakawaleta kule kwa ajili ya kupata ajira na hali tunasikia kwamba ajira hii hutolewa kwa share, kila Mkoa unakuwa na share yake. Lakini cha ajabu ni kwamba ile *share* ya Mkoa wa Kusini kwa maneno yanayozungumzwa ni kwamba inachukuliwa si ajabu kusikia wamevuka watu kutoka Tanga, Dar es Salaam kuja kuchukua nafasi ile.

Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli alifuatilie hili na kama kweli lipo basi alikomeshe kwa sababu ubaguzi ni mbaya na ulitugharimu sana sisi Watanzania. Tulikuwa mstari wa mbele sana sisi kuhakikisha kwamba ubaguzi Kusini mwa Afrika na ulimwenguni kote tumeupiga vita. Sasa itakuwa ni watu wa ajabu sisi tulifanya kazi hiyo kwa gharama kubwa lakini badala yake tunaukaribisha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli na hili aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu hizi *speed governors*. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kweli suala la *speed governor* limefeli. Hivi karibuni mimi nilikuwa natoka safari toka Moshi kuja hapa. Gari nililokuwa nimepanda lilikuwa linakwenda kwa *speed* ya kilomita mia moja na hamsini na tano. Mbele yetu kulikuwa na basi la abiria tulijitahidi sana lakini hatukulipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gari tulilopanda sisi, lilikuwa linakwenda kwa *speed* ya kilomita 155, mbele yetu kuna basi la abiria lakini hatukulikuta kabisa. Sasa hiyo inaonyesha kwamba kwa kweli hizi *speed governors* imekuwa ni hadithi tu lakini hazifanyi kazi tena. Kwa hiyo, kama inaonekana kwamba hiki kweli ni chanzo cha ajali nyingi basi Serikali ione kwamba kwa hapo kwa kweli tumefeli.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasema kwamba ilizungumzwa jana hapa kwamba pengine baada ya uchaguzi wa mwaka 2000 sisi tukaonekana tumekuja wachache humu na nini, lakini nasema kwamba masuala hayo hatuna haja ya kuyazungumza sasa hivi, yapo katika siri ya Mwenyezi Mungu na zaidi ni kwamba wakati ukifika ndiyo utakaojibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. PONSANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze na kuishukuru Wizara hii kwa kuweza kukamilisha jengo la Polisi Kituo cha Wilaya ya Nkasi pale Namanyere, ingawa jengo hili limechukua muda mrefu tangu mwaka 1983, sasa linakamilika katika miaka ishirini iliyopita. Kwa hiyo, ninashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja mbalimbali nakumbuka alikuwa anajibu hoja ya Mheshimiwa Margareth Bwana, aliahidi kwamba watajitahidi kuleta *speed boat* katika Ziwa Tanganyika. Eneo letu ili kuweza kukabiliana na matukio mbalimbali ya ujambazi yanayofanyika katika eneo lile za Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kumkumbusha tena kwamba atusaidie kutuletea hiyo *speed boat*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kirefu kidogo ninaomba kuongelea suala la *Vote* ya Uhamiaji, kuna haja ya kuwa na vote ya Uhamiaji. Naomba mnisikilize vizuri na kwa kweli baadaye nitaliomba Bunge hili tuweze kutoa uamuzi kabisa. Uhamiaji haina vote, inatumia *Vote* namba 51 ambayo ni ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Nianze kusema kwa wakati huu haina *Vote* kwa sababu ya ubinafsi wa baadhi ya watendaji ambao wameng'ang'ania Uhamiaji isipewe *Vote*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe hoja kama ifutavyo:-

Kwa upande wa

SPIKA: Hutoi hoja wewe unatoa maelezo, hoja iliyopo mezani ni ya Waziri.
(*Makofi/Kicheko*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Nashukuru kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika, *Vote* namba 51 ina Idara kama tisa hivi ina Utawala, Fedha na Uhasibu, Sera na Mipango, Huduma za Jamii, Uhamiaji Zanzibar, Uhamiaji Bara, Zimamoto, Chuo cha Zimamoto na Wakimbizi. Ukitazama katika eneo hili ni nani ambaye anazalisha zaidi ni Idara ya Uhamiaji. Kwa mfano, wakati Utawala peke yake katika mwaka 2001/2002, walizalisha kiwango cha shilingi 50,000,000/= tu lakini Uhamiaji ilizalisha shilingi bilioni 6.813. Hadi kufikia Aprili, mwaka 2003 wakati utawala umezalisha shilingi milioni 84.9, Uhamiaji walikuwa wamekwishazalisha 5.289 bilioni na kwa hiyo, kwa wakati huu watakuwa wapo kwenye 6.0 bilioni. Malengo wanayotegemea kuzalisha mwaka 2003/2004 kwa upande wa Utawala ni shilingi 150 milioni wakati Uhamiaji inategemea kuzalisha shilingi bilioni 7.398.

Mheshimiwa Spika, ukitazama katika Idara zote zile nilizozitaja hadi kufikia mwezi Juni, 2003 kwa upande wa Wizara pamoja na Idara zile nyingine zilizobakia wamekuwa na shilingi bilioni 1.953. Wakati Uhamiaji wamekuwa na shilingi bilioni 8.976. Ukiwaomba kwamba watoe *vote* na hili limeanza muda mrefu Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge imekuwa ikipendekeza kwa muda mrefu, lakini uongozi unaohusika wa Wizara ya Mambo ya Ndani hasa watendaji wakuu wamekuwa wakikataa pamoja na Wizara ya Utumishi ambayo nitaelezea hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki ambapo wameomba fedha wanategemea pia pengine kuzalisha kiasi gani pamoja na fedha ya Serikali watakuwa wamepewa kwa ujumla wake, wanatazamia kwamba *vote* hii itakuwa ni bilioni 9.668. Lakini katika hizo bilioni 6.842 ni za Uhamiaji na Wizara pamoja na Idara nyingine zile zote zilizobakia saba jumla yake ni bilioni 2.825. Wingi huu unatosha kabisa kwa Idara ya Uhamiaji kupewa *vote* yake kamili ili waweze kutumia fedha hizo kikamilifu badala ya Wizara kunyofonyofoa mafungu kutoka katika subvote za Uhamiaji na kuvuruga mipango ambayo ingeweza kufanywa na Idara ya Uhamiaji kwa manufaa ya umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nasema ni muhimu Uhamiaji wakapewa *vote* yao kwa sababu nimelishughulikia suala hili mimi mwenyewe na baadhi ya Wabunge na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa muda mrefu bila mafanikio kwa ukaidi wa viongozi watendaji wakuu wa Wizara hizo na Mawaziri wao wanawatazama tu sijui wanawaogopa. Wanasema aah hawa hawawezi wakapewa *vote* kwa sababu kwanza ni wachache, fedha zao pia chache, mara *Accounting Officer* sijui amefanya nini

Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa uthibitisho kidogo wa baadhi ya taasisi ambazo zimepewa *vote* zao lakini fedha ni ndogo sana kuliko zile za Uhamiaji na pia mtandao wao ni mdogo sana kwa sababu wanakuwa na *vote* moja na *subvote* moja tu.

Kwa mfano, moja hii ilitajwa jana sina haja ya kuirudia, nije katika *vote* kwa mfano Na.33 ya *Ethics Secretariat* hawa hawazalishi chochote na fedha yao wanayoipata mara nyingi haizidi mia tano milioni. *Vote Na.36 Civil Service Commission* hawa hawazalishi chochote na wana *Subvote* moja tu lakini fedha yao wanayopata haizidi shilingi mia sita milioni. *Vote Na.45 Exchequer and Audit Department*, wana *vote* hiyo na *subvote* moja ambayo ni ya utawala lakini fedha yao wanayoipata haizidi shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, ipo *vote* Na.55, nazidi kutoa uthibitisho ili muone kwa nini *Immigration* wasipate *vote* yao. *Vote Na.55 Commission of Human Rights and Good Governance*. Hawa pia hawazalishi chochote lakini fedha yao wanayopata haizidi shilingi bilioni mbili. *Vote Na.59 Law Reform Commission* hawa hawazalishi chochote wana *vote* na *subvote* moja tu ya utawala, fedha yao wanayoipata haizidi shilingi mia nne milioni. *Vote Na. 63 Local Government Service Commission* hawazalishi chochote na wana *subvote* moja, fedha yao wanayoipata haizidi shilingi mia sita milioni lakini wana *vote*. Halafu kuna *Vote Na.67 Teachers Service Commission* hawazalishi chochote fedha yao haizidi shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, ya mwisho *Vote Na.90 Land Court* hawazalishi chochote lakini nao wanayo *vote* yao na *subvote* ni moja hawapati zaidi ya shilingi milioni 400 na kuna *Vote 91 Anti-Drug Commission* na yenyewe nayo hivyo hivyo. Hawataki kupewa *vote* kwa sababu ya ubinafsi nimesema wakati ambapo imefikia mahali Wizara ya Mambo ya Ndani wakasema wapate *vote* Makatibu wanaohusika wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Utumishi wanagoma kwamba hawawezi wakapewa na wanasababu za ubinafsi ambazo sina haja ya kuzitaja hapa lakini kwa vile nakusudia kutumia kanuni Na. 38(A)3(b) nafikiri kinatimiza haja nitakuwa nimewasiliana na wahusika kabla ya kujadili matumizi ya Wizara ya Utumishi, nategemea kuzuia kwanza suala hili muhimu lijadiliwe nje ili kusudi *vote* hii iweze kupatikana kwa njia ya dharura. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wakipata *vote* yao, kwa sasa hivi itawasaidia kwa sababu utakuta wanasema wanatengeneza mambo ya *passport*, hati za uingiaji na utokaji, nyaraka nyingine wanazotengeneza zao na nyingine za Wizara, utunzaji kadhaa wa nyakara, wanahitaji masomo ya ndani na nje ya nchi, vitambulisho vya uraia tunavyopigia kelele, upelelezi na uendeshaji wa kesi Mahakamani, mitambo mbalimbali, ujenzi wa majengo mbalimbali vyote vinawahusu lakini *vote* hawana wanategemea kwenda kubembeleza kwa mtu ambaye naye anaamua kuitoa anavyotaka au kunyofoa. Nina ushahidi wa baadhi ya Makatibu waliopita pale wakaiba fedha kutoka *subvote* za Uhamiaji, bahati nzuri nililalamika hapa waliondolewa haraka sana na sielewi sasa hivi wako wapi hawako kwenye Ukatibu tena huu

Mheshimiwa Spika, kila siku hapa tunalalamikia kuhusu vitambulisho, vitambulisho vinahitaji mtu ujue mambo ya uraia yakoje na Waheshimiwa wengi hapa

hasa mfano wa Pemba kuhusiana na upatikanaji wa *passport* inavyokuwa ngumu. Moja ya sababu ni kutokuwa na vitambulisho vya Kitaifa. Kwa sababu katika kupata *passport* ni lazima apate mtu ambaye ni raia wa Tanzania. Mimi nimeishi Pemba karibu mwaka mmoja na miezi kama nane maeneo ya kule Wambaa, Makombeni, Kangagani, Olekiyuyu, Mtambile na kadhalika nilikuwa kwenye shughuli za umma, unamkuta mtu mweusi mwenye pua kama ya kwangu hii hapa ya mviringo, anasema mimi Mwarabu yakhe.

Sasa wewe Mwarabu kwa vipi? Anakwambia wewe usijali bwana mimi Mwarabu. Kwa hiyo, suala la uraia hapa linatakiwa kwa undani na kwa kweli kitu pekee kinachoweza kutofautisha hapo ni kitambulisho cha uraia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kitambulisho cha uraia ni haki yetu, ni usalama wa Taifa letu, ni uzalendo wetu. Leo hii unakuta Idara ya Uhamiaji ina kazi kubwa sana ya kuweza kuwatambua Watanzania waliomo ndani ya utumishi na nje ya utumishi nani ni raia wa kweli wa Tanzania. Ugumu unakuja ni kwamba hatuna vitambulisho. Nchi hii itakuja kuchukuliwa kinyemela.

Hivi nyie hamuoni tunavyosumbuliwa? Wanaokuja kuuu hata askari Polisi wetu wa usalama ni watu wanaotoka nje ya nchi na hili ni tatizo. Kuna viongozi wengine wanafanyakazi hata kwenye mambo ya utumishi nyeti kule na wameingia hata kwenye ofisi zetu kuu za usalama kule si raia wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *vote* ya Uhamiaji ikishapatikana wakii-*control* wenyewe kazi hii itafanyika vizuri. Mheshimiwa Waziri naomba nipate maelezo ya kina, vinginevyo wakati ule tutakapokuwa tumekaa kwenye Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima, mimi nitaondoa shilingi kwenye Bajeti yako, sitakubaliana kama sitapata maelezo sahihi. Lakini vile vile kama sitapata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kwamba *Vote* itapatikana kipindi hiki. Nategemea kabla ya kusoma maombi yake ya kuomba fungu lake la fedha nitaizuia kwa muda.

Mheshimiwa Spika, siuingi mkono hii mpaka nitakapopata maelezo. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Ponsiano Nyami, usiweke matumaini ambayo hayana msingi. Kanuni namba 38 haihusiki kabisa na jambo hilo unalolizungumzia. Kwa hiyo, hutaruhusiwa kuzuia kwa mujibu wa Kanuni hiyo. Masharti ya Kanuni namba 38, yako kwenye 38(a)(3).

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi niuangane na wenzangu kumpongeza kabisa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake.

Pili vilevile napenda niwapongeze Wataalam kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kutayarisha hotuba hii nzuri sana ambayo kwa kusema kweli imelenga kuondoa matatizo ambayo yalikuwa yanaisumbua sana Wizara hii. Natanguliza kabisa kuunga mkono hoja

hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba kuna fedha ambazo zimeongezewa katika hii Wizara safari hii. Ninaamini kabisa wakizitumia vizuri wanaweza wakatatua matatizo makubwa ambayo yalikuwa yanaikabili Wizara hii kwa kiwango kikubwa na hasa upungufu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, mimi nazungumzia askari Polisi ambao wako Wilayani ndiyo kioo changu, mimi naweza kuzungumza nao. Pale Wilayani nina hakika kabisa vyombo vyao wana *Radio Call* moja ambayo wanatumia kuwasiliana na Makao Makuu.

Kwa hiyo, ni vizuri kwa sababu miji yetu imekuwa mikubwa kidogo wanapofanya doria wawe wanawasiliana na ofisini. Siku hizi kama watu wakifanya kazi bila mawasiliano kuna matatizo makubwa ambayo yanaweza yakawakabili.

Ningeomba kabisa kuna hizi *Radio Call* ndogo kabisa wanavyotembea navyo barabarani, mimi sioni kabisa sababu ya kutowapa askari Polisi wanapofanya doria katika Mji mimi sioni sababu. Kama tunazo hizi *Radio Call* za mikononi kwa nini wanapotembea wasipewe, kuna mitaa yangu kabisa ya Ngaranaror, Kaloleni, askari Polisi akikabwa kule hana mawasiliano na kituoni. Kwa hiyo, naomba kabisa kama tumeongezewa asilimia 30 basi pale Wilayani angalau hata wanaofanya doria wawe na mawasiliano. Sasa hivi tuna matatizo makubwa na kwa haya mambo lazima twende na wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *uniform*, mimi tangu sasa nadhani mmeshabadilisha sijui mara mbili. Suala la kuwa mtanashati vilevile hizi *uniform* za askari Polisi hazijanivutia mimi kwa kwa kusema kweli na mimi ni askari vilevile. Lakini kuna haja ya kuangalia tena *uniform* zinakwenda na wakati ama haziende na wakati.

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa naangalia kwenye *Television* askari wengine wanavyovaa wana vikorobwezo vingi sana na jinsi wanavyotembea namna hiyo wana virungu na wana mikoba midogo. Sisi kwetu askari Polisi wanapoondoka, wanaondoka na kirungu kidogo hivi, hivi kuna tatizo gani ya kumpa hata silaha na mguu wa kuku aweke kwenye mkoba anapoenda kufanya doria, kwa nini tuna wasiwasi nao.

Mheshimiwa Spika, sasa askari Polisi anapokuwa na vitendea kazi hata ukimwita ana vitu vya kukusaidia. Sasa askari Polisi wa hapa hana kitu chohote na wewe huna kitu chochote, sasa ukimwita askari Polisi anaanza kumkimbua adui sasa ni matatizo gani. Tuwape askari Polisi wetu vifaa ambavyo vinaweza kabisa kumsaidia ili aonekane ana vitendea kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi katika Wilaya yangu ya Kiteto kwanza nitoe shukrani nyingi sana kwa Wizara hii. Nitoe shukrani nyingi sana kabisa kwa kazi nzuri ambayo

wametufanyia kwa sababu wametujengea nyumba za askari Polisi nzuri sana na *modern* katika nchi hii, tunawashukuru sana. Lakini bado suala la umeme wanauweka taratibu. Sasa tatizo ambalo tunalo sasa hivi tunapambana ni kutafuta mahali ambapo askari Polisi wanaweza wakakaa wakapumzika. Hili suala la kupuuzia mambo ya askari Polisi nao lazima wawe na kantini yao wanapomaliza kazi wanapumzika. Sasa askari Polisi anapomaliza kazi anakwenda mitaani kule basi ndiyo anakwenda kutobolewa jicho na kupata matatizo haya.

Nashauri kuwepo na mahali pa faragha katika sehemu hiyo ambayo tumeitengeneza tunataka askari Polisi wetu wafanyiwe kama Wanajeshi kuna *Seniors Officer Messy* na kadhalika wawe na mahali pa kupumzika, na hii ni *ethic* ya askari polisi ni lazima tuanze kufanya hivyo. Kwa hiyo, naomba sana hilo tuliangalie katika masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, tumejengewa Kituo cha Polisi kizuri sana nashukuru sana, juzi wametuletea milioni 3 hiyo ni ndogo sana nawashukuru. Tunaomba mtuongeze, tumetengeneza Kituo cha Polisi kizuri na tunakimaliza na tunakifungua. Ila wasiwasi wangu vifaa vitakavyoingia pale. Meza ya *OCD* ukiingiza katika lile jengo ni kichekesho.

Kwa hiyo, tunapojenga Kituo cha Polisi vifaa vinavyoingia mle vifanane na jengo lile. Ukienda pale Kituoni ukiangalia vifaa vinavyotumika pale unafikiri kabisa ni meza imeokotwa kule mitaani. Ofisi ya *OCD* anajaribu kuweka vitambaa vyeupe, lakini ukifunua hiyo meza ni hatari.

Kwa hiyo, naomba sana meza ya *OCD* ifanane kabisa na majengo ambayo tunayajenga. Kwa hiyo, katika fedha hizo ambazo mmeongezewa muimarisha hivyo vitendea kazi. Kuhusu viti kama unavyoenda Mahakamani ukiangalia kiti cha Mahakama au ukikaribishwa ukakae kwenye kitini pale basi unaona kiti kinalegea tu namna hiyo yaani ni matatizo. Viti vyao lazima viwe na hadhi. Tunaomba tumaliziwe kujengewa Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru watu wa Magereza kwa kumaliza Gereza la Mahabusu la Kiteto nawashukuru sana. Tulikuwa tunapata matatizo ya kupeleka wafungwa kutoka Kiteto mpaka Kondo. Sasa katika hilo wakati wa masika tulikuwa na matatizo ya kwenda kuwachukua hakuna fungu la fedha. Lakini tumeishamaliza kujenga gereza kwa ajili ya wafungwa pale tunaomba mfungue hilo gereza. Maana tumemaliza kujenga gereza na liko tayari sijui kwa nini tena mnatupa tena tabu toeni amri gereza lifunguliwe kusudi lifanye kazi. Kwa hiyo, kazi nawapongeza sana na tunawashukuru sana kwa kumaliza kujenga hilo gereza.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika suala lingine inaelekea niwe nasifu tu kwa kazi nzuri mliyoifanya. Sijawahi kufanya hivyo tangu niingie Ubunge kusifu tu yaani ni Wizara ya kipekee kabisa labda nije katika matatizo kuhusu msongamano wa wafungwa, tafadhalini sana suala hili linatuletea aibu. Wafungwa wanasongamana sana na kuna matatizo makubwa ambayo yanawafanya hivyo.

Kwanza ile Kamati ya kuchunguza iko wapi, bado haijafanya kazi sawasawa. La pili, kuna watu ambao wanafungwa bila sababu yoyote ni mahabusu tu. Mimi Kiteto kuna watu ambao wamepelekwa Kondo wa askari Polisi sasa hawana haja ya kwenda kuwaangalia kama wamepelekwa Kondo au hawajapelekwa. Mtu anakaa miaka miwili, mitatu, bila kesi yake kusikilizwa.

Kwa hiyo, haya matatizo yapo katika pande zote katika Mahakama na upande wa Jeshi la Polisi tunaomba sana, na sasa linafanya hakuna kabisa *discipline* ya Magereza kwa sababu ya msongamano mkubwa. Kama mtu hakuna haja ya kufungwa si aachiwe huru. Pia katika huu msongamano ambao ni wa mateso, mtu kabla hajafungwa anabanwa namna hiyo, hiyo si kifungo tayari. Mtu halali usingizi anabanwa, ameteswa na hukumu bado, kwa nini hamhesabu huo msongamano wa namna hiyo kama ni kifungo. Kama wafungwa wamekuwa wengi zaidi katika magereza, wale waliozidi kwa nini wasipunguziwe adhabu kwa kupunguza msongamano. Mimi naomba hilo mlichukulie kabisa kwamba ni kukiuka haki za binadamu, watu mnawatesa bila sababu yoyote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu vitambulisho. Naomba sana katika suala la vitambulisho na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, amelizungumzia sana tangu nimeingia katika Bunge ni suala la vitambulisho linazungumziwa. Sasa tumefikia mahali ambapo tunahitaji vitambulisho. Kama kweli sababu ni vote ya Uhamiaji ndiyo inanyimwa vitambulisho hiyo vote itolewe haraka na vitambulisho vitoke, kama ni suala la vote au kama ni suala la ubinafsi la mzabuni huyo ambaye mmepatana naye tafuteni. Mimi nasema sasa imefika wakati wa kutoa hivyo vitambulisho. Tulikuwa tunadanganyana tunafanya hivi na nini sasa hakuna na hatufahamiana sasa, kwa hiyo kama hatufahamiana tunauana sasa bila kufahamiana. Kwa hiyo nawaombeni mtoe hivyo vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, juzi wameuawa askari Polisi mnaanza kuhangaika, kila siku sisi tunauawa uraiani. Lakini nyie mlipoguswa juzi, nyie mkakasirika wakati kila siku sisi uraiani tunakufa. Kwa hiyo, sasa tunahitaji vitambulisho kusema kweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la *OCD* mimi sina gari katika Wilaya ya Simanjiro na Wilaya Kiteto tunaomba gari. Wilaya hii ni kubwa sana ina vituko kila siku kwenye redio watu wanapambana na wahalifu, *OCD* wangu hawana gari. Kuna watu ambao wamekaa kabisa katika Wilaya ambayo haina gari basi hakuna usalama.

Kwa hiyo, tunaomba gari, kuna gari bovu la zamani tunashukuru sana kama inawezekana mtutengenezee hilo gari ili mtupatie kwa haraka sana na Manyara mmeshatenga sehemu ya Makao Makuu ya Mkoa ya muda tunawashukuru mmeweka katika vote mtuharakishe katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu semina. Wakubwa mnafanya semina, wadogo hawafanyiwa semina. Kila siku sisi tunawaona *Sea View, White Sand* wakubwa mnafanya semina hawa wadogo kwa nini hamuwafanyi semina Wilayani kule.

Hivi kuna kazi askari Polisi anakaa miaka 6 mpaka miaka 7 hakuna kupata semina. Mimi Wilayani kwangu sijaona askari Polisi anasema leo wana semina. Lakini kule juu semina zinafanyika, kwa nini askari Polisi wadogo hamuwafanyii semina huku chini kuna tatizo gani. Ni ninyi tu wakubwa ndiyo mnataka elimu, lakini askari Polisi wa chini ni kuamriwa tu wewe funga mkanda kwenda, hata siku moja humuelekezi mambo. Kwa hiyo, hicho kibao sasa kigeuke semina zifanyike kwa askari Polisi wa chini waelimishwe wajue mbinu zote. Tangu wengine wamalize Chuo hawajakaa tena darasani kwenye semina, ni asubuhi tu kwata, kaa hapa, nenda kule, kaa hapa nenda kule. Sasa safari hii inabidi muwafanyie semina askari Polisi wa chini halafu muwaelekeze mbinu na maadili ya kazi zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya na natangulia kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Omar Ramadhan Mapuri, ni mchapakazi, nawaomba Makamanda washirikiane naye katika kutekeleza majukumu yao waliyonayo.

Moja, katika kazi muhimu sana ya vyombo vya ulinzi wa nchi yetu ni kuendeleza amani na utulivu tulionao na kazi hii ili ifanyike tunahitaji kuwa na Jeshi la Polisi ambalo lina uwezo, ujuzi na maarifa na vifaa vya kufanyia kazi. Lakini vifaa vya kufanyia kazi peke yake havisaidii sana kuliko kujenga human intelligence na hii inafanyika wakati wa kuajiri askari Polisi na pia inafanyika kwa kuwa na Chuo chenye watu wenye taaluma nzuri ya kufundisha.

Kwa hiyo, moja ninaloliomba kwa Wizara pamoja na kujitahidi kupata vifaa na kutafuta vifaa *human intelligence* ni kitu cha msingi sana. *Pentagon* isingepigwa, *World Trade Center* isingepigwa kama ni suala la vifaa. Lakini human intelligence inazidi vifaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana kufanya hiyo kazi ya kupata askari Polisi wenye ujuzi kwa maana ya uwezo wa kiafya, elimu na *power* ya *ku-think*. Wakifanya hivyo yatafikiwa yale malengo yanayokusudiwa kuhudumiwa raia. Raia anatakiwa alindwe yeye na mali yake na raia anayefanya kosa anatakiwa afikishwe Mahakamani.

Sasa ili raia afikishwe Mahakamani lazima askari Polisi awe na uwezo wa kumkamata mtu kabla hajafanya tendo, awe ana nia tu ya kutaka kufanya kosa basi aweze kudhibitiwa. Kwa mfano, jambazi amekaa mahali ana silaha anataka kwenda kufanya ujambazi, basi kuwe na uwezo wa kumdhhibiti kabla hajafanya lile tendo madhali mmeishapata ushahidi kwamba anayo silaha. Hiyo ni hatua muhimu sana.

Ikishindikana hapo basi azuiwe asiwahi kufanya lile tendo yaani amefika mahali anataka kufanya tendo lakini asiwezi kufanya lile tendo. Hiyo ni hatua ya pili. Hatua ya tatu, awe amefanya tendo lakini amekamatwa na afikishe Mahakamani na ikishindikana kabisa inaingia hatua ya nne, inabidi wapambane baina ya wahalifu na askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu ya hii skilled kupungua, linalotokea zaidi sasa hivi ni mapambano baina ya wahalifu na askari Polisi na hatimaye wahalifu kutokufikishwa Mahakamani.

Sasa mimi nawaomba sana askari Polisi suala la kutumia nguvu za ziada linaruhusiwa katika sheria, lakini kwa mazingira maalum. Sasa imekuwa ni tradition lile lengo la kumfikisha mtu Mahakamani limekuwa linapungua siku baada ya siku, na hii si hali nzuri katika Jeshi la Polisi.

Kwa hiyo, nawaomba sana askari Polisi, naelewa sana mazingira mnayofanyia kazi na naelewa mnapolazimika kutumia nguvu. Lakini raia aliyekosa asipofikishwa Mahakamani bado kazi hiyo haijakuwa nzuri. Raia wanaposikia jambazi ameuawa basi hiyo hatua bado siyo nzuri, *professionalism* bado haijafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana hili litazamwe namna gani watapata askari Polisi wenye *skills* za kuweza kudhibiti uhalifu kabla haujatendeka au utakapotendeka basi mhusika aweze kufikishwa Mahakamani badala ya kuuliwa au kuumizwa, ya kuuliwa na kuumizwa iwe ni hatua ya mwisho kabisa iwe hakuna budi, kwa sababu sheria inasema mtu afikishwe Mahakamani ili apatikane na hatia. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, ni suala la msongamano wa mahabusu na kuwa na kesi nyingi. Tumeruhusu Makampuni binafasi sasa hivi hapa kufanya kazi ya ulinzi yapo mengi tu, kuna *Group Four* na kadhalika.

Naishauri Serikali, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba wakae waruhusu *private investigation*, tumeingia katika utandawazi askari Polisi ni wachache. Wakati mwingine raia haridhiki na utaratibu wa askari Polisi anavyofanya upelelezi, awe na uhuru wa kwenda mahali pengine kutafuta *private investigator* amfanyie kazi yake na aweze kuwa *prosecuted*. Itatusaidia kupunguza lawama na itatusaidia kutumia *resources* zetu vizuri na itakusaidieni kupunguza msongamano wa kesi ambazo tunao hivi sasa. Kwa hiyo, *private investigation* ifanyiike. (*Makofi*)

Tatu, hivi sasa *Prosecutors* wako chini ya *CID*, lakini wakati huo huo wako chini ya *DPP*. Anayepeleleza ni askari, anaye *Prosecute* ni askari chini ya Ofisi moja ya *RPC* na *DCI* inakuwa ni vigumu kupata haki. Kazi ya ku-*prosecute* ni kazi ya *DPP* naiomba sana Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Utumishi wahamisha kazi ya *Prosecution* iende chini ya *DPP*, waachiwe askari Polisi wafanye upelelezi, wakimaliza kufanya upelelezi wampelekea faili *DPP* na awe na ma-*prosecutors* kutoka juu mpaka chini.

Hivi sasa *DPP* anashughulikia Mahakama Kuu tu, huku chini kote amewaachia askari Polisi wanafanya kazi hiyo. Sasa achukue hawa askari Polisi ambao ni *Prosecutors trained* tayari wawe chini ya *DPP* moja kwa moja, ili kuwe na mkondo wa upelelezi mbali na upande wa *Prosecution* mbali na ili raia aweza kupata haki yake na hiyo itawapunguzia mzigo ninyi askari Polisi hivi sasa ya kuwa na mafaili na kesi nyingi ambazo hamwezi kuzi-attend.

Nne, kulikuwa na utaratibu wa *Case Management Flow System*, nafikiri bado unaendelea. Ningeomba Mheshimiwa Waziri ukazanie sana. Hali ya magereza ni hali mbaya sana, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri siku moja alinitania akaniambia kila mwanasiasa ni mteja wa kuwa gerezani. Kuna mwanasiasa mmoja alipelekewa mapendekezo ya kufanya ukarabati katika shule na kwenye gereza. Alichofanya aliharakisha sana kufanya ukarabati wa gereza. Alipoulizwa akasema kwa sababu wakati wowote naweza kwenda gerezani na kweli alikwenda gerezani. Lakini akapelekwa kwenye gereza ambalo alilifanyia ukarabati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la wanaraia kubandikizwa kesi, na nitatoa mfano halisi. Wakati tuko kwenye kesi ya uhaini Zanzibar, kuna kijana mmoja alikuwa anatafutwa anaitwa Said Zam ni mwanachama wetu wa Chama cha *CUF*. Askari Polisi walipokuwa hawajampata wakamkuta kaka yake anaitwa Abbas Zam, kwa hiyo, wakamchukua Abbas Zam, ili wampate Said Zam. Said Zam alipofika nyumbani akapata habari kwamba kaka yake amekamatwa akaende Kituo cha Polisi, akasema mimi ndiyo Said Zam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana Abbas Zam alitegemea kuachiwa, askari Polisi anasema aah na yeye muweke tu huku, tumekaa naye jela miaka 3 *innocent person*. Kuna mama mmoja anaitwa Zena hana uhusiano na siasa kabisa alikuwa ameletewa nguo na ndugu yake akaambiwa ameleta nguo za Jeshi, akahusishwa yeye na Mheshimiwa Juma Duni Haji, wakati walikuwa hawajuani kabisa. Mama huyo mpaka amepata *pressure* miaka mitatu jela pamoja na sisi *innocent* kabisa na tumezikuta hizo kesi gerezani ni nyingi sana za watu kubandikizwa kesi.

Nawaomba sana askari Polisi najua mnafanyakazi katika mazingira magumu sana, lakini kumbandikiza mtu kesi ukamweka gerezani bila ya hatia ni dhambi kubwa sana. Tuache utaratibu wa kuwabandikiza watu kesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tano, mwaka 1982 nilikwenda kufungua mkutano wa Jeshi la Polisi Moshi, wakati ule nchi yetu ilikuwa imefunga mpaka na Kenya, basi kulikuwa na manung'uniko kwamba askari Polisi wanapokea pokea rushwa kuwaruhusu watu kuvuka mpaka. Nikawaambia askari Polisi pale nasikia kuna habari hizi nielezeni mimi msemaji wenu Mkuu niwasaidie kama kweli ni tatizo hilo. Askari wakaniambia umekuja hapa wewe mtoto mdogo, ukatutukana na nini hata hotuba yako hatutaki kuijadili, basi tukagongana pale.

Baadaye mimi nikawambia basi mkimaliza mkutano basi tuje tuonane tena. Nikarudi mkutanoni siku ya pili, nikawambia askari Polisi. Baba yangu ameniambia

hivi, ukiitwa mchawi na wewe siyo mchawi huna sababu ya kuhangaika. Pili, nikawambia ningechukua miezi 6 kulisoma Jeshi la Polisi, lakini nimechukua siku mbili nimelisoma Jeshi la Polisi. Ahsante sana, kwa herini, nikaondoka.

Mheshimiwa Spika, tulipofika Dar es Salaam, siku ya pili Mwalimu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa anasafiri, *Airport* pale akasema Hamad njoo, *IGP* njoo tukakaa pembeni ya ndege. Akasema hivi: “Kule Uingereza Serikali na Malkia wanaliheshimu sana Jeshi la Polisi, lakini na Jeshi la Polisi na lenyewe linajiheshimu sana. Maana ni kioo cha nchi, ukitokea tu nje mtu wa kwanza kumwona ni askari Polisi kwa hiyo ni kioo, na ndiyo maana kioo hiki kila wakati kinatakiwa kiwe safi, kikiwa na vumbi kinatakiwa kisafishwe, kikipasuka kinatakiwa kiondolewe endelea na juhudi ya kuondoa vumbi, ukishindwa kikipasuka tutakiondoa.”

Mheshimiwa Spika, wewe ni kioo chetu hapa na mimi nakuhusudu sana kila wakati ukiona kuna vumbi linakuja wewe mwenyewe unafanya juhudi ya kuliondoa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kioo chetu hapa, Waziri Kiongozi wa Upinzani ni kioo chetu, vioo hivi vikipata vumbi vinahitaji kusafishwa haraka. Lakini vikipasuka lazima viondolewe na ndiyo maana Kiongozi wetu sisi hapa wa Upinzani alipopata upasuko tukamuondoa. Nafikiri kioo chetu kimoja kimepata upasuko ndani ya Bunge hili na ndani ya Taifa letu kinahitaji kuangaliwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tumepata habari anachunguzwa na Tume ya Rushwa ni mpasuko mkubwa na kwa *image* ya nchi yetu na kwa *image* ya Serikali yetu tunahitaji Wabunge kupata taarifa rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi sisi tumekubali kuingia kwenye *International Criminal Courts* kwa madhumuni ya kwamba kama raia wanafanya makosa basi wapelekwe kwenye Mahakama hiyo. Lakini hivi sasa nchi ambazo hazitaki kuwa wanachama wa *International Criminal Courts* tunawachukulia raia wetu kuwapelekea wao kuwahukumu, wakati wao wanakataa raia wao wasiende kwenye Mahakama hizo.

Namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie orodha ya Watanzania ambao wanapelekwa nje kwenda kuhukumiwa hasa kutokana na hii sheria ya Ugaidi au wageni ambao tumewapa *resident permit* hapa tukawambia wakae hapa wafanye shughuli zao. Lakini baadaye wakaondolewa wakapelekwa kwenye hizo nchi zinazohusika, pia Mheshimiwa Waziri atupe taarifa. Kwa sababu zifuatazo kwanza ni haki ya raia kupata taarifa, katika *Detention Act* tuliyoipitisha katika Bunge hili tulisema kwamba katika kipindi cha siku 14 mtu lazima ajulishwe kwa nini anawekwa ndani.

Mheshimiwa Spika, leo watu wanachukuliwa wanapelekwa nje ya nchi raia hawana habari, ndugu zao hawana habari, hii si sahihi. Tunaomba kabisa Mahakama zetu ziheshimiwe tuwahukumu watu ndani ya nchi yetu, suala la kuwapeleka watu katika nchi nyingine kwenda kuhukumiwa tunadhaliisha Mahakama zetu. Tumezipitisha wenyewe tumeviweka wenyewe vyombo hivi. Hii namwomba kabisa Mheshimiwa

Waziri atusaidie. Mwisho kabisa namwambia rafiki yangu kwamba uraia sio pua, uraia ni Katiba na Sheria inavyosema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ambayo ndiyo hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri, Naibu Waziri, kaka yangu, Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu Bwana Mchomvu, IGP Bwana Omar Mahita, Makamishna wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii pamoja na watendaji wote. Kwa kweli Bajeti hii ni nzuri. Ni nzuri kwa sababu ina uchambuzi wa kina. Imetoa picha kamili ya jinsi gani walivyojitahidi kuitekeleza Bajeti ya mwaka jana na bado imetuonyesha mikakati ya utekelezaji wa Bajeti ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaongea tu kwa kuwa Wabunge lazima tuzungumze, lakini wenzetu wamefanya kazi nzuri. Nitumie pia nafasi hii kuwapongeza Makamanda wa Mkoa. Mwaka 2002 nimewapongeza Kamanda wa Mkoa wa Singida na Kamanda wa Mkoa wa Dodoma. Safari hii naongeza idadi Makamanda wengi wamejitahidi kiasi kikubwa. Wenzangu wametaja Kamanda wa Mkoa wa Dar es Salaam na mimi naunga mkono. Bwana Alfred Tibaigana, amejitahidi kiasi kikubwa sana. Kamanda wa Mkoa wa Kilimanjaro naunga mkono amefanya kazi nzuri sana. Kamanda wa Mkoa wa Tabora kazi yake ni nzuri tunaiona na tunaisikia, Kamanda wa Mkoa wa Kagera simuachi tunamsikia anavyojituma. Hata Kamanda wa Mkoa wa Kigoma anajitahidi kwa kweli. Kazi yote hiyo nadhani ni mfano wa Singida na Dodoma maana ndiyo walikuwa waanzilishi wa kuchemka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii pia niipongeze Serikali. Mwaka 2002 Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja mbalimbali hapa wakasema ni bora basi hawa Makamanda wetu wakapewa semina. Kati ya Waheshimiwa Wabunge waliotoa mchango huo ni pamoja na mimi. Tunashukuru Serikali ilitusikia semina hizo zimefanyika kwa Makamanda wetu wa Mikoa pamoja na Makamanda wa Upelelezi wa Mikoa nadhani ndiyo sababu hata idadi ya Makamanda waliofanya kazi vizuri imeongezeka. Ni matunda ya semina hizo. Semina hizo zimewasaidia kubadilishana uzoefu. Nafasi hizi za uongozi zinatakiwa pia kubadilisha mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu tuliomba pia hawa Makamanda wapewe safari za nje Waswahili wanasema: “Tembea uone.” Na hilo limetekelezwa. Limetekelezwa na limekuwa changamoto kwa Makamanda wetu. Ndiyo maana wameongeza bidii katika utendaji wao. Waswahili wanasema: “Mcheza kwao hutunzwa.” Hiyo ni zawadi vile vile ni changamoto kwa watendaji wetu. Unajua wanapotoka nje kidogo angalau unatakasa macho macho. Sio kutakasa macho tu wanajifunza. Wewe umezaliwa Shelui, ukakulia Shelui ukajiona wewe katika ule Mji wa Shelui wewe ndio unajua kuvaa kuliko wenzako

wote hujafika hata Singida Mjini hivi siku ukifika ndio utaonekana kwamba unajua kuvaa. Hata Kibaigwa hujafika ndio utaonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli suala la watendaji wetu hawa Makamanda wetu na Ma-RCO wetu kwenda nje kujifunza imekuwa ni changamoto kubwa. Hata Waheshimiwa Wabunge wenzangu walisema hapa. Mimi nadhani sasa kuna haja ya zoezi hilo likaendelea hata kwa maafisa wa ngazi za chini. Kwa sababu utendaji huu unategemeana. Wote wa ngazi za juu wakategemeana na hawa wa chini matunda yake ndipo yanapokuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuishukuru Serikali kwa kuuteua Mkoa wa Singida kuwa mwenyeji wa Sherehe ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Kitaifa mwaka huu. Mimi ni imani yangu kwamba hii tumepewa kama tuzo kwa sababu ni kweli Kamanda wetu na vijana wake wanafanya kazi. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika, pamoja na Bunge lako Tukufu zoezi kwa Mkoa wa Singida linafanywa kikamilifu kwa sababu wameanza kufanya kwa vitendo, sasa miezi mitano. Wanatoa elimu kwa wananchi, matumizi ya alama barabarani, wanatoa elimu mashuleni, Shule za Msingi na Sekondari, wanatoa semina kwa madreva wetu mimi nadhani kuna haja ya Serikali kuona umuhimu basi kuwapeleka Makamanda wengine wa mikoa mingine kwenda Singida wakajifunze. Kazi inayofanyika si ndogo kule. Wanachemka kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, yule bwana afande *RPC* ni mdogo mdogo tu mwili wake ni mdogo mdogo tu, lakini kazi zake kwa kweli ni mkali anachemka kweli kweli. Kwa sababu pamoja na kugawa madaraka lakini yule bwana huwa hatosheki. Huwa inabidi na yeye aende nyuma kwa nyuma kuangalia je haya malindo niliyogawa yanakwenda sawa na ndiyo utendaji. Huwezi ukagawa kazi ukabakia Ofisini lazima na wewe utoke hujiridhishe. Je, haya niliyoyagawa yanakwenda sawa. Wewe utakaa Ofisini tu si utashangaa jambazi limekufikia Ofisini. Toka uone vijana wako wanafanya kazi kiasi gani na lazima ushirikiano nao. Nimeamini Kiongozi yeyote anayewatenga vijana wake, utendaji wao kazi yake huwa ni ngumu. Kwa sababu Umoja ni Nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza hayo basi, sasa nianze kuzungumzia mapungufu ambayo yapo ndani ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Kwanza naanza na askari, askari ni wachache. Unakuta lindo moja lina askari mmoja, hivi huyo askari hata uani haendi? Hivi huyo askari hata chai hanywi? Hivi huyo askari ni saa ngapi atalegeza mikanda angalau hewa ipite kwenye *boot* zake. Kuna haja ya kuongeza askari angalau lindo moja linakuwa na watatu, wawili kidogo inatia moyo. Hata dharura yoyote ikimshika mtu kwa sababu askari na wenyewe ni binadamu kama sisi ataondoka anamwachia mwenziwe. Lakini anapokuwa peke yake ataondokaje na hilo lindo atamwachia nani?

Nimeona Bajeti inatosha tosha sijui kama kuna mikakati ya kuongeza hapa. Kupeleka vijana wengine wakapata haya mafunzo, kwa sababu tatizo naona ni askari kidogo. Lakini kama vyuo vyetu vipo si waende vijana mtaani wako wengi tu wenye sifa. Kuna haja ya kuongeza idadi ya vijana wa kwenda kuchukua mafunzo haya ili

kuwatia moyo askari waliopo kazini. Maaskari wanachoka kwa sababu ni wachache. Kazi nzuri angalau ya kupokezana akitoka huyu aingie mwingine.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee juu ya suala la rushwa ndani ya Jeshi hili la Polisi. Rushwa ipo tena ni kubwa kweli kweli. Lakini tukiendelea kusema tu rushwa rushwa haisaidii tutafute chanzo chake. Mimi nadhani chanzo ni ukata. Hivi mtoto kama amekula ameshiba ana haja ya kwenda kudowea kwa jirani. Sidhani kama anaweza kufanya jambo la namna hiyo. Tujitahidi kuboresha mazingira ya wenzetu kuwaongezea mishahara yao, posho na mambo mengine ya muhimu wapate.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia sana kuhusu suala la sare za askari. Kweli hii ni kero, askari anavaa *uniform* zinabana ina maana alipopata alikuwa bado mwembamba labda ameongezeka mwili. Ama imepauka, Waswahili wanasema: “Kauka nikuvae.” Inafuliwa usiku inavaliwa asubuhi. Je, hii si kero? Hivi nalo hili lina ugumu gani jamani la unifomu. Pamoja na ufinyu wetu wa Bajeti mengine ya muhimu yana uzito wake.

Mheshimiwa Spika, mimi pia sitaacha kuchangia suala la nyumba ingawa limeongelewa sana. Tunaliongea sana suala la nyumba kwa sababu ni kero. Askari wetu wanakaa mitaani, nyumba moja anapanga na jambazi askari hapo hapo na jambazi hapo hapo. Hivi unadhani askari huyo atamfichua huyo jambazi. Kwa sababu atakavyomfichua huyo jambazi ana timu yake, huo uhai wake atakuwa ameuweka wapi, hili ni tatizo. Na sio hilo tu hata nyumba hizi ni ndogo. Hivi kweli chumba na sebule *godown* anakaa askari anaweka *partition* pazia, *full suit* hivyo askari hawatakiwi kuzaa? Hata wenyewe wanatakiwa kuzaa jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mwalimu nilichojifunza kutoka kwa watoto wa maaskari wengi walikuwa hawana nidhamu kwa sababu ya mazingira wanayoishi. Matendo makubwa makubwa yanafanyika watoto wanaangalia. Hivi mengine mimi nadhani yanataka mahusiano tu hivi Jeshi la Polisi likishirikiana na Magereza pale wakatumia hata wafungwa wakajitolea wakajenga wenyewe. Hivi nayo Serikali itashindwa kutoa bati jamani angalau wajenge hata nyumba ya vyumba viwili na sebule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongee suala la vitendea kazi. Vitendea kazi ni kero. Kitengo cha Usalama Barabarani, hawa watu wana-*deal* hata na maiti. Wanahitaji gari la kubeba majeruhi, maiti hawana. Hata magari tu kwa ujumla huko kwangu nina Wilaya tatu mimi ni Mbunge wa Mkoa kuna Iramba, Manyoni, Singida hivi mkiongeza hata gari moja moja la kisasa linaloweza kufukuzana na haya majambazi ambayo yanatoka nchi za nje si itakuwa afadhali jamani. Hata karatasi askari hana anaweka rekodi nzuri karatasi ambalo huku nyuma limeandikiwa. Jamani hii si tunashusha hadhi ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la Idara ya Zimamoto. Hii Idara ndiyo kabisa mimi naisikia tu, lakini kazi zake hata sizijui. Mimi naomba Jeshi hili liimarishwe kwa kutoa mafunzo kwa askari waliofuzu. Mwaka 2002 sisi tumeunguliwa na Kituo cha Polisi cha stendi ya basi, *RPC* amehangaika na askari wake hana hata kifaa kimoja.

Kituo cha Stendi kimeteketea hivi hivi tunakiangalia. Jitahidini basi angalau kila Mkoa upate hata gari la Zimamoto. Nafhamu kwamba Kitengo hiki kinakaa Halmashauri ya Miji, Manispaa, Jiji basi wawepo na wenye kufuzu na pia wawe na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kupongeza Jeshi la Magereza. Kwa kweli haliko mbali na suala zima la upandaji miti. Kwa kweli nimepita hapa Gereza la Isanga kuna miti imepandwa pale inapendeza. Mpaka Magereza Singida wamepanda miti, wasafi, wanalima, wanakula chakula chao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri waliotuwakilishia hoja iliyopo mbele yetu Mheshimiwa Waziri Mapuri na Mheshimiwa Capt. John Chiligati kwa hotuba yao nzuri. Lakini vile vile naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza watumishi wa Jeshi la Polisi, *I mean* Mambo ya Ndani wakiwa wanaongozwa na Katibu wao Mkuu Bwana Mchomvu. Vile vile naomba pia nimpongeze kaka yangu *IGP* kwa kazi nzuri ambayo anazifanya. Vile vile naomba niwapongeze wafanyakazi wote kwa kweli, kwa kazi nzuri na ngumu ambayo wanayoifanya kwa usalama wetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba vile vile niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia baadaye nitaweza nikapata nafasi tena lakini nisije nikasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu na kama Mheshimiwa Waziri alipoileta hoja yake kwa kweli mimi naipongeza kwa sababu amesema kwamba: “Majukumu makubwa ya msingi kwa Wizara yake kwa kweli ni kudumisha amani, utulivu, usalama wa raia na vyombo vyao na mali zao hifadhi za wafungwa, mambo ya Wakimbizi, Uhamiaji.” Kwa kweli Wizara hii ni kubwa sana na ina majukumu makubwa sana, lakini kwa kweli wanajitahidi sana. Mimi nawapa pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Pamoja na pongezi hizo basi naomba na mimi nichangie kidogo ili niweze kuboresha ili kuweza kuweka nyama na kuifanya iwe nzuri zaidi. Kwanza kabisa naomba nizungumzie kuhusu suala la Magereza.

Naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kuweza kutupatia fedha kule Wilayani Handeni na kumalizia lile gereza letu la Handeni ambalo lilikaa miaka zaidi ya 10. Hiki kilio nilisema wakati ule wa Bajeti lakini kwa bahati nzuri kabisa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati ule aliahidi na Waziri aliyefuatia sasa hivi nikaona kwamba mambo yamekuwa ni mazuri na kwa taarifa ni kwamba lile gereza letu la kule Handeni limeenda vizuri mpaka nikaenda pale Handeni unakuta kila mtu anasema kwa kweli kazi uliyoifanya ni nzuri.

Mimi nakushukuruni sana na tunaomba sasa na kwa vile mmetaja katika matarajio yenu kwamba gereza la Maweni ni mojawapo ambalo litatengenezwa basi nawaombea dua ili hiyo azma basi iweze kutekelezeka ili hatimaye Mkoa wa Tanga na baadaye hatutachoka tutaleta muangalie na Lushoto, Korogwe ili Magereza yote basi yawe mazuri na kupunguza msongamano. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nizungumzie kuhusu suala la Wakimbizi. Naipongeza sana Serikali ikishirikiana na *UNHCR* kwa kutujengea Kambi nzuri sana kule Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga Kambi ya Chogo. Kambi hii imeweza kuwapatia makazi wenyewe wanaita Makaazi wale Wakimbizi wenye asili ya Kisomali, lakini katika historia wanaonekana kwamba wana asili ya Kizigua. Kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa sababu kweli kabisa ile Kambi ni nzuri sana ile ukilinganisha na iliyokuwepo kule. Mimi napongeza sana Kambi ni nzuri sana na wale Wasomali kule kweli wanaonekana kwamba wamejaliwa na wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba labda nitoe pia na angalizo kidogo. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba upo utaratibu sasa wa kuweza kuwapa uraia. Mimi sina pingamizi kabisa ukizingatia kwamba mimi ni Mzigua na wale ni Wazigua wenzetu.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono hiyo hoja isipokuwa ninachokiomba sijui mpaka sasa hivi imekuwa kuna utaratibu gani, lakini tunafahamu kwamba uraia watu wakiomba kuna taratibu. Isipokuwa ninachoomba kwa vile wale Wakimbizi walikuwa kule Handeni na wakafanywa kama ni Wakimbizi basi ni bora taratibu zifanyike ili wananchi wapate kuelezwa wasije baadaye wakawa wamepata uraia wakaona kama ni kitu kigeni kwao.

Kwa hiyo, tusaidiane kama viongozi tuwaelimishe kupitia Serikali na chama chetu Tawala tuwafahamishe hawa wananchi wa kule Handeni ili waweze kuwapokea vizuri wale Wakimbizi wasije wakaona kama vile tena wamekuwa ni tatizo kwao. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hilo suala labda tulifikirie na tuone kama kutakuwa na uwezekano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile. Samahani

SPIKA: Naibu Spika, hayupo hapa. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Samahani Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kule kwenye ile Kambi ya Chogo kwa kweli wamepata ardhi kubwa sana ambayo ina rutuba sana. Kwa vile walipokuwa kule Mkuyu walikuwa wale Wasomali-Wakimbizi walikuwa wanajitahidi katika kilimo mimi ningeshauri pia kupitia *UNHCR* wasaidiwe ili waweze kupatiwa nyenzo wapate kulima zaidi ili waweze kupata chakula baadaye waweze kujitegemea na kingine waweze kuuza labda nje ya mkoa au sehemu nyingine huo ni ushauri ambao ningetoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi tena kwenye suala la *PF3*. Suala la *PF3* kwa kweli hili nimekuwa nikilizungumzia sana hapa Bungeni. Nalizingumzia hili kwa sababu mimi ni Daktari wa Binadamu. Nilishawahi kukumbuwa na matatizo ya *PF3*. Nimekuwa nikilizungumzia hapa sio kwamba kutaka kuleta kero au nini lakini kweli naomba kabisa tuweze kusaidia. Tatizo la *PF3* kama lilivyokuwa nilipokuwa nikiuliza maswali yangu humu Bungeni imeonekana kama upungufu upo. Lakini inaonekana ile kasi ya kufanya marekebisho bado inakuwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ukurasa 41 katika kitabu cha hotuba hapa iliweza kuainishwa kwamba kuna makosa makubwa ambayo yameainishwa katika ukurasa wa 11 jedwali na 1B. Kubaka ni mojawapo ya makosa. Lakini nilikwenda tena kuangalia ukurasa wa 51 nikakuta kwamba katika idadi ya wafungwa ambao wako ndani ya Magereza sijui labda Mheshimiwa Waziri baadaye atakapokuwa anafanya majumuisho atanifahamisha uzuri kwa sababu nimeona hapa wameandika kujamiiiana yaani wafungwa walioko ndani kwa sababu ya kujamiiiana.

Mheshimiwa Spika, lakini neno kujamiiiana labda tungeliboresha vizuri zaidi *I mean* ingeelezwa vizuri kwa sababu huku kujamiiiana ni kule kubaka au kujamiiiana kupi. Kwa sababu mara nyingine kujamiiiana ni kujamiiiana ambako hakuna matatizo, katika makubaliano. Sasa lakini katika hii orodha ya wale wafungwa waliomo humu ndani hawakueleza kama wamejamiiiana wamebakana au wamefanya nini. Kwa hiyo, mimi ningeomba atakapofanya majumuisho naomba Waziri aweze kunifafanulia kidogo hili ili aniweke sawa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ningeomba hili tatizo la fomu ya *PF3* kwa kweli lifanyiwe uharaka kweli kabisa litatusaidia. Kwa sababu unapokwenda Mahakamani kama kuna kesi ya kubaka, Daktari unaposimama pale unaonekana wewe ni msomi. Anapokuja *prosecutor* kuanza kukuuliza maswali ya kitaalamu kutokana na mapungufu yaliyopo katika hiyo *PF3* kweli kabisa unaonekana hujaenda shule. Mimi naomba kabisa jambo hili lifanyiwe kazi ili kuweza kuwasaidia Madaktari wenyewe wana taaluma yao sasa wasikwamishwe kwa sababu ya hiki kitu ambacho kinaweza kurekebika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tena nizungumzie suala la Usalama Barabarani. Tumekuwa tukizungumza hapa kuhusu hawa askari wa Usalama Barabarani. Kweli kabisa tumezungumza sana na tunaendelea kuzungumza na hakuna hata mmoja wetu awe sisi humu Wabunge na wale wataalamu wa viongozi mlioko kule.

Kweli kabisa mmeona hizi kero za wale askari wa Usalama Barabarani. Kweli limekuwa ni tatizo. Wana tabia ya kutafuta rushwa, saa nyingine kwa kweli inakera na inatia aibu. Sijui tatizo ni nini lakini kweli tungefanya tafiti tuone kwamba hivi kweli ni kwa sababu ya kwamba mafao yao ni madogo au mishahara yao ni midogo ndiyo maana wanafanya hivi au ni basi tu ni tabia ya kujiendekeza?

Mheshimiwa Spika, hebu tujiulize huyu Mwalimu anayefanya kijijini kule shuleni au huyu mganga anayefanya kazi kule kijijini ina maana yeye kabla hajakuja basi am-

search mtu amchukulie fedha yake halafu ndiyo aende kupata huduma. Mbona wote wana maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mheshimiwa Waziri hili suala tuliongelea na litafutiwe ufumbuzi. Kuhusu kweli masuala ya nyumba kama tatizo ni mafao yao baadaye uwekwe utaratibu waweze kufanyiwa mpango kujengewa nyumba za *low cost* ili baadaye hatima yao iwe nzuri. Lakini sio mtu anatoa, anakamua fedha unasimamisha halafu unakuta yaani hata sielewi nizungumzie vipi lakini nadhani Mheshimiwa Waziri amenielewa na mwenzake pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu hao hao Askari wa Usalama Barabarani. Tunapokuwa barabarani tunaendesha magari wengi tumekumbana nao hawa. Unamkuta askari anajificha porini ghafla anatokea na ile kimulika chake cha *speed* (*Speed meter*) ile.

Sasa huyu anataka kutuua au anataka kufanya nini. Kwa sababu unakuta tuko kwenye *speed*, sawa, tunaendesha *speed* kubwa mara nyingine aidha umechelewa au unataka kuwahi. Lakini tendo lake la kutoka ghafla huko anasimama katikati ya barabara hivi tukimgonga atasemaje? Tukimgonga atasemaje. Yeye afanye kazi yake kama inavyotakiwa sio anakuwa katikati ya barabara labda wewe unafunga *break* pale na nini si anataka kutuua.

Kweli hii tabia sio nzuri tunaomba kabisa hawa watu wa Usalama Barabarani wafanye kazi kutokana na maadili yao ya kazi, vinginevyo aidha watatuwa au tutawakanyaga. Sasa sijui itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, mimi naomba hawa wenzetu sisi hatuna nia mbaya ya kuwagonga. Lakini akiona amesimamisha halafu akiona mimi sikusimama kweli asinilaumu kwa sababu mimi niko *speed* nikisimama pale kwa ghafla wakati ametoka kichochoroni basi ujue aidha mimi nitaanguka.

Sasa ili mimi nisianguke atashangaa mimi nampita ataona labda nimefanya jeuri. Atasoma namba ya gari na kadhalika lakini kweli akinipiga risasi, risasi hawezi kunipiga lakini ni kwamba tu wajirekebishe tu watumie yale maadili mazuri.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri cha mwisho naomba niipongeze Serikali kwa juhudi kubwa sana Wizara hii inavyotusaidia. Kweli kabisa pamoja na wale wachache ambao wanaharibu Wizara hii lakini kweli wako maaskari waadilifu, wapo viongozi waadilifu kazi wanayoifanya ni kubwa kwa kweli wanatulinda na wenyewe wengine wanapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, mazingira magumu wanayofanyia kazi kama hivyo *uniform*. Unawakuta sio tu suruali za kubana hata wale akinamama unakuta shati limekuwa chafu jamani hawa akinamama barabarani mle unakuta nguo zao zimewabana sketi fupi yaani imepanda huku juu kweli kabisa jamani tunaomba muwasaidie wapate vitendea kazi ili

waweze kufanya kazi yao vizuri vinginevyo kweli wataendelea tusiwe tunawalaumu upande mmoja lakini pia na sisi tuangalie mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kabla kengele haijanigongea naomba tena niwapongeze kwa kweli kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wake naomba pia nikupongeze na wewe kwa kunipa nafasi hii mimi naunga mkono hoja asilimia kwa mia, lakini nakumbusha suala la *PF3* nitakuwa naliongelea naomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli ili tusiwe tunazozana naye tena. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja kati ya watu wanaoamini kwamba ili Jeshi la Polisi liweze kufanya kazi yake vizuri na kufanikiwa, mashirikiano yake kati ya Polisi na raia ndio kitu cha lazima na cha msingi. Bila mashirikiano haya, Polisi hawezi kufanikisha kazi yake na raia hawezi kupata msaada wa Polisi ili kuhakikisha kwamba anaishi kwa utulivu na amani na mali yake inalindwa bila matatizo yoyote. Ikifikia mahali ambapo raia anaona kwamba hakuna haja ya kutoa mashirikiano yake kwa Polisi na vile vile Polisi akaweka mazingira ambayo yanamsababisha raia amuone ni mtu hatari kwake, mashirikiano haya hayawezi kuwepo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri iwapo raia wataamua kutokwenda Polisi kupeleka matatizo yao au kuripoti matatizo yanayowapata ndani ya mazingira yao, naamini Vituo vingi vya Polisi vitafungwa kwa kukosa wateja. Wote wawili wanategemeana, hivyo, suala la kuheshimiana na kutonyanyasana kati ya Polisi na raia ni jambo la msingi na ni jambo linalotegemeana na ni lazima lienziwe kwa gharama yoyote au kwa njia yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayazungumza haya yote kwa sababu moja kubwa, kwamba vijana wa Bukoba Mjini, ambao maisha yamewawia magumu, watu ambao ni maskini wameshindwa kukunua magari wakaamua kununua usafiri wao, yaani baiskeli au pikipiki, wamefikishwa mahali pabaya hadi wamenituma niulize kupitia Bunge hili kwamba wameichukiza nini Serikali! Ni kwa nini Serikali haiwapendi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mtu wa Bukoba Mjini kuwa na baiskeli ni balaa, mwanzoni ililetwa katika sura ya kwamba utaratibu uliokuwepo awali wa kuwaruhusu vijana kufanya biashara ya baiskeli yaani kubeba watu ilizuiwa kwa msingi kwamba Sheria zilikuwa zimegongana, tukakubaliana. Nami kama Mbunge nikawa mmojawapo katika kuhamasisha vijana waachane na utaratibu huo, nikafikiri imefika mwisho, lakini kumbe haikuwa mwisho! Hata raia ambaye amejinunulia baiskeli kwa shughuli zake, mfano kubeba maziwa katika harakati za kutafuta soko, kubeba ndizi juu ya *carrier* au kupeleka mgonjwa hospitali, imefika mahali wananyanyasika, wanapigwa na wanapata kipigo kibaya mno kutoka kwa baadhi ya askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Waziri akate mzizi wa fitina kabisa, wakati ana-*windup* atueleze Wananchi wa Bukoba tutaishije katika mazingira ya namna hiyo!

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, alikwenda Bukoba. Unapopita njia ya Polisi, kama unatoka uwanja wa ndege, ile *yard* ya Polisi, pale vijana wa *traffic* wanapoweka baiskeli na magari yanayokamatwa inaonekana, kulikuwa na lundo na baiskeli, si chini ya 750, ziko ndani ya *yard* ya hiyo. Kwa kujua kwamba Rais atapita na ataweza kuchungulia, walizisomba asubuhi asubuhi sijui walizipeleka wapi, zikaondolewa pale! Hilo lilikuwa ni lundo la pili. Lundo la kwanza, watu walinyang'anywa baiskeli zao kwa kupigwa na matokeo yake hizo baiskeli zikauzwa, zilipoisha wakaanza kukamata nyingine na lilikuwa ni lundo la baiskeli zaidi ya 750.

Mheshimiwa Spika, nilipoona kasheshe inazidi nilimfuata Mheshimiwa Waziri ofisini kwake na ninamshukuru kwa sababu alinikaribisha vizuri, nikakaa pale karibu saa moja na nikanywa chai. Nilimweleza tatizo la baiskeli pamoja na pikipiki Bukoba Mjini kwamba hali ni mbaya, ni kero. Mheshimiwa Waziri aliniahidi kufuatilia suala hilo na tuliporudi hapa Bungeni aliniambia ameongea huko na Vyombo vinavyohusika na kwamba suala hilo linafanyiwa kazi, lakini *kasheshe* ikaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nashukuru, kwani kabla ya kuingia ndani ya Bunge hili nimepiga simu Bukoba wanasema: “Sasa hivi rusha roho kidogo imepungua.” Maana vijana walipokuwa wanasema leo kuna rusha roho ujue kwamba leo ni mshike mshike ndani ya Mji. Lakini bado baiskeli za watu zinaozea Polisi!

Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*windup* anieleze hatma ya baiskeli za watu wa Bukoba Mjini na Vijiji vya karibu hata kwa Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, maana hao ndiyo wanatusumbua na baiskeli zao Bukoba Mjini, nazo zimekamatwa zimo ndani ya *yard* ya Polisi. Kwa sababu Wananchi wa Bukoba wanatuita *nshomile*, tumeendelea, watuambie kama baiskeli kule hazitakiwi tena yaani watu wote wanatakiwa kuwa na magari kwa *level* ya maendeleo ya Bukoba. Mheshimiwa Waziri atueleze kama mwananchi wa Bukoba hapaswi kuendesha baiskeli na wala hapaswi kumbeba ndugu yake kwenye *carrier* ya baiskeli, ili tuelewe kwamba Serikali inatuweka katika *group* gani watu wa Bukoba!

Mheshimiwa Spika, iwapo kuna Sheria inayozuia suala la watu kufanya biashara ya baiskeli, sisi hatupo kwa ajili ya kuwa watumwa wa Sheria. Bunge hili ndio linatunga Sheria, linapaswa kuziangalia na kuzifanyia marekebisho, kama Sheria mbalimbali ambazo zimekuwa zinaletwa katika Bunge hili, tena nyingine *under certificate of agency*. Sasa, Sheria inayowakandamiza Wananchi wa Bukoba kama ipo na inaruhusu hivyo, Mheshimiwa Waziri alete hiyo Sheria hapa Bungeni ili sisi hapa kama Wabunge tuiirekebishe, tusinyanyasike.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika suala hilo ningependa kujua, sijui Bukoba tunawekwa upande gani! Nimetembelea Kwimba, Maswa, Bariadi na bahati nzuri

Mheshimiwa Waziri nafikiri ana mahusiano huko, kuna *taxies* nyingi za baiskeli, nimekuta watu wametengeneza *carrier* nzuri tu, Msukuma anapiga *pedal* hata kilomita hamsini kumpeleka abiria, sasa nashindwa kuelewa, hawa wako nchi gani? Ni Sheria gani inayowalinda hawa, lakini Bukoba inaonekana hiyo Sheria ni matatizo? Naomba tuelezane na tuwekane sawa.

Mheshimiwa Spika, wakati ninamtembelea Mheshimiwa Waziri ofisini kwake, nilimueleza kwamba masuala haya yasipozuiwa, yasipoingiliwa kati na kufanyiwa kazi kuna hatari itatokea. Nakumbuka baada ya kupitia siku mbili tangu nimetoka ofisini kwake na bahati nzuri nilimpigia simu, iliripotiwa kwamba kijana mmoja akiwa amempakia kijana mwenzake wanakwenda kwenye nyumba ya tajiri mmoja, aliwaita kwenda kufanya kazi ya *welding* walikuwa wanakwenda kupima madirisha, vijana hao walikumbana na askari, askari wakawatisha na baada ya hapo kijana huyo alianguka, baadaye saa 1.30 iliripotiwa kwamba kijana huyo amefariki. Kijana huyo alikuwa anaitwa Elvis Elias Bina, alifariki tarehe 25 Februari, 2003 saa 1.30. Tumefuatilia suala hilo na Ndugu zake wamefuatilia ili kupata ripoti ya *postmortem* kwamba ni kwa nini kijana huyo amefariki, lakini wamekuwa wanazungushwa, wanapewa majibu ya kukatisha tamaa na ya kuwatisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri inawezekana hana taarifa na pia sisi hatuna nafasi ya kutoa taarifa rasmi hapa Bungeni kwa sasa hivi, lakini naomba suala la kifo cha kijana huyu Elvis Elias Bina, ambaye alifariki ndani ya kasheshe, ninaamini hivyo kwa sababu *postmortem* haijatoka, alifariki kwa sababu ya *kasheshe* hiyo ya baiskeli ambayo nimeripoti, suala lake lichunguzwe na kutolewa taarifa rasmi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia, kuna suala ambalo napenda liwekwe bayana kwa sababu nafikiri Polisi wanatumiwa katika suala hili na nadhani linakuwa ni la kisiasa zaidi kuliko hata utekelezaji wa kisheria, kanuni na taratibu za nchi na ninapenda nizungumze kwa uwazi. Wakati wa kampeni za kugombea Ubunge katika Jimbo dogo la Bukoba Vijijini, Viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi katika kumnadi mgombea wao, mojawapo ya suala walilozungumza ni kwamba: “Nyeie kama mnataka kupata matatizo kama ya vijana wa baiskeli Mjini Bukoba chagueni Mpinzani mtaona cha mtema kuni!”

Mheshimiwa Spika, maneno hayo waliyazungumza bayana. Sasa, naomba kujua kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, hawa watu waliokuwa wanazungumza maneno haya, kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo iliwatuma au ni maneno yao wenyewe, ili Wananchi wa Bukoba waweze kuelewa na wajue msimamo wa Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aagize Polisi wake na pia kwa kuhusisha Vyombo na Mamlaka mbalimbali wakae kwa pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala la baiskeli Bukoba Mjini, badala ya kutumia njia za nguvu, njia hizo haziwezi kusaidia na wala hazitatumia tatizo. Kwa jamii ambayo ipo katika hali ya umaskini kama Bukoba Mjini na Bukoba Vijijini na Wilaya nyingine zinazozunguka pale, kitendo cha kutumia nguvu na mabavu hakiwezi kusaidia, njia muafaka ya kutatua

tatizo hili ni kukaa chini, kutumia busara na maarifa ili tuweze kuona tatizo hili tunalitatua katika namna ipi.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuzungumzia suala la baiskeli tu kwa leo kwa sababu ni kero. Sina matatizo na Bajeti ya Mheshimiwa Waziri kabisa, lakini tutakapokuja kupitisha mafungu hapa, kabla ya hapo nategemea kuwa nimepata maelezo mahsusi kuhusu suala hili. Mambo ya kuja kupitisha fedha za kwenda kuwapelekea askari kwa ajili ya kuwapiga watu wa Bukoba Mjini, sitakuwa tayari kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya kuwapelekea pesa ili waanze kukimbizana na vijana wenye baiskeli, tena njia wanazotumia wanawafukuza na *defender*, magari tunayonunua kwa kutumia bajeti hizi, wanawagonga kwenye *carrier*, wakati watu wamebebana na wanawapiga virungu, sitapitisha Bajeti hiyo kama nitakuwa sijapata maelezo na kusikiliza tamko la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nilimpa vielelezo na leo kwa kumsaidia, kupitia Bunge hili nampa picha halisi za malundo ya baiskeli zilizopo Polisi, Bukoba Mjini. Pia, nampa picha za watu ambao wameng'olewa meno na watu waliopigwa ngeu ili afanyie kazi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili tulipisha mashirikiano ya *East African Community*, kitendo cha kwenda ku-*copy* shughuli zinazofanyika Uganda nafikiri ni kitendo kimojawapo cha maendeleo, suala kubwa lililopo ni kuboresha shughuli ambazo vijana wanafanya na kuboresha mambo ya ubunifu ili kila mmoja aweze kunufaika kutokana na busara zake na mambo anayoweza kuyabuni kwa ajili ya kupata lishe ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, lakini naomba kupitia meza yako Mheshimiwa Waziri apokee hii kitu (picha) ili aweze kuona na atolee tamko.

SPIKA: Mkabidhi Katibu.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri pamoja na timu yake nzima. Pili, nachukua nafasi hii kumpongeza *IGP*, Mheshimiwa Omar Mahita, kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninampongeza *RPC* wa Dodoma pamoja na timu yake kwa kazi nzuri. Pia, nampongeza *RPC* wa Lindi kwa sababu ameamua kupambana na upatikanaji wa silaha. Ametangaza hadharani kwamba yeyote mwenye silaha aisalimishe na Polisi hawatamchukulia hatua yoyote. Itakuwa ni vizuri na ma-*RPC* wengine waige mfano huo. *RPC* wa Iringa ninampongeza kwa sababu Kitengo cha Usalama Barabarani amekiimarisha vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa, lakini Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba ni kwa nini nimesimama. Kwanza, nimpongeze kwa sababu ni Mwalimu na Mwalimu siku zote mtu anaposimama kutaka kuongea, anajua wazi kwamba anataka kuongea nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku zote nimekuwa nikiongea kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi bado haijaboreshwa vya kutosha. Katika bajeti iliyopita nilizungumza kuhusu vifaa. Vifaa vya Wizara hii ni duni inapaswa wapewe vifaa vinavyokwenda na wakati. Katika Bajeti hii hata zile fedha walizoomba naona ni chache, kama wangeomba zaidi ningeomba wapitishiwe kwa sababu kama hatutakuwa na usalama, hakuna lolote litakalofanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa, napenda kuzungumzia kidogo kuhusu hizi Wilaya mpya ambazo Mheshimiwa Rais amezianzisha, zinaitwa Wilaya za Mkapa. Amezianzisha Wilaya hizo na hataongeza nyingine, kwa hiyo ni Wilaya zake. Nafikiri Wilaya hizo ziwe ni za mfano katika ujenzi mpya wa nyumba za Polisi, Magereza na Uhamiaji, yaani zijengwe vizuri na kisasa.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu katika Wilaya ya Kilolo kulikuwa na Kambi ya Wakimbizi ambayo sasa hivi ni Gereza la Mgagao. Katika kambi hiyo walipita Wapigania Uhuru wengi na maarufu. Nachukua nafasi hii kutoa ombi ambalo limekuwa ni la muda mrefu na ambalo Kamati ya Bunge iliwahi kufika kule na kutoa mapendekezo, kwamba sehemu ile ifanywe Shule kwa sababu wenzetu wa Afrika Kusini wanataka kufanya iwe ni sehemu ya kumbukumbu, tumekwishaasiliana nao na wako tayari kutusaidia.

Sasa, kwa kuwa tumekiwshaanza ujenzi wa Wilaya mpya, tunaomba tuwatengee eneo lingine kwa ajili ya Gereza. Ile sehemu inaweza kuchukua zaidi ya watu 3,000, lakini sasa hivi wanakaa wafungwa 30 na majengo yake ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itufikirie. Gereza lile liko katikati ya Vijiji, wale watu hawalindwi wanatembea wenyewe, wanazunguka tu, hakuna kinachofanyika pale zaidi ya ukataji wa mbao, kitu ambacho hakina manufaa. Sasa hivi hasa kwa Wilaya yetu mpya tunataka tuwape eneo ambalo watalima na watazalisha vizuri ili wasinunue chakula na wauze ziada nje kwa sababu ni sehemu ambayo inafaa kwa kilimo na ili tufanye Gereza isiwe ni wodi ya kulala wagonjwa au hospitali, bali iwe ni sehemu ya watu kwenda kujifunza mbinu za kilimo na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mambo mengine yanayohusu lile Gereza, najua kutakuwa na kipingamizi na nisingependa yaingie kwenye *Hansard*, nitaongea na Mheshimiwa Waziri na kumpa habari nzuri zaidi ili aweze kuturuhusu tuweze kuanzisha Shule. Sasa hivi tunaingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunatakiwa tuwekeze sana kwenye elimu, *otherwise* ushindani wetu utakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumza jana kuhusu kuwapa *vote* watu wa *Immigration*. Kitengo kile cha *Immigration* ni muhimu, wapewe *vote*, msipowapa *vote*,

watakaokwama ni Utumishi. Nawahakikishia kabisa kwamba watu wa Utumishi watakuwa na tatizo kwenye bajeti yao kama watu wa *Immigration* hawatapewa *vote*.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuzungumzia kuhusu baa la Ukimwi kwa ujumla. Sasa hivi watu ambao wamekuwa wakiathirika na vifo vingi vya Ukimwi ni watu wa Polisi, Magereza, *Immigration* na Jeshi. Hii inaonyesha kwamba bado elimu ya kutosha kuhusu Ukimwi haijafika huko. Kwa sababu Jeshi letu tunalihitaji, kama Kitengo hicho cha Elimu ya Ukimwi hakuna, basi mchukueni Mama Terry, yule mama anajitolea na anazungumza vizuri, mlipeni awape elimu ya kutosha ili watu wetu wasiendelee kufa, tunawahitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo linanipa shida kidogo. Serikali ilipoamua kufuta kodi ya maendeleo, tuliambiwa kwamba sehemu ambayo tunategemea sana kupata kodi hizo si kutoka kwa wafadhili ni kutoka kwenye baadhi ya Mashirika ambayo tumeyabinafsisha kwa mfano *Tanzania Breweries*, hivyo Serikali iliamua kupandisha bei za bia na sigara.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinanipa shida ni kwamba, toka limetangazwa agizo hilo, mauzo ya bia yameshuka, kwa sababu ilitangazwa kwamba mwisho wa kinywaji ni saa tano. Kinachotokea ni kwamba, kuanzia saa tatu hawatakiwi kunywa katika baa, wanatakiwa kujitayarisha ili kurudi nyumbani, *otherwise* utaitwa jambazi na mzururaji. Sasa, hizo fedha na kodi tunazotegemea kukusanya kwenye bia tutazipataje?

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kwamba baadaye tutawaambia Wananchi wetu waanze kulipa kodi. Naomba tukae chini turekebishe suala hilo kwa sababu ni la kiuchumi. Wale watu wa baa sasa hivi wamekwishafukuza wafanyakazi wao na kwa sababu hiyo, kazi itakuja kwa Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, wale watu watakuwa ni wake. Pia, *taxi drivers* hawafanyi kazi tena kwa sababu walikuwa wanasubiri watu watakaochelewa kurudi majumbani kwao wawachukue. na pale kwenye baa siyo kwamba wote wanaokuwa huko wanakunywa pombe, wengine wanafanya vikao vya harusi, misiba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuhakikishia kwamba, majambazi hata siku moja hayawezi kwenda kukaa kwenye baa kunywa, atafanyaje kazi yake kama amelewa? Wanakaa kwenye *guest houses* na majumbani, majambazi tunawatunza wenyewe. Naomba turekebishe suala hili kwa sababu unapotamka kitu ni lazima uwe makini, *otherwise* tutaumia wenyewe. Kwa hiyo, naomba tushirikiane na wenzetu wa Polisi ili tuone namna ya kufanya, maana huo umegeuka kuwa ni mradi tena mkubwa wa watu fulani fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo nina wasiwasi nalo ni kwamba, sasa hivi kuna Polisi, Usalama wa Taifa na *PCB*, yaani kuna tatizo kwani haieleweki nani ni nani! Wenyewe kwa wenyewe wanapigana vita, mara Polisi kashikwa na *PCB*, *PCB* kashikwa na Polisi! Wawekeni chini waelewane na wakae vizuri, *otherwise* itakuwa ni tatizo ambalo litakuwa ni aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwanamichezo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Omar Mahita, kwa kuamua kushirikisha zile timu zake katika daraja la kwanza. Yeye pia ni mwanamichezo na ni *referee* mzuri tu na ana uzoefu. Kwa hiyo, nina hakika kabisa kama mtu anashiriki michezo maana yake ni mzima kiafya kwa asilimia mia moja. Lakini kama unaona askari hashiriki kwenye mchezo wowote maana yake ni kwamba hafai, ondoa huyo mgonjwa na mfano mzuri ni Mheshimiwa Omar Mahita mwenyewe, anafanya mazoezi kila siku. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia na ambalo litakuwa ni la mwisho ni kwamba, tuangalie Askari wetu wanapotumwa nje ya vituo vyao ni kwa nini hawapewi posho? Yaani wanatakiwa wa-*claim* baada ya kumaliza kazi! Mfano Askari anatakiwa akamkamate mtuhumiwa Kilolo akishakwenda kule, hajui atarudi vipi na huyo anayemkamata ndio ana posho, hivyo inabidi huyo ndiyo amgharamie, sasa hapo kweli haki itakuwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, askari apewe posho yake kwani nyingine anaacha nyumbani kwa mama na nyingine anakuwa nayo kwa kujikimu. Twende na wakati. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu mara kwa mara tumesikia askari wetu wamekwenda Marekani na sehemu nyingine kujifunza mbinu mbalimbali. Hiyo ni njia mojawapo ya kuboresha Jeshi letu, tusifanye mambo ya mwaka 1947.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwani amezungumzia sana suala la upatikanaji wa gari la Polisi Wilayani Kilolo. Ukiona mtu anatoka Visiwani, halafu anaongelea kuhusu mambo ya Kilolo ujue hilo ni tatizo kubwa. Hata Magereza tulikuwa hatuhitaji sana kwa sababu wengi wanachukua uamuzi wa kujihukumu, sasa akiishajihukumu anakaa pale kwenye mti mpaka anaoka, gari halijaenda na askari hajaenda. Matokeo yake yule mtu unayemzika, unamzika kama mdudu maana ananuka. Naomba gari liende Kilolo haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, napenda kuwashukuru Viongozi wa Wizara hii kutokana na kazi nzuri waliyoionyesha, tunawaomba utekelezaji mwema. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea kuongea yale niliyokusudia, kuna usemi usemao: “Mjenga nchi ni mwananchi na mvunja nchi ni mwananchi.” Hapa ilizungumzwa sana kuhusu ajira dhidi ya askari Polisi. Kama kuna ubaguzi jambo hilo si kweli kama kuna ubaguzi, Chombo hiki kina wajibu wa kuangalia yule kijana ambaye anastahili, siyo kwamba kila kijana anastahili tu kuajiriwa, ni lazima mwenendo wake uangaliwe, tabia, taratibu na historia yake ndiyo utapata ukweli wa kijana huyo. Kwa hiyo, bado nawapongeza wale wanaojiri Jeshi la Polisi waendeleo na mwendo huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza itaendelea kuwa, kuhusu kuondolewa Sheria za kikoloni ndani ya Jeshi la Polisi. Vijana na Viongozi wengi hapa walizungumza kuhusu suala hili, lakini tuelewe wazi kwamba, wakati wa ukoloni Kanuni za Jeshi la

Polisi zilitungwa kwa maslahi ya wakoloni na siyo kwa maslahi ya raia wa Taifa hili. Hali hii iliwafanya vijana wengi ajira zao kuwa ni za kiinua mgongo na walikuwa hawana uhakika hasa wa maisha yao au wataendelea kwa muda gani na shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, hivi sasa tunawajibika kurekebisha taratibu zetu za kuajiri ndani ya Jeshi la Polisi. Mnamo tarehe 25 tulizungumziwa baadhi ya *PGO*, ambazo ni namba 3, 54, 254 – 277, lakini utaona kwamba hasa iliyowaokoa Jeshi la Polisi ni *PGO* namba 354, kwamba ili kumchukua mfungwa inabidi na yeye afungwe pingu ilikuwa kweli inawadhalilisha! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, *PGO* namba 54 nakubaliana nayo kutokana na marekebisho yake, lakini kuna ile sehemu ambayo nahisi kama kwa Wazanzibari itawabana. Kwa jinsi Tanzania Bara ilivyoendelea na katika taratibu za Muungano wetu kuna kipengele kinachoeleza vijana wetu kwamba waanze kuchukuliwa wakiwa na *division I, II na III* kwa wale wa *form four*.

Napenda kuweka wazi suala hili, kwa sababu mara nyingi ikifika wakati wa ajira tunapata matatizo na suala hilo linakuja kwa kasi kubwa sana na vijana wetu wanapata matatizo makubwa. Tunasema kwa upande wa Zanzibar *division III* wakati *combination* zake zinaoana, bado tuna nafasi ya kumpeleka mtoto yule *form V*. Kwa hiyo, kwa wakati huo kama tunawahitaji watu hao kwa kweli inakuwa vigumu.

Sasa bado kwa Zanzibar na mara nyingi zikija nafasi hizo mnatuletea hivyo. Kwa hiyo kipengele hicho nashukuru kwamba wameturudishia kati ya futi 5 na futi 8 mmerejesha mpaka futi 5, 6 ndiyo *PGO* katika maelezo yake alivyosema, hilo nawashukuru kwa sababu Wazanzibar kwa kweli hawana urefu kama watu Tanzania Bara. (*Makofi*)

Lakini sehemu hiyo pia iangaliwe kama ni chombo cha Muungano kinawajibika kuangaliwa kabisa na tumekubaliana Muungano huu tusiwe tumekubaliana lakini ndani kuna kitu ambacho hakifahamiki. Kwa hiyo, nasema bado baadhi ya *PGO* ambazo mmerekebisha hazijaleta mafanikio kwa askari wetu. Kilio kikubwa kwa askari wetu ni *PGO* namba 48. Wabunge wengi hapa walizungumzia suala la *PGO* hiyo inawadhalilisha askari wetu. Askari anafika kufanya kazi miaka 21, 34 *Sergeant Major* kama yeye kiinua mgongo *not pensionable* utaona anapata shilingi 1,300,000/= lakini yule ambaye ni *pensionable* anapata shilingi milioni 10 wakati wa kustaafu. Wakati wa ukoloni kuzidiana hakukuwa kama hivyo. Walikuwa wanazidiana lakini siyo kima kama hiki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunawajibika hivi sasa kwenda na wakati na kuangalia hali halisi tusiangalie upande mmoja tu tusiwe sehemu hii. Maana hata kuna *PGO* inasema kwamba polisi akifa azikwe kwa shilingi 100, itazika kweli shilingi 100? Kwa hiyo, bado tunahitaji marekebisho ya sheria hii. Kama Waziri utarekebisha *PGO* namba 48 utakuwa umewamaliza askari kwa sababu ni kilio chao kikubwa. Kwa hiyo, tunaomba sehemu hii kwa kweli irekebishwe ili tuweze kupata mafanikio. (*Makofi*)

Sasa kwa kuwa mkataba huu haubadiliki mpaka apandishwe cheo cha *assistance inspector*, wangapi watafika cheo hicho? Hawawezi kufika! Kwa hiyo kuna mapendekezo mawili kwamba kuanzia sasa askari yeyote aliyesaini akifikia umri wa utendaji miaka 21 mkataba wake ubadilike awe *pensionable*, au moja kwa moja hivi sasa katika ajira yetu askari wote wawe *pensioner*.

Mheshimiwa Spika, hakuna idara hata moja ambayo imefanyisha kazi mtu zaidi ya miaka 30 halafu akawa yeye ni mtu wa kiinua mgongo, ni kitu ambacho hakistahili hakuna haki hata mara moja. Hata Jeshi la Wananchi wa Tanzania pia hawana taratibu hizi. Hivi kwa nini hatujaweza kuondoa mambo kama haya? (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba hapa yafanywe marekebisho kisiwe ni chombo peke yake, vyombo hivi kwa kweli vimefanya kazi katika Tanzania hii tena kwa nguvu zote kwa hiyo lazima tuwathamini askari wetu na hivi sasa muda mwingi watu wanapigania suala hili. Kwa hiyo, itakuwa ajabu kwamba msikutane viongozi na mkaweza kuleta mabadiliko katika suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mwaka 1999 hapa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha sheria ya kustaafu wafanyakazi wote wa Tanzania kwa miaka 60 ya badala ya miaka 55. Lakini cha ajabu na kushangaza baada ya kutoka sheria hii kuna baadhi ya maeneo ya kazi waliweza kubadilisha na wakaweza kuwaongezea japo kwa miaka miwili. Lakini Jeshi la Polisi halikufanya hivi, walianzia *ASP* hadi *IGP*.

Kama wewe unataka kula na mwenzako anataka kula hivyo hivyo, kama wewe una shida na mwenzako ana shida hivyo hivyo na uungwana wa mwanadamu ni kufikiriana. Hali unayohisi ndani ya moyo wako ikiwa kwa watoto wako, ikiwa kwa jamii yako sema na mwenzangu hali kadhalika vile vile anahitaji. Hapo utakuwa umekamilisha uungwana na ubinadamu. (*Makofi*)

Sasa kama hili halikuwezekana hivyo ina maana inashangaza kabisa kwa hiyo ingelikuwa watu hawa bila shaka kufanya utaratibu huo. Utaona kwamba kuna sehemu kama *Sergeant Major* toka mwanzo alikuwa afikirie miaka 60 kutokana na *PGO* hapo nyuma lakini hakuna. Kwa hiyo, utaratibu wa kustaafu polisi hivi sasa, *Coplo Sergeant* kustaafu kwa hiari ni miaka 45 ya lazima ni miaka 50, *Sergeant Inspector* miaka 50 ya hiari na lazima miaka 55, *ASP, IGP* miaka 55 ya hiari, lazima miaka 60.

Mheshimiwa Spika, kwa nini hawa wengine hatukuwapa japo kwa miaka miwili nao wakaongezwa? Halafu hapa tunajibiwa kwamba eti wao siyo watendaji, ni watu ambao ni *initiative*, wako katika kuwaza tu, pita hapa fanya hivi. Nasema *energy* inapotea kwa kufikiri zaidi kuliko mambo mengine, *energy* inapotea kama kiongozi kazi hiyo, nasema akili yako haiwezi kufanya vizuri inachoka zaidi kuliko yule ambaye anahangaika ina maana anaweza ku-*survival* kuliko wewe ambaye unatumia akili, akili inachoka. Kwa hiyo, katika utendaji hautakuwa mzuri. Nasema bado marekebisho yafanywe yarekebishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile kengele ya kwanza imeshalia nilikuwa na mengi sana ya kuchangia. Tokea mwaka 1996 kwa kweli taratibu vile vile zilikwenda vizuri. Baada ya miaka 3 askari ndiyo walizidishiwa fedha na utaona kwamba kwa muda wa miaka 3 askari alikosa shilingi 282,000/= hadi shilingi 384,000 alizikosa kwa kukaa miaka 3 baada ya kupata nyongeza. Kwa hiyo, lazima waweze kufikiriwa. Hali kadhalika posho ya shilingi 33,000 Polisi walikuwa wanapewa shilingi 16,500 lazima tuwafikirie watu hawa. Kwa hiyo, askari walidhulumia shilingi 797,000 hadi hivi leo, polisi wanapewa shilingi 24,700/= tunawapeleka wapi watu wetu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Kituo cha Chwaka. Kuna Kituo cha Chwaka huu ni mwaka wa saba, kuna matatizo naomba hapa kila mwaka hakuna lililofanyika. Sielewi sababu ni nini. Hivi sasa Kituo cha Chwaka hakina hadhi kuwa kituo. Kituo kiko katikati ya kijiji. Muundo wa jengo lenyewe halikujengwa kwa shughuli za kituo cha polisi ni nyumba ya kawaida labda ya kurithi.

Kwa hiyo, tunahitaji kupata kituo. Askari Chwaka wameshatenga eneo jirani na barabara Mheshimiwa Waziri unapajua njia ya kwenda Uroa, wameshatenga eneo pale ambako pana sheli upande mwingine kwa ajili ya kituo. Sasa kwa kweli tunahitaji hawa watu wapate kituo cha polisi kwa sababu hakipo pale. Kituo katikati ya mji watafanya kazi vipi? Hivyo Chwaka inawajibika kuwa na kituo karibu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pana askari lakini hakuna usafiri. Nilidanganywa hapa katika Bunge hili, mwaka 2001, ilikuwepo gari ikapelekwa na gari ile walisema itahudumia Wilaya ya Kati ya Kituo cha Dunga, Kituo cha Chwaka, lakini hakiuonekana, kumbe gari ile ilikuwa ni gari kwa kuwa pale kituo kasimamia mzee ikaonekana ipeleke sisi hatukuhesabia kwamba gari ile kweli tulipewa katika maombi ya Bunge hili. Kwa sababu kituo kasimamia mzee kwa hiyo tumpelekee na gari pale. Tunakwenda wapi je, hawa wadogo? Mimi nahisi sijui kuna busara, tunasema bado tunahitaji gari Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Kituo cha Mwera kina kazi zake, pale mimi nafikiria Dunga itashirikiana na Chwaka eneo lile ndiyo tutafanya kazi tukipata gari. Juzi nilipigiwa hodi na mtu akiendesha honda nasikia tukutukutuku! Wanakwenda kumtafuta kijana ambaye amefanya maasi kwa kutumia honda tena mafuta hawana wakaja pale wakasema tupatie mafuta, wakaenda pale mitini, maana nazungumzia kitu kwa uwazi wakaenda mitini walau kutia mafuta. Je, tunakwenda wapi?

Sasa tunahitaji kuwa na gari hatutaweza sehemu ile bila shaka kuna mahoteli ya utalii, leo unaletewa habari ghafla utakwenda vipi, vipi utafuata adui iwapo utaletewa habari ghafla na pale hapana gari ya kusaidia? Kuna honda nayo ni mbovu mbovu imeshapitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, miongoni mwa wale waliomba kuchangia kwa mdomo baadhi yao wameondoa majina yao, mwingine hakuwepo Bungeni wakati zamu

yake ilipofika. Kwa hiyo, sasa namwita msemaji wa mwisho, Mheshimiwa Ali Said Salim.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kunijalia mimi pamoja na sisi wote kufika hapa Bungeni tukiwa katika hali nzuri kiafya na tukaweza kushiriki katika shughuli za Bunge salama salimini.

Mheshimiwa Spika, pili, nataka nichukue nafasi hii tena nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwa msemaji wa mwisho katika kuchangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na tatu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufanya ziara maalumu Pemba kuja kuonana na Viongozi wa Vyama vya Siasa. Huu ni utaratibu mzuri aliouanzisha Mheshimiwa Waziri, bila shaka nimshukuru pamoja na Waziri wake kwa kuwa najua mipango hii itakuwa imepangwa kwa ushirikiano na Mheshimiwa Waziri. Nashukuru kwamba mimi ni miongoni mwa viongozi wa kitaifa wa vyama nilishiriki katika mkutano huo. Nakupongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba utaratibu huu uendelee ili kuweza kuwa karibu zaidi na Vyombo vya Dola na Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nataka nianze kuchangia suala la ajira za polisi. Niliipitia hii hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sikuona sehemu yoyote ambayo kuna idadi ya askari ambao walijiriwa katika kipindi cha 2002/2003. Sasa nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, katika mwaka uliopita hakukuwa na waajiriwa wowote kwa upande wa askari na kama ulikuwepo naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze aliajiri askari wangapi kwa Tanzania na upande wa Zanzibar pia walijiriwa askari wangapi na kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi walizungumza suala la ajira za polisi. Nilishtushwa jana baada ya kumsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja akitaka ajira zifanywe kwa watu ambao ni wanachama wa CCM. Sijui Mheshimiwa Mbunge huyo alisahau kwamba hii nchi ni ya Watanzania na miongoni mwa Watanzania kuna CCM, CUF, UDPD, CHADEMA, NCCR, TLP nakadhalika.

Hata hivyo inaonekana yeye na wengine baadhi waliochangia hasa upande wa Zanzibar walikuwa wanamshauri Mheshimiwa Waziri, afikirie utaratibu huu. Sawa sisi hatuna tatizo lakini kama hivyo ndiyo basi ni vizuri Mheshimiwa Waziri, atakapofanya majumuisho atuambie waziwazi humu Bungeni, kwamba kuanzia sasa utaratibu wa kuajiri polisi sifa inayotakiwa ni kadi ya Chama cha Mapinduzi, hatuna ugomvi. *Otherwise* ningemuomba Mbunge aliyetoa kauli ile Bungeni afute kauli ile mara moja na kuomba radhi mbele ya Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumze suala la ujenzi wa nyumba 53 za polisi Kisiwani Pemba. Napongeza Wizara kwa kufikiria suala hilo, lakini kuna manung'uniko ya hapa na pale kwamba eneo lile lilojengwa nyumba zile bado wananchi hawakulipwa haki zao. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi je, suala hili ni kweli na kama ni kweli, je, Serikali imewalipa hawa watu au bado na kama bado ni kwa nini? Pia

Mheshimiwa Waziri afikirie hapa ambapo zimejengwa nyumba hizi za polisi basi ni vema pakawekwa kituo kidogo cha afya ili mbali ya askari polisi watakaokuwepo hapo kupata matibabu ya awali basi pia na wananchi wa vijiji jirani waweze kunufaika na kituo hiki cha afya kwa kupata huduma za afya za mwanzo.

Mheshimiwa Spika, lingine napenda nichukue nafasi hii kulipongeza Jeshi la Polisi jinsi walivyoweza kufanya kazi kipindi chote cha uchaguzi mdogo Kisiwani Pemba, kuanzia uandikishaji, tukaingia katika hatua ya kampeni, upigaji kura, uhesabuji kura na hatimaye kutangaza matokeo. Sina wasiwasi wowote ni kwamba yote haya yalifanyika kwa kufuata maelekezo mazuri ya muafaka. Muafaka ambao nasikitika sana kwamba baadhi yetu tunaubeza.

Jana Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumza kwamba kila kitu siku hizi Zanzibar ukitaka kufanya hivi askari wanakuambia aah! huu ni muafaka, kwa kweli nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa muafaka huu na nichukue nafasi hii kuwashukuru baadhi ya Viongozi Serikali ya Muungano walivyosimama kidete katika kuhakikisha kwamba muafaka huu umefikia lengo zuri. Mheshimiwa Rais mwenyewe alisimama kidete na akatumia muda wake ambao si wakazi kuweza kushughulikia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, kwa kweli kama tungekuwa na viongozi kama Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru angalau tu wanaopata 50 Tanzania ingekuwa mbali. Ni kiongozi wa aina yake. Lakini siishii hapo vile vile Mwenyekiti Mwenza Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, amechangia sana katika suala la muafaka. Sasa kama mtu atatokea kuubeza muafaka sijui kwa kweli tutamhifadhi katika kundi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ugaidi limezungumzwa sana, lakini naomba Serikali ichukua tahadhari kubwa katika suala hili la ugaidi kwa sababu tayari sasa hivi kuna fikra ndani ya wananchi wetu kwamba sheria ya ugaidi imepitishwa kwa ajili ya kudhibiti Waislam tu.

Sasa hata kama uhakika wa suala hilo sivyo ulivyo, lakini tayari baadhi ya waumini, fikra hizi wanazo kwa hiyo ni vyema katika kutekeleza sheria hii basi Serikali na Vyombo vya Dola vikalichukulia suala hili katika hali ya tahadhari ili wananchi wakose sababu ya kusema kwamba sheria hii imeundwa *special* kwa ajili ya Waislam tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tumesoma katika ripoti ile kwamba kuna watu wa rumande 17 walikufa na wengine baadhi walijeruhiwa.

Nashukuru kwamba Serikali ilichukua hatua ya kuwachukulia hatua hawa ambao walihusika na uzembe huo. Lakini haitoshi ni vema wakafidiwa kwa sababu watu wamepoteza roho na hawa waliopoteza roho zao wameacha familia wake na watoto.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wale wote waliopoteza maisha ya hawa watu kwa uzembe huo basi Serikali iwafikirie kuwapa fidia familia za marehemu hawa.

Pia semina mbalimbali zilifanywa za haki za binadamu na utawala bora kwa upande wa Tanzania ningeomba semina kama hizi zifanywe kwa upande wa Zanzibar pia na Kisiwani Pemba na hapa ambapo zitafanywa basi ziwashirikishe viongozi mbalimbali wakiwemo Wabunge, Wawakilishi na wale wananchi wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tulikuwa tunazungumza kuna kuvunja Muungano nakadhalika. Sasa suala la Muungano kwa kweli kuna baadhi ya Wizara ambazo ni za Muungano kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa ili waweze kupata la kuzungumza basi ni vema zikafanywa shughuli zake katika mfumo wa Muungano. Rais wa Jamhuri ya Muungano mara nyingine anatoka Zanzibar na wakati mwingine anatoka Bara.

Sasa hii Wizara ningeomba Mheshimiwa atakapo- *wind up* aniambie tokea tumeanza kuwa na Serikali ya Muungano na hii Wizara ikiwa ni Wizara ya Muungano, Mkuu wa Polisi wa Tanzania (*IGP*) ni mara ngapi ametoka Zanzibar? Kama hajatoka Zanzibar ni kwa nini? Hakuna Mzanzibar ambaye anasifa hii? Hapa hamuoni kwamba wenyewe mnauchokonoa huu Muungano? Ndiyo kabisa.

Kwa hiyo, haya mnayoona kwamba ni mambo madogo hata kama hatupati chochote, lakini ile kuwepo *figure* ya Mzanzibar inatosha. Kwa nini Kiongozi Mkuu wa Nchi apatikane kutoka Zanzibar kama Rais, Waziri wa Mambo ya Ndani mara nyingi anatoka Zanzibar kwa nini *IGP* wakati mwingine asitoke Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, huku ni kuchezechezea Muungano. Naomba hizi sababu ndogo tuziondoe ili watu wasipate cha kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa tumesoma katika Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ndani, kwamba wananchi wanaonekana kusaidia sana polisi kufanikisha ama kukamata mali ama kukamata wahalifu. Ni utaratibu mzuri na tunawapongeza wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, ni vema Wizara ikafikiria kwamba hawa wananchi ambao hupelekea kwa sababu moja ama nyingi kukamatwa mali au wahalifu basi Wizara ifikirie kuwapa ahsante hawa wananchi. Tukiweza kuwapa ahsante hawa basi kitakuwa ni kichocheo hata kwa mwingine akiona kuna uhalifu wowote ataweza kutoa taarifa mahali panapohusika.

Mheshimiwa Spika, lakini kama mtu atachukua juhudi za kuweza kukamatisha mali au majambazi halafu hakuna chochote ambacho atapata mara nyingine anaona ni kupoteza muda kwa hiyo, tunaweza kusababisha tukapata hasara kubwa kwa kuogopa kutoa kitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo nakushukuru tena na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Menejimenti yote kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti kuwa katika hali hii ya kuridhisha mno. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Kuhusu Magereza. Gereza letu la Meatu halina chombo cha usafiri kama vile gari la aina *CERES* kama yalivyo Magereza mengine. Mahabusu na wafungwa wapelekwao Wilaya ya Maswa hupata shida, shida ambayo hata askari nao huipata katika kuwasafirisha mahabusu na wafungwa. Kwa hiyo Gereza la Meatu linahitaji kupata usafiri kama nilioutaja hapo juu.

Inspector General of Police (IGP) Omar Mahita katika safari zake za kuja Wilaya ya Meatu aliahidi kukipa gari kituo kidogo cha Polisi kilichoko Mjini Mwanhuzi Makao Makuu ya Wilaya ya Meatu. Mpaka sasa hakuna lolote lililofanyika. Naomba utekelezaji huo ufanyike ili Jeshi la Polisi hilo lipate nyenzo ya kufanyia kazi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba haya mawili yatekelezwe mwaka huu wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula ni kubwa kimaeneo na mauaji ni mengi hasa kwa wakazi wa kabila la Wasukuma waliohamia hapo kutokana na kuibiana mifugo na imani ya kichawi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alipe uzito wake kwani uhalifu wa mauaji, wizi wa mifugo na uporaji wa mali, askari wanashindwa kutoa msaada kutokana na masafa marefu na msitu mnene kwa askari kufuatilia matukio kwa miguu. Hata baiskeli kwao ni ndogo, je, pikipiki si ndiyo kabisa?

Mheshimiwa Spika, kutoka Igalula hadi mpaka wa Mkoa wa Tabora na Singida ni kilomita 130 askari atembe kwa mguu au kwa kutumia ungo?

Mheshimiwa Spika, Wizara isaidie kuweka *Grill* kwenye *Armaury* jengo kubwa, zuri, imara ambalo limejengwa na wananchi karibu asilimia 90 na asilimia nane ni

Halmashauri je, kituo bila silaha itakuja kweli, eti tu chumba cha silaha akina mlango wa grill kwa nini wananchi wasipewe msaada kwa kusaidiwa mlango huo?

Mheshimiwa Spika, naomba kazi hii ya kuweka *grill* ifanyike ili nikimaliza Bunge mwezi Agosti, nikute kazi hiyo ndogo imefanyika na ifanyike ili wananchi waendeleo kuamini kuwa kazi wanazozianza Serikali inaunga mkono juhudi zao hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuomba gari ambayo niliahidiwa naomba baiskeli japo mbili za kuwasaidia askari angalau kusaidia kupeleka summons. Askari hawa wanafanya kazi na kuishi Kijijini, waonewe huruma ingawa ni kazi yao.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kungojea majibu.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kumpongeza Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake ambayo imetuwekea matumaini yaliyoboreshwa kwa usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, askari polisi ni wanajeshi ambao wanajitahidi kufanya kazi kwa nguvu zozote. Askari wetu hawa kama utalinganisha kazi zao wanazofanya ni kubwa kuliko mishahara wanayopewa hasa ukizingatia kuwa wanapambana na majambazi na hata ukizingatia mfumo huu wa Vyama Vingi wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana kwani wanatuliza ghasia na vurugu kwa marungu na askari wetu hupigwa mawe na kuumizwa au kukatwa miguu kwa kuwa hawana silaha za moto basi raia hawaogopi kwani huwa wamekusudia kuwaumiza askari wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa makusudi kabisa naiomba Serikali yetu iwatazame askari wetu kwa mishahara yao kwani bado ni midogo na haikidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kule Zanzibar, kwa kuwa katika fukwe zetu tuna hoteli za kitalii na majambazi hutumia fursa hiyo ya kutokuwepo kwa vituo vya Polisi huweza kuvamia watalii na kudhoofisha utalii wetu. Kwa hiyo, Serikali ijenge vituo vya Polisi ili tuweze kuwa na hali ya usalama kwa watalii ambao wanaingia nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isicheleweshe mafao ya askari anayestaafu kwa sababu askari wetu hawana miradi kwani hawana huo muda wa kufanya shughuli nyigine wakiwa ni askari na kuchelewa kuwapa mafao yao basi ni kuwaua mapema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono mia kwa mia Wizara hii. Ahsante sana.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Ramadhan Mapuri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na katika muda mfupi huu ameonyesha kwa vitendo kuwa atamudu vema kuongoza Wizara hiyo. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Yeye ni kiongozi anayependa kazi yake, anayewasiliza watu,

anayawaheshimu Wabunge wenzake hasa anapojibu maswali bila kusahau uwezo wake wa kufuatilia masuala ya Wabunge. Nawatakia kheri sana katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ingawa fupi lakini iliyo makini na yenye undani. Nampongeza pia Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hiyo chini ya Katibu Mkuu kwa kazi kubwa ya kuandaa hotuba hiyo iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amebainisha kwamba mwaka jana 2002/2003 bajeti ya Wizara hii iliongezeka kwa asilimia kubwa kuliko ilivyowahi kuongezwa hapo nyuma. Kiasi cha bilioni 3.3 zilitengwa kwa ajili ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za Polisi na *FFU*.

Mheshimiwa Spika, tumaini langu lilikuwa kwamba hata nyumba za askari Mkoa wa Kagera zingekarabatiwa. Nyumba za askari kwa kweli zinatisha, ni mabanda mabovu ya zamani ambayo yanahitaji kukarabatiwa au kuvunjwa na kujengwa nyumba mpya zenye hadhi. Ukiangalia nyumba za line ya *FFU* Nshambya zinatisha, zile za Polisi line ya Buyekela pia hazifai, nyumba zilizoko nyuma ya Kituo cha Polisi Bukoba nazo hali ni ile ile. Nimezungumzia nyumba zilizoko Bukoba Mjini lakini hali ni hiyo hiyo katika Wilaya zote. Mwaka huu pia bajeti imeongezeka sana (bilioni 5.3). Mazingira ya kuishi ni kivutio na hamasa kubwa kwa mtumishi kufanya kazi kwa bidii. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo na takwimu ni kiasi gani cha fedha iliyotengwa kwa ajili ya matengenezo au ujenzi wa nyumba za askari Mkoani Kagera. Katika hotuba sikuona maelezo yoyote.

Mheshimiwa Spika, jengo la Askari Magereza Mjini Bukoba linatia aibu, ni chafu ndani na nje na hata mfumo wake wa maji machafu nadhani ni mbovu maana kila mara maskini wafungwa wakichota na kumwaga ovyo maji machafu bila hata kuwa na *gloves*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo napenda kuwashukuru na kuwapongeza Askari Polisi na wale wa *FFU* kwa namna wanavyojitahidi kukabiliana na ujambazi Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe na pia niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa juhudi za kuandaa bajeti hii na kuileta hapa Bungeni, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa nyumba za watumishi, juhudi zipi na ni viporo vipi kwa nyumba za watumishi zilizoanza kujengwa mfano, Wilaya ya Misungwi hakuna jengo la nyumba ya *OCD*. Je, Serikali isingeona vema kutoa fedha kwa ya ujenzi kama huo ili kupunguza tatizo linaloikumba Wilaya hiyo inayoendelea kupata huduma kutoka Wilaya ya Kwimba?

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nipate ufafanuzi kuhusu Jeshi la Zimamoto. Jeshi hili linategemewa sana kwa suala zima la uokoaji wa mali za watu walizojenga kwa kuvuja jasho kwa muda mrefu. Mali nyingi zimekuwa zikiteketea na wao wapo. Je, Waziri amejizatiti vipi kuboresha huduma hii muhimu ikiwa ni pamoja na kupeleka magari maeneo mengine mfano, Jiji la Mwanza na pia Wilaya ziangaliwe kwani wenye mali si Mijini tu hata Wilayani wanakumbwa na matatizo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, tatu, ajira za askari wapatao 2000. Naishukuru Wizara, niombe baada ya ajira hiyo kufanyika ni vema wakaangalia upungufu wa watumishi najua askari hawatoshi lakini hata hivyo mgawanyo uangaliwe ili askari hao waweze kusaidiana na wananchi kupitia Sungusungu. Vile vile semina zitolewe kuwaelimisha Sungusungu majukumu yao ili wafanye kazi kwa pamoja. Hii itaondoa uhasama unaoendelea wa kutowatambua Sungusungu na badala yake kutegesheana na baadaye kuwatia ndani (Mahabusu), Sungusungu hii inakatisha tamaa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake walione suala la semina juu ya Sungusungu ni jambo muhimu na litasaidia mauaji yta watu, raia wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SHAMIM P. KHAN: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wakuu wote wa Idara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi. Nampongeza Mheshimiwa Omar Mahita *IGP* na Mapolisi wenzake kwa kazi nzuri wanayofanya kupambana wimbi la ujambazi humu nchini. Ushauri wangu ni kwamba *this has to be an ongoing process* na siyo tu tukio au matukio ya mauaji yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uhamiaji, pasi za Afrika Mashariki. Naomba kufahamu wangapi hadi leo wanapatiwa hizo kama ikiwezekana “me” na “ke”. Nimeuliza hivyo kwa sababu nadhani Wizara zote zimegeuzwa kuwa na dawati la jinsia (*gender desk*) na mtaalam atakayeshughulikia masuala ya kujinsia. Wote tunatakiwa kuvaa *gender lenses*, wakati wa kupanga, kutunga sheria, kuandika sera zetu na kadhalika. Mikutano yote ya Kimataifa inasisitiza *desegregated data* (me na ke).

Pili, je kuna mpango wowote wa kuwa na *diplomatic passport* ya Afrika ya Mashariki? Inaelekea watu wengi bado hawajui faida za kuchukua pasi za Afrika Mashariki. Nashauri waelimishwe kupitia vyombo vya habari, *seminars* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Magereza. Pongezi kwa Kamishna Mkuu wa Magereza Mheshimiwa Banzi kwa kazi nzuri anayoifanya akisaidiana na wenzake.

Mheshimiwa Spika, nashukuru wako wafungwa walioachiwa huru lakini ningependa kufahamu kati yao me, ke na watoto wangapi? Nashauri suala la jinsia lipatiwe kipaumbele. Its important.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bweni la wanawake ukurasa wa 26. Nawapongeza na naomba kufahamu bweni hilo litawapokea wanawake wangapi? Nchini yapo mabweni mangapi ya wanawake na wanaume na yapo wapi? Uwiano ukoje kati ya “me” na “ke”? Hatua za makusudi zinachukuliwa au zitachukuliwa kuziba pengo hilo? Hongereni.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Spika, ninaomba awali ya yote kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba yafuatayo yaangaliwe:-

Mheshimiwa Spika, moja, hali mbaya ya jengo la Polisi la Wilaya ya Kasulu. Makao Makuu ya Wilaya ya Polisi Kasulu hayana jengo la ofisi zaidi ya gofu lililojengwa na Serikali ya Kijerumani ambalo muda wowote linaweza kuanguka na kusababisha vifo vya wale wote watakaokuwemo yaani askari na raia. Serikali iangalie uwezekano wa kujenga kituo kingine hata kama kitakuwa kidogo ili tunusuru maisha ya watumiaji wa gofu hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, vitambulisho vya uraia maeneo ya mipakani. Hali ya ulinzi na usalama mipakani, hususan Mkoani Kigoma, inadai Serikali ifanye kila liwezekanalo kutoa vitambulisho ili kutofautisha raia na wageni. Ieleweke kuwa Waha (wakazi asili wa Mkoa wa Kigoma) na Warundi wanaongea lugha moja na hivyo ni rahisi kwa Mrundi kujichanganya katika kundi la Waha na kuchukuliwa kuwa ni Muha. Serikali itoe kipaumbele kutoa vitambulisho vya uraia kwa wananchi wa maeneo kama Kigoma ili kudhibiti hali ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, tatu, usajili wa *NGOs*. Je, ni kweli usajili wa *NGOs* unaendelea kufanya na Wizara hii na wala siyo Ofisi ya Makamu wa Rais kama ilivyoelezwa wakati Bunge hili Tukufu linapitisha sheria mpya ya usajili wa *NGOs* mwezi Novemba, 2002? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, nne, uingizaji kinyemela wa bidhaa toka nje ya nchi. Serikali iangalie mipaka yake vizuri zaidi kudhibiti bidhaa kama vile vinywaji (Konyagi na sigara-*sportsman*) ambazo zinaingizwa nchini kinyemela kutoka nchi jirani ili kushindana na bidhaa zizalishwazo hapa nchini. Bidhaa za namna hiyo hazilipiwi kodi yoyote na mara nyingi zinakuwa na ubora duni, hivyo zinaathiri uchumi wa nchi yetu. Jeshi la Polisi lisimamie vema kwani ni vigumu kuelewa jinsi makontena kadhaa yanavyoweza kuingizwa nchini bila kugunduliwa au kuonekana kwa vyombo vya dola husika.

Mheshimiwa Spika, tano, maslahi duni ya Polisi. Serikali ichukue hatua za makusudi kuboresha maslahi ya Polisi hasa wale wa vyeo vya chini. Hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya hatari na hivyo wanastahili hata kupewa posho ya hatari (*risk allowance*) kama Madaktari na kada zinginezo.

Mheshimiwa Spika, ninawatakia kila la kheri katika mwaka 2003/2004. Naunga mkono hoja.

MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB: Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Polisi (*IGP*), Mkuu wa Uhamiaji, Mkuu wa Magereza, Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi na Kamishna wa Zimamoto na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wafanyayo katika kusaidia kuleta usalama nchini. Napongeza kwa kupata fedha nyingi kidogo za maendeleo hasa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni muhimu askari kuwekewa utaratibu wa kuweza kukopeshwa saruji, mabati na kadhalika vikiwemo vyombo vya usafiri kama *Vespa* na kadhalika. Natambua kuwa Zanzibar wamefanikiwa sana. Naamini huku bara nako itawezekana tu. Vema pia kuwajengea askari wetu mazingira bora ya baadaye wakiwemo Polisi, Magereza na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, pili, kuboresha mafao ya fidia kwa askari wanaoumia kaziniau kuuawa. Fedha wapewazo askari ni kidogo sana kwa wanaoumia na wanaokufa. Matukio ya Pemba ya tarehe 27/1/2000 na ya Kawe ya tarehe 25/5/2003 na ya juzi juzi huko Chakechake ya askari wenyewe kuuana. Matukio yote haya yamepoteza maisha ya askari na wengine kupata ulemavu. Mifano hiyo inabainisha kuwa kuna umuhimu wa kuwawekea bima askari au kuboresha mafao ya fidia ya askari wetu au yafanyike yote mawili.

Mheshimiwa Spika, tatu, Idara ya Zimamoto ipatiwe mafunzo ya kisasa pamoja na zana. Aidha, majengo yajengwayo katika Jiji yawe na ramani ya kuweza kutoa huduma za zimamoto endapo moto utatokea. Tunavyo vifaa kama ngazi au nguvu za maji ifikayo maghorofa makubwa huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema naunga hoja na nawatakieni heri na nafaka.

MHE. LYDIA T. BOMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa pongezi sana kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo ametolea maelezo kila kipengele. Nampongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote walioshirikiana katika kuiandaa taarifa tunachokusudia wananchi ni kuona utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia *RPC* wa Mkoa wa Mtwara anavyojitahidi akishirikiana na raia wema katika kuiweka amani Mkoani. Amekuwa akishirikiana vizuri na askari wake kama Wilaya ya Newala mwanzoni mwa mwaka majambazi walibomoa

milango na kuiba mali katika nyumba ya Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum. Jitihada za uhakika zilifanywa hatimaye mali zote zilipatikana kwa kipindi cha siku saba vitu vilikuwa vipo mikononi mwa askari, navyo vilikuwa vimevushwa nchi jirani. Katika jitihada hizo ni pamoja na kitengo cha upelelezi. Haya niliyoyataja na mengine ambayo sikuyataja yasingeweza kupatikana kama sio kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuwa matatizo ya askari wetu ni nyumba zenye stahili. Wanaishi baadhi yao katika nyumba za tangu tupate uhuru, hivyo tunasema zimepitwa na wakati. Naomba mbinu za haraka zitafutwe za kuwapatia nyumba askari wetu ambao wana jukumu kubwa la ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, askari na hasa wapelelezi kuwaweka kituo kimoja kwa zaidi ya miaka kumi ni tatizo kwake hata kama anafanya kazi vizuri. Anajitahidi tu siyo kuweza kwani anaweza kudhurika na raia wabaya wakishamgundua na kazi yake anayoifanya. Nashauri taratibu za kuwahamisha kila inapowezekana zifanyike pamoja na hali ngumu ya kifedha. Pia kikosi hiki kipatiwe pikipiki hasa ukiangalia Mkoa wa Mtwara upo mpakani, chombo hicho wakipata kitawawezesha kukimbia hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, kikosi cha askari wa barabarani. Raia wengi wanalalamika kwamba wanasumbuliwa kwa kuwataka wasimamishe magari ili watoe fedha (baadhi yao) na wengine wana tabia nzuri. Ukiongea na madereva kwa nini mnatoa fedha mnaposimamishwa na wawataje askari wanaowasumbua sana hawasemi wala kuwataja. Jibu lao wanasema tunatoa ili waturuhusu na mradi wa kusafiri, kama hutoi chochote utasumbuliwa.

Hivyo nashauri tusichoke tuendeleo kutoa elimu kwa wananchi wajue kuwa kitendo cha kutoa ni kibaya na askari wapatiwe semina kila mara zikiwaeleza athari za kutojali maadili. Kazi ya askari ni nyeti sana kwani ndiyo wanaohusika kulinda raia na mali zao, hivyo ajira zisiangalie vyeti tu ni vema kupata historia yake pia, maana kazi zimepotea, kwa hiyo anaweza akajiunga tu hata kama hana moyo wa kazi hiyo. Baada ya muda mfupi anaweza akaendelea na tabia yake mbovu. Tuanze sasa kuwa makini katika ajira.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la askari inasemekana vijana wanaokwenda katika mahojiano wengi wao hukosa vyeti vya shule na vinavyoonyesha kuhitimu. Kwa kuwa hana yeye huazima kwa rafiki yake au cheti cha kughushi. Nashauri sana tuwe makini tusije tukapitisha wakorofi na hili halipo ndani ya Mkoa ni la Kitaifa, kwani wenyewe vijana hueleza hayo ukitaka wataje hawasemi. Hivyo lisemwalo lipo kama halipo liko njiani. Mbinu mpya ya majambazi wanayoitumia kama kujipaka rangi usoni, kuvaa gunia, kutumia jiwe Fatuma, noti jinsi zinavyotengenezwa si vizuri kutangaza katika redio kwa sababu redio ni elimu inayotoka mara moja na inatoka muda ule ule na wengine hujifunza mbinu na imekuwa hivyo ila kama askari wanapata ushindi hakika iko kila sababu ya kutangaza katika *RTD* itasaidia majambazi kuogopa nguvu ya askari, kuliko kutangaza na wakati wao hawapatikani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawatakia Wizara utekelezaji mzuri wa malengo waliyojiwekea katika bajeti katika mwaka wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa hatua ya hali ya juu ya kupambana na uhalifu nchini hususan ujambazi. Naishauri Serikali iongeze vitendea kazi hasa magari na mawasiliano. Katika Mkoa wetu naomba ofisi ya Mkoa na Wilaya angalau kila Wilaya iwe na gari angalau tatu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Shinyanga Mjini askari hawana nyumba za kuishi. Naomba Wizara katika Bajeti ya fedha za maendeleo tusaidiwe nyumba za askari mpya na kukarabati zilizopo ambazo zina hali mbaya sana. Askari hulala kwenye bwalo. Naomba sana Wizara itusaidie kutatua tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Pia wapo askari waliofanya kazi ama kuhamishwa lakini hawajalipwa haki zao. Naomba Wizara itatue mapungufu haya.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa Magereza tunaomba pia tupatiwe kazi za kufanya ukarabati wa Gereza na kumalizia ujenzi wa Gereza la akina mama linaloendelea kujengwa. Nashauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba kuwatoa mahabusu wanaokaa mahabusu zaidi ya miaka miwili kufutiwa mashtaka na kuwaachia na endapo wanatenda uhalifu tena kurudishwa rumande. Msongamano kwenye Magereza upunguzwe, watu wanakaa rumande kwa muda mrefu kwa sababu Mahakama na Polisi wanashindwa kukamilisha kesi mapema na kuwafanya mahabusu kukaa magerezani miaka mingi na kuongeza gharama za kuendesha Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzee wa helikopta ya Polisi nashauri tuendako hasa mwaka wa fedha wa 2004/2005 Wizara ipange kununua helikopta mpya na zilizopo zikarabatiwe (*overhaul*) kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na uzee wa helikopta husika.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya Watanzania sharti viharakishwe ili kuwabaini Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na nawatakia mafanikio mema katika kutekeleza malengo mliyojiwekea kwa Bajeti ya 2003/2004.

MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wakuu wote wa vitengo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya na hasa katika kupambana na majambazi. Nashauri mkazo utiliwe katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Idara ya Upelelezi (*CID*) *Specialized Training*. Hapa nasisitiza tu kwani hayo yamo katika mapendekezo ya Kamati ya Ulinzi na

Usalama. Uchaguzi wa nani aingie katika Idara hiyo ni muhimu sana. Nashauri kuongezwe mafunzo ya kisasa na vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na usafiri wa kasi.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vifaa vya zimamoto bado ni tatizo. *Agents* wa kuuza vifaa hivyo wawe katika kila Wilaya na maoni hayo yatekelezwe haraka. Sera ya suala hili iletwe haraka.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya nyumba za askari yanajulikana, lakini askari katika Mkoa wa Ruvuma hasa Wilaya ya Songea Mjini yatazamwe kwa karibu sana kwani hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kila zinapotokea ajali kubwa za magari makubwa au madogo kuna tabia ya watu ambayo imezuka siku hizi ya kuiba mali za abiria na wakati mwingine kuwamaliza walio hai kwa lengo la kuiba pasipo kutambulika. Jambo hili linazidi kukua na kuendelea kukua. Jambo hili lazima likomeshwe. Jambo hili pia linahitaji elimu kwa umma na kampeni nzito. Nashauri kwa nguvu zote Kamati iundwe chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kulifanyia kazi suala hili. Wajumbe watoke, uraiani, Polisi na Usalama wa Taifa. Suala hili nimelizungumza mara nyingi sana lakini halipewi uzito wa kutosha na Wizara hii. Mheshimiwa Waziri tukiacha tabia hii iendele tutajenga Taifa lenye tabia ya kijambazi na ukatili mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuyasema mapendekezo haya.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa pongeza kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Mkuu wa Jeshi la Magereza, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai na Uhamiaji, watumishi wote wa Wizara hii na bila kusahau Idara ya Zimamoto kwa kuandaa vizuri bajeti hii ya 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia fursa hii naomba kutoa pole kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi pamoja na familia za marehemu askari watatu waliouawa na majambazi. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi na nawaombea wafiwa wawe na subira.

Mheshimiwa Spika, upande wangu naomba nichangie kidogo kuhusu Jeshi la Polisi kitengo cha *Marine*. Kitengo hiki hakikuzungumzwa kabisa na kikizungumzwa basi ni kwa maeneo ya Dar es Salaam tu. Sasa basi naomba Wizara iangalie idara hii kwa kuongeza ufanisi wake wa kazi kwa kutanua kikosi hiki kwa mfano katika Wilaya ya Mkuranga, Mafia, Rufiji, Kilwa hadi Lindi sijui kama kuna kituo chochote cha Polisi kilichokuwa na boti ya doria au ya usalama kwa wananchi wanaotumia Bahari ya Hindi. Kwa mfano, juzi tarehe 8/7/2003 kuna boti iliyokuwa inatoka Kilwa kwenda Mafia imezama na ndani yake mnakadiriwa kuwa na watu zaidi ya kumi na tano. Kwa taarifa nilizozipata katika kuhangaika kwa kutumia maboti ya watu binafsi wamepatikana watu kama watano tu waliobaki zaidi ya watu kumi bado hawajapatikana. Hii inaonyesha laiti

kungekuwa na boti ya nguvu ya Polisi na kuwa na askari wazoefu basi labda yasingetokea maafa kama hayo. Hivyo naomba sana kuiomba Wizara kuleta boti moja ya nguvu iendayo kwa kasi ili isaidie kuboresha *patrol* na kusaidia pale yanapotokea maafa katika maeneo hayo ya bahari niliyoyataja kati ya Mkuranga, Mafia, Rufiji na Kilwa. Naomba kituo kikuu kiwekwe Mafia kwa sababu ndiyo katikati ya Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka kueleza kuwa katika Wilaya ya Mafia askari hawana nyumba za kuishi, zile wanazotumia ni za Idara ya Ujenzi tena ni mbovu hazifai kabisa kwa kuishi askari. Hivyo naomba Wizara iliangalie suala hili la makazi ya askari waliopo Wilaya ya Mafia. Kule Mafia kuna askari mmoja tu mwanamke hivyo anafanya kazi sana na hana msaidizi mwenzake basi naomba tena ikiwezekana aongezwe askari mwingine mwanamke ili asaidiane kazi na mwenzake.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo natoa shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mafia na kutoa pongezi zangu kwa Jeshi la Polisi kwa kupambana fika na majambazi. Narudia tena kusema naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii nzito iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba hii kwa umakini na umahiri mkubwa. Hongera sana. Niruhusu pia nitoe pongezi kwa ndugu na jamaa wa marehemu askari waliouawa na majambazi wakati wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia hoja hii naunga mkono kwa asilimia mia moja hasa baada ya kuona kazi nzuri waliyofanya askari Polisi baada ya mauaji ya wenzao. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi sheria, kanuni, muundo na mafunzo ya Polisi bado kuna aliyotuachia mkoloni. Ni dhahiri kwamba Jeshi la Polisi pamoja na ukweli kwamba halina vitendea kazi vya kutosha. Linahitaji kutazamwa upya siyo kwa lengo la kulifuta bali kuboreshwa hata ikibidi kulisuka upya ili liweze kwenda na wakati na kuliwezesha kupambana na uhalifu unaotumia teknolojia ya kisasa. Tukizingatia kwamba msingi mkuu wa Polisi ni uwezo wake wa kupeleleza makosa au hata kutabiri uvunjaji wa amani na hivyo kuzuia uhalifu. Sambamba na hayo nchi yetu imeridhia mikataba mingi ya Kimataifa kwa mfano, kudhibiti silaha ndogondogo, kupambana na madawa ya kulevya, kupambana na ugaidi wa Kimataifa na kadhalika. Utekelezaji wa Mikataba hiyo unahitaji upelelezi mahiri. Uhalifu wa kughushi kutumia kompyuta ndiyo unapamba moto, uhalalishaji wa fedha haramu ni tatizo ambalo uchumi wa nchi yoyote unaweza kuangamia.

Mheshimiwa Spika, matatizo yote haya ni mapya kwa hiyo tunahitaji kuwa na Chuo Kikuu kitakachoshughulikia upelelezi badala ya kutegemea Chuo cha Moshi ambacho haina *facilities*. Nashauri Wizara ianzishe utaratibu wa kuanzisha Chuo cha aina hii kwa kuleta Muswada wa Sheria hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu suala la kuwa na *economic intelligence system*, utaratibu ambao utawezesha kufuatilia masuala ya kiuchumi hasa katika ulimwengu huu wa utandawazi. Utaratibu huu utatuwezesha kubaini wawekezaji bandia au wale wanaowekeza kwa lengo la kuhalalisha fedha haramu zinazotokana na madawa ya kulevya, uporaji wa maliasili yetu hususan madini, nyara za Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la Uhamiaji katika nchi yetu halina budi kufanyiwa tathmini ya kina. Pamoja na kwamba mipaka yetu ni mikubwa lakini jitihada za kudhibiti wahamiaji haramu bado ni ndogo. Nashauri hatua za kidiplomasia zichukuliwa na kupewa kipaumbele ili kufungua vituo zaidi vya uhamiaji mipakani baina ya Msumbiji na Tanzania. Hivi sasa hakuna kituo cha Uhamiaji kati ya Msumbiji na Mkoa wa Ruvuma hali inayofanya watu waingie na kutoka kana kwamba hakuna mpaka.

Hali pia siyo nzuri kwa upande wa Ziwa Nyasa ukiacha Mbamba Bay hakuna Afisa Uhamiaji kwenye baadhi ya bandari. Meli zinabeba abiria kutoka nchi jirani na kuingia nchini kinyume cha sheria. Matokeo ya kukosekana kwa huduma za Uhamiaji yamepelekea raia wengi wa nchi jirani kuiba uraia wa nchi yetu na hata kuchukua nafasi za uongozi. Kama hatukuwa makini katika suala la Uhamiaji ni dhahiri nchi hii inaweza kutawaliwa na raia wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusu ahadi yake ya kutoa gari nzima kwa Afisa Upelelezi wa Wilaya ya Mbinga. Ieleweke kuwa Wilaya hii yenye wakazi zaidi ya laki nne ndiyo yenye mazingira magumu. Kwa mfano, milima mingi, shughuli nyingi za uchimbaji madini na hivyo kuongoza katika uhalifu katika Mkoa wa Ruvuma. Kadhalika Makao Makuu katika Wilaya hiyo hayana umeme na badala yake wanatumia taa ya chemli hali ambayo inasikitisha. Je, Mheshimiwa Waziri hawezi kuondoa kero hiyo.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru wewe binafsi kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Omar Mapuri (Mwalimu wangu) kwa hotuba yake nzuri inayoleta matumaini kwa idara zake zote. Mimi naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kazi za Polisi. Polisi ni miongoni mwa wafanyakazi walio muhimu sana katika Taifa lolote lile liwe changa au limeendelea kiuchumi. Pia Polisi ni kioo kwa uimara na umakini kwa chini husika. Polisi wapo kwenye kazi karibu muda wote, kwa hiyo basi mtu anayefanya kazi kwa kitambo kirefu ni lazima awe anatunzwa vizuri. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kila juhudi ili:-

* Awapatie Polisi makazi mazuri ama wanapokuwa katika makambi na hata kufanya mpango wa kuwajengea nyumba na kuweza kulipa kidogo kidogo.

* Mishahara yao bado haijaendana na wakati wa sasa ambapo kila kitu kinahitaji hela. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara iwaongezee mishahara askari Polisi ili waweze kukabiliana na maisha.

Mheshimiwa Spika, hili suala la mishahara midogo kwa askari ndilo linalowafanya baadhi yao kushirikiana na wahalifu ili kujipatia kipato cha ziada kwa kukidhi haja zao. Suala la uajiri katika Jeshi la Polisi bado lina utata mkubwa sana hasa kule kwetu Pemba. Mimi nina ushahidi wa vijana pale Jimboni kwangu ambao walimaliza taratibu zote na walikuwa wamekamilisha sifa, elimu, urefu, mwili smati, vijana wa umri chini ya miaka 24. Wakatiwa tamaa sana kwamba kwa jinsi walivyokamilisha sifa basi watachukuliwa tu.

Hatimaye hakuna hata mmoja kati ya vijana wapatao wanne aliyepata nafasi. Hali hii inaashiria kuwa uajiri katika Jeshi hili unafanywa kichinichini na kwa kuzingatia itikadi za Vyama kama ambavyo imedhihiri leo hii Bungeni pale Mheshimiwa Mbunge mmoja alipochangia na kusema kwamba Polisi waajiriwe wana CCM tu kama kwamba wengine hawana haki ya kuajiriwa katika Serikali ndani ya nchi yao ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti finyu lazima Wizara ifanye kila juhudi ili iweze kuajiri askari wengi zaidi. Hii ni hatari na ngumu zaidi kwa askari mmoja kuweza kuwalinda watu 1500 kama alivyoainisha Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake ukurasa wa 13. Uwiano huu bado ni mkubwa sana. Kwa hiyo, ili kufanya kazi ifanyike kwa makini tunamwomba Mheshimiwa Waziri awaajiri vijana zaidi katika Jeshi lake na pale Jimbo la Ole nao wapate ajira.

Askari ni kwa ajili ya kuwalinda raia na mali zao nchini bila kuzingatia itikadi kama wanavyodai baadhi ya Waheshimiwa. Tunawapongeza sana askari kwa jinsi walivyofanya kazi zao vizuri katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni kule Pemba. Hii inaashiria kwamba kama askari hawatoelekezwa vibaya, watafanya kazi zao kama mkondo unavyoruhusu. Tunashauri hili liendeleo kudumisha sio tu kwa uchaguzi ujao wa 2005 bali iwe tabia ndani ya Jeshi letu la Polisi na vyombo vingine vya dola. Katika ukurasa wa 42 kwenye Jedwali la 1(c) kuhusu makosa makubwa dhidi ya maadili ya jamii nchini Mheshimiwa Waziri kaeleza idadi ya kesi na washitakiwa kwa kipindi cha Januari mpaka Desemba, 2002. Katika jedwali hilo idadi ya kesi za madawa ya kulevya kwa Mikoa ya Zanzibara ni 71 kwa idadi ya washtakiwa 80. Tungependa wakati Waziri atakapotoa majumuisho atueleze katika kesi hizo na washtakiwa hao wangapi tayari wanatumikia kifungo kwa makosa hayo?

Mheshimiwa Spika, suala hili la madawa ya kulevya linalitia aibu Taifa letu. La kushangaza ni kwamba watu ambao wanaendesha biashara hii wanajulikana lakini wanaoshikwa ni wale wadogo ambao wanatumwa tu. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kulikomesha hili na njia pekee ya kumaliza tatizo hili ni kuwashika bila haya hao wafanyabiashara wa madawa ya kulevya. Mimi binafsi nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hatua anayochukua kwa suala la rushwa katika Jeshi lake.

Tunamwomba aendelee kuwabana askari wanaocheza mchezo huu haramu ili alisafishe Jeshi lake la Polisi.

Mheshimiwa Spika, hali ya Magereza nchini hasa kwa baadhi ya Magereza siyo nzuri hata kidogo. Katika baadhi ya Magereza kuna mrundikano mkubwa wa wafungwa na mahabusu. Kwa mfano, Gereza la Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba katika kipindi cha 1990 - 1992 mimi binafsi nilishuhudia mrundikano mkubwa sana wa wafungwa na mahabusu katika Gereza lile. Pamoja na mrundikano huo vifaa vya huduma ya malazi hakuna, binadamu analala chini muda wote wa kifungo chake.

Mheshimiwa Spika, mbali na hali hiyo niliyoieleza hapo juu, hali ya vyoo katika Magereza hasa hilo Gereza nililolitolea mfano hamna, bado upo mtindo wa kuburuta ndoo za vinyesi kila asubuhi na kumimina vyooni nje ya vyumba vya kulala. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri alitazame suala hili kwa jicho la huruma ili wafungwa na mahabusu wengine waondokane na kero hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Jeshi la Polisi kwa jinsi walivyoshughulikia kikamilifu majambazi waliona askari na mbwa wao hapo tarehe 25/5/2003. Utendaji mzuri na wa haraka ndiyo ambao wananchi wanalolitaka na Jeshi wamethibitisha kuwa wakitaka wanaweza na wala si nyenzo. Kinachotakiwa kwa askari yeyote ni uzalendo, *commitment*, akili na nyenzo. Kamwe nyenzo haichukui nafasi ya *commitment* au uzalendo. Ninachokitara jia ni kwamba kasi hii idumishwe ili kusitokee tafsiri miongoni mwa wananchi kuwa kasi hii ilitokea kwa sababu tu waathirika ni Polisi wenzao au tatizo lilikuwa kukosana katika mgawo wa mafao ya ujambazi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la maofisa wakubwa kuwakatisha tamaa wanaotoa taarifa za uhalifu na ujambazi wakiwemo wananchi na Polisi wa kawaida. Mara nyingi wamekuwa wakiuza taarifa hizo kwa wahusika kwa nia ya kujinufaisha. Hii pia huhatarisha usalama wa watoa taarifa na kukatisha tamaa askari ambao nao hushawishika kujiunga katika nyendo hizo mbaya. Uhusiano binafsi wa wakubwa na wahalifu na mara nyingine kuwa kwenye *payroll* zao ndiyo chanzo cha kuharibu kazi. Kuna kulindana sana ndani ya Jeshi la Polisi ambapo hata watendaji wabovu hupandishwa vyeo. Yuko ofisa mmoja ambaye kwa matendo yake yaliyokuwa wazi anaitwa Noriega, lakini aliendelea kupandishwa vyeo hadi kuwa *RPC*. Kamati ya *PAC* ilipendekeza *RPC* mmoja ambaye hata Kamati ya Adadi ilimwona ana makosa bado anaendelea kazini pamoja na mapendekezo kwamba aachishwe kazi. Huku ni kulindana na kuharibu kazi ndani ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakimbizi, ni vema makambi yawe mbali na mipaka. Jumuiya ya Kimataifa iwe tayari kugharamia uwekaji wa makambi mbali na mpaka ambako wakimbizi husika hutoka. Ugomvi ulioko kati ya Tanzania na Burundi kwa kiwango kikubwa hutokana na ukaribu wa mpaka na kambi zilikowekwa, hili libadilishwe. Ni vema badala ya kuendelea kuwapokea wakimbizi, Jumuiya ya

Kimataifa iwe tayari kuhudumia wakimbizi katika maeneo salama ndani ya nchi wanazotoka. Hii itazifanya nchi kuona matatizo ya ukimbizi badala ya kupeleka matatizo nchi za wengine.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za kurudisha wakimbizi wa Burundi kwao. Lakini Wizara iwe makini na Mashirika ambayo huhudumia wakimbizi makambini. Wengi wao hawataki warudi na wana-frustrate juhudi za Serikali. *UNHCR* nayo haitaki kwani Kibondo inalenga kurudisha wakimbizi 24,000 katika miezi sita wakati katika miezi miwili tu zaidi ya 10,000 wamerudi *spontaneously!* Lakini badala ya kuona jambo hili lina *positive way*, *UNHCR* wanasema Tanzania inawafukuza wakimbizi. Pia kuwa inazuia wakimbizi wasiingie eti kwa kuwa ni wakimbizi 200 tu walioingia makambini. Serikali ikemee lugha kama hizi. Jumuiya ya Kimataifa pia iwajibike kutoa chakula cha kutosha kwa wakimbizi kwani au *empty stomach knows no law*. Wizi wa vyakula vya Wananchi umezidi hasa maeneo yanayozunguka makambi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri lakini ni kati ya Idara ambazo zimekithiri kwa kuwa kwenye *payroll* wa kugeuza wahalifu au wahamiaji haramu kuwa mradi. Ebu wachunguze jinsi viwanda vya nguo ambavyo vimeajiri hata *spinners* ambao hawana *work permits*. Pia wajisafishe kwani kwa sababu za ubinafsi wamekuwa wakitumiwa kutoa *P.I* za chuki. Kesi ya Ernest Mokaka au ya Chavda au hata ya yule mama aliyepewa *P.I* sababu alikuwa hapendwi na wakwe zake ni mfano dhahiri. Napendekeza wanawake walioolewa rasmi na Watanzania ambao si Watanzania, baada ya muda fulani wa uchunguzi wapewe uraia ili watoto wapate haki ya kulelewa badala ya mama kupelekwa kambi za wakimbizi. Kuhusu Magereza. Kuna msongamano mkubwa sana wa wafungwa hasa vijana. Ni vema Sheria ya *Community Service* ianze kufanya kazi kikamilifu. Juhudi za kufanya Magereza kuwa na kilimo ziendelezwe ipasavyo ili Magereza yaweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, *RPC* huripoti kwa *IGP* katika utendaji wa kila siku, lakini ni mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Kwa nini asiwajibike kwa *RC* ili utendaji wake udhibitwe ipasavyo na nyendo zake kujulikana pale pale Mkoani badala ya Dar es Salaam kwa *IGP*? Ni kweli ugaidi hauna mipaka wala dini. Tunakubaliana na dhana nzima ya kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kupiga vita ugaidi. Ni vema lakini taarifa zitakazotolewa kila wakati ziwe za kweli badala ya zile ambazo zimesababisha upungufu wa utalii nchini mwetu. Taarifa zikanushwe kwa nguvu zote na hao waongo wawajibishwe Kimataifa.

Kampuni binafsi za ulinzi zimekuwa nyingi sana na sina hakika waajiriwa wao wamepata mafunzo gani, wanaaminika kiasi gani na kama hawahusiki na baadhi ya matukio. *Vetting* ya Makampuni ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hiyo wakishirikiana na wataalam wake.

Kwanza kabisa, nianze na ndugu zetu Polisi kwa kweli hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hawana vifaa vya kufanyia kazi mfano, magari, silaha za kisasa na ukizingatia majambazi wanatumia silaha za kisasa. Hawana *radio call* katika vituo vyao kwa ajili ya mawasiliano.

Polisi hawana nyumba nzuri za kuishi pamoja na kazi wanazozifanya za kulinda mali na usalama wa Watanzania, mishahara yao ni midogo sana ukilinganisha na kazi wanazozifanya kwa kweli wanatakiwa kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya Jeshi la Polisi kuna baadhi ya Askari wa barabarani wanalipaka matope Jeshi hilo kwa tamaa zao za kupokea rushwa ndogo ndogo kwa Madreva, hivyo tunaomba Waziri akemee tabia hii mbaya inayochafua Jeshi letu la Polisi.

Suala lingine ni sare za Polisi kwa kweli kuna baadhi ya Askari wetu sare zao zimechakaa sana na zinatia aibu kwa Askari kuvaa sare zenye viraka, tunaomba suala hili liangaliwe hii ni pamoja na viatu.

Mheshimiwa Spika, Magereza yetu mengi yamejaa kuliko uwezo wake, hii inatokana na kutomalizika haraka kwa kesi na kesi nyingi ni za kusingiziana au kulipiziana kisasi kwa Askari na raia kwa mambo ya mitaani.

Mheshimiwa Spika, raia wamekuwa wakifunguliwa kesi za uongo kwa sababu ya ugomvi wa kugombea wanawake na hawafunguliwi kesi ambazo hazina dhamana kwa mfano kesi za mauaji ili tu kumkomoa mshtakiwa. Tunaomba Waziri afuatilie jambo hili kwa makini ili wananchi wetu watendewe haki katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii na nina itakia Wizara utekelezaji mzuri wa Bajeti yake.

MHE. LEPHY B. GEMBE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utagusia hasa suala la ulinzi na usalama katika Wilaya yangu ya Mpanda.

Wilaya yetu ya Mpanda ni Wilaya inayopakana na nchi jirani, nchi ambazo kwa kweli zimekuwa katika matatizo makubwa ya vita za kudumu hivyo kusababisha kuwa na wimbi kubwa la wakimbizi kukimbilia nchini mwetu hususani Wilaya yetu ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, usalama wetu katika Wilaya yetu upo mashakani kwa sababu wakimbizi hawa wamezagaa sana hivyo udhibiti wao wa kukaa kwenye makazi yao ambayo ni Katumba, Mishamo kushindikana kuwadhhibiti kwa sababu makazi haya hayana wigo wa kuweza kuwafanya wasipenye sehemu yoyote na kutoka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii tunaioimba Serikali iweke mikakati mahususi ya kuongeza idadi ya Askari katika Wilaya yetu, hasa katika vituo vya Polisi vilivyopo mipakani mfano Karema, Ikola na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya barabara ya kuelekea katika maeneo hayo ni mbaya sana kutoka Makao Makuu, ni vyema Serikali ikaona uwezekano wa kutoa usafiri wa uhakika kwa ajili ya vituo hivyo tu vya mipakani. Bila kufanya hivyo kunapatokea tatizo mpaka waombe usafiri toka Makao Makuu Wilayani. Ni ombi muhimu hili la usafiri wa uhakika mwambao mwa Lake Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwa na matukio kadhaa ya utekaji nyara wa wananchi wetu kupelekwa kusikojulikana na Askari wa kutoka *DRC*. Suala la kuwa na *speed boat* kwa ajili ya Askari wetu ni muhimu sana kwa sababu inapatokea matukio hayo, Askari wetu wanakuwa hawana cha kufanya kwa sababu hawana *speed boat*. Ombi ni kwamba mwambao wapewe *speed boats* itakayosaidia ulinzi na usalama katika eneo lote la mwambao.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Karema, kumejengwa vituo viwili vya Polisi kwa nguvu za wananchi. Tunaomba Wizara isaidie vifaa vilivyobaki ili kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo na mahitaji hayo yalishatumwa tayari kwenye ofisi yenu. Ni imani yangu nitapata majibu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuna tetesi kuwa kuna baadhi ya bidhaa zinatengenezwa nchi jirani na kuingizwa humu bila kufuata utaratibu mfano sigara zinazobandikwa nembo ya *Sportsman*, zinakuwa zimeigilizwa tu hiyo inasababisha *Sportsman* zinazotengenezwa hapa nchini kuingiliwa na bidhaa ambayo imefanana na ambayo imekwepa kodi, kusababisha bidhaa inayotengenezwa nchini kuuzwa kidogo kuliko kiwango kilichotegemewa. Tunaomba chombo hiki huko mipakani kuwa macho na hujuma hii. Vile vile kufanya utafiti wa kutosha wa njia za panya.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia tena kuunga mkono hoja hii.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na wataalam wao wote kwa kuandaa hotuba nzuri kwenye bajeti hii ambayo imelenga zaidi kwenye utekelezaji na uendelezaji wa shughuli za Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuamua kwa makusudi kuliombea fedha za kutosha Jeshi la Polisi ili liweze kufanya shughuli zake za kawaida za ulinzi wa raia na mali zao katika nchi yetu hii ambalo hivi sasa limekuwa tatizo kubwa kwa kuongezeka wimbi la ujambazi kwa wale wachache ambao wamekuwa na tamaa ya kutaka utajiri wa haraka haraka kwa kuzulumu roho za watu wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, kuwapatia vifaa vya kutendea kazi Askari wetu ni suala muhimu sana kwani kwa kufanikisha utendaji bora ni kuwa na moyo wa utendaji bora na kusaidiwa na nyenzo za kufanyia kazi hapo unaweza kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuwajengea nyumba za kuishi Askari wetu utaweza kupunguza matatizo mengi kwani kukaa kwa pamoja kwa Maaskari wetu hiyo peke yake itapunguza Askari kuchanganyika sana na raia kwani humu wanamoishi hao wenye nyumba wao ni miongoni mwa watu wenye tabia mbaya lakini Askari anawawa pindipo atamchukulia hatua za kisheria kesho atakaa wapi na huyu aliyemfanyia hayo ndiye tajiri wake.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha hapa Bungeni kupewa haki ya kumiliki *Diplomatic Passport* kwa mume au mke wa Mheshimiwa Mbunge na kukubaliwa. La kushangaza maamuzi yale kumbe yaliishia humu humu ndani ya Bunge lako Tukufu kwani hadi hii leo ukifika kwenye Ofisi za Uhamiaji basi wanajibu kuwa wao hawaelewi lolote kuhusu hilo kwa hiyo tunachokipata hivi sasa ni usumbufu tu. Tungependa kuelewa sheria ile iliishia kwenye debe la taka au kwenye jaa ili tujue mahali pa kwenda kuiokota na kuileta tena hapa Bungeni kwa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kukiri kwa wazi kabisa ka upungufu wa Askari katika Jeshi la Polisi na kutaka kuajiri Askari wasiopungua 2000 ambao wataongeza nguvu ya utendaji katika Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, Waziri amethibitisha kuwa kwa kuondoa msongamano ndani ya Magereza wanategemea kuanza kuitumia sheria mpya ya *Parole* ambayo itaondoa kwa kiasi kikubwa msongamano ndani ya Magereza kwa wale ambao watatimiza masharti watu wasiopungua 1500 hii ni faraja.

Mheshimiwa Spika, nimefarajika sana kusikia kuwa kazi ya kuwarejesha kwao wakimbizi wote wa Rwanda imekamilika kwa kuwarejesha kwao wote hiki ni kitendo chema kabisa kwani watu wa Rwanda kuendelea kuishi hapa Tanzania ni kuongeza uhalifu wa ujambazi ambao ni tishio kwetu kwa raia na mali zao. Kwa hiyo, kwa kulifanikisha hilo, napenda kutumia nafasi hii kwa kuipongeza Serikali kwa kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda kutoa salamu zangu za rambirambi kwa ndugu Polisi waliouwawa kwa kushambuliwa bila ya kujua wakati wakiwa katika doria zao za kawaida. Mungu azilaze roho zao pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kazi nzuri ya kulinda amani nchini. Hongera sana. pia Mawaziri hawa kwa kushirikiana na watendaji

wao kwa kuandaa hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri wa dhamira ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya kuondoa kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Napongeza Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa hivi sasa ya kukabiliana na ujambazi nchini. Lakini kuna sehemu imejitokeza kuwa patrol za usiku hazifanywi na Polisi mpaka wananchi wa Kata wachangie fedha kwa ajili ya ulinzi huo wa usiku. Sasa naomba kufafanuliwa endapo huu ni utaratibu halali au inategemea tu matashi ya mahali husika?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni jinsi Askari wa Barabarani (*Traffic Police*) wanavyojitahidi kufanya kazi nzuri lakini wachche bado wana tabia ya kutaka chochote kwa Madreva wa magari ya mizigo, abiria na kadhalika hata kama magari husika hayana tatizo lolote. Kwa msingi huo, inakuwa ni kero kwa wasafiri na wasafirishaji. Wakati mwingine Askari hawa huwaachilia wakosaji baada ya kupea chochote na wakosefu hao. Nashauri kuwa yafaa Wizara iangalie jinsi ya kuongeza maslahi ya Polisi kwa ujumla ili kuwasaidia waweze kufanya kazi ya kulinda amani na haki za raia bila vishawishi vya rushwa ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya haya, napenda kuzungumzia umuhimu wa kuwa na nyenzo za kazi za kisasa kwa Jeshi la Polisi ili liweze kukabiliana na matukio ya ujambazi, kwa sababu wananchi wanapotoa taarifa kuhusu matukio ya jinsi hiyo, Askari wanaweza kuchukua muda au kutofika kabisa kwenye tukio kwa ukosefu wa usafiri na kadhalika. Hivyo kwa vile katika bajeti hii 2003/2004 kuna ongezeko la fedha, nashauri Vituo vya Polisi nchini vipewe magari ya kutosha ili kero hii ya raia kukosa msaada wa Polisi unapohitajika iishe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo imegusa Idara zote za Wizara kwa uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Mbunge wa Tabora Mjini, nimefarijika kusikia juhudi za Serikali ya CCM katika mambo yafuatayo:-

- Ukurasa wa 14 Operesheni za Jeshi la Polisi Tabora tarehe 18 Aprili, 2003 mpaka tarehe 4 Mei, 2003.
- Ukurasa wa 19 na 21 Ujenzi wa jengo la *RPC* Mkoa wa Tabora katika mwaka 2003/2004.
- Ukurasa wa 25 Ukarabati na uboreshaji wa Gereza la Uyui

- Ukurasa wa 29 Ununuzi wa nyumba kwa ajili ya Ofisi na makazi ya watumishi katika Mkoa wa Tabora wa Idara ya Uhamiaji. Naipongeza sana Serikali kwa juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la ujambazi limekuwa sugu nchini kwetu. Katika Jimbo langu la Tabora Mjini wananchi wanaishi kwa hofu. Haipiti wiki bila kusikia tukio la ujambazi. Tukio la kusikitisha sana kwa wakazi wa Jimbo langu lilitokea mwaka huu, ni mauaji ya Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Kanyenye, Mheshimiwa Ibrahim Daudi Mluloh. Wananchi wa Manispaa ya Tabora wangependa kujua matokeo ya uchunguzi wa Polisi ili wawe na uhakika wa usalama wao. Nitafurahi kama Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akimaliza maelezo ya hoja yake atueleze Polisi wamefikia wapi katika uchunguzi wao.

Mheshimiwa Spika, ujambazi unaofanywa nchini mwetu, unafanywa kwanza kwa kutumia silaha kutoka nchi jirani na kwa kiasi kikubwa wahusika wanatoka nchi za jirani. Kwa hiyo basi, naiomba Serikali ianzishe operesheni maalum mipakani kwetu ili kupunguza kwa kiwango kikubwa udhalimu huu. Majambazi tuyasake kila mahali, majumbani kwetu, nyumba za kulala wageni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako natoa rai kwa wananchi wote wapenda amani na usalama, wasaidie vyombo vya dola katika kuwafichua majambazi maana tunawajua wahalifu hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Magereza, juhudi kubwa na za makusudi zifanywe ili kupunguza misongamano katika Magereza yetu kwa kutumia sheria ambazo Bunge lako Tukufu limeishapitisha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu ugaidi. Ugaidi ni tishio siyo tu kwa maisha yetu na lakini linatishia maisha yetu na uchumi wetu kwa ujumla. Kwa hiyo basi, tumpige vita kwa nguvu zetu zote. Katika suala hili tuwape mafunzo wananchi wetu ili waweze kuwatambua magaidi mapema na kupeleka taarifa katika vyombo vya Dola.

Mheshimiwa Spika, wapiganaji wetu wa vyombo vya dola katika Wizara hii wanaishi katika makazi duni sana. naiomba Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa nyumba zao ili nao waweze kufanya kazi kwa kuridhika ikiwa ni pamoja na kuangalia maslahi yao kwa huruma. Wapiganaji wetu hawa wanakaa kwa muda mrefu bila kupandishwa vyeo. Napenda tena kusema kuwa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MOHAMED A. ABULAZIZ: Mheshimiwa Spika, kwanza, Jeshi la Polisi lina kazi ngumu na ya hatari kwa kupambana na wahalifu ambao wote wana silaha. Kupambana na jambazi ni kazi ya kubahatisha kama utarudi ukiwa mzima. Nini mipango ya Serikali kutoa msaada wa kifuta machozi cha ukweli na kinachofanana na maisha ya mtu badala ya kutegemea tu huruma na ubinadamu wa *IGP*? Sote tunahitaji usalama lakini ni kwa kiwango gani tunajali maisha yao?

Mheshimiwa Spika, pili, hali ya nyumba za Askari ni mbaya, Serikali iwaondolee aibu Askari hao kwa kulazwa kwenye mabwalo na katika nyumba ambazo zilikuwa maalum kwa ajili ya mbwa. Hivi ni Polisi wa wapi wanaolala katika mazingira mabovu kama Polisi wa Tanzania? Ninaomba maelezo ya mipango ya kweli ya Serikali ya kupunguza tatizo la nyumba kwa Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara, Bunge na wananchi kwa pamoja tunao wajibu wa kupongeza kazi nuri inayofanywa na Polisi katika mazingira magumu badala ya kusubiri makosa nakutoa lawama ambazo zinakatisha tamaa Askari.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu Uhamiaji, naomba Wizara inipe maelezo ni sababu gani za msingi zinazofanya Idara ya Uhamiaji isipewe *Vote* yake kama ilivyo taasisi nyingi ndogo kama *Low Reform Commission*, Tume ya Utumishi Serikali za Mitaa na Tume ya Maadili ya Viongozi. Naomba maelezo katika Kamati ya Bunge zima, endapo sitapata maelezo ya kutosha kutoka kwa Waziri wakati anajibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza Jeshi la Polisi kwa jinsi liliyofanya kazi kipindi chote cha uchaguzi mdogo Pemba hali iliyopelekea uchaguzi uende katika hali ya haki, huru na usalama. Kifungu cha Nane, ukurasa wa nne, Wizara iangalie kwa undani zaidi udhaifu wa huduma za Zimamoto Kisiwani Pemba na hasa kwenye Kiwanja cha Ndege cha Karume.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18, ukurasa wa sita, kuna haja ya kuangalia kwa makini suala zima la Sheria ya Ugaidi kwani sheria hii inaonekana zaidi kubana upande mmoja wa dini. Kuepusha hili ni vyema Jeshi la Polisi likwa makini katika kutekeleza sheria hii ili isije ikaleta mgongano katika jamii.

Kifungu cha 24 ukurasa wa 9, kwa kuwa wananchi wengi wanaonekana kuwasaidia Polisi katika kutoa taarifa za ujambazi na uhalifu ambazo hupelekea ama kukamatwa mali iliyoporwa au kukamata wahalifu ni vyema Serikali iweke utaratibu wa kuwapa ahsante yaani chochote hawa wananchi ili iwe kivutio kwa wengine kuweza kutoa taarifa kama hizi.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 28, ukurasa wa 9, naipongeza Serikali kwa kuwafikisha Mahakamani wale wote waliohusika katika vifo vya mahabusu Mbarali. Lakini hili tu halitoshi ni vyema basi Serikali ikafikiria kuwalipa fidia familia za wale wote waliofariki katika tukio hili la kusikitisha. Kifungu cha 40, ukurasa wa 15, naipongeza Wizara kwa kufanya semina mbalimbali kuhusu haki za binadamu na utawala bora hasa kwa upande wa Tanzania Bara. Naishauri Wizara pia ifanye semina kama hizi kwa upande wa Unguja na Pemba na iwashirikishe viongozi kama Wabunge na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 46, ukurasa wa 18, naishauri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ifanye utaratibu wa kujenga Kituo kidogo cha Afya katika nyumba za Polisi zilizopo Mfikiwa ili pia kiweze kuwasaidia huduma za awali za afya wananchi wanaoishi jirani na kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 53(xii), ukurasa wa 21, tunaishauri Wizara kuangalia upya utaratibu wa kuajiri Askari wapya ili haki itendeke bila kuangalia mwombaji ni mtu wa wapi au wa chama gani. Tukifanya uadilifu katika kuajiri ni wazi wananchi watajenga imani kwa Jeshi la Polisi na Wizara kwa ujumla.

MHE. JANETH E. MASHELE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba yake nzuri. Pia napenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa jitihada zake wanazozifanya kwa kuwakamata majambazi na wahalifu mbalimbali. Pamoja na hayo, napenda kuliomba Jeshi hilo waongeze juhudi kudhibiti wimbi la majambazi na wahalifu mbalimbali linaloongezeka siku hadi siku. Vile vile napenda kuipongeza Serikali kwa kuiongezea bajeti Wizara ya Mambo ya Ndani hasa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la ukarabati wa majengo muhimu ya Polisi kwa mfano nyumba za Polisi kwani Polisi wanaishi katika mazingira magumu ukiangalia nyumba zao wanazoishi kwa kweli nyumba zao zimechakaa hazifai ukizingatia kwamba Polisi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunacho Chuo kimoja cha Polisi ambacho kipo Moshi. Chuo hicho ndicho pekee cha mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi hapa nchini na kinachopokea wanachuo kutoka nchi za nje. Aidha, bila Chuo hicho tusingefika hapa tulipo.

Hivyo naiomba Serikali iangalie mpango thabiti wa kukarabati Chuo hicho kwani kinatia aibu kwa jinsi kilivyochakaa. Suala lingine nililotaka kuchangia ni juu ya Askari ambao wanaishi uraiani. Napenda kushauri Wizara wafanye mpango na wahakikishe Polisi wanaishi kwenye makambi badala ya kuishi uraiani ili kudumisha nidhamu za Askari wetu katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la wizi wa magari. Naomba Serikali iangalie kwa makini suala hilo kwani kumekuwa na ongezeko la wizi wa magari na uingizaji wa magari ya wizi kiholela. Hivyo tushirikiane na wenzetu wa nchi za jirani kuyakamata magari hayo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia suala la uraia. Serikali iweke pango maalum wa kudumu kuwataka wasio raia hapa nchini kujitokea Serikali iangalie upya utoaji wa uraia wa Tanzania. Vile vile Serikali iwe makini katika kutoa vibali vya kufanya kazi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali iendelee na juhudi za kushawishi Jumuiya ya Kimataifa ili wakimbizi kutoka Burundi na Kongo watengewe maeneo ndani ya nchi zao badala ya kuishi kwetu.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Vile vile naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Wizara yake kwa ujumla kwa jinsi wanavyojishughulisha na wimbi la ujambazi na uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza kwa kutoa ushauri ili nchi yetu iendelee kuwa na amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ujambazi Mikoa ya mipakani, napendekeza:-

- (i) Kuwepo na Askari wa doria katika pori la Biharamulo ambapo ni wazi majambazi wanajificha na wamesababisha uporaji wa magari na kusababisha vifo.
- (ii) Ifanyike *ambush* kwa kutumia Askari Jeshi kuzungukia sehemu zenye ujambazi. Hii ifanyike mara kwa mara.
- (iii) Kuwepo na Vituo vya Polisi angalau katika kila kijiji cha wavuvi mwambao mwa Ziwa Tanganyika na katika vituo hivi kuwepo ushirikiano wa Askari na Sungusungu ili kupanga mikakati ya ulinzi. Vituo hivi viwe na mawasiliano au ya simu au *radio call*.
- (iv) Wakimbizi wasitoke makambini na kamwe vibali visitolewe vya kuwaruhusu kwenda uraiani. Hakuna sababu ya wao kutoka kwani wanazo huduma makambini.
- (v) Magulio yawe ndani ya makambi, wananchi ndiyo waingie makambini na siyo wakimbizi kuwa uraiani.
- (vi) Iwepo misako ya mara kwa mara ndani ya makambi kuona kama hakuna wakimbizi wenye silaha.

Mheshimiwa Spika, pili, wahamiaji haramu, kuna wahamiaji haramu wengi hasa katika Mkoa wa Kigoma. Kwa kuwa tunapakana na nchi za Burundi na Kongo, wahamiaji hawa ni wengi. Naomba nipendekeze yafuatayo:-

- (i) Vitambulisho vya uraia vitolewe haraka iwezekanavyo.
- (ii) Kabla ya vitambulisho kutolewe basi vitambulisho vya muda na wahamiaji haramu waende makambini. Ili kuwatambua watu hawa, ufanyike msako au wapigiwe kura za maoni na kusiwepo na huruma katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tatu, madawa ya kulevya, madawa haya yamezagaa na wahusika wanajulikana. Naomba Polisi iwahusishe wananchi kuwafichua. Kuna sehemu

za kubadilishana biashara hii na sehemu za kuvutia hivyo kura za maoni na masanduku ya maoni kuwafichua wahusika yatumike.

Mheshimiwa Spika, nne, Zima Moto, vituo vya mafuta vimeongezeka katika mji wa Kigoma. Moto ukitokea, mji mzima utakuwa hatarini. Kwa kuwa gari ni moja, naomba huduma ya zima moto iongezewe vitendea kazi ili kuepukana na janga la moto. Vitendea kazi na huduma kwa Askari, kwa kuwa ujambazi umezidi Kigoma, naomba Polisi wawezeshwe kupambana. Hivyo kuwepo na magari imara, simu za mawasiliano, lakini vile vile maisha yao yaboreshwe. Nyumba zao zikarabatiwe ingawa zimepitwa na wakati vyumba ni vidogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Askari wajengewe nyumba zenye hadhi yao zilizopo hazifai kabisa. Itakumbukwa mwaka 2001 niliuliza swali la Askari Polisi Kigoma kulala katika vyumba vya bar na kwamba nyumba zao zilikuwa hazikarabatiwi kwa muda mrefu jibu ni kwamba Serikali ilikuwa imeanza kuzikarabati nyumba hizo jambo ambalo mpaka sasa hivi halijatimizwa. Je, ni lini ukarabati huu utatimizwa kwa nyumba za Polisi wa Mkoa mzima? naomba ukarabati uhusishe na *drainage system* nzima. Nyumba/vyumba vinanuka Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, naomba yote niliyoorodhesha yatiliwe maanani kwa ufanisi na usalama wa nchi yetu.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hotuba hii 100%.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa nne, unaelezea hali ya usalama nchini, usalama wetu hivi sasa inaonyesha kuchezeza sana na nchi za Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya ambapo majambazi walioibia Benki ya *CRDB* wametoka nchi hizo. Kwa hiyo, Serikali iwe makini sana.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa sita unaelezea juu ya ugaidi na kusema kuwa ugaidi umekuwa tishio kubwa la Kimataifa la amani na usalama katika nchi zote ulimwenguni. Kitu kikiwa ni tishio kubwa linahitajia kufanyiwa udhibiti wa hali ya juu sana. kwa hiyo, Serikali lazima ijenge nguvu kwa vyombo vyake kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, ukurasa 28, umeelezea Idara ya Uhamiaji. Ninaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuipa uwezo mkubwa sana wa vifaa na huduma nyingine Idara hi ambayo ni jicho kubwa na muhimu kwa usalama wa Taifa letu.

Ukurasa wa kumi, umeelezea juu ya tukio la Mbarali na kama utasoma maelezo ya tukio hilo utagundua kuwa tukio hilo lilitokea kwa:-

- Baadhi ya mahabusu walikufa kwa kukosa hewa safi.
- Uzembe uliofanywa na Maafisa na Askari Polisi waliokuwa na dhamana wakati wa tukio hilo.

- Pia ilibainika kuwepo mapungufu katika mazingira ya kazi.
- Lakini kubwa lililonipa kuelezea suala hili ni kuona kuwa mahabusu hawa waliwekwa baada ya kuharibika kwa gari la kusafirishwa mahabusu na kusababisha mahabusu hao kuwekwa katika chumba hicho kidogo cha mahabusu cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache niliyoyanukuu yanawatiaje hatiani Askari wa kawaida ambao inasemekana kuwa wapo ambao wamechukuliwa hatua na wengine kufungwa.

- Kwa usiku ule Askari hawa wangepanya nini?
- Kwa nini hili gari lililosafirisha mahabusu halikuwa na *escort* yoyote au *radio call*?

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kuwatoa Gerezani Askari hawa waliowafunga na kusaidia familia zao ikiwa ni pamoja na kusimamia masomo kwa watoto wao na kadhalika. Hili naliomba sana sana na kwa kweli Askari hawa wameonewa sana na wala Serikali haikuwatendea haki wala kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache ninamwomba sana sana Mheshimiwa Waziri na wahusika wote wa Wizara hii na Serikali kwa ujumla kusimamia kazi hii kubwa na ngumu kwa Taifa letu hili la Tanzania. Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante.

MHE. TEMBE K. NYABURI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na watendaji wote wa Wizara yake. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa kuzungumza Bungeni, ninapenda kuchangia kwa maandishi kuisitiza maombi yangu. Wakati nachangia kwa kuzungumza Bungeni katika hoja hii niliomba kuisitiza ombi la wananchi Wilayani Bunda kuwapo Ofisi ya Uhamiaji Wilayani pale. Uongozi wa Wilaya uko tayari kutoa chumba sehemu ya jengo la Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya kuanzisha Ofisi hii ambayo itasaidia sana wananchi kwa mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri afikirie suala hili kwa karibu zaidi tusaidiwe Ofisi ya Uhamiaji kumweka Afisa wake Wilayani Bunda. Kutokana na jioografia ya Wilaya ilivyo na shughuli za kiuchumi tunayo mambo mengi mfano:-

- (1) Tunavyo viwanda (*ginneries*) vya pamba vipatavyo vitano kati ya hivyo vitatu vinafanya kazi na kimoja kinamilikiwa na wageni kile cha *Virian T-Ltd* ukiacha kile cha *Bulamba S&C* na kile cha *Mara Lint Ltd*.

(2) Bunda iko Mkoa wa mpakani na nchi za Kenya/Uganda. Kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi hasa kutokana na uvuvi na uchimbaji madini kuna ongezeko kubwa la wahamiaji kutoka nchi za jirani.

(3) Pamoja na hayo itasaidia utoaji huduma kwa urahisi na nafuu kwa wananchi wengi ambao wanashughulikia vyeti vya kuzalisha watoto (*Birth Certificates*), *Passport* za Dharura kwa wasafiri wa magari ya abiria kupitia Kenya kwenda Arusha/Moshi na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba ombi hili liwe miongoni mwa yale yatakayofikiriwa na kupewa kipaumbele mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani kwa ushirikiano wako.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanazosimamia katika ulinzi wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili la Polisi sasa hivi wanafanya kazi nzuri sana, nawapongeza sana vijana wetu waliofanikisha zoezi la kuyaua majambazi katika maeneo ya karibu na Dodoma yaliyotokea Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Polisi ni wito hivyo naomba sana Serikali hawa Polisi walipwe haki zao wanazostahili wasizungushwe, itawakatisha tamaa sana wakati tunawategemea sana katika ulinzi wa wananchi wetu.

Naiomba Serikali kuanzisha mafunzo ya mara kwa mara kwa Askari wetu ili nao wawe na haki katika kujiendeleza kielimu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kusimamia zoezi la kurudisha wakimbizi makwao. Zoezi hili lilikuwa ni gumu sana nchi nyingine ziliona wanafanya ukatili lakini hawakuona athari zilizokuwa zikitokea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, wakimbizi wametuletea silaha, ujambazi, uharibifu wa aina mbalimbali nchini hapa. Hivyo naungana na Serikali kwa uamuzi mzuri huu wa kila mtu abebe mzigo wake mwenyewe. Hongera sana kwa kufanikisha zoezi hili.

Naleta ombi kwa Serikali ilione hii Askari wasikae maeneo ya kazi kwa muda mrefu, atazoeleka sana na heshima itapungua kwa kazi zao. Hivyo uwekwe muda maalum wa kukaa katika kituo kimoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hotuba hii mia kwa mia, fedha zote wapewe na baadaye waongezwe nyingine ili wakidhi haja ya matumizi yao.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri iliyojaa ukweli na uwazi. Naungana

nanyi katika kutoa pole kwa familia za Marehemu mashujaa wetu, wale Askari watatu waliouawa wakiwa kazini. Mungu azilaze roho zao peponi, *amin*.

Mheshimiwa Spika, nalishukuru sana Jeshi la Polisi kwa kutupatia *Landrover reconditioned* kwenye Tarafa yetu ya Kaliua, Tarafa ambayo mambo ya mauaji, ujambazi na ujangili yameshamiri. Tarafa ambayo ni kubwa sana kieneo na ina wanyama wengi wakali. Kwa kweli tulihitaji gari hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya gari ilipofika ilikwama Wilayani kwa muda mrefu sana, matumizi yake yakawa ya kupita uwezo wa gari. Kwa hiyo, gari hili sasa iko kwenye mawe baada ya muda mfupi sana engine mbovu, mipira imekwisha yote. Tunaomba fedha za kutosha ili ikarabatiwe upya.

Mheshimiwa Spika, gari ilipoletwa hatukutengewa fedha za *petrol*, tunaomba tuwe tunapatiwa fedha za *petrol*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. KARIM SAID OTHMAN: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo. Pia nampongeza kwa dhati kabisa Naibu Waziri wake pamoja na wataalam wake wote.

Baada ya pongezi, naomba kutoa mchango wangu kwa minajili ya kuboresha na kutoa mapendekezo yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu *passport*, kupata *passport* katika nchi hii ni kazi kubwa sana. sijui ni utaratibu wa Wizara au ni vitimbi vya Maafisa wa Uhamiaji? Kupata *passport* ni haki ya kila raia kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, urasimu wa kupata *passport* ni mkubwa sana na gharama yake ni karibu shilingi laki mbili au zaidi. Inawezekana Waziri hili huna habari nalo lakini napendekeza ufanye utafiti.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe taarifa rasmi kwa watendaji wake kupitia Bunge hili kwamba kila mwenye kutaka *passport* apewe bila usumbufu na akizungushwa aje kwake.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inasomesha vijana lakini uwezo wa kuwaajiri wote haina je, tukiwapatia *passport* vijana badala ya kukaa vijiwani kula unga watapata nafasi ya kusafiri kwenda nchi za nje kutafuta kazi na watakachopata wataleta nyumbani. Mfano hai ni India ambapo katika nchi hii mara ukifikia umri wa miaka 18 unapewa *passport* yako hata kama hujaomba. Vijana hao husambaa duniani kote kufanya kazi kwa mkataba maalum (wafanyakazi nafuu) mapato wanayopata vijana hawa huwa wanapeleka asilimia ndogo Serikalini kwao na bakaa hujenga nyumba zao kwao na

mambo mengine ili kuipunguzia mzigo Serikali yao. Wahindi wameenea duniani kote hasa hasa Falme za Kiarabu. Kwa nini na sisi vijana wetu wasipewe fursa kama hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni uajiri wa Askari wako wapya lina athari ya rushwa na upendeleo. Kwa sababu ukitokea uajiri wa Askari kwa kawaida hugaiwa nafasi kwa bara na visiwani lakini Maafisa wengi wa Jeshi hili Zanzibar ni kutoka bara hutumia ukubwa wao kuajiri ndugu zao kutoka bara kwa mgao wa Zanzibar. Huko Zanzibar kwa hizo nafasi zinazobaki kuna Upemba na Uunguja, kama hili Waziri halielewi afanye utafiti. Katika uajiri huu unaofuata tutafuatilia kwa karibu sana na tutakuletea taarifa ya ugavi utakavyokuwa.

Kwa sasa naona sharti la kuajiri Askari ambao ni warefu limeondoka? Askari wengi wanaojiriwa ni wafupi sana hawapendezi katika kazi hii, Askari ni lazima atishe kwa ukubwa na sio kibafuti.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu wana kazi ngumu sana ya kutulinda sisi na mali zetu hivyo kuna haja ya kuwahurumia kwa kuwapa mishahara mizuri, kupata mikopo ya kujenga nyumba, kupatiwa *save* ya kutosha, kupatiwa likizo na usafiri pia kuwekewa bima ya maisha.

Mheshimiwa Spika, waendesha kesi Mahakamani washirikiane na Mahakimu kuhakikisha kesi zinamalizika haraka iwezekanavyo ili kuondoa msongamano wa watuhumiwa Magerezani. Pia watuhumiwa ambao huwekwa kizuizini kwa upelelezi wasiadhibiwe hata kidogo wapewe fursa ya kufanya kila kitu ambacho walikuwa wakifanya walipokuwa nje, sigara, pombe, redio, magazeti, *TV*, waruhisiwe, isipokuwa lile ambalo akifanya litavuruga upelelezi au ushahidi.

Mheshimiwa Spika, pia upelelezi uende haraka kama kuna la kujibu Mahakamani ajibu na hukumu itolewe vinginevyo ni kuvunja haki za kibinadamu kumwadhibu mtu bila kuwa na uhakika kwamba amefanya kosa ni kukiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya uraia ni muhimu sana lakini haielekei kwamba Serikali ina mpango wa kweli na haraka wa kuvitayarisha. Kwa nchi za wenzetu mara mtoto akizaliwa anapewa kitambulisho cha rangi ya kijani kuonesha kwamba yeye ni (alwatan) raia na kitambulisho rangi ya manjano kama mtu ni mgeni (mkaazi) si raia. Kama kuna haja kweli ya kulinda nchi yetu na mipaka yake kwa wanaoingia basi ni vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, madawa ya kulevyo yanauzwa nchini hivi sasa kama njugu. Madawa haya yanaingia nchini kupitia milango mitatu, bandarini, mipakani na viwanja vya ndege. Milango hii yote ina walinzi wa kutosha inakuwaje madawa yafike mitaani na yazagae namna hii? Watumiaji wa madawa haya ni vijana na ndio nguvu kazi ya Taifa, baada ya miaka mitano ijayo vijana wote ni vichaa. Namwomba Mheshimiwa Waziri akae chini afikirie lakini wanaongiza madawa wanajulikana kwa kuti. Nakukumbusha UKIMWI unashambulia vijana, madawa ya kulevyo yanashambulia vijana je, Taifa hili atalijenga nani?

MHE. OMAR JUMA OMAR: Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni chombo tunachokitegemea sana kwa ajili ya ulinzi pamoja na usalama wa raia. Pia Polisi hutumia jina lao vibaya kwa kunyanyasa raia na kukosa imani kati ya raia na Polisi. Ile vile Polisi kuingia ndani ya nyumba na kupekua kwa visingizio tu vya kutafuta vitu ambavyo eti vinataka kuuzwa kwa njia ya magendo kama vile karafuu wakati ikiwa ni katikati ya mavuno na kuchukua mali hizo kwa nguvu na hatimaye mtu huyo kukoseshwa mali yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Magereza hali yake ni mbaya kwa Magereza yetu kwani kuna mrundikano wa mahabusu katika Magereza hayo hadi kupelekea watu kufa ndani ya mikono ya Askari au mahabusu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Polisi linajaribu kuendeleza rushwa badala ya kuondoa hiyo rushwa na hii inatokana na ugumu wa maisha hata kupelekea Askari hao kujiingiza ndani ya biashara ambazo huwasaidia angalau kuboresha maisha yao. Hata hivyo Askari *Traffic* husumbua sana Madreva na yule ambaye hata kubali kuwapatia angalau soda anaweza kupelekwa Mahakamani kwa kosa tu la kupangiwa au kusingiziwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muafaka ndio kitu pekee ambacho kimetuletea amani na utulivu katika nchi yetu kwani Askari Polisi wameelimishwa kutoegemea upande wowote wa Chama bali wao kazi yao ni kulinda wananchi na mali zao kwa jumla na ndio uliopelekea kufanyika kwa uchaguzi mdogo ambao ulikuwa huru na wenye utulivu chini ya usimamizi wa Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za Askari suala hili naomba liangaliwe vizuri bila ya kuangalia huyu ni kutoka Chama gani. Ieleweke kwamba kila anayetaka kuajiriwa ni Mtanzania na anazo sifa ambazo zinafaa kuajiriwa kwani kuajiri katika hali ya kubagua itaturudisha katika hali ya matatizo ambayo hatupendi yatokee.

Kuhusu suala la ujambazi bado ni tatizo sugu. Kwa hiyo, ipo haja ya Watanzania kuwa na vitambulisho ili kuweza kumtambua yule ambaye si Mtanzania ambaye ameingia nchini kwa ajili ya kufanya hujuma

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Maafisa Wakuu wa Polisi, Magereza, Uhamiaji na Asasi zote zilizo chini ya Wizara kwa Bajeti na mpango mzuri sana uliowasilishwa hapa Bungeni leo asubuhi.

Mwezi February, 2001, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nikamwomba kuwa Wizara iwasaidie wananchi wa kijiji cha Lang'ata Bora; eneo la nyumba ya Mungu kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi (*Lang'ata Bora Police Post*).

Mheshimiwa Spika, wakati huo wananchi walikuwa wamejenga ukuta na kutenga vyumba vinavyohitajika. Wamepanua, wameweka mihimili na kupiga ripu. Kilichobakia ni kuweka *ceiling board*, sakafu na milango na kupiga rangi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alinijibu kuwa Wizara inawapongeza sana wananchi wa Lang'ata Bora kwa kujitolea na kuwa Serikali itatoa msaada ulioombwa mara moja. nikafurahi sana na kuwaarifu wananchi wa Lang'ata Bora kuwa msaada utafika haraka. Tuliomba shilingi laki nane. Hadi mwezi Aprili, 2002, hatukupata msaada huo. Nikamwandikia Waziri kumkumbusha akanijibu kuwa msaada utafika kabla ya *June, 2002* lakini hadi leo msaada huo bado haujafika.

Mheshimiwa Spika, ninayo shauku kubwa ya kujua ahadi hii itatekelezwa lini? Ahadi hii imegeuka kuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa kituo nilichokitaja, wananchi wa Mwanga wana miradi mingine mitatu ya ujenzi wa *Police Posts*.

(i) Kituo cha Polisi - Kisangara. Ukuta tayari. *RPC Kilimanjaro* aliahidi mabati 70 tangu mwaka 2000 hadi leo ahadi hiyo haijatekelezwa. Sasa niwaambie nini wananchi?

(ii) Kituo cha Polisi, Msangeni - Ugweno. Kituo hiki kimekamilika kwa 95% (*about 95% complete*). Imebakia mifuko 50 ya saruji na rangi ya kupaka. Pia tunaomba kifunguliwe.

(iii) Kituo cha Polisi Mangio - Ugweno. Ukuta tayari.

Mheshimiwa Spika, kumaliza Vituo vyote nilivyovitaja, kuna hitajika vifaa vya thamani ya T.Shs.2.8 milioni. Naomba Wizara itupatie msaada huu.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hasa Jeshi la Polisi kwa dhamira na mikakati yake ya kupambana na ujambazi hapa nchini kwa kiwango cha kujitoka mhanga kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, unyang'anyi wa kutumia silaha umeongezeka kutoka matukio 977 mwaka 2000 hadi 1237 mwaka 2002. Pamoja na hayo, uhalifu mkubwa unaohusisha raia kutoka nje ya nchi umeanza kushamiri hapa nchini hali inayoonyesha kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika Idara ya Uhamiaji na pia ndani ya Jeshi lenyewe.

Mheshimiwa Spika, mifano ifuatayo inajieleza:-

(i) Wizi wa fedha Benki ya *CRDB* tarehe 15/11/2002, wizi ambao umehusisha watuhumiwa kutoka nchi jirani ya Kenya. Je, taratibu zote zinaweza kuthibitisha kwamba watuhumiwa hao walifuata taratibu zote za kuingia na kuishi Tanzania kihalali kabla ya tukio hilo la wizi? Je, baada ya tukio la wizi watuhumiwa wote waliwezaje kuvuka mipaka kurudi Kenya wakiwa na fedha hizo hata bila kutiliwa mashaka? Katika

mazingira kama haya ipo haja ya kuimarisha Idara ya Uhamiaji na Polisi wa Upelelezi katika maeneo ya mipakani.

(ii) Mauaji makubwa ya Polisi yaliyotokea Kawe Dar es Salaam tarehe 25/5/2003. Mauaji haya pia yanaonyesha kuwa watuhumiwa ni wageni kutoka nchi jirani ambayo Mheshimiwa Waziri hakuitaja.

Mheshimiwa Spika, kwa matukio hayo mawili, ni lazima tujiulize ni kwa nini wageni toka nje ya Tanzania wanapata mwanja wa kirahisi wa kufanya ujambazi na mauaji ya raia na hata walenzi wetu wa Taifa (Askari)? Ni lazima tukubali kwamba yapo mazingira ya rushwa na uzembe ndani ya Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji ambapo watendaji wachache wanaweza kuangamiza raia na watendaji wenzao wema kwa tamaa zao binafsi. Ni lazima tujue vema jambo hili na tuwachuje wale wote walio miongoni mwetu ambao wanatusaliti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya makazi yanayokaliwa na wageni mfano eneo la Sinza, Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam ni eneo la hatari. Eneo hili lina wageni wengi toka nje ya nchi ambao wanamiliki nyumba, aidha kwa kupata viwanja na kujenga au kwa kununua. Yapo pia maeneo mengine ambapo wageni wengi wanaishi kama Watanzania halali.

Mheshimiwa Spika, katika hali iliyojitokeza ipo haja ya kufanya operesheni maalum katika maeneo hayo ili kubaini kuwepo au kutokuwepo kwa wageni kuishi na kumiliki nyumba na biashara nchini isivyoo halali. Msako huo uhusishe Idara ya Polisi na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara ya Mambo ya Ndani inachelewa sana kuunga mkono jitihada za wananchi katika kusaidia miradi ya Jeshi la Polisi. Mifano ifuatayo inajieleza kwa Wilaya ya Muheza:-

(i) Msaada ya ujenzi wa chumba cha kuhifadhi silaha Kituo cha Polisi Amani. Kampuni ya Chai ya *EUTCO Amani*, Wilaya ya Muheza ilisaidia kujenga chumba cha kuhifadhi silaha Kituoni hapo. Hadi sasa chumba hicho hakitumiki licha ya kwamba hilo ndilo lilikuwa tatizo la Kituo hicho. Kampuni hii imekuwa tayari hata kusaidia ukarabati wa nyumba za Askari Kituo hapo ili kuongeza idadi ya Askari lakini wanaona itakuwa hivyo hivyo hakuna litakalofanyika hata msaada ukitolewa. Hii inakatisha tamaa.

(ii) Kucheleweshwa kufungua Kituo Kidogo cha Polisi eneo la Mkanyageni Kata ya Ngomeni. Ucheleweshaji ulitokana na ujenzi wa Chuo. Hata hivyo Kituo kikaachwa kwa zaidi ya mwaka mmoja. Wizara haikuona haja ya kuweka msaada wake mapema kuunga mkono nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara iratibu miradi ya wananchi na kupanga programu za misaada mapema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA: Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii ya kutoa mchango wangu walau mdogo kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Omar R. Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuchaguliwa kuongoza Wizara hii nyeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni moyo kwa Jamhuri kwa pande zote mbili za Muungano, pia kwa mtiririko mzuri na kulenga moja kwa moja na dhamira iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nimpe hongera msaidizi wake (Mhe. Capt. John Chiligati), Naibu Waziri kwa umahiri na umakini wake wa kujibu maswali na hoja za Wabunge. Mimi kabla ya kuingia katika nyumba hii nimekuwa kwa siku nyingi nikifuatilia kwa karibu kupitia vyombo vya habari shughuli za Bunge, ahsanteni na endeleeni na utaratibu huo mzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Jeshi la Polisi kufanya shughuli zake bila ya kupendelea upande wowote wala kushabikia Vyama. Kwa kiwango kikubwa imani ya wananchi imerudi kwa kuona kwamba walinzi wa usalama wa nchi na mali zao wanatimiza wajibu wao kama ilivyo katika maadili ya kazi yao hususani ni katika sehemu ya upande wa Zanzibar ambapo mimi natokea. Askari wanapotimiza wajibu wao kama inavyotakiwa wananchi wanakuwa wepesi kushirikiana na Vyombo vyao vya Dola.

Mheshimiwa Spika, mfano ulio dhahiri, ni jinsi Askari walivyotoa ushirikiano wa kutosha katika hatua zote za uchaguzi mdogo tarehe 18/5/2003 huko Kisiwani Pemba kuanzia hatua ya uandikishaji, upigaji kura na utoaji wa matokeo lakini hata katika hatua ya kampeni, mambo yote yalikwenda shwari kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ushauri katika hili, Mheshimiwa Waziri aendeleze utamaduni huu mzuri kwa kuwa karibu sana na watendaji na watekelezaji wake ili wadumishe amani iliyopo, kwani hivi karibuni Zanzibar kutaanzishwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa yale Majimbo ambayo hayakuwa na chaguzi ndogo.

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika ajira ya Askari Polisi. Hapa bado pana tatizo hususani kwa Pemba. Zinapokuja nafasi za ajira pengine kwa nia nzuri na safi kutoka Makao Makuu lakini zinapofika Mikoani na Wilayani mara nyingine Masheha hushirikishwa, Masheha nao vigezo vyao vikubwa ni kwa watu wenye itikadi yake tu ndio wenye haki ya kupata ajira hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika hilo, nashauri Wizara kwa kupitia Mheshimiwa Waziri inapofika wakati wa kuajiri basi waweke vigezo maalum ambapo mimi naamini vinawekwa lakini visimamiwe ili sifa inayotakiwa ipatikane kwa uwazi na wenye haki wapatikane bila ya kupekua anatokana na watu wa itikadi gani ya siasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madawa ya kulevya, uingizwaji wake, usambazaji wake na uuzaji wake, unatokea wakati walinzi wetu wakiwa humu humu nchini na pengine pale wanapopitia mfano uwanja wa ndege, bandarini, barabarani na mipakani wanakuwepo walinzi na vifaa vya kuyatambua madawa hayo. Kwa upande mwingine wafanyabiashara au wale wanaowatuma pia ni watu ambao wanatajwa kwa njia yoyote au wanatiliwa shaka hapo ndio mahali pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, *process* yote hiyo niliyoitaja ndiyo inayotia shaka ya kutokuwa makini kwa walinzi wetu kuweza kupambana na janga hili. Kwa hili pia nashauri itumike njia ya kura ya siri hususani kwa wale ambao ni waagizaji na wale wauzaji ili watambuliwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu ukamilishaji wa kupatikana kwa ushahidi Mahakamani, watu husota mahabusu siku nenda rudi kwa kile kinachoambiwa ushahidi haujakamilika na mara nyingine haupo hata mdogo. Nashauri Mheshimiwa Waziri aandae utaratibu mzuri wa upepelezi kwa kiwango kikubwa ndio mtuhumiwa ashikwe au apelekwe Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Mheshimiwa Waziri atekeleze haya ili kupatikane ufanisi unaokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. MARIAM SALUM MFAKI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu na wataalam kwa kuandaa hotuba hii makini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu hali ya usalama nchini, hali ya usalama katika nchi yetu imekuwa ya wasiwasi kufuatia ujambazi unaofanywa na kundi la watu wachache kabisa na matokeo yake imefikia hata majambazi kuwaua Askari wetu. Naishauri Serikali kuandaa mazingira mazuri zaidi ili hata wakikutana na hali ya kustukizwa wawe na namna ya kujitetea. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha Askari kuuawa. Nawapa pole wazazi wa watoto hawa baya zaidi wameuawa na majambazi kutoka nje ya nchi maana yake ni kwamba hatuko makini katika kudhibiti watu wanaoingia nchini. Naishauri Serikali iwe na utaratibu wa kushirikiana na viongozi kama Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji ambao wanaweza kujua wageni wanaoingia kila siku na hiyo itasaidia kujua majambazi hao.

Mheshimiwa Spika, nchi za nje huwa wanakuwa waangalifu katika nchi zao lakini nchini kwetu kidogo hatuko makini. Sasa msingoje mpaka Askari wauawe ndio kazi kubwa ifanyike. Askari fanyeni kazi kwa juhudi zote kila siku.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu nyumba za Askari, nashauri Serikali ijitahidi kuwajengea nyumba katika eneo moja ili iwe rahisi kupatikana kwa urahisi. Vile vile Askari akiwa na nyumba akaiacha familia yake katika hali ya usalama atafanya kazi ya uhakika. Ni aibu Askari kuishi katika nyumba ambazo hazina hadhi. Ujenzi wa nyumba za Nzuguni umeishia wapi? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, tatu, nashauri mishahara ya Askari iongezwe, walipwe marupurupu yao na hasa Askari wa ngazi za chini maana hawa ndio wanaokimbizana na majambazi kila siku.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali iweke wazi upandaji wa vyeo kwani kuna baadhi ya Askari wamekaa zaidi ya miaka kumi kwenye Jeshi hawapandishwi vyeo.

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu dawa za kulevya. Ni jambo la kushangaza Askari wanawashughulikia zaidi vijana wanaotumia madawa ya kulevya. Naishauri Serikali kuwatafuta wale wanaowatuma vijana kwenda nje na kuwafanya wameze madawa na hata kutumia njia mbalimbali za kuingiza madawa, wakamatwe bila kuwaonea aibu. Bila kufanya hivyo madawa haya yakiendelea kuja watoto/vijana wengi wataharibika na kuharibu Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, sita, naomba Serikali iwachuje wanawake waliopo rumande na Mageeza kwa waliofungwa kwa makosa madogo madogo na iwaachilie au kuwapa vifungo vya nje ikizingatiwa mwanamke hana ujasiri wa kukimbia hasa wale wenye watoto.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali itoe motisha kwa Askari wanaofanya kazi nzuri hasa ile ya kupambana na majambazi.

Mheshimiwa Spika, nane, naomba Serikali iongeze usafiri katika Vituo vya Polisi na hasa magari yenye mwendo mkali ili yatumike kupambana na wahalifu ikiwa ni pamoja na vyombo vya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tisa, viongozi ndani ya Jeshi wawe na tabia ya kukutana na Askari wa vyeo vya chini na hata wale wasio na vyeo ili kusikiliza matatizo yao na ushauri wao na hayo yatafanya kujiona wanathaminiwa na viongozi au wakuu wao na hasa matatizo yao yakisikilizwa hata wakafarijiwa. Katika mahusiano ya utendaji wa kazi mzuri, madaraka yatumiwe kwa uangalifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, kuhusu kumaliza ujenzi wa Kituo cha Polisi Ikola. Mheshimiwa Waziri wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wako, mlikubali kimsingi kumaliza ujenzi wa kituo hiki tangu mwezi Aprili, 2003. Hadi ninatoka Mpanda mwezi wa sita kuja kuhudhuria kikao hiki, hakuna jitihada zozote ambazo zimeishafanywa na Wizara katika umaliziaji wa jengo hilo la polisi ambalo lilijengwa na wananchi wa Kata hiyo kwa msingi wa kujitolea muda mrefu tu uliopita. Wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakipata shida sana ya kuwasafirisha watuhumiwa kuwapeleka Karen ambapo ni mbali sana, ukizingatia kuwa hawana hata usafiri katika vituo.

Hali ambayo Watendaji inawaweka katika hali ngumu sana katika usafirishaji wa watuhumiwa. Mheshimiwa Waziri nilishaahidi kule kuwa Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo hicho haraka iwezekanavyo. Je, Mheshimiwa Waziri unaeleza nini sasa katika ukamilishaji wa kituo hicho? Tuwaeleze neno gani wananchi sasa?

Mheshimiwa Spika, suala la vitendea kazi kwenye vituo vya polisi. Hali ya mazingira wanayofanyia kazi polisi hawa ni magumu sana, wanatembea kwa miguu kufuatilia matukio mbalimbali kwa umbali mkubwa; je, Serikali ina mpango wowote wa kuwapa nyenzo za usafiri ili kuwarahisishia kazi yao hiyo? Hususan katika maeneo magumu kama vile Mkoa wa Rukwa, Kigoma, Kagera, Ruvuma, Lindi na Mtwara

Mheshimiwa Spika, suala la wakimbizi katika eneo la Ikola. Ikola ni Kata ambayo iko karibuni sana na nchi ya Burundi, Congo na Zambia. Kuna watu wengi sana wanaishi katika maeneo hayo kinyume na taratibu za uhamiaji. Naomba Serikali iwatume Maafisa wanaohusika ili kuweza kuwabaini wanaoishi kinyume cha Sheria ili wapelekwe kambini. Hali hii itasaidia sana kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo maana idadi ya wakimbizi inazidi kuongezeka na itafikia mahali hata kuzidi idadi halisi ya wananchi wa maeneo hayo. Naomba Serikali mlifuatilie suala hili kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, suala la *speed boat* katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Tuwapeleke na wenzetu wa Burundi na Congo kwa sababu mara kadhaa kuna matukio mengi ya ujambazi ambayo yamekuwa yanajitokeza katika maeneo hayo. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walishaahidi kununua boti moja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo. Je, utekelezaji wake utakuwa lini? Maana wananchi wa Rukwa wanapata shida sana na uvamiwa mara kwa mara na majambazi hayo na siku zote yanakimbilia huko Ziwani. Naomba jibu la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wakimbizi. Wakimbizi tumewahifadhi na kuwahakikishia usalama wao, lakini wakimbizi hawa wamehusika kwa kiasi kikubwa

katika uharibifu na mazingira na baadhi yao kujihusisha na matukio mbalimbali ya ujambazi. Katika hili *UNHCR* ilikwishajitoa kuusaidia Mkoa katika kuwahudumia wakimbizi, wakati wanaopata shida ya kuharibiwa mazingira na adha mbalimbali ni wananchi wa Rukwa. Kwa msimamo huo tunaomba jitihada zifanywe ili wakimbizi hao wapelekwe makwao. Je, utaratibu huo wa kuwarudisha wakimbizi wote makwao umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, nitafurahi kupata majibu kuhusu yote haya niliyoyauliza.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, kwa mawasilisho yake mazuri ya hotuba ya Bajeti. Vile vile, nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa kuandaa Bajeti nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unalenga kwanza kwenye matatizo ambayo wananchi wanayapata ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu katika kufuatilia haki zao zinazoporwa na wahalifu. Mwananchi anapokwenda kutoa taarifa ya uhalifu alitoendewa na mtu fulani katika Serikali ya Kijiji, hutakiwa kutoa fedha ili kuwagharamia Mgambo ambao huenda kumkamata mhalifu huyo. Mhalifu huyo akifika Ofisini Kijijini mtu aliyedhumiwa haki hutakiwa kutoa gharama za kumhudumia mhalifu kuanzia akiwa Kijijini, kusafirishwa hadi kituo cha polisi, gharama za mtuhumiwa akiwa kituo cha polisi na wakati mwingine hutakiwa kutoa fedha ili kufidia gharama za karatasi hapo kituoni.

Mheshimiwa Spika, malalamiko haya niliyapata kutoka kwa wananchi ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu. Wananchi wengi hawana uwezo wa kumudu gharama zote hizo hivyo huamua kuwaachia huru wahalifu wanaowakamata. Hali hii husababisha uhalifu huko Vijijini kuongezeka sana lakini taarifa zinazojulikana ngazi za juu huonyesha kuwa matukio ya uhalifu yanapungua.

Kwa hiyo, ikiwa Serikali haitachukua hatua za kuwasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kuwagharamia wahalifu kufikishwa mbele ya vyombo vya Sheria, hakutakuwa na haki huko Vijijini. Naomba Serikali iandae sera nzuri na kusimamiwa kikamilifu, sera ya kudhibiti uhalifu ili wananchi wema waishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimesemea ukubwa wa Jimbo langu la Nanyumbu na ukosefu wa gari la polisi katika Kituo cha Polisi Mangaka. Jimbo lina eneo zaidi ya kilometa za mraba 10,000 hivyo polisi kuhudumia bila ya gari inakuwa ngumu sana. Kunapotokea uhalifu sehemu moja ya Jimbo huchukua muda mrefu sana ili taarifa kufika Masasi Mjini na hadi gari lije basi watuhumiwa huwa tayari wamekimbia

au ushahidi mwingine kuharibiwa. Naomba Serikali ifikirie jinsi ya kulipatia Kituo cha Polisi Mangaka ambapo ni Makao Makuu ya Jimbo la Nanyumu gari la polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile, Serikali ivipatie vituo vidogo vya polisi pikipiki ili zivasaidia askari kwenda kwenye matukio ya uhalifu kwa haraka zaidi huko Vijijini. Pikipiki hizo vile vile zitasaidia sana katika kufanya *patrol* hivyo kuzuia uhalifu. Hivi sasa askari hutumia baiskeli katika kufuatilia wahalifu, kitu ambacho kinahatarisha maisha yao hasa ukichukulia kuwa njia nyingine hupitia kwenye misitu ambayo imejaa wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Jeshi la Polisi, kwa kazi nzuri hasa wanapopambana na majambazi na uhalifu wa kila aina. Kazi ni ngumu na ni ya hatari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzungumzia Kituo cha Polisi cha Longido. Kituo cha Polisi cha Longido kimejengwa enzi ya ukoloni. Tangu tupate uhuru hakuna nyumba iliyojengwa. Askari hawana nyumba naomba wajenge.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Longido hawana gari. Wananchi wa Jimbo la Longido hawapeleki matatizo sehemu nyingine ila Longido. Kuanzia Kilimanjaro mpaka *Lake Natron* mpaka huo ni mrefu sana, wana matukio mengi sana, wanahitaji gari wakati wa *operation* na kadhalika. Wananchi wanaleta matukio yote Longido mpaka askari waombe gari Monduli ndipo waende kwenye tukio siku ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba ujenzi wa Kituo cha Polisi kilichojengwa na wananchi huko *Gilay/Lumbwa*, *Lake Natron* ambacho kimefikia lenta, sasa wananchi wasaidiwe kumaliziwa.

Mheshimiwa Spika, Uhamiaji Namanga wanastahili pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa bidii sana. Namanga ni mlango wa kuingilia na kutoka watu wa kila aina na mizigo ya kila aina inapitishwa, inapita pale. Lakini pamoja na kazi kubwa wanayoifanya hawana umeme. Sehemu ambayo haina umeme kama Kituo cha Namanga kunawezekana kukatokea jambo kubwa ambalo litahatarisha maisha ya watu. Pili, sehemu ambayo inaingiza mapato nchini kwa wingi kama Namanga ingefaa wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, watu wa Jimbo langu wako mpakani wanahitaji vitambulisho ili wajulikane kwani ni vigumu sana kuwatambua Watanzania au Wakenya.

Vitambulisho vinahitajika mipakani kwani hata wahalifu wa nchi jirani watatumia kwetu kuwa maficho ya wahalifu. Naomba sana wapewe vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, kulundikana kwa wahalifu mahabusu au magerezani. Mara nyingine wafungwa wanapopata shida kupita kiasi au mateso, inakuwa ni kuvunja haki za binadamu. Naomba magereza yaongwezwe ili wafungwa wasirundikane.

Mheshimiwa Spika, kwenye majumuisho naomba unijibu kuhusu msaada niliouomba wa ujenzi wa Kituo cha Polisi *Gilay Lumbwa* ambayo ni Makao ya Wasomali wakati wa *operation* na gari la polisi Kituo cha Polisi Longido.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mungu awasaidie kwa kazi ngumu ya mapambano magumu.

MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, aliyoitoa asubuhi ya leo tarehe 10 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Capt. John Chiligati, pamoja na uongozi wote unaohusika na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia natoa salamu za pekee kwa *IGP Mahita* kupitia Mheshimiwa Waziri, kwa kitendo cha kutualika Waheshimiwa Wabunge kwenye futari aliyoandaa katika Bwalo la Maafisa Ziwani Mwezi wa Ramadhani.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa nami nitapenda kuanza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka jana 2002/2003 nilichangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nilitoa kilio changu kuhusu vituo ambavyo vimo ndani ya Jimbo langu la Mwembe-Makumbi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitapenda kuanza kukielezea Kituo cha Karakana *Police Post*. Kituo hiki ingawa ni kidogo lakini kinahudumia eneo kubwa sana. Kituo hiki kinahudumia Jimbo la Chumbuni, Jimbo la Amani, Jimbo la Kwamtipura, Jimbo la Mwera na Jimbo la Dole.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa huduma eneo lote hilo, kituo hicho kinatumia taa za mkono au mishumaa. Kwa upungufu huo naomba Mheshimiwa Waziri akisaidie kupatiwa umeme kituo hiki kwani katika eneo hilo umeme umezunguka wala hautaki nguzo kwa kuingiza umeme kituoni hapo.

Pia Kituo cha *Maruhubi Police Post* ambacho kipo pembeni mwa Jimbo langu, kituo hiki kimepata umeme lakini hakina simu. Kituo hiki kipo katika mazingira magumu na ya kutisha kwani sehemu hiyo ina giza zito wakati wa usiku na ni njia kuu ya

kwenda Pwani ambako kuna Bandari ndogo ambayo baadhi ya wahalifu huweza kuitumia Bandari hiyo kusafirishia au kuingiza magendo katika bandari hiyo. Leo napenda kumwomba tena Mheshimiwa Waziri kwamba akipatie simu kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nyakati za usiku Jeshi la Polisi liongeze doria na ulinzi sehemu ya kuanzia Kinazini hadi Saateni. Sehemu ya eneo hilo panakuwa na vitendo vya ujambazi na uporaji wa mali za wapita njia wanaopita sehemu hizo. Pia zimewahi kutokea taarifa za vifo mbalimbali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pia vile vile, barabara ya Bububu imekuwa ni barabara inayoongoza kwa ajali za barabarani na ndiyo inayoongoza kwa vifo. Namwomba Mheshimiwa Waziri aongeze askari wa usalama barabarani kuanzia Kinazini hadi Bububu Kituo cha Polisi. Vile vile siku za *weekend* kama Jumamosi magari ya polisi yafanye doria kwa barabara ya Bububu kwani magari mengi huenda kwenye sehemu za starehe kwa mfano kwenye fukwe za Bububu. Wakati wa kurudi magari hayo madreva huwa wamelewa na kusababisha ajali wakati magari yakielekea Mjini. Kama ikiwezekana pawekwe *road block* katika Kituo cha *Beit-Ras* na Kituo cha Maruhubi kwa kuyasimamisha magari yanayohatarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kupongeza sana juhudi zinazofanywa na Wizara hii katika vitengo vyake vyote ukianzia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, polisi, uhamiaji, magereza na kadhalika, kazi yenu ni nzuri sana. Ni matumaini yangu ufanisi utaongezeka na kuboreka zaidi. Vitendea kazi na Bajeti sasa vinaongezwa. *So far* mmefaya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, pili, napendekeza kuelekeza nguvu ya ziada katika maeneo korofi hasa mipakani. Maeneo yanayopakana na nchi zenye matatizo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe mfano maeneo ya Bukombe huko Mkoani Shinyanga, Kagera, Kigoma na kadhalika. Pia nguvu (*personnel plus* vitendea kazi) zaidi ielekezwe kwenye maeneo ya migodi. Maeneo haya yana uhalifu mwingi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tatu, Polisi Magu wamechanga fedha kwa ajili ya kupatiwa umeme kwenye makazi yao. Naomba Polisi Makao Makuu iwasiliane nao ili waongezewe fedha zilizopelea. Pia tatizo ama hitaji hilo la umeme na mengine kwenye makazi ya Polisi Magu liangaliwe upya kwa maana ya kulitatua *once and for all*.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo malalamiko ya wafanyabiashara wa daladala hasa huko Mbeya Mjini kuhusiana na utendaji wa Trafiki, wafanyabiashara wa daladala wamewahi kutoa malalamiko yao. Pia nilipofanya mkutano na wafanyabiashara na wenye viwanda Mjini Mbeya walinieleza kwamba wanakabiliwa na kodi na ushuru aina nyingi kiasi cha biashara yao kutoingiza faida. Kukamatwa mara kwa mara na Trafiki

bila makosa wakati mwingine lilipelekea kuwepo mgomo wa wenye daladala. Naomba suala hili liangaliwe upya na ufumbuji upatikane, *mainly administratively*.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji inafanya vizuri sana. Sijawahi kusikia malalamiko na scandals kwa miaka ya hivi karibuni. *Keep it up*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na *Management* yote ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kuhusu madawa ya kulevya, Mlandege. Bado vijana wengi wa Jimbo langu la Mlandege wanatumia madawa ya kulevya. Jambo la kusikitisha ni wale wanaotumia sindano kuwa wamepata ugonjwa wa Ukimwi. Vijana 20 wameambukizwa virusi vya Ukimwi hivyo kuongezeka kwa tatizo la kuwa na matatizo mara mbili, moja la madawa ya kulevya na la pili, ni la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie Mlandege, vijana watamalizika na wao ndio nguvu kazi yetu. Baadhi ya vijana wengine wamesita kutumia madawa ya kulevya. Hawa tunawaomba Kituo cha Mafunzo ili waweze kuji-*reform* wasirejee tena kutumia madawa hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kusaidiwa kujenga Kituo cha Polisi Vikokotoni. Sehemu hii ni ya biashara zaidi kwa hiyo wananchi wanaoishi hapo ni kidogo sana.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inayo kazi kubwa ya kuhakikisha usalama wa raia. Nchi inapokuwa salama inakuwa furaha kwa kila mwananchi na inarahisisha kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumekuwa tunashuhudia uvunjaji mkubwa wa Sheria, ujambazi unazidi kuongezeka, ajali za magari na vifo vya watu vinazidi kuongezeka badala ya kupungua, raia hawaogopi kuvunja Sheria kwa mfano kutukanana hadharani, kutishiana na mengineyo yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini hayo niliyoyataja ni *indicators* za hali ya utulivu na amani katika jamii yetu. Mbaya zaidi wahalifu sasa wamejizatiti, hutumia ujanja na vifaa vya mawasiliano vya hali ya juu. Kwa hali hiyo, ni vema tukafahamu kama askari polisi wetu wamewezeshwa kukabiliana na mazingira haya magumu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuboresha hali ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inaridhisha lakini ni vizuri ikaongezwa. Serikali

ihakikishe inatoa mafunzo zaidi kwa askari, Serikali ihakikishe inanunua vifaa vya *electronic* ili kurahisisha mawasiliano na pia magari ya kutosha yanunuliwe. Kwa eneo hili *OCD* wangu wa Babati hana usafiri, hana gari hivyo anashindwa kukamata gongo. Kwa hiyo, tatizo kubwa la msingi ni uwezo/vifaa duni vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hali ya motisha kwa askari wetu iangaliwe upya na kupewa kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri akisaidiana na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Capt. John Chiligati na timu ya wataalam wa Wizara hii, kwa uchambuzi wa kina na fasaha wa mikakati ya kuimarisha usalama nchini. Kwa sababu ya maandalizi haya mazuri napenda kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninayo maombi machache kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kituo cha Polisi cha Wilaya mpya ya Kilindi kilichopo Makao Makuu ya Wilaya pale Songe hakina silaha hata moja yaani askari zaidi ya 15 waliopo kituoni hulinda Wilaya kwa fimbo badala ya bunduki. Jambo hili ni hatari kwa usalama wa askari. Naomba utusaidie silaha maana *armoury* ipo imejengwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, sasa hivi yupo *OCS* akiongoza kituo. Tunaomba tupewe *OCD* ili Wilaya ijitegemee kiulinzi wa polisi. Tunaomba tupate utaratibu ambao tunapaswa kuufuata kupata *OCD* kama kikwazo kiko kwetu sisi wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kituo hiki cha Polisi cha Songe ambacho kiko zaidi ya kilomita 100 toka kile cha Handeni, Kibaya na Kilosa kinahitaji sana kuwa na gari ili kutoa huduma za usalama katika eneo la Wilaya ya Kilindi lakini pia maeneo ya Wilaya ya Kiteto, Kilosa na Simanjiro yaliyo mbali na Makao Makuu ya Vituo vya Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Songe kilikuwa na gari lakini lilichukuliwa na *OCD* wa Handeni na halijarudishwa hadi leo, nadhani limefia hapo Handeni. Naomba sana msaada wa gari la Polisi Songe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, mimi ninaiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wizara imeanza kupendeza hasa kwa kudhibiti majambazi ila Wilaya ya Geita bado ujambazi ni tishio, kwa hiyo, naomba yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, kwanza, polisi Geita wapatiwe magari mapya mawili, moja aina ya *Pickup Land Courser*, mkonga na *110 Station Wagon*. Wilaya ni kubwa sana na machimbo yanachangia uhalifu. Ni Wilaya yenye idadi kubwa ya watu kuliko Wilaya zote nchini, inalingana na Mkoa wa Lindi na inakaribia nchi ya Tanzania Visiwani. Tunaomba Wizara iangalie kwa misingi hiyo. Pili, tunaomba idadi ya askari waongezwe, waliopo ni wachache sana na hawana usafiri.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba msaada wa Serikali ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Rwamgasa. Wananchi wanajitahidi kuunganisha nguvu zao kwa harambee na michango mbalimbali. Basi tunaomba Serikali ichangie ili kuwapa nguvu wananchi wa Rwamgasa.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba Gereza la Butundwe lipatiwe pembejeo za kilimo. Gereza hili lina uwezo wa kulima na kulisha Kanda ya Ziwa kama wakipewa pembejeo. Naomba wapatiwe japo ma-*tractor* mawili ili wazalishe badala ya kukaa bila faida. Hili ni gereza la kilimo lakini hakuna shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, tano, tunaomba boti ya doria katika Visiwa vya Geita kwani majambazi yanavitumia kama vichaka kwa kujificha.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu tafadhali yafikiriwe. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina majukumu muhimu sana ya ulinzi na usalama wa raia. Bila hilo kuwepo shughuli nyingine zote za kijamii na kiuchumi zitasimama. Kwa hiyo, ni muhimu sana Bajeti ya maendeleo ikawa ikiongezwa mwaka hadi mwaka ili kuweza kujenga ofisi, nyumba za askari polisi na magereza.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo makubwa sana ya ujambazi katika eneo la Wilaya ya Kongwa hasa kwenye barabara kuu ya Morogoro - Dodoma katika maeneo ya Pandambili, Kibaigwa, Mtanana na Mbande. Wizara iwezeshe kupatikana kwa *highway patrol vehicle* itakayokuwa pale Kongwa badala ya kuwategemea askari wa kutoka Dodoma. Pia, pale Kibaigwa pawe *stationed*, askari wawe pale *permanently* badala ya hali ya sasa ambapo wanatoka Kongwa kila siku na usafiri wa kipolisi haupo, wanadandia magari *daily*.

Ni vema basi askari hawa wa Kongwa wakapewa gari la kawaida la kazi za kipolisi jipya ili kuboresha huduma. Wanalo gari aina ya *pick-up, LR 110* ni mbovu sana na ndilo gari pekee la kazi za polisi kwa Wilaya nzima yenye watu 250,000 (laki mbili na nusu)

Mheshimiwa Spika, tafadhali *OCD* wa Kongwa apewe gari katika mgao ujao wa magari yatakayogawanywa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pale Kibaigwa wananchi wamejitahidi sana kujenga Jengo la Kituo cha Polisi. Tumechangisha mno, wananchi wanaomba Wizara iwaunge mkono katika umaliziaji na ku-*post* askari wa kutosha pale ili kuimarisha usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Vodacom* wanaweka mawasiliano barabara kuu ya Dodoma - Morogoro, askari hao wakiwa na gari wanaweza kufanya *patrol* nzuri katika eneo la barabara hiyo lenye matukio mengi ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Gereza la Kongwa lipewe ma-*tractors* mawili ili wazalishe chakula cha kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanyie marekebisho fomu ya *PF III* kama ilivyokwishaahidi. Pia marekebisho yafanywe ya namna ya kuipata iwe ni mahospitalini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hati za uraia hasa cheti cha kuzaliwa kipatikane Wilayani katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa rika zote na masharti yapunguzwe ya upatikanaji wa hati hizo ili wananchi wasikose fursa mbalimbali za mafunzo, kazi na kadhalika ambazo ni lazima mtu aonyeshe cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, hayo mawili hapo juu najua yanahitaji ushirikiano wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, fanyeni hayo ili tupunguze kero. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi ambazo wamekuwa wakizifanya. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nimeshawishika kuchangia hoja hii kwa mambo muhimu mawili ambayo ningependa kupata majibu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza, itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 17 Novemba, 2002 kulitokea tukio la vifo vya mahabusu 17, tukio ambalo lilikuwa ni la kiuzembe, kiukatili na la kusikisisha sana kwa sababu mahabusu hawa walikufa kwa kukosa hewa kutokana na kurundikwa wengi ndani ya chumba kimoja kidogo kisicho na hewa ya kutosha. Mahabusu zaidi ya 100 waliwekwa kwenye chumba chenye uwezo wa kuwekwa mahabusu 30 - 40.

Mheshimiwa Spika, baada ya tukio hilo la kusikitisha kulitokea hali ya kutupiana mpira kati ya Mahakama, Polisi na Magereza kwamba nani alaumiwe kitu ambacho kwa kweli si cha msingi kwani jukumu ni la Serikali tu. Nani alikuwa mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa mahabusu hawatoroki na wanakuja kutoka kwa hali ya usalama kwani haki za kibinadamu zinamgusa kila mtu, hawa mahabusu walikuwa hawajahukumika, wengi walikuwa ni *suspect* tu.

Baada ya tukio hilo wananchi wa Mbarali wafiwa waliambiwa na Serikali kuwa hatua zitachukuliwa ikiwemo kuunda Tume ya Uchunguzi ambayo ilipewa muda wa siku 14 kukamilisha kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mbarali kujionea mwenyewe aliambiwa kuna Tume ya Uchunguzi inafanya kazi yake na itatoa taarifa baada ya kipindi cha siku 14. Wananchi walimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya fidia kwa ndugu na jamaa wa mahabusu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema tsubiri uchunguzi ukamilike. Wananchi Mbarali wamekuwa wavumilivu kusubiri Serikali ifanye nini hasa baada ya kupata maelezo na elimu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, leo hii Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majibu, naomba anipe majibu ya uhakika kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, je, Tume ya Uchunguzi iliyoundwa ilikwishatoa taarifa yake ya matokeo ya uchunguzi na kama ilitoa ni lini? Na ni nani mwenye haki ya kujua taarifa hiyo? Je, mwananchi huyu wa Mbarali hana haki ya kujua? Na je, na mimi Mbunge wao sina haki? Ukizingatia kuwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa Mbunge si Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, pili, je, fidia kwa ndugu waliokuwa wanawagetegemea marehemu hawa watapewa, kama ndiyo ni lini? Je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa wote waliohusika au waliosababisha tukio hilo kutokea, wale wote waliohusika na uzembe huo uliosababisha mauaji haya ya mahabusu 17?

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwa upande wa zoezi la uraia linalofanyika hususan Wilaya ya Mbarali. Inaonekana Sheria hii haijaleweka vizuri kwa wananchi na kwa baadhi ya Maafisa wa Uhamiaji, naomba kujua ni nani ambaye anapaswa kujiandikisha au kujaza fomu za uraia kwa sasa hasa ukizingatia kuwa kifungu cha Sheria ambacho kilikuwa kinawaruhusu wale wote waliozaliwa Tanzania kabla ya uhuru akiwa na mzazi mmoja ambaye ni Mtanzania anatakiwa kuwa raia hata bila kukana uraia wa nchi ya mzazi asiye raia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba zoezi hili litolewe uamuzi haraka na wananchi waelimishwe ingawa namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, alipotembelea Mbarali alitoa elimu ya kutosha. Lakini zoezi hili linaonekana hatma yake bado ni kitendawili.

Mheshimiwa Spika, naomba mwenye dhamana ya uhamiaji ahakikishe zoezi linakamilika haraka ili kila mwananchi awe huru na utendaji wa kazi katika ujenzi wa Taifa hili.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya Bajeti ya mwaka 2003/2004. Napenda kutamka kwamba hoja hii naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu, Ndugu Bernard Said Mchomvu, *IGP*, Ndugu Omar Idd Mahita na Wasaidizi Wakuu wote Waandamizi wa Wizara hii kwa hoja yao inayoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwanza, mchango wangu ni kuhusu sungusungu. Inaelekea viongozi wakiwemo *IGP* wanakiri kwamba kutokana na udogo pamoja na ufinyu wa Bajeti kwa Wizara hii, kazi ya ulinzi na usalama na mali za raia umekuwa hauridhishi hasa kutokana na matukio ya hivi karibuni ya mauaji yaliyofanywa na majambazi, yametushtua sisi sote na kutambua jinsi tulivyo wanyonge kiusalama. Tunahitaji zana na vifaa vya kisasa ili kulipa jeshi letu uwezo wa kukabiliana na wahalifu hao. Hivyo huku tukisubiri vifaa hivyo kwa sasa, basi umuhimu wa ulinzi wa sungusungu unakuwa ni wa lazima sana. Wananchi wanapenda kujiunga na sungusungu lakini wanadai kwamba endapo wataumia au watapata majereha makubwa wao hawapewi fidia kama vile polisi wanavyopewa. Ni ombi langu basi kwamba huku tukisubiri Bajeti ya Wizara kuwa ya kuridhisha, Serikali iweke Sheria ya kumhama au ya kumpa fidia na kijinga raia huyu wa sungusungu sawa na polisi. Vinginevyo wengi wa wananchi wanasita sana kujiunga na sungusungu na hivyo kushindwa kuwasaidia polisi, hivyo kazi yao ya ulinzi na usalama kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo linalojitokeza pale ambapo wananchi wanajenga *Police Post*. Wananchi wanaambiwa wawatafutie nyumba na kugharamia kodi hiyo kwa Maafisa wa Polisi watakaokaa katika eneo la nyumba hiyo, sidhani kama hili ni jukumu la wananchi. Huyu *Police Officer* tayari yuko kwenye *payroll* ya Serikali hivyo maslahi stahili na madai yake yote yanakuwa ni ya Serikali katika kutimiza matakwa hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, polisi katika vituo hivyo wanakuwa wachache sana kiasi kwamba panapotokea tukio la uhalifu polisi anasita kwenda kwenye tukio hilo kwa maelezo kwamba yuko peke yake na kadhalika na kwamba hawezi kuacha kituo. Sasa lazima Serikali irekebishe uchache huu wa polisi kwa kuongeza idadi ya mapolisi kwenye vituo vya polisi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi barabara nyingi Jijini Dar es Salaam zinapitika vizuri hivyo naomba sana magari ya doria yaongezwe na yawe yanapitapita kila baada ya nusu saa. Kwenye maeneo nyeti na korofi, maeneo yanayofahamika kwa ukorofi basi magari ya doria yapite mara kwa mara lakini si chini ya robo saa. Hii itasaidia kuwatawanya wahalifu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mapema, mimi ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Spika, jitihada za Wizara hii kwa ulinzi na usalama wa raia na mali zao zinaonekana kujipanga upya kwa Jeshi la Polisi katika kupambana na ujambazi uliokithiri nchini, zinaungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mikoa yote chini ya Wakuu wa Mikoa, ishiriki kikamilifu katika kupambana na ujambazi kwa kutamka waziwazi imejiandaa na imewaandaa vipi wananchi kushiriki katika zoezi hilo tangu Vijijini, Wilayani na Mkoa wenyewe. Tuuige Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pili, vitambulisho vya uraia wa nchi ni muhimu sana hasa kwa sasa kutokana na hali halisi ya dunia ilivyo sasa kuwa ni vigumu kuwakagua na kuwatambua raia.

Mheshimiwa Spika, tatu, Idara ya Uhamiaji kwa sasa ijipange upya au vizuri zaidi katika utoaji na udhibiti wa hati za kusafiria (*passport*). Umuhimu wa kufanya hivyo wakati tulionao ni mkubwa. Aidha, pawepo utaratibu wa kukagua pasi hizo kila baada ya mwaka mmoja ikiwezekana. Raia asiyepeleka pasi yake kwa ukaguzi ahesabiwe amevunja Sheria na ashitakiwe kwa kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, nne, mrundikano wa *traffic police* barabarani katika kizuizi kimoja na kwa vizuizi vya hapa na pale umezidi sana na unapunguza idadi ya polisi wanaofanya lindo la kawaida. Jambo hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, tano, kwa mazingira magumu ya kazi ya polisi, ni vema Serikali ianze kufirikia upya motisha zaidi. Kazi ya kulinda inahitaji motisha. Nashukuru kwa Mheshimiwa Waziri, Serikali kwa kuona umuhimu wa kuimarisha Vituo vya Tunduma na Vwawa (Mbozi).

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba sana Kituo cha Tunduma kipewe umuhimu wa kipekee kwa kuzingatia unyeti wake pale mpakani ambapo kinahudumia nchi za Zambia, Malawi, Zimbabwe, Afrika ya Kusini, Congo na kadhalika. Pawepo na vitendea kazi vya kisasa ikiwa ni pamoja na gari jipya. Uhalifu mkubwa unafanyika mpakani, gari jipya litasaidia sana. Pili, *OCD* Wilayani hana gari badala yake anakodisha gari la raia mmoja ambaye sidhani kama anacho kiasi gani, rekodi nzuri. Polisi na *OCD* hutumia gari la mtu binafsi katika kazi za Serikali za kiulinzi, nadhani siyo sahihi na siyo mila ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Makao Makuu ya Polisi Wilayani ni ya zamani yaliyotumiwa kuwalaza manamba kabla ya kuwasafirisha kwenda Pwani/Tanga. Tutashukuru sana endapo Makao Makuu mapya yatajengwa kama ahadi au mpango unavyoonekana katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, wakimbizi wamesababisha kero na madhara makubwa katika nchi yetu, mazingira yameharibiwa na pia utamaduni wetu wa thamani ya utu wa mtu umeharibiwa. Sisi hatujazoea kuuwana, wao wamezoea kuuwana na hivyo wameanza kuwauwa raia wetu, hapo lazima huruma yetu ifikie hatma/iangaliwe upya ili kila nchi ibebe mzigo wa raia zake. Wakimbizi watengewe maeneo ndani ya nchi zao na ni jukumu la *UN* kuwalinda huko huko nchini mwao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nami naomba nichangie hotuba hii kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kuchangia katika suala la usalama wa barabarani. Wakati nikiangalia matarajio ya majukumu ya Wizara 2003/2004 pale katika ukurasa wa 20 - 22, sikuona mpango ama mikakati iliyowekwa kupunguza ajali za barabarani. Kama ilivyo katika jedwali ukurasa wa 44, kati ya mwezi Januari hadi Desemba, 2002 jumla ya matukio ya kuvunja Sheria za usalama barabarani ni 174,884, Jiji la Dar es Salaam likiongoza (30,208), Mwanza ikifuata (16,173), Arusha (14,596) na Pwani (14,460) ikifuatia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, katika matukio 174,884 yaliyotokea jumla ya watu waliofariki na kujeruhiwa ni 18,256. Kwa kuwa sikupata takwimu za miaka iliyopita, nitatumia majibu ya swali langu Na. 92 wakati Serikali ikijibu kuhusu mkakati wa kudhibiti ajali za barabarani zinazoongezeka licha ya vidhibiti mwendo kuwepo na Sheria ya kutotembeza magari ya abiria usiku. Serikali ilikiri ukweli wa ajali mbaya kuendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuchukua hatua za kuwapatia mafunzo madereva wa magari ya abiria wenye leseni, kuwa na vyuo vinavyotambuliwa na Serikali kwa ajili ya mafunzo ya udereva na *VETA* ikipewa kipaumbele, polisi kiongeza doria barabarani kama miongoni mwa mikakati ya kudhibiti ajali za barabarani, ajali mbaya zimeendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, katika kutafakari nimebaini kuwa zipo sababu nyingi lakini kubwa zaidi ni kutokana na kazi ya usalama barabarani imeonekana ni ya Serikali tu. Kwa hiyo, ni kazi ya upande mmoja na hivyo vita vya kupunguza na hatimaye kudhibiti ipasavyo ajali za barabarani kuendelea kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri ifuatavyo: Kwanza, kiazishwe kitu ninachoweza kukiita pembetatu ya usalama barabarani. Katika hii pembetatu Serikali/polisi itakuwa na wajibu na majukumu yake, pili, madreva mwenye magari watakuwa na wajibu na majukumu yao wakati wote gari liwapo barabarani na tatu, abiria/mdau naye atakuwa na wajibu.

Mheshimiwa Spika, pili, kuanzishwe Gazeti la Usalama Barabarani. Ninaimani mapambano ya usalama barabarani yanaweza kuboreka kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyo sasa. Kazi hii ifanyikeje? Polisi iendelee kudhibiti ipasavyo kwa hatua zote inazochukua, ikiwa ni pamoja na magari ya abiria na tekisi, kuwasomesha madereva wote, kudhibiti utoaji wa leseni na doria za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikubali pia kuwa vidhibiti mwendo pekee haviwezi kubaki kuwa vigezo pekee vya kupunguza kasi ya magari barabarani. Hii ni kutokana na ukweli kwamba madreva wengi siyo waaminifu, wanaviharibu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kuwe na kitu kipyaa yaani *in built vehicle monitoring system*. Katika hii *system* dreva hawezi kukichezea kifaa hiki kilichojengewa ndani ya gari la abiria, kina uwezo wa kutunza kumbukumbu ya mwenendo mzima wa gari kama ilivyo kwenye ndege. Kitaweza kuonyesha mwendo mkali na kuyumba kwa gari husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ianzishe Kitengo cha Wataalam wa Usalama Barabarani ambao wana vitambulisho rasmi lakini hawavai sare wala kutumia magari ya polisi. Wataalam hawa wanaweza kuitwa “Meneja wa Safari”. Hawa watakuwa katika Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo, Morogoro, Dodoma, Singida na kadhalika kulingana na gari linaelekea njia gani?

Mheshimiwa Spika, wataalam hawa watapewa mamlaka ya kuyapangia magari yote ya abiria ratiba ya safari ambayo itaheshimika. Ratiba hii itakabidhiwa kwa dereva wa gari la abiria, dreva atatakiwa atii. Aidha, kutakuwa na mawasiliano ya simu ama redio kati ya mtaalam aliyeko Kituo Kikuu na wengine katika kila kituo. Na kila dreva atapaswa kuwasilisha ratiba kwa kila kituo ama polisi ili isainiwe kwamba hajavunja ratiba. Akiiunja kwa kuwahi sana ama kuchelewa atapaswa kujieleza na ni lazima adhibitiwe. Chombo hiki kitadhibitiwa na Serikali/Polisi. Wajibu wa dreva/mwenye gari ni pamoja na kutii niliyotangulia kueleza. Lazima atoe ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vilivyowekwa ili kumdhibiti.

Mheshimiwa Spika, wajibu mwingine wa dereva/mwenye gari ni kuhakikisha anakagua gari lake kila siku. Na hapa Serikali inatakiwa kutoa fomu maalum atakayotakiwa kuijaza kila anapotaka kuliweka gari lake barabarani. Fomu hii ataijaza kwa mwaka mzima na itakaa ndani ya gari husika. Fomu ionyeshe ukaguzi wa maji katika gari, *oil*, ukamilifu na breki za gari, mikanda, vioo vya kuongozea magari, uwezo wa betri, uimara wa matairi na mengine yote muhimu. Fomu hii ni kwa *vehicle safety* bila kujali ataulizwa au la. Manufaa ya fomu hii ni pale inapotokea tatizo litajulikana ni la nani, dreva/wenye gari, gari lenyewe au watumiaji wengine wa barabara na mengineyo mengi. Fomu hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa abiria/mdau hasa kwenye magari ya abiria, ni lazima aifahamu ratiba ya gari analotaka kusafiri nalo. Abiria ambaye ni mdau lazima ajue gari alilokatia tiketi litaondoka saa ngapi na litawasili saa ngapi. Ratiba hii ni ile ambayo imeandaliwa na wataalam na kukabidhiwa kwa dreva wa gari lile. Ratiba hii pia

niitolee tahadhari kwamba lazima ijaribu iwezavyo kwa magari yaendayo njia moja kuepusha yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, kwanza, magari yasisimame njiani ambapo ratiba haikutaja isipokuwa kwa dharura. Pili, gari lisipakie abiria asiye na kiti na lisipakie njiani, hii itafanywa na magari ya masafa mafupi. Tatu, kati ya gari na gari iwepo interval walau isiyopungua saa moja ili kuzuia kufukuzana.

Mheshimiwa Spika, abiria/mdau lazima awe na hati ya kuyajua yote hayo na pale anapokuwa na wasiwasi awe huru na asikilizwe kulalamika kwa askari wa usalama barabarani wanayekutana naye. Abiria awe na uhuru wa kulalamika hata kama ni mwisho wa safari, akieleza mwenendo wa gari alilosafiria akiwa na tiketi halali ambalo hakuridhika nalo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la mwisho ni uanzishwaji wa Gazeti la Usalama Barabarani. Gazeti hili litatoa habari za ajali zinazoripotiwa zote nchini na hata nchi jirani. Gazeti hili lichapishe picha halisi (photo) za tukio, ielezwe wazi sababu za ajali hiyo. Gazeti pia lililoandikwa na wataalam waeleze mafunzo na kutoa tahadhari bayana. Gazeti hili siyo lazima liwe la kila siku hata mara moja kwa mwezi itasaidia.

Mheshimiwa Spika, ninakusudia kuona mawazo siyo tu yanapata majibu wakati wa kujumuisha michango mbalimbali itakayotolewa hapa bali pia yanayofaa yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba kuchukua nafasi hii katika kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa kweli ni hotuba nzuri na kama itafanyiwa kazi kama ilivyopangwa basi nategemea ya kwamba mambo mengi yatakaa vizuri kwa muda mchache ujao.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu *Marine Police*. Kwa kweli kikosi hiki ni muhimu sana kwa nchi yetu hasa kwa wakati kama huu ambapo uchumi wetu unakua. Kwa muda mrefu sijaona wala kusikia jinsi Wizara inavyochukua hatua za makusudi ili kuboresha kikosi hiki ambacho hivi sasa kina matatizo mengi na miongoni mwa matatizo sugu ni ukosefu wa vitendea kazi na hasa speed boats za uhakika.

Hivi sasa magendo mengi yameshamiri hasa sehemu za baharini na kwenye maziwa yetu. Kama hatua za haraka hazijachukuliwa basi naogopa kusema kwamba uchumi wetu huenda ukaathirika. Hivi sasa kuna vitu vingi vya magendo huko kwenye Mkoa yenye maziwa ambavyo vinaingizwa nchini kwa njia ya kinyemela. Kwa mfano Mkoa wa Mwanza kuna sigara feki za *sportman* na *sweet-menthol* ambazo zinatengenezwa nchi za jirani na kupitishwa kwa njia hizo za magendo. Baya zaidi ni

kwamba sigara hizo zinatengenezwa nchi za jirani na kuandikwa kwamba zinatengenezwa hapa nchini. Na hivi inatokana na kwamba wahalifu wanafahamu kwamba sehemu hizo za bahari na maziwa hazina ulinzi wa kutosha. Karafuu zetu pia huondoshwa kwa njia kama hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kulipongeza Jeshi letu la Polisi hasa hapa Dodoma kwa jinsi linavyowajibika katika suala zima la ulinzi. Hii inaonyesha wazi kwamba pindi jeshi letu likiboreshwa kwa zana za kisasa litakavyoweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninaomba kuishia hapo na kusema kwamba ninaunga mkono hoja kwa mara ya pili.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi ninapenda kuzitoa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Katibu Mkuu, *IGP, Director CID*, Idara ya Usalama Barabarani, Idara ya *IB*, Idara ya Kuzuia Madawa ya Kulevya, Makamanda wa Idara zote, Bara na Visiwani, Idara ya Magereza na kwa Makamanda wa Mikoa na kadhalika. Napenda kuwakaribisha Dodoma, karibuni sana Dodoma, mliokuja wapewe salamu hizi wale ambao hawakufunikiwa kuja.

Mheshimiwa Spika, Muda wa Mahabusu Kukaa Gerezani. Kuna taarifa kuwa vibaka wadogo wadogo ndiyo wateja wakubwa wa magereza na kujaza magereza nchini. Kwa nini hukumu zao zisifanywe kwa utaratibu wa haraka ili muda wa kukaa mahabusu usiwe mrefu kuliko ule wa kufungwa kwa hukumu? Hali hii itafanya mahabusu aliyekaa mahabusu miaka mitano, akifungwa miaka miwili kama adhabu, atakuwa mzoefu katika eneo hilo na aina ya adhabu inayoitumikia.

Mheshimiwa Spika, Utunzaji wa Magari na Vifaa vya Kazi. Hili ni wazo, Idara nyeti kutunza kwa makini sana vifaa vyote vilivyomo ndani ya mamlaka yao, taarifa nyeti, utunzaji wa siri na kuhifadhi wenyewe magari yao na dhana za kazi kama *radio calls* na kadhalika ili vidumu, “kitunze kidumu”.

Mheshimiwa Spika, Idara ya *CID*. Idara hii ni muhimu katika kuwasaidia polisi kabla ya tukio lolote baya. Hii Idara katika afya inaitwa “kinga”. Tahadhari ni kwamba Idara hii ipatiwe fedha zaidi ili iweze kupeleleza vizuri na kuweza kuzuia matukio ya hatari. Mfumo shirikishi ungetumika ili kuwahusisha raia wema wa nchi hii. Polisi na Vyombo vyake. Napenda kutoa pongezi kwa matukio ya hivi karibuni. Serikali iangalie jinsi gani inaweza kulisaidia Jeshi hili la Polisi. Tunasema Watanzania tujilinde wenyewe lakini “nanasi lina miba” lakini huliwa.

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wake, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wakuu wa Idara chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kituo kidogo cha Polisi cha Mnazi katika Jimbo la Mlalo kiko kilomita karibu 130 hivi kutoka Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya Mjini Lushoto. Kituo hicho ambacho kiko jirani na Mbuga ya Wanyama ya Uмба pamoja na mpaka mrefu wa nchi jirani ya Kenya hakina silaha wala usafiri wa aina yoyote. Hivi kuna faida gani ya kuwa na kituo cha polisi cha namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo *radio call* iliyoko hapo ni ya aina ya zamani sana kiasi kwamba huwezi kuwasiliana na Wilaya mpaka kupitia Mkoani. Ingawa Mnazi hakuna barabara rasmi ya kuunganisha Tanzania na Kenya hata hivyo eneo hilo ni njia kuu ya magendo na wizi wa magari. Nasikia kituo hicho kidogo ni mahali pa adhabu kwa askari wanaoharibu maeneo mengine. Sijui kuna ukweli kiasi gani lakini kwa hali inayoonekana hainiwii rahisi kukataa dhana hiyo. Naomba kituo hicho kiimarishwe na kionekane kweli ni kituo cha mpakani na sio eneo la adhabu. Askari wa kituo hicho hawana kazi ya kufanya kwa sababu ya uduni au hakuna kabisa vifaa na mazingira ni magumu sana. Nakumbuka *IGP* Mahita aliwahi kufika hapo kwa ndege yaani helicopter.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujambazi nchini, inawezekana kabisa tulijisahau kidogo. Ni Jeshi la Polisi na Uhamiaji kuwa macho wakati wote hasa katika suala la majambazi kutoka nchi jirani. Hata hivyo, naamini kwamba suala hili haliihusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pekee bali Serikali nzima pamoja na raia wote. Ni vema pia kwamba chama chetu, Chama cha Mapinduzi kikachukua nafasi yake ya kuongeza hamasa kwa wananchi kuhusu masuala ya ulinzi na usalama. Suala hili limezorota sana siku hizi hata kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, naomba kuunga mkono hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake yenye mwelekeo na pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kiwango kikubwa napenda kuwapongeza Mkuu wa Polisi nchini, Kamishna Mkuu Magereza na Mkurugenzi wa Uhamiaji nchini na pia Katibu wa Wizara na Wasaidizi wake wote. Mwaka jana 2002 Pantoni ya Mto Kilombero ilizama. Gari la polisi na askari wa polisi wamepoteza maisha yao. Lakini nasikitika hadi leo Wizara haijapeleka Mahenge gari badala ya lile la polisi lililozama.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli mimi kama Mbunge niilalamikie Wizara juu ya kutopelekwa kwa gari Mahenge ambapo Wizara inajua hili ni jambo la kwanza katika umuhimu wa kazi yake?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ajali za barabarani zinaongezeka lakini kila gari linapoharibika njiani dreva mhusika kwa tahadhari anaweka majani. Wizara inashindwa kusimamia kwamba kila dreva anakuwa na vifaa vya kuweka mbele na nyuma pindi gari

lake likiharibika? Mbona ukaguzi wa leseni, makosa ya kuendesha zaidi *speed* zisizotakiwa na kuvaa mkanda ukiendesha vinakaguliwa?

Mheshimiwa Spika, naomba, nashauri, nasisitiza tamko litolewe katika Bajeti hii kwenye majumuisho ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuanzia leo kila drevu/mwenye gari anatakiwa kuwa na vifaa hivyo katika gari lake. Na maagizo hayo yatolewe kwa askari wote wa barabarani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. YETE S. MWALYEGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri wanayofanya na hotuba safi aliyotoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie jambo moja jimbo la Mbeya Vijijini kama kituo cha polisi Inyala km. 25 kutoka Mbeya Mjini. Kituo hiki kilijengwa na *TAZAMA*. Kuna kituo kikubwa, rumande nzuri na nyumba za askari kama tisa hivi. Kambi hii haijafanyiwa ukarabati miaka mingi. Naomba bajeti hii ifanye ukarabati wa nyumba, rumande na Ofisi za Kituo. Jengo ni kubwa kuliko la Mkoa. Kituo hiki kipo mpakani na Mbarali. Mara nyingi kipo tupu. Mbarali wanaweza kukitumia kwa sasa wanaposubiri chao.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, naomba Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri. Mimi naunga mkono hotuba mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi *Mbamba Bay* kiko mpakani ni kituo muhimu sana kwa ajili ya kuimarisha ulinzi mpakani, kituo kina upungufu mkubwa wa askari, kilitakiwa kiwe na askari ishirini (20) lakini wapo tisa (9) tu. Tunaomba Wizara iongeze polisi katika kituo hiki kwa madhumuni ya kuboresha ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *Mbamba Bay* pamoja na nyumba za polisi ishirini (20) toka zijengwe yapata miaka 37 iliyopita hazijafanyiwa ukarabati hata mara moja, kwa sasa ziko katika hali mbaya sana Ofisi na nyumba za polisi zinavuja. Naomba Mheshimiwa Waziri ufanye uwezalo kuondoa matatizo haya yanayowasumbua askari wa Kituo cha *Mbamba Bay*.

Mheshimiwa Spika, kituo cha *Mbamba Bay* kiko mpakani na askari wanahudumia eneo kubwa hivyo wanasumbuka mno na tatizo la usafiri ni vema Mheshimiwa Waziri ukawapa gari liwasaidie katika kufanikisha kazi zao.

Mheshimiwa Spika, lingine kituo pia hakipati fedha kwa ajili ya kugharimia mahabusu. Shida inakuwa zaidi ikiwa raia wa kigeni akiwekwa mahabusu hakuna anayeweza kumsaidia. Mheshimiwa Waziri ingefaa sana kituo cha *Mbamba Bay* kipewe fedha kwa ajili ya kuwahudumia mahabusu kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbinga iko mipakani inakumbana na matatizo ya uhamiaji na kwa kukosa Ofisi za Uhamiaji mipakani wageni kutoka nchi jirani wanaingia nchini mwetu kila kudhibitiwa. Hali hii si nzuri, naomba sana utafiti unaofanywa na Wizara yako, ukakamilika mapema ili Ofisi za Uhamiaji zikajengwa Kata ya Chiwanda, Kata ya Tingi na Kata ya Liparamba. Hizi Kata tatu zinaambaa ambaa mipakani kati ya nchi yetu na Msumbiji. Ahsante sana.

MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLA: Kwanza napenda nianze na kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara hii. Pia nachukua nafasi hii kumpa pole Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kufiwa na askari wake wawili. Mungu azilaze roho zao Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu ukarabati wa baadhi ya vituo, ningemwomba Waziri aliangalie sana vituo vya mashamba kama vile vya Kengeja na Mtambile.

Mheshimiwa Waziri kwa kweli vituo hivi viko katika hali mbaya sana vinavuja ikinyesha mvua na havilingani na hadhi ya Polisi nakuomba Mheshimiwa Waziri atuangalie kwa jicho la huruma sana sana juu na hali ya ufinyu wa Bajeti hii lakini ningepomba aliangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie kuhusu kuhusu mafao ya askari wetu, tukizingatia askari wetu ndio wenye dhamana wa nchi yetu na wananchi wetu kwa ujumla kwa kweli askari hawa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana ya kimaisha na makazi ningekuomba Mheshimiwa waziri angalau wakapatiwa mikopo midogo midogo angalau ikawasaidia kwenye maisha yao. Baada ya hapo Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi kwa askari wetu Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya vituo kama hivyo nilivyovitaja havina mawasiliano ya aina yoyote wala usafiri Mheshimiwa Waziri hiyo ni hatari. Ikitokea tatizo lolote askari hawa wafuatilie kwa miguu hata baiskeli imewashinda kuipata ningekuomba basi angalau askari hawa wapatiwe japo Vesper moja kila kituo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nazungumzia kuhusu uingizaji wa biashara kiholela. Lazima Serikali iwe na uangalifu mkubwa wa biashara zinazoingizwa kiholela, hasa biashara zile zisizoonekana haraka kwa mfano kama sigara.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *T.B.S.* iweze kutafiti bidhaa kwa uwezo wake wote ili kuhakikisha ubora, watumiaji na ubora wa bidhaa husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

MHE. MWADINI ABASS JECHA:Kwanza Mheshimiwa Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa matumaini mema iwapo itatekelezwa ipasavyo.

Aidha, nimpongeze pia kwa ujasiri wake akishirikiana na wenzake katika suala zima la utekelezaji wa muafaka wa kisiasa uliofikiwa baina ya vyama vya *CUF* na *CCM*, jambo ambalo limepelekea kufanyika kwa semina maalum ya Makamando wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, matunda yake, kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri, yameonekana kwenye uchaguzi mdogo uliofanyika Mei mwaka huu. Ni imani yangu kwamba Makamanda hao nao watachukua juhudi ya kuwaelimisha askari wa chini kabisa ambao ndio wanaofanya kazi kwa kushirikiana na raia ili kuondoa msugurano baina yao ambao umedumu kwa muda mrefu sasa kutokana na sababu kwamba Jeshi la Polisi (na majeshi mengine) yamekuwa yamejawa na ushabiki wa kisiasa. Jambo ambalo lilipelekea kuwanyanyasa wafuasi wa vyama vya upinzani.

Mheshimiwa Spika, laizma nikiri kwamba unyanyasaji wa Polisi kwa vyama vya upinzani umeondoka kwa kiasi kikubwa hali inayopeleka vyama hivyo kufanya shughuli zao za kisiasa bila bughudha yoyote. Ingawa bado wapo baadhi ya Polisi wachache ambao wanatumiliwa na wanasiasa kutekeleza utashi wao. Mfano mdogo wa hayo, ni lile sakata la Mheshimiwa Abdubakar Khamis Bakar, Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni namna alivyodhalilishwa na *RC* wa Mkoa wa Kaskazini kwa kutoa matangazo kupitia vyombo vya habari kuwa Mheshimiwa Abubakar alijiandikisha mara mbili kuwa Mpiga kura katika uchaguzi mdogo uliopita. Jambo ambalo Mheshimiwa Spika halikuwa la kweli na lililenga katika kumdhalilisha yeye pamoja na chama chake cha siasa.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri achukue hatua za ziada kuona kwamba vikosi vyake vinajisafisha na aibu hii. Aidha, ninamwomba pia ajitahidi kuhakikisha kwamba ile nidhamu inayoonyeshwa na Jeshi la Polisi kule Zanzibar basi na kwa upande wa Tanzania Bara pia iimarishwe.

Uajiri katika Jeshi la Polisi. Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo kuhusu suala la uajiri linavyotekelezwa na Jeshi hili hususan kule Pemba. Kwanza naomba niupongeze utaratibu ambao umebuniwa wa kuzigawa nafasi za uajiri kwa kila Mkoa. Ni utaratibu mzuri unaotoa fursa ya uajiri katika Mikoa yote ya Tanzania. Na ninaomba utaratibu huo uendelezwe kwa maslahi ya Watanzania wote.

Lakini Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tuna utaratibu mzuri, pamejitokeza tabia mbaya miongoni mwa wakubwa wa Jeshi hasa katika ngazi za Mikoa na Wilaya zinapokuja fursa za kuajiri vijana kujiunga na Jeshi hilo, mambo yanafanyika kwa upendeleo mkubwa. Baya zaidi ni ile tabia iliyoshamiri ya kugawa ajira hizi kwa ndugu na jamaa wa wakubwa hata kama ndugu na jamaa hao hawaishi katika maeneo yaliyokusudiwa. Wale wanaostahili wanazikosa nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linakatisha tamaa vijana na wanaliona Jeshi la Polisi kuwa ni jeshi la watu maalum na wengine hata kama wanazo sifa lakini hawastahili kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri suala hili alitupie macho sana na kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote watakaonekana kufanya upendeleo katika uajiri na ile Mikoa ambayo imeathirika basi wapewe nafasi za uajiri za ziada kufidia dhuluma waliyofanyiwa. Tukifanya hivyo jeshi la Polisi litajenga heshima yake mbele ya macho ya jamii.

Suala la Paspoti: Mheshimiwa Spika, miongoni mwa haki za raia ni kusafiri nje kwenda nchi anayotaka alimuradi havunji sheria. Na ili uweze kusafiri nje ya nchi unalazimika kumiliki paspoti ambayo pia itakuwezesha kuingia nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, aidha paspoti ni moja ya vitambulisho rasmi wa uraia wa mtu. Na kwa hiyo kuna ulazima wa kila raia kumiliki paspoti yake.

Mheshimiwa Spika, kilio cha Watanzania walio wengi ni upatikanaji wa paspoti kutoka katika Ofisi za Uhamiaji. Maombi yanakuwa ni mengi lakini wanaopata ni wachache na pengine baada ya usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiambiwa mara kwa mara kwamba upatikanaji wa paspoti utaratibu wake ni rahisi kutekelezeka. Lakini hali halisi haionyeshi hivyo hasa ukizingatia idadi ndogo sana ya Watanzania wenye kumiliki paspoti. Sasa ili kuliondoa tatizo hili angalau kwa kiasi fulani basi ninamshauri Mheshimiwa Waziri kwanza aongeze kutoa taaluma kupitia vyombo vya habari namna ya utaratibu unavyopaswa ufuatwe ambao utamrahisishia Mtanzania kumiliki paspoti bila usumbufu mkubwa. Aidha utaratibu wenyewe nao ufanyiwe marekebisho au uboreshwe ili kupunguza urasimu ambao umekuwa ni kero kwa wananchi.

Baada ya kuchangia hayo Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Spika, naomba kusema naunga mkono hoja hii na namwomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake utekelezaji mwema.

Pamoja na hayo napenda kuchangia machache yafuatayo:-

(1) Kumeanza kujitokeza mtindo mbaya (*syndicate*) ya wakazi wanaokaa karibu na barabara kuu kufanya vitendo vinavyosababisha ajali kubwa na halafu kuiba vitu vya majeruhi lakini baya zaidi ni kuwavua nguo na hata kuiba vifaa kutoka kwenye magari kwa mfano matairi, redio na kadhalika. Napendekeza utaratibu uandaliwe ili uongozi wa Wilaya ziliopo katika barabara kuu wahamasishwe ili waweze kuwadhibiti watu wao.

(2) Napendekeza makao makuu yawe yanapeleka migao ya Wilaya huko huko ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji. Makamanda wa Wilaya wawezeshwe kifedha na vitendea kazi kwa vile wao ndio walio karibu na wananchi.

(3) Naomba kurudia kilio na ombi langu la miaka miwili (mfululizo) ya kutaka nyumba za askari polisi kituo cha Mazizini - Zanzibar zimalizwe kujengwa kituo hiki ni moja katika vituo muhimu sana Zanzibar na kiko katika maeneo ambayo viongozi wote wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano - Tanzania Bara wanakaa. Hivyo naomba sana kiimarishwe ili kiweze kutoa huduma nzuri zaidi.

(4) Napendekeza suala la magereza na haki za binadamu litazamwe kwa undani sana ili tusifikishwe mahali tukaja kuona aibu siku za usoni.

Napenda kusema tena naunga mkono hoja hii, Ahsante.

MHE. MARTHA M. WEJJA: Naunga mkono hotuba ya Wizara hii.

Jeshi la Majini (*Police Marine*) limesahauliwa wala halitajwi kabisa. Linakosa gani? Jeshi hili lipewe boti za kufanyia kazi, kwani eneo hili linafanya kazi kwa hali ngumu. Halina vitendea kazi - wapewe.

Rushwa inaonekana kwa sababu tumewasahau mno. Manne liongezwe mishahara ili wanapopambana na wahalifu wasiwe wanashawishika kupokea rushwa. Kituo kibaya, nyumba mbovu, vitazamwe upya.

Kitengo cha Uhamiaji nacho kimesahauliwa. Uhamiaji ndiyo inaingizia Serikali kipato. Naomba askari hawa wakumbukwe kupewa maslahi ya kutosha kuepuka vishawishi vya rushwa.

Kuhusu maslahi, Jeshi hili litazamwe upya mapato yao yako chini sana bila maslahi ya mishahara tunasababisha kuwapa tamaa watumishi hao na kushawishika kupokea kidogodogo.

Magereza: Jeshi hili ni jeshi lenye uwezo kabisa wa kuzalisha. Mfano:-

Kilimo: (1) Kilimo chakula;
(2) Ufugaji kuku na ng'ombe.

Viwanda: (1) Ushonaji nguo;
(2) Utengenezaji sabuni;
(3) Utengenezaji vikoi na kadhalika.

Kama jeshi hili lingewezeshwa nina hakika wangeweza kujitoleza kwa vyakula magerezaji, kujitosheleza kwa kupata fedha za kuendeshea jeshi zima kutokana na mapato ya uzalishaji niliyotaja hapo juu.

Inasikitisha kuwa uzalishaji huo sasa hakuna yote haya yameletwa kutokana na kutowezeshwa. Nyumba za wafanyakazi. Jeshi hili lina uwezo kabisa wa kujenga nyumba za kutosha za Maofisa Magereza.

Tatizo: Uwezeshwaji au viongozi wanaohusika hawatili mkazo suala la ujenzi wa nyumba kwani magereza wafungwa huenda kujifunza na kufanya kazi. Naomba ari ya kuinua uchumi kwa kutumia vyanzo nilvyovitaja.

Maslahi: Jeshi hili litazamwe upya mishahara yao ili wapate moyo wa kutenda kazi zao vizuri.

Kupandishwa vyeo: Inasikitisha sana jeshi hili kupandishwa vyeo lazima waende kusomea (kuhenyeshwa). Lakini hupelekwa chuoni baada ya kuwa ametumikia jeshi miaka mingi amezeeka ndipo anaenda kuhenyea cheo. Akitoka chuoni hukaa miaka miwili mitatu anastaafu. Naomba jambo hili litazamwe upya. Mtu aende chuoni angali na nguvu, ili naye afurahie masomo yake.

Hivi kweli Wizara haijui kwamba jeshila Polisi upande wa *Traffic* linanuka? Linajenga majumba ya ajabu kwa ajili ya kazi za rushwa. Au na sisi Wabunge tutoe rushwa Wizarani ili Wizaa itusikie. Jeshi hili liondoshwe patafutwe njia nyingine *Traffic* rushwa inanuka haina dawa kama ugonjwa wa ukimwi unavyonuka hauna dawa. Wizara iseme hakuna dawa ya kuondosha rushwa kwenye jeshi la *Traffic*. Ili tusiendee kupiga kelele bure bila mafanikio. Naunga mkono.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Omar Mapuri, Waziri na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuleta hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hotuba hii na kupendekeza bajeti ya Wizara ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kunga mkono hotuba hii naomba nimkumbushe Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa kwa upande wa jeshi la Polisi nilileta kero maalum inayohusu kukosekana kwa usafiri katika kituo cha Polisi cha Ndanda, Wilaya ya Masasi katika jimbo langu la Masasi, Mkoa wa Mtwara. Kituo cha Polisi Ndanda sio kituo cha kawaida kwani kinahudumia wananchi karibu laki mbili (170,000 watu), umbali wa km.70 toka Chigugu mpaka Nanganga. Kuna askari polisi 22 lakini hawana usafiri hata kidogo. Ipo pikipiki ya zamani ambayo hata kwa kuiwasha inabidi msukume, yaani haifai kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya aina hii huduma wanayotoa polisi ni duni na haifai. Uhalifu ukitokea inabidi mwathirika binafsi atafute usafiri wa kumpeleka mhalifu kituo cha polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilipoandika barua mwanzoni mwa mwaka huu kuelezea hali mbaya hii, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alimwandikia barua Inspekta

Jenerali wa Polisi ili atusaidie mpaka wakati huu wa Bajeti, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na polisi makao makuu kutatua tatizo hili. Wamekaa kimya tu.

Mheshimiwa Spika, kukaa huku kimya ndiko kunakoongeza kero na hasa hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la wachimba madini sehemu za Nanganga, Nangao na Mbwinji, ambao wamekuja toka karibu mikoa yote ya Tanzania. Hali ilivyo ni ya kuharibu amani na utulivu na polisi wasio na usafiri wanashindwa kabisa kuzuia uhalifu. Wananchi wa eneo hili hawakuzoea hali ya uhalifu wa kitaifa na kimataifa unaoanza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anielezee hatua atakazochukua kuondoa ama kupunguza matatizo ya usafiri katika kituo cha polisi cha Ndanda, kabla sijaunga mkono kwa dhati hoja yake. Kero hii, mimi kama mwakilishi wa eneo hili, imefikia mahali ambapo taifa lisaidie kwani mkoani nako hali yao ya usafiri sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, endapo Waziri hatanitosheleza kujibu hoja yangu, suala hili nitalileta wakati wa majadiliano katika Kamati ya Matumizi ya Wizara hii.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA: Mheshimiwa Waziri kwanza ninakupongeza wewe, Naibu Waziri na wataalam wako wote kwenye Wizara. Hotuba yako ni nzuri na fupi ya kutosheleza.

Mheshimiwa Waziri jimbo la Morogoro Kusini hali sasa ina vituo viwili vya polisi, kimoja kipo Matombo na kingine ni Polisi wa *Railway* kituoni *TAZARA Station*. Vituo viwili havishirikiani sana kwani kile cha Kisaki Station kinashughulikia huduma ya reli ya *TAZARA*. Kituo cha polisi cha Matombo kinafanya kazi kubwa ya kuhudumia jimbo lenye eneo la sq. km. Efu 9.43 na lenye milima mingi mirefu, na kuenea kiasi cha theluthi mbili cha jimbo zima.

Mheshimiwa Waziri kwa hivi kuna juhudi ya kujenga vituo vya polisi katika vijiji vya Tawa, Mocha na Duthumi.

Matatizo ya Kituo cha Polisi Matombo ni haya yafuatayo:-

1. Kituo hakina polisi wa kutosha;
2. Maeneo ya kufanya kazi ni makubwa na mapana mno;
3. Kituo hakina usafiri wa aina yoyote.

Mheshimiwa Waziri hapa ipo haja ya kuzungumzia suala la usafiri. Polisi hawa wachache inabidi wasafiri mwendo mrefu sana kwa aidha kutembea kwa miguu ama hupanda ma-bus huku wakiwa wamebeba silaha. Pale ambapo inabidi kuwa na wahalifu hakuna budi ila kufuatana nao kwa miguu ama kwa malori.

Mheshimiwa Waziri naomba nitoe la upendeleo la kukuomba uwapatie kituo cha Matombo gari ili lisaidie sana kazi ya polisi ifanyike kwa ufanisi. Kituo cha Polisi Matombo nyumba mbili zimebomoka miaka mingi iliyopita. Naomba nyumba hizi mbili zijengwe upya ili polisi wasiishi kwenye nyumba za raia.

Pale vituo vya Mvuha na Duthumi vikikamilika naomba wapewe *Radio Calls* ili kufanya kazi zao vizuri zaidi. Ni vizuri zaidi kama kituo cha polisi Duthumi kikikamilika kipewe usafiri ili kuhakikisha ufanisi wa kazi za polisi.

MHE. ALLY SAID JUMA: Mafunzo ya polisi: (a) Chuo cha Polisi cha mafunzo ya awali Tanzania nzima ni kimoja. Hii ni hatari sana kwa nchi kubwa kama hii ya Tanzania na ndio maana polisi wa Tanzania hasa Zanzibar mara nyingi hufanya kazi zisizo wahuu na hata kujaribu kutumbukia katika mchezo wa siasa matokeo yake huingia hatiani. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri nakuomba uongeze vituo Tanzania nzima angalau vinne badala ya kimoja.

(b) Ulinzi kwa vyama vya upinzani: Mheshimiwa Waziri, kuna ubaya gani kwa vyama vya upinzani kua na ulinzi wake? Naomba jibu. Mheshimiwa Waziri hakuna chama chochote cha upinzani Tanzania kinachomiliki silaha. Sasa kuna ubaya gani kua na vijana wake kukilinda chama hicho. Ni vyema Mheshimiwa Waziri unipe ufafanuzi wa wazi kuhusu suala hili ndani ya Bunge hili tukufu ili kuwepo na uwazi juu ya vyama vya siasa na ulinzi wao.

Tafsiri ya neno *Intelligence Officer's*: Mheshimiwa Waziri naomba unifafanulie maana ya neno *intelligence officers*. Mheshimiwa Waziri, katika mawizara ya Serikali ya Tanzania mna *intelligence officers*? Ni nini hasa *intelligence officers*. Bajeti ya Wizara yako tumeipitisha au hatutaipitisha kwa moyo mkunjufu lakini pia ni vyema utupe maana ya madukuduku yanayo tukereketa, kama hili la *intelligence officers*; kwenye Mawizara ya Serikali ya Tanzania. Naomba jibu ndani ya Bunge hili tukufu. Ahsante.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika:-

(1) Katika hotuba ya Waziri ameeleza mpango wa Wizara yake 2003/2004 kujenga/kukarabati magereza ya Butimba, Maweni, Vyui na Ukonga:-

(a) Je, inakuwaje katika Wilaya ambazo hazina kabisa magereza au mahabusu kwa mfano Igunga ambao wanategemea zaidi gereza la Nzega.

(b) Kwa nini jesho la magereza lisitumie nguvu kazi kubwa waliyo nayo (wafungwa) ili kuanzisha majengo ya magereza, nyumba za askari, mahabusu, halafu Serikali ikakamilisha kama inayofanya MEM?

(2) Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi wao na mali zao ni dhana sahihi kinachotakiwa ni Wizara kuwapa semina walinzi wa jadi (i.e. sungu sungu; wasalama). Inakuwa mara nyingi walinzi wa jadi kutumika Serikali inaposhindwa

kupambana na majambazi. Walinzi hawa ambao hawana silaha, elimu ya sheria na kupambanishwa na majambazi yenye silaha.

- Kwa nini sungu sungu huandamwa sana na polisi hasa wanapoua majambazi?
- Mwisho naunga mkono hoja.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kuchangia angalau kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya yote napenda kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyoiwasilisha hapa kwa niaba ya kuipitisha. Ila napenda kutoa kilio changu cha Wilaya ya Geita. Katika miaka ya 1995 Wilaya yetu ilikuwa na idadi ya watu laki nne (400,000) lakini hivi sasa imeongezeka kama mara mbili ambapo sasa ina wakazi (712,195) idadi hii kiwilaya ni kubwa mno hivyo matukio mbalimbali yanaweza kujitokeza hasa na kutokana na machimbo makubwa ya dhahabu na baadhi ya wakimbizi kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la watu hawa naomba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yafuatayo:-

- (i) Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza magari ya *patrol* katika Wilaya ya Geita ambayo ni kubwa kiutendaji.
- (ii) Kuongeza askari hasa katika vituo vya Tarafa za Kasamwa, Bugando, Butundwe, Bukoli, Nyang'hwale na Kharumwa.
- (iii) Askari kuongezewa mishahara ili waondokane na tamaa ya rushwa.
- (iv) Wizara isaidie kumalizia vituo vidogo vya polisi kama kile cha Kasamwa ambacho hivi sasa kimebakia kupigwa bati tu. Kama Wizara itapata na kutoa msaada wa bati basi kituo hiki kitaanza kazi mara moja.
- (v) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iwashirikishe wananchi na jeshi la sungusungu katika kukabiliana na matatizo mbalimbali ya uhalifu.
- (vi) Wizara iongeze fungu la mafuta katika Wilaya kwa kuwa ni kubwa na inahitaji kuzngukiwa mara kwa mara.

Mwisho, naunga mkono asilimia mia moja.

MHE. ROBERT K. MASHALLA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hotuba hii naiunga mkono asilimia mia. Lakini kabla sijatoa mchango wangu kwenye bajeti hii, nitoe pole kwa ndugu na jama wa marehemu waliopoteza maisha yao

kwa ajali ya bus lililoanguka na kuua watu wanne kwenye eneo la kijiji cha Msonga (W) Bukombe. Mungu azilaze mahali pema roho za marehemu, amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie matatizo yaliyomo kwenye jeshi la Polisi ambayo pia yanasababisha kero kwa wananchi wetu. Kwanza kabisa jeshi la polisi linashindwa kuwajibika ilvyo kwa sababu ya mawasiliano duni yaliyopo kwenye vituo vya polisi. Matukio mengi yamekuwa yakitokea na sasa kukosa msaada wa polisi kwa vile polisi wedtu hawana mawasiliano. Kwa mfano, Mwaka jana katika wilaya yangu ya Bukombe majambazi waliteka mabasi na gari za mizigo muda wa saa 9 mchana na utekaji huo ulichukua muda wa masaa matatu wananchi hawa hawakupata msada wa polisi kwa vile hata makao makuu ya polisi (w) hakuna simu hivyo Serikali inatakiwa kuimarisha ulinzi kwa kuwa na mawasiliano ya uhakika Wilayani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la usafiri kwenye vituo vyetu vya polisi hasa makao makuu ya Wilaya. Binafsi namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Chiligati kwa ushirikiano wake alioutoa wakati nikifuatilia gari la kituo cha polisi Ushirombo gari hili nilipewa na sasa linahudumia wananchi na askari wa Ushirombo pamoja na huduma hiyo niliyoipata bado tatizo la usafiri halijaisha kulingana na ukubwa wa eneo na idadi kubwa ya watu walioko kwenye wilaya hivyo naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza magari kwenye makao makuu ya Wilaya ikiwemo Wilaya ya Bukombe yenye vijiji 128 na wakazi 396,426.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe Serikali juu ya malalamiko ya wananchi wa Bukombe juu ya utendaji mbovu wa baadhi ya askari wa kituo cha polisi Ushirombo. Malalamiko haya ni ya siku nyingi sasa na Serikali ina taarifa nayo kwa vile yamewasilishwa kimaandishi lakini hata mimi kama mwakilishi nimeeleza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali mpaka sasa haijachukua hatua yoyote. Naomba Serikali ichukue hatua kwa wahusika ili wananchi waendeleo kuwa na imani na jeshi lao la Polisi. Wahamishwe wananchi wa Bukombe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RITA L. MLAKI: Kwanza nakupongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayofanya katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaelewa kuwa ni Wizara kubwa na ngumu sana.

Natoa pongezi kwa hotuba nzuri ya bajeti na pongezi zifike kwa watendaji wote wa Wizara yenu kwa kazi nzuri wanayofanya kipekee niwataje *IGP* na *DCI* kwa kazi nzuri isiyo na kifani ya kupambana na ujambazi kwa kiwango kikubwa. Naomba nichangie jambo moja tu la rushwa.

Tunapata malalamiko mengi kuhusu kero ya rushwa katika eneo la *Traffic* barabarani. Ni *petty corruption but* inawakera sana wananchi na kuchafua jina lenu kabisa. Wananchi wanashukuru kwa juhudi mnazofanya lakini bado vijana wenu hawasikii. Naomba nitoe ushauri ufuatao:-

(1) Kuwepo na campaign maalum ambayo mtaitangaza kwa nguvu kabisa kupiga vita rushwa ya *Traffic Police*. *It's a psychological campaign* ili polisi wajue na waogope. *Campaign* hiyo ifanyike *may be for a month* na hakika mtawakamata wengi. Wananchi watafurahi kuona Serikali inajali na watakuwa wakitoa ushirikiano mkubwa.

(2) Ombeni bajeti yenu iongezwe ili mwongeze mishahara ya polisi na vitendea kazi kusema ukweli *Police/Traffic* wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Labda kwa hali hiyo wanajikuta wanaomba rushwa kwa nguvu. Nawatakia kila la heri ktika kazi hiyo ngumu na naomba kusema naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED ALI SAIDI: Mheshimiwa Spika, naomba mishahara ya askari polisi iangaliwe vizuri, kwani mishahara yao bado haijakidhi haja kulingana na ugumu wa kazi zao na mtiririko wa maisha tulio nao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu paspoti tunajua kua kwa mujibu wa Katiba yetu, basi paspoti ni haki ya kila raia wa Tanzania, kwa hivyo hatuoni kua kuna haja ya kunyimwa au kusumbuliwa kwa haki hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni vitambulisho, ili kudhibiti uhalifu basi ni vyema kila Mtanzania apatiwe kitambulisho bila ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msongamano mkubwa ulioko kwenye magereza naomba mambo yafuatayo yashughulikiwe:-

(a) Askari wanaoshughulikia uchunguzi wa kesi za watuhumiwa wawekewe muda maalumu katika uchunguzi wao.

(b) Wale watuhumiwa wanaowekwa mahabusu wapewe dhamana ya kuwoko nje huku wakiendelea na kesi zao baada ya wiki mbili (2) kukaa kwao gerezani. Isipokuwa wale wenye makosa makubwa kama ujambazi, mauaji na kadhalika.

(c) Wale watuhumiwa wanaopatikana na makosa madogo madogo kama wizi wa nazi, ndizi, kuku na kadhalika kifungo chao kisizidi miaka miwili.

(d) Magereza yaongezwe kujengwa, angalau chumba chenye ukubwa wa *square ft.* 100) kichukue watu wasiozidi wanne.

(e) Vyumba vya magereza visafishwe na viwekwe vitanda au japo magodoro yaliyo mazuri.

(f) Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa nchi yetu askari tulionao bado ni kidogo sana. Kwa hiyo tunaomba askari zaidi wafikiriwe. Lakini pia katika kuajiri askari masuala ya ubaguzi lazima yasiwepo kwani kule kwetu Pemba mtu ambaye ana itikadi ya *CUF* basi ni vigumu kuajiriwa hata ikiwa ana sifa zote zinazotakiwa.

MHE. MCHANDE SALIM MCHANDE: Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi na makadirio na matumizi ya Wizara hii lakini napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wastaafu wengi wa jeshi la polisi hata baada ya kustaafu kazi na kurudi uraiani ni muda mfupi tu huanza kuhangaika na maisha baada ya kutumikia taifa kwa muda mwingi kwa uaminifu kuanzia vyeo vya Kamishna kuja chini.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba wastaafu basi wapewe kitu cha msingi ili kuendeleza maisha yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi kufanya ukarabati baadhi ya majengo ya vituo vya polisi Kisiwani Pemba hasa lile jengo la kituo cha polisi lililopo katika jimbo langu la Konde (Kituo cha Polisi Konde).

Mheshimiwa Spika, aidha naishauri Serikali kupitia Wizara husika kituo hicho cha polisi Konde kupatiwa gari kwani gari lililopo ni bovu. Naiomba Wizara iyafikirie hayo.

Mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Ahsante.

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Spika, nianze maelezo ya mchango wangu wa maandishi kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP, DCI*, Kamishna Mkuu wa Magereza, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii kwa hotuba na mpango mzuri wa Wizara yao katika jukumu lao kubwa na gumu la kikatiba katika nchi yetu - Ibara ya 147 kifungu kidogo cha (2), Ibara hii inaweka bayana jukumu la Wizara hii lile la ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao. Hivi sasa hali na jukumu hili la kikatiba limelegalega kwa sababu ya maeneo yafuatayo kuonyesha udhaifu kwa kuachiwa huru kwa miaka mingi tangu tupate uhuru.

Bila shaka zimekuwepo sababu za kisiasa hasa kutokana na harakasti za ukombozi wa Bara letu la Afrika na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika kung'ang'ania utawala wa nchi Barani Afrika. Nchi nyingi za Afrika na hata nje ya Afrika wakatuchukua sisi ni *PANAFRICAN COUNTRY*. Viongozi wetu nao ndio uliokuwa wimbo wao mkuu ndani ya nchi na nje ya nchi. Hali hii ilitufikisha kubaya na hata kuathiri uchumi wa nchi yetu na kutufikisha hapa tulipo! Sasa lazima kuweka mikakati ya kujihami na hii historia ya *Panaffricanism* ambayo kwayo tuligharimia ukombozi wa nchi nyingi za Afrika bila mikataba ya fidia na kutuacha maskini baada ya nchi hizo kujitawala! Tusililie maji yaliyomwagika bali tujizatiti upya kwa kuboresha maeneo yafuatayo katika ulinzi na usalama wa raia wetu ndani ya Tanzania.

La kwanza ni kudhibiti raia wa nchi za jirani kupenyeza na kuishi kiholela nchini. Sambamba na hli ni kudhibiti wakimbizi. Hili linawezekana kwa kuweka vitambulisho vya raia wetu. Pia kuhakikisha wakimbizi wote wanapewa vitambulisho vya mashirika

ya kimataifa wanaowahudumia wakiwa nchini kwetu. Kweli zoezi zima la vitambulisho ni ghali lakini wahenga wamesema: “Rahisi Ghali”, “usipoziba ufa utajenga ukuta” na “Ukitaka asali chonga mzinga”. Kwa sababu ya mwanya huu nchi yetu imetumbukia katika wimbi la ujambazi. Naiomba Wizara iletee “Haki ya Raia” katika katiba ya nchi - Ibara ya 30(2). Iko mifano hai ambapo watu ambao ni raia wa nchi zingine wamejipenyeza hapa nchini na kuishi hadi kusoma mpaka Chuo Kikuu kwa gharama za nchi na hatimaye kupewa uteuzi wa ngazi za *IGP, DC*, na kadhalika. Hivi sasa ninazo habari kutoka mkoa wa Morogoro kuwa wapo Wahutu/Watusi wameingia hapo kununua nyumba na mashamba ya watu kwa bei nzuri katika vijiji vya Dutumi na Mvuha. Naiomba Wizara iwe macho na utaratibu wetu wa ulinzi wa zamani wa kudhibiti wageni ufufuliwe.

Jambo la pili mafunzo na upungufu wa askari nchini. Ipo haja ya muda wa mafunzo haya kuongezwa ili kupata *Police Constable* wenye mafunzo imara. Hili liendane na kuweka mitaala au *curriculum* mpya itakayoendana na mabadiliko ya uchumi na kijamii duniani. Naamini mitaala yetu inayotumika sasa imepitwa na wakati. Sambamba na hili ni askari waliopo katika jeshi la polisi au magereza bila elimu. Hawa wangeondolewa na kupangiwa kazi zingine zisizo za ulinzi/usalama wa raia. Kama nitakavyoshauri hapo baadaye askari wanaostafishwa wawe bado katika uangalizi wa Serikali vinginevyo wao wenyewe wakikosa njia za kipato watageuka kuwa majambazi kwa sababu wanazifahamu mbinu hizo. Ili pia kukabili upungufu wa askari nashauri Wizara iweke chuo cha pili cha mafunzo kwa kile cha *Moshi CCP*. Hali hii itaongeza idadi ya askari ili kutosheleza mahitaji. Kule katika wilaya yangu ya Same tunao upungufu wa askari hasa Idara ya upelelezi.

Ukitoka kwa *OC-CID* askari anayefuata na ambaye ni yeye pekee katika Idara hiyo ni P/C. Idara ina watumishi/askari wawili tu! Namwomba Mheshimiwa Waziri alipatie hili majibu katika majumuisho yake. Askari wawili au hata watatu hawawezi kazi za upelelezi wa Wilaya nzima ya Same - Wilaya ambayo ndiyo kubwa zaidi ya Wilaya zote Mkoani Kilimanjaro. Wilaya hii ni mara mbili kwa ukubwa kwa Wilaya ya Hai, Mkoani Kilimanjaro na ina mazingira magumu sana ya kukosa miundombinu ya barabara, simu na umeme. Vyote hivi ni vigezo vya kuhamasisha usalama wa raia.

Lingine Mheshimiwa Spika, ni kuhusu mazingira ya ajira ya askari. Mazingira hayo yamepelekea baadhi ya askari katika vitendo vya rushwa kwa kukosa mishahara mizuri, sheria ya kulinda ajira zao, huduma ya nyumba na maji, usafiri kwenda eneo la kazi. Haya yanahitaji yaboreshwe ndani ya majeshi chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kule katika Wilaya yangu ya Same kuna uhaba mkubwa wa maji ambao bado Halmashauri ya Wilaya ya Same haijapatia ufumbuzi. Tunajitahidi kuweka mikakati ya kutukwamua lakini majibu yake sio ya upesi! Ili kuwahamasisha askari katika kazi yao ngumu; naiomba Wizara iwapatie magereza na polisi Same kisima kimoja cha maji chini ya ardhi (*borehole*), *pump* na tanki la kuhifadhia maji kwa matumizi yao. Maji haya yatawafaa pia wafungwa wapatao 300 katika gereza la Wilaya Same.

Nilipotembelea Gereza hilo mwezi Mei, 2003 niliona mazingira magumu ya mashimo ya *lessipit* kufurika jambo ambalo linaweza kuleta mlipuko wa magonjwa na kuua sio wafungwa peke yake bali na wananchi wanaolizunguka gereza hilo. Naiomba Wizara ikarabati *sewage system* ya gereza hili na itoe majibu katika kuhitimisha hotuba yake. Maji pia huduma yake ikiwepo itaweza kupatia gereza hili usalama wa afya za wafungwa katika gereza hili. Kwa hiyo naomba liangaliwe!

Mambo mengine ya mwisho ni ya ujumla. Lipo la kudhibiti askari/watumishi wa Wizara wasio na maadili (*reject*) hawa wadhibitiwe badala ya kuhamishwa kutoka Wilaya moja kwenda nyingine au Kata (Kituo) moja kwenda Kata au Kituo kingine. Nashauri pia ianzishwe mahakama/jela ya watoto watundu ili kuwadhibiti raia wa kesho wakiwa wadogo hususani pale ambapo wazaz/walezi wa watoto wamewashindwa na watoto kutobadilika! La mwisho kabisa ni usajili wa *NGO (AZISE)*.

Hizi tunaomba usajili wao ushirikishe wawakilishi wa wananchi ili pale zinaposhindwa ku-*deliver* huduma inayotarajiwa na *AZISE* hiyo katika eneo husika (*Intervention zone*) Wizara iweze kupata *overseer* wa *AZISE* hizi anayekereketwa. Wakuu wa Wilaya ambao wamekuwa *overseer* wa *AZISE* wamekuwa *ineffective* kwa sababu sio wakereketwa. Kuwapatia/kuwashirikisha wawakilishi wa wananchi kutaleta changamoto mpya katika utendaji wa *AZISE* nchini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ayafanyie kazi hayo niliyoyasema na naunga mkono hoja.

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri Omar Ramadhan Mapuri, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mbunge na Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na timu yao kwa juhudi zao za kupambana na vitendo vya ujambazi nchini. Baada ya pongezi hizo naomba nitoe maoni yafuatayo juu ya shughuli za ujambazi ulivyokithiri Jimboni kwangu Kilwa eneo la Kipatimo.

Mheshimiwa Spika, Kipatimu kulikwa na Kituo cha Polisi, lakini ghafla mnamo mwaka 1999 Kituo hicho kilifungwa na Askari walienda Wilayani. Kuna kituo kimejengwa karibu kikamilika. Mheshimiwa Rais mstaafu alipotembelea Kipatimu tarehe 18 Septemba, 2000 aliwaahidi wananchi kwamba Mheshimiwa Rais kuwa atachangia shilingi 2,000,000 ili kumalizia Kituo hicho. Ahadi hiyo haijatekelezwa hadi sasa, jambo ambalo limeleta tafsiri nyingi.

Mimi kama Mbunge nimejitahidi kufanya kila juhudi ili Kituo kimalizike, lakini bado zijafanikiwa. Hivyo naiomba Wizara inipige jeki angalau shilingi 20,000,000/= (shilingi 5,000,000/= kumalizia kituo na shilingi milioni 15,000,000/= kujenga nyumba za Askari wanne. Tayari nimepanga nyumba mbili ili Askari waanze kutoa huduma ya ulinzi na kutokana na ukarabati wa nyumba hizo mbili Askari watakuja Kipatimu katikati ya Septemba 2003. Wananchi wanauawa na

wanayang'anywa mali zao. Kwa hiyo, wanalazimika kulipa kodi mbili ya ulinzi na maduka yao. Kodi ya kwanza ni ulinzi wa kawaida shilingi 2,500/= kwa mwezi, na kodi ya pili ni kwa ajili ya ulinzi wa majambazi shilingi 2,500/ kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, hali hii inatisha. Nitoe shukrani kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye anadhibiti hali hiyo. Lakini Mkuu huyo hana gari. Gari moja limekufa kabisa. Gali la polisi limekufa *injectorpump*. Mheshimiwa Yahya Kassim Issa Mbunge wa Pemba CCM kachangia shilingi 50,000/= na sisi Wabunge wawili wa Kaskazini na Kusini tumechangia shilingi 50,000/= kwa kila mmoja. Kwa kweli gari hilo haliweza kukidhi matatizo yaliyopo kwani Wilaya ya Kilwa ni kubwa. Tunaomba Landrover haraka sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nitoe wito kwa viongozi wa Wizara, Makao Mkuu ya Polisi ya Upelelezi kuwa na utamaduni wa kutembelea Mikoani na Wilayani kujionea matatizo na maendeleo mbalimbali kabla ya kungoja yatokee matukio makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaamini Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri atayatafutia jibu. Nami naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ni tabia mbaya sana kwa Idara ya Uhamiaji kukamata kote Mikoani wazaliwa kutoka Kigoma kwamba ni Warundi na siyo raia. Je, swali Wajaruo, Wamakonde, Wamasai, Wahaya na Wangoni nao wanatumia na Idara ya Uhamiaji? Naomba jibu ya wazi.

Tatizo la Polisi D 8601 ambaye ni marehemu pesa yake ililiwa na Polisi kwa sababu familia yake imekwishakata tamaa kabisa kabisa. Mimi nimefuatilia kwa muda mrefu sana bila mafanikio. Naomba jibu leo hii la pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya uraia vitapunguza vurugu na Daftari la Orodha ya Wapiga Kura. Ninawatakia kila la kheri.

MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI: Mheshimiwa Spika, na mimi naungana na Waheshimiwa wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao kwa hotuba yao nzuri waliyowasilisha katika Bunge lako Tukufu, taarifa ambayo imeeleza majukumu yaliyotekelezwa na ambayo yamo katika maandalizi ya kutekelezwa kwa mwaka huu 2003/2004 na matarajio yao katika kutekeleza malengo yao. Mimi pamoja na hayo napenda kueleza juu ya hali duni ya Askari Polisi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Askari wa Polisi wa Kituo cha Polisi cha Mkokotoni.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Kituo cha Mkokotoni baadhi yao hawana nyumba za kuishi hapo Mkokotoni, wakitoka kazini Mkokotoni wengi wao wanakwenda Gamba katika nyumba za kupanga, ambapo kwa hali ya wakati wa sasa wa harakati nyingi ni vizuri wajengewe nyumba hapo hapo Mkokotoni. Vilevile wapatiwe vitendea kazi vinayohusika kama gari zao za kufanyia doria za mashua ili

na wao waweze kufuatilia katika kazi zao kama Tumbatu, ambako hakuna barabara ya kupita gari kwani ni bahari yaani ndiyo vipando vyao au wapatiwe boti

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Askari Polisi wanajitahidi katika hatua ya operesheni mbalimbali na wanashirikiana na vyombo vyingine vya dola katika sehemu mbalimbali. Vilevile Askari Polisi wawe na mashirikiano na wananchi kwani ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna masikitiko kwa baadhi ya Askari Polisi kwamba wanapostaafu kazi wanachelewa kupewa mafao yao. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pindi Askari wanapostaafu kwa kumaliza muda wao wapewe mafao yao ili waweze kujiimarisha kufanya kazi zao binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache sina zaidi, ila naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Mbunge Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, kwa hotuba yake nzuri sana na yenye takwimu muhimu. Aidha, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mbunge, Naibu Waziri, Bwana B.S. Mchomvu Katibu Mkuu, *IGP* Mahita, *PCB* Banzi pamoja na watendaji wengine Waandamizi katika Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi wa hali ya juu. Kwa hiyo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ombi kutoka kwa wapiga kura wangu ambao ni Wazabuni wa Idara ya Magereza na wanayo madai yao ya tangu mwaka 2001. Naomba Wizara izidi kuhimiza Hazina ili walipwe mapema maana wanaathirika kibiashara. *PCB* Banzi anaelewa jambo hili vizuri.

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na wasaidizi wao wote ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Magereza, na Uhamiaji kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ninawashauri waendeleze jitihada hizi kwa sababu hali ya usalama wa raia na mali zao inaonyesha kuwa nzuri siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Wizara pamoja na Jeshi la polisi kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kibakwe kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kibakwe. Sasa Kituo kinafanya kazi na hali ya amani na utulivu imerejeshwa pale kijiji na vijiji vyote vya jirani.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki cha Kibakwe hakijapatiwa umeme, radio call na chombo cha usafiri. Ninafahamu hali ya kifedha ya Wziara inaweza isiruhusu kupata vyote hivyo, lakini kama wakiunganishiwa umeme na radio call itakuwa ni hatua

kubwa. Kwa hiyo ninaomba Kituo hiki ambacho kilizinduliwa na Makamu wa Rais, kisaidiwe. Aidha, lipo tatizo la mwasiliano na Kituo cha Polisi cha Mtera.

Tunafahamu umuhimu wa Kituo hiki ambacho kipo kwenye eneo nyeti la uzalishaji umeme nchini. *Radio Call* yao ilikuwa mbovu na ililetwa Dodoma kwa ajili ya matengenezo muda mrefu uliopita hadi leo haijarejeshwa Mtera. Kama *Radio Call* hii ni mbovu kiasi haiwezi kutengenezeka basi ninashauri wapelekewe *Radio Call* nyingine.

MHE. SUMRI A. S. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hotuba nzuri na yenye ufanisi ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Nami naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja.

Katika Jimbo langu kuna matukio mengi ya ujambazi yanayotokea. Mojawapo ni tendo la ujambazi lililotokea mnamo tarehe 7 Machi, 2003 muda wa saa 8.00 usiku katika vitongoji vya Kasanga Tongwe, na Kaselamyage katika Kata ya Ikula. Tarafa ya Karema, na kusababisha kuporwa nyavu, karabai na mali kiasi cha shilingi 2,350,000/= . Kibaya zaidi ni kuwa katika tukio hilo kuna vijana walitekwa na kuchukuliwa na majambazi hao hadi huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika mji wa Moba. Vijana hao bado hatujui hatma yao je, wapo hai au waliuawa . Majina yao ni Tunu Wansenka, Simon Feruzi, Maganga Sokola, John Kilimo, Gervas Pima, naomba tujue hatma ya vijana wetu hao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara itupe msaada wa kumalizia majengo ya Kituo cha Kolisi Karema na Kituo cha Ikola.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusifu huduma zote za Wizara hii, na kutoa pole nyingi na rambirambi tele toka kwangu na wananchi wa Jimbo la Mpanda Magharibi kwa ajili ya vifo vilivyotokea kwa Askari wetu mashujaa . Mungu alaze roho za marehemu hao mahali pema peponi . *Amin.*

Mheshimiwa Spika, tena naunga mkono hoja hii.

MHE. SHARIFA MBAROUK KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba niunge mkono hoja hii. Niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa ufanikishaji Bajeti hii yenye kueleweka na kufahamika

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kutaka kuendeleza ujenzi wa Kambi ya *F.F.U* Pemba. Kambi hii pamoja na uhaba wa majengo inakabiliwa na tatizo kubwa la umeme na mawasiliano na hii kiusalama sio nzuri. Naomba suala hili lizingatiwe na kupata ufumbuzi wa haraka. Pia Kituo cha *F.F.U* kilichopo Matangatuani Konde ambacho kimehamishiwa Finya, lakini bado baadhi ya *F.F.U* wanaendelea kufanya kazi kwenye hicho Kituo ambacho hali ya majengo yake ni mabovu pia naomba nao waangaliwe na wafikiriwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano. Suala la mawasiliano kwa Jeshi la Polisi ni muhimu sana hivyo naomba Wizara kuwapatia Jeshi hili vifaa vya kisasa vya mawasiliano ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Aidha, kuwe na utaratibu mzuri hasa kwenye Mkoa kuwasilisha malipo ya simu ili kuondoa usumbufu wa kukatiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ninaomba jengo la Uhamiaji lilioko Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba lifanyiwe ukarabati kabla ya jengo hilo halijaathirika zaidi.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja sasa naomba msaada wa kuhitimisha mipango ya kujenga Kituo cha Polisi kijijini Kitanda Wilayani Namtumbo (Mkoani Ruvuma). Kamati ya Usalama ya Wilaya Namtumbo imeidhinisha ombi la wananchi kijijini Kitanda kujenga Kituo cha Polisi kwa mpango wa kujitolea. Faida ya kituo hicho ni kama ifuatavyo:-

Moja, Usalama wa mali na watu wa Kata ya Kitanda katika kijiji hiki cha Kitanda kipo zaidi ya umbali wa kilomita 80 toka mji wa Songea (Kaskazini). Pili, Kituo kitasaidia sana kudhibiti ujangili wa *Selous Game Reserve*. Tatu, Kituo kitaimarisha usalama wa watalii (*selous*) Nne, kwa vile mipango ya Wilaya ya Namtumbo tunataka kutoboa barabara kati ya kijiji cha Kitanda na kijiji cha kwa Mpepo Wilayani Ulanga. Tunahitaji *Police Post*.

Mheshimiwa Spika, nilipoonana na wapiga kura wangu kijijini Kitanda hapo tarehe 31 Mei, 2003 wananchi walisema kuwa wao wangechangia yafuatayo:-

- (i) Kufyatua matofali ya kuchoma kwa ajili ya kujengea;
- (a) Kituo cha Polisi na kuweka silaha;
- (b) Nyumba ya *OCS*;
- (c) Nyumba mbili za kukaa familia nne (*units* nne);
- (d) Kujenga nyumba hizo, nne nilizozitaja;
- (e) Kupasua mbao za boriti na mbao za milango/madirisha. Hata hivyo wananchi hawataweza kufanya yafuatayo:-

- (I) Kununua rangi, saruji na nondo za madirisha;
- (II) Misumari ya kenchi na kupigia bati milango na madirisha;
- (III) Kununua bati za nyumba zote;
- (IV) Kununua bawaba za milango na madirisha;
- (V) Kununua vitasa vya milango na madirisha;
- (VI) Kununua komea za milango na madirisha;
- (VII) Mlingoti wa kufunga bendera ya Polisi;

(VIII) Vifaa vya kujengea chumba cha kutunzia silaha.

Tayari Mwenyekiti wa Kijiji Kitanda amepata Ramani ya majengo yote manne. Aidha, Afande (*OCD*) wa Songea - Namtumbo anayo ramani za majenzi hayo (nakala zake).

Pili, naomba sasa tupewe *OCD* au polisi wa Wilaya Namtumbo ili tusitegemee tena polisi (*OCD*) toka Songea kuanzia Julai, 2003. Namtumbo ni Wilaya kubwa sana. Aidha, *DC* yupo Namtumbo. Yupo vilevile *DAS* na Ofisa Usalama wa Taifa (W) Mjini Namtumbo chonde chonde tupate *OCD* wetu wa Namtumbo, Makao Makuu yapo katika highway (Mtwara-Songea).

Mwisho, Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

MHE. DR. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara kwa ushirikiano wa kazi nzuri wanayoifanya. Tatu, pongezi kwa Askari wema wanaojituma katika kulinda amani na utulivu nchini. Nne, yapo maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Askari kukaa muda mrefu katika eneo moja. Hii inawafanya wazoeaana sana na raia na kusahau maadili yao ya kazi. Askari kujiingiza katika masuala ya siasa bila kificho. Ni ukiukwaji mkubwa wa madili yao na kutotendea haki kwa wengine. Bado wapo wasio waaminifu kwa nchi yao na ndio hao wachache wanashirikiana na majambazi katika uporaji; rushwa kwa wasafirishaji, kwa Askari wa barabani *traffic* na kadhalika.

Baadhi ya walinzi katika maeneo ya viongozi wanajisahau na kuacha maadili yao kwa mfano, wanafika katika lindo wamechelewa, wamelewa, na wanaondoka saa wanayopenda. Upo umuhimu wa kuwa-vet Askari wote kabla ya ajira. Wakati umefika sasa wa kuchukua re-recruit ambao wana sifa nzuri, tabia na mienendo inayokubalika na jamii kabla ya kuanza masomo. Upatikanaji wa nyenzo kwa ulinzi na maeneo yasiyofikika kwa miguu *e.g helicopter* na *fast boat* kwa wanamaji. Nyumba za Askari Polisi ni chache na ndogo zinatengenezwa ziko katika hali mbaya

Mheshimiwa Spika, tano shukrani kwa upanuzi wa nyumba Pemba kwa Askari, kuweka katika bajeti. Uendeshaji wa Kambi ya *FFU* Finya (Pemba) ipo haja ya kuweka umeme na simu katika eneo hili. Mafunzo kwa Askari raia (upelelezi) ili waende na wakati, wengi hawajapta *induction course* au *course* za kujiendeleza baada ya *course* za awali lifikiriwe hilo. Udhibiti wa madawa ya kulevya *efforts* zaidi ziongezwe kutafuta *source* ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, nawatakieni mafanikio na shukrani lukuki kwa ushirikiano na Wizara yangu.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, bila kusita napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri wake pamoja na Maafisa, Askari na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi duniani kote ndio moyo wa nchi, hivyo pamoja na kuipongeza Wizara lakini Jeshi linapaswa liongeze nguvu zake katika kuimarisha vifaa vya mawasiliano yaani radio call, kutokufanya mkakati huo ni sawa na kufukuza mwizi usiku wa giza na kubahatisha. Hivyo, ushauri wangu ni bora 'kukata pua kuunga wajahi' ili kuboreka sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itenge fedha maalum kuboresha Jeshi la Polisi upande wa upelelezi, hii itasaidia sana katika kuikinga uhalifu wowote kabla, hii ni kwa sababu wahalifu wote wanatokea mitaani hivyo kuimarisha *section* hii kuanzia ngazi za mitaa kutasaidia sana kupunguza uhalifu.

Mheshimiwa Spika, sifa ya Jeshi la Polisi kwanza lianze kujisafisha lenyewe hivyo nalipongeza Jeshi kwa kumfukuza Afisa wake ambaye alijihusisha na rushwa, lakini pia tungelipata maelezo juu ya kuhusishwa Askari wengine 10 maamuzi yao yamefikia wapi ili haki kwa upande wao ipatikane.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto lazima liimarishwe zaidi ya hapo, na hasa kwa kuongeza magari pamoja na mafunzo juu ya vijana wake, lakini pamoja na lilivyo hivi sasa bado kuna makosa madogo madogo yarekebishwe, hasa kwenda katika matukio bila maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kulizungumzia Jeshi la Polisi bila kutoa mchango wa kuboreshe *section* ya trafiki bado kuna udhaifu wa Askari wachache wanaojifanya Mahakimu wanapowashika wavunjaji wa sheria barabarani kwa kuchukua fedha zao kwa njia ya kificho, hivyo Jeshi liwaangalie Askari hawa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lazima hivi sasa liongeze juhudi za kuimarisha alama za barabarani kwa mashirikiano na Asasi nyingine kwani zipo kila dalili za alama hizo kutoweka kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lilikuwa na Kikosi Maalum cha Majini kikosi ambacho kilitoa msaada mkubwa kwa matukio mbalimbali pamoja na kujikimu wenyewe kwa shughuli zao za ndani, lakini kwa muda mrefu Jeshi limekuwa halitoi sababu ya kutosha kwa kutotoa uzito kwa Askari hawa wa majini.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la kuongezeka kwa uhalifu nchini ni matatizo ya wakimbizi kwani silaha zimekuwa zinaingia kiholela nchini pamoja na wahalifu walioboea kutoka nchi jirani, hivyo nalishauri Jeshi liongeze jitihada za ulinzi wa mipakani pamoja na utaratibu mzima wa uchunguzi kwa wakimbizi walio ndani ya makambi.

Mtindo wa Maafisa wa zamu katika Vituo lazima usisitizwe kufanya ukaguzi wa Vituo vyao hadi mahabusu kwani kufanya hivyo kutasaidia kufahamu mambo yalivyo katika Vituo hasa kujua kama ulinzi unakwenda sambamba na ulivyopangwa pamoja na ukaguzi wa mahabusu, ili kuepusha kasoro ambazo si lazima kukumbana nazo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia napenda kutoa pongezi zangu binafsi kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, hasa kwa kitendo walichochukua baada ya mimi mwenyewe kuibiwa simu yangu ya mkononi usiku wa saa 2.30 baada ya kuliafu Jeshi la Polisi walifika baada ya dakika saba, na baada ya kuwafahamisha walichukua hatua ya kufuatilia na baada ya nusu saa walifika na mwizi wangu wa simu pamoja na simu yenyewe na hivi sasa kesi ipo Mahakamani. Hivyo kupitia kwa Mheshimiwa Waziri napenda kulipongeza Jeshi lote na hasa kupitia Kitengo cha Upelelezi. Ahsante. Kwa mara nyingine naunga mkono hoja hii.

MHE. FRANK G. MAGHOB: Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba yangu ya asubuhi leo tarehe 10 Julai, 2003 naongezea mambo yafuatayo:-

Moja, Serikali ifanye uchunguzi wa kina kabisa juu ya ndege (*helicopter*) zinazotua kwenye mahotel ya Kitalii huko Jimboni kwangu Kigamboni, Tetesi zipo kuwa kuna kitu kama hicho.

Pili, Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo hapa Dodoma na pia Serikali ifanye hivyo hivyo kwenye Mahakama ya Mwanzo (Wilaya) Temeke, Mahakimu hawa hawaisaidii Serikali, bali wanasaidia wahalifu hasa majambazi, kuna malalamiko kutoka kwa baadhi ya Polisi wa kawaida kuwa Hakimu aliyeko hapa Dodoma amekuwa na tabia mbaya hasa anapowaachia watuhumiwa kwa madai kuwa ushahidi uliotolewa hautoshi kumtia hatiani mtuhumiwa, hayo yanazungumzwa wakati mtuhumiwa amekamatwa red handed. Sasa Hakimu kama huyo anataka ushahidi gani zaidi ya kitendo alichokifanya mtuhumiwa. Hakimu huyo amekuwa anatumika sana na majambazi hasa wanaotumia silaha. Pia Hakimu aliyeko Mahakama ya Wilaya ya Temeke ni Hakimu ambaye anatumia vibaya madaraka yake, naomba Serikali imchunguze Hakimu huyo kwani kama huna pesa huwezi kupata haki hata kama wewe mlalamikaji. Tafadhali watu kama hao ndiyo wanaoharibu sifa nzuri ya Serikali yetu.

Naelewa Wizara ya sheria ndiyo inayohusika, lakini vijana wetu wanaofanya upelelezi hushirikiana na Mahakimu wasio waaminifu kwa kutengeneza kesi ili kuhakikisha kuwa watuhumiwa na walalamikaji wasio na uwezo hawapati haki zao, ni vyema Serikali ikiondoa kero kama hizo ili kuisafisha Serikali yetu ambayo imepania kuleta amani kwa wananchi wake na kuwaondolea kero.

Mwisho, Polisi waliofukuzwa kazi huko Mbarali Mbeya kwa sababu ya uzembe wa kusababisha wafungwa (mahabusu) kufa wasitolewe kafara Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kujua chanzo na sio kuwatia hatiani Askari wadogo na Askari hao

warudishwe kazini haraka na bila majadiliano hata kama kwa siri lakini siyo vinginevyo.

MHE. COL. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uwezo nami kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ingawaje machache.

Pili, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya Wizara hii, pamoja na mipango mizuri ya azma ya utekelezaji wa kazi katika Wizara hii kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ya hotuba yake ilivyokuwa nzuri, ninaamini wakipatiwa fedha walizozomba watatekeleza vyema majukumu yao, kwa maana hiyo sina budi kutamka mapema kwamba ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri huo wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini ningeomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi. Nalipongeza Jeshi kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya, lakini ninaomba mafunzo ya mbinu za kijeshi lazima ziongezwe na ziende kulingana na hali ya wakati unavyokwenda, hali hiyo inaendane kwanza na vifaa bora vya kisasa na pili mafunzo yenye mbinu ya kisayansi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Kikosi cha Polisi kilichoko katika Jimbo langu la Bumbwini huko Unguja.

Mheshimiwa Spika, niliomba mwaka jana 2002/2003 kushughulikiwa Kituo hicho kutokana na ubovu wake wa jengo, hakina gari la usafiri wa aina yoyote na hakina radio call ya mawasiliano wala simu ya kuaminika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha masuala yake, naomba anipe jibu aidha, kuna Kituo cha Polisi tumekijenga kipo maeneo ya Magapwani, Kituo hicho kimejengwa na wananchi pamoja na wafadhili na Kituo hicho kimebakia kujengwa vyoo na mambo machache tu, Mheshimiwa Waziri namwomba aende akakiangalie na ninaomba mchango wake ili kimalizike kwani hivi sasa kina karibu miaka 10 hajamalizika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magereza. Ninalipongeza Jeshi la Magereza kwa juhudi na bidii yao ya kazi za kuwalinda wahalifu na kuwafunza katika kujirekebisha ili wawe wananchi wema. Lakini bado kuna matatizo katika magereza yetu hali ni mbaya mengine ni mabovu kama lile la Ukonga. Magodoro yao ni mabovu, viroba vile ni kilio mwilini endapo ataenyeshewa na mvua hakuna kingine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri azisaidie sana Magereza kwani ninashauri afanya ziara za ghafla katika majengo hayo ya Magereza. Aidha, namwomba Mheshimiwa Waziri awasaidie vitendea kazi na huduma kwa Askari na Maofisa wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, magereza ilikuwa na viwanda vizuri na vya mfano, lakini leo vimekufa vyote sivyo seremala wala ushoni, utengenezaji wa sabuni na kadhalika. Mheshimiwa Waziri uvifufue kwani vinao uwezo wa kuingia kwenye soko la ushindani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri na Mheshimiwa Capt. John Chiligati pamoja na Katibu Mkuu, Makamishna na wataalam wote waliohusika na kutayarisha hotuba hiyo nzuri yenye kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ninaipongeza Wizara kwa kazi nzuri pamoja na ufinyu wa bajeti wa Wizara hiyo ukilinganisha na majukumu makubwa yaliyopo katika Idara zake zote; Polisi, Magereza Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji na ile ya huduma kwa wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa jumla ninashauri Idara zote zipate mafunzo kwa watumishi wake ili waweze kumudu kazi zao vizuri. Mbinu za uhalifu ni za kisasa na zinatumiwa kwa ulimwengu wa kisasa. Hivyo mbinu za polisi na magereza kiutendaji lazima ziende na wakati kwa kupewa mafunzo ya kisasa katika taaluma mbalimbali. Pia nashauri maslahi yao yaongezwe kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, naomba Idara ya Polisi iwe macho sana wakati huu ambao wananchi wanapotarajia kuuza mazao yao mbalimbali nchini kote kwa tahadhari ya fedha bandia. Hivi karibuni Benki Kuu imetoa fedha au noti mpya ambazo zinaendelea kusambazwa na za zamani kutoweka. Kwa bahati mbaya baadhi ya noti hizo mpya zimeishaigizwa na noti hizo bandia zinazidi kuzagaa katika maeneo mbalimbali nchini mwetu.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na polisi kufuatilia uhalifu huu napendekeza Polisi Wilayani na vijijini watumike katika kuelimisha wananchi kuzitambua noti bandia, kwa sababu baadhi ya wananchi wengi hawajapata kuiona noti halali ya sasa, hivyo wananchi hao hata wakipewa noti za bandia wanapouza mazao yao hawatajua. Uhalali wa fedha umehamasishwa zaidi mijini ambako mzunguko wa fedha unakwenda haraka. Vijijini mzunguko wa fedha ni wakati wa msimu wa mauzo ya mazao. Napendekeza wakati wa msimu wa mauzo ya korosho, unaofuata na kadhalika, Askari wawe macho sana ili wananchi wakulima wasitapeliwe kwa fedha bandia. Kiutendaji nashauri Polisi wetu wote wapewe mafunzo ya Polisi na ya Trafiki. Baadhi ya nchi za Ulaya wameacha kutenganisha kati ya Polisi wa kawaida na trafiki. Kwa kufanya hivyo Askari wote watawajibika kufuatilia uhalifu wa aina zote kikamilifu na hivyo

kutumia vizuri idadi ndogo ya Polisi tulionao. Pia itasiadia kupunguza hisia ya kwamba kuwa trafiki polisi ni kupendelewa.

Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Liwale, Ofisi za Polisi ya Wilaya haikujengwa kwa madhumuni hayo hivyo ina mapungufu sana. Hii ni ofisi ya mpito hivyo nashauri ijengwe mapema hasa kwa vile eneo la kujenga limeshapatikana na kukabidhiwa kwa Mkuu wa kituo.

Wilaya ya Liwale ina eneo kubwa 39,000 sq kms, asilimia 53 ya eneo hilo ni *selous game reserve* yenye wanyama wakali tembo, simba, chui na kadhalika. Barabara za kwenda vijijini ni mbaya hivyo wanahitaji magari imara yenye uhakika kusafiri kwenda vijijini kufuatilia shughuli zao. Liwale kieneo ni kubwa kuliko Wilaya tano zilizobaki Mkoa wa Lindi (Ruangwa, Nachingwea, Kilwa, Lindi Mjini na Lindi vijijini) pamoja na Mkoa wote wa Mtwara. Hivyo safari za kipolisi Wilayani Liwale ni kama ziara za Mikoa miwili ya Mtwara na Lindi, hivyo ni muhimu sana kwa Kituo cha Polisi cha Liwale kuongezewa gari la polisi.

Mheshimiwa Spika, Liwale kuna gereza lisilokamilika kimajengao linaitwa gereza la Kipule. Gereza hilo lina uzio *fence* ya miti ambayo siyo salama. Bweni la wafungwa lilijengwa zaidi ya miaka 7 iliyopita halijapauliwa tangu wakati huo na gharama ya kulikamilisha sio zaidi ya shilingi milioni 10. Ni vema gereza hili likafuatiliwa kukamilishwa kwa bweni hilo haraka. Haelelweki kwa nini majambazi wenye uwezo wa kuvunja nyumba imara au kufanya ujambazi mkubwa wa silaha akafungwa kwenye gereza hafifu?

Ninashauri ujenzi wa gereza la Liwale ukamilike haraka. Pia kutokana na mazingira ya wanyamapori gereza hili linahitaji gari la uhakika kwa safari za usiku na pia eneo hilo lina mchanga sana. *KIA* haina uwezo kabisa kwa barabara za Liwale, inahitaji *Four Wheel Drive*.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema tena naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. SALOME J. MBATIA: Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja iliyo mezani. Pili, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wenye dhamana ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Naibu Waziri wake pamoja na timu yao yote kwa kutayarisha mpango wa bajeti ulio mzuri na fasaha uliowasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia katika maeneo kadhaa, Wizara hii inashughulika na usalama wa raia na mali zao, na hivi sasa kumeibuka raia ambao wanahatarisha usalama huo na wana mbinu nyingi hatari na za kisasa za kutekeleza azma yao hiyo mbaya. Jeshi la Polisi linatakiwa kwenda na wakati na kwa kweli kuwa mbele ya wakati kwa mafunzo; zana na vitendea kazi vya kisasa ili kukabili hali hii. Inatia moyo katika hotuba hii kwamba dhana ya mafunzo imezingatiwa na hasa mafunzo ya computer. Mtandao wa kompyuta ni budi usambazwe (*network*) katika

Mikoa yote ili kuongeza ufanisi wa uhakika na kasi ya kazi. Mtandao wa kompyuta utarahisisha hata kukamata wezi wanaoiba katika eneo moja na kulikabili eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kompyuta itasaidia pia katika identification ya wahalifu endapo habari wajihi, picha, zitakuwa zimeingizwa katika mtandao na hivyo kuweza kutumika katika Mkoa wowote kwa wakati ule ule tukio linapotokea.

Mheshimiwa Spika, nigusie vilevile rushwa. Rushwa imekuwa ni kama kansa katika jamii yetu. Siku zote kuzuia ni bora kuliko kuonya. Ninashauri Serikali iwe pia intaoa adhabu aidha, kwa kuwaondoa madarakani au kuwashusha vyeo maofisa au viongozi wanaotuhumiwa kwa rushwa. Si rahisi kumshika ready handed mtoa au mpokea rushwa. Kadhalika tunao uzoefu sasa vile vile kuwa mfumo wetu wa Mahakama ni mrefu na ni vigumu kumtia hatiani mla rushwa. Lililobaki na hasa hasa ili kuwajengea wananchi imani ni kutoa adhabu kama hizo za kuwaondosha wahusika kutoka katika nyadhifa zao pindi inapobainika au kutokana na kilio cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa sana wa Serikali kurahisisha zoezi kubwa la elimu ya raia hasa baada ya mfumo wa Vyama vingi kuanza kukomaa. Kwa bahati mbaya mfumo wa Vyama vingi umechukuliwa na wenzetu Wapinzani kana kwamba ili uwe Mpinzani mzuri ni sharti pia ukose uzalendo uananchi na kadhalika. Hii ni trend mbaya na Serikali isipokuwa macho hali hii ikijengeka wananchi watakosa element ya uzalendo, uananchi na utaiifa. Hali hii inaonekana hasa katika maeneo yeye Upinzani uliokolea kama Pemba.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono sana dhana ya Serikali kutoa muda maalum kwa walio na silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha silaha hizo polisi au mahali ambapo patakapokuwa pameandaliwa kwa kazi hiyo. Watakaosalimisha kwa wakati wasipate adhabu yoyote japo ni vizuri kuchukua majina yao *for any repeated offence in the future*. Baada ya muda huo, yeyote atakayepatikana na silaha kinyume cha sheria apate adhabu kwa mujibu wa sheria na pia kwa kukosa kusalimisha silaha hizo. Zoezi hili likifanywa nchi nzima litapunguza wimbi la ujambazi na wizi wa kesi kubwa.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kuwa ni vizuri kuwapata polisi kutokana na vijana kutoka JKT. Lakini labda kwa kuwa JKT ndiyo kwanza inaanazishwa upya ni vizuri pia kutazama vijana wenye sifa kutoka katika open market/Jamii. Mradi awe na sifa zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, ninatoa tena shukrani na ninaunga mkono hoja hii.

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ila naomba nipatiwe maelezo ya kuridhisha kuhusu yafuatayo:-

Moja, kuhusu magereza. Wilaya ya Igunga hana gereza lake hivyo huletwa Wilayani Nzega wafungwa na mahabusu na kusababishia gereza la Nzega kufurika watu mara mbili zaidi ya uwezo wake. Vilevile kwa Polisi Igunga haipatiwi pesa za kutosha

kuwasafirisha mahabusu kwenda Igunga Mahakamani kitu ambacho husababisha mahabusu wasifikishwe Mahakamani kuhukumiwa au kupatiwa dhamana.

Mheshimiwa Spika, hali hii pia huwalazimisha ndugu wa mahabusu hawa kugharamia usafiri wa ndugu zao toka Nzega kwenda Mahakamani Igunga ambako kwa bahati mbaya sana wakati mwingine mashahidi hukosekana Mahakamani na husababisha maandalizi ya kesi kuwa magumu kutokana na wahusika kutoka maeneo tofauti yasiyounganishwa kwa urahisi kama ambavyo ingetegemewa.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni lini Igunga itapata gereza lake. Mahabusu wanaosababishiwa kukaa ndani ya magereza kwa muda mrefu wana haki kuidai Serikali fidia kwa kupotezewa muda endapo hatma ya kesi yao ni kushinda? Polisi ni muhimu sana kwa ulinzi wa raia na mali zao. Pamoja na kufahamu hayo Serikali inaelekea kutokuwa makini na hili vijijini kitu ambacho kuanzishwa kwa ulinzi wa jadi. Katika Mikoa fulani. Walinzi hawa wa jadi wamefanya kazi nzuri sana katika sehemu zao. Pamoja na mafanikio haya zipo kasoro zinazosababisha mtafaruku kati ya sungusungu na walinzi wenzao (polisi) na Serikali kwa jumla. Mambo haya ni:-

(I) Sungusungu kuchukua jukumu la Mahakama la kuwahukumu watuhumiwa wao wenyewe kwa sababu sungusungu hawaridhiki na dhamana zinazotolewa kwa watuhumiwa ambao huwatabia baada ya kuwa wamepewa dhamana na kurudi vijijini.

(II) Wanamiji ambao nao huchukua sheria mikononi mwao huwa wakati mwingine kuwachoma moto watuhumiwa. Pamoja na yote hayo hatua zinazofuata ni matamko ya kauawa na watu wenye hasira. Je, wenye hasara ni watu wa mijini tu? Sungusungu wakichukua hatua wanafuatiliwa mithili ya mtu anayetafuta chawa kwenye kichwa cha mtu mchafu. Kwa nini kuwe na tofauti hii kati ya raia wa nchi moja hii ?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchache wa Vituo vya Polisi. Nchini mwetu ukiondoa miji kama Dar es Salaam vituo ni vichache mno na uwiano wa Askari mmoja na raia plus eneo ni mkubwa mno. Wilayani Nzega kwa mfano, tangu tupate uhuru Serikali yetu imeongeza Kituo kimoja tu cha Puge. Enzi za ukoloni kulikuwa na Vituo viwili vya Nzega na Bukene. Hata hivyo, Vituo hivi vyote pamoja na kile chetu cha Puge havina nyumba nzuri na za kutosha kwa ajili ya Askari wetu, havina magari, hata *OCD* hana gari la kuaminika. Kituo cha Bukene kimekatiwa hata simu. Katika hali kama hii tunaweza kusema raia wanalindwa wao na mali zao? Wasiwasi mtupu.

Wanamgodi wa Lusu wanatujengea Kituo kizuri cha Polisi katika Kata ya Mwangoye, wameweka pia *Generator*, hata hivyo upo wasiwasi generator hii itaachiwa Serikali ya kijiji ambayo haitamudu kuiendesha. Tunaomba wana Nzega hapa Wizara iangalie kwa macho mawili ili zijengwe nyumba za Askari. Naunga mkono hoja hii.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kwenye bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie pia nafasi hii ya awali kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu, *IGP*, Makamishna wote pamoja na wote walioshiriki kuandaa bajeti hii yenye uchambuzi wa kina. Kwani imetoa picha ya mambo yaliyotekelezwa katika bajeti iliyopita na mikakati ya bajeti tunayojadili leo.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Makamanda wa Polisi, wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma na Tabora. Pongezi hizi ninazitoa kutokana na kazi nzuri wanayoifanya ya kudhibiti ujambazi katika Mikoa yao. Naomba Makamanda wengine waige mifano yao kwani kuna Mikoa inayotia aibu kama vile Arusha na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, niendelea kutoa pongezi kwa Serikali, kwani imeweza kutoa semina kwa *RPC's* na *RCO's* kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge katika bajeti ya mwaka jana nikiwemo na mimi. Hii imekuwa changamoto kubwa kwani wameweza kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu na matunda yake ndiyo haya tunayoyaona kwamba ujambazi hauna nafasi kwa Mikoa mingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imefanya vema kuwapeleka *RPC's* na *RCO's* nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu wa kazi zao. Naomba Serikali ianze kufanya hivyo hata kwa Maafisa wa ngazi za chini pale inapobidi ili kuimarisha zaida Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kipekee kuuteua Mkoa wa Singida kuwa mwenyeji wa sherehe za wiki ya nenda kwa Usalama Kitaifa. Kwa kuwa Jeshi la Polisi Mkaoni Singida linajitahdi kufanya mambo mengi mazuri, niimbe basi Mikoa mingine waende mapema kabla ya sherehe kwa ajili ya kujifunza kwa kuwa zoezi hili kwa Singida lilishaanza mapema kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizingumzie kuhusu upungufu wa Maaskari. Naishukuru Serikali kwa kutambua kuwa ongezeko la watu sasa ni kubwa, sasa wakati umefika wa kutoa mafunzo kwa vijana wengi wenye sifa ili kuongeza nguvu katika Jeshi la Polisi. Tatizo hili lina uzito wa kipekee kwani Askari wetu wanashindwa hata kwenda kula kwa kuogopa kuacha malindo yao. Kumbé wangukuwa wawili au watatu wangeweza kupokezana.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la rushwa viongozi wengi wamepiga kelele/ kuongea sana juu ya suala la rushwa, lakini mimi naamini ni vyema tukajjuliza chanzo cha rushwa ni nini? Hivi kama mtoto amekula nyumbani kwao na akashiba ataenda kundoa kwa jirani? La msingi ni kuboresha maslahi na mazingira ya kufanya kazi Askari wetu. Tutakuwa tumewapunguzia Askari wetu vishawishi kwa asilimia, kwani rushwa ni ibilisi mkubwa sawa na gonjwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, tutazame sare za Askari wetu kwa kweli zinatia aibu, zimechakaa wengine zinawabana, zimepauka wengine wameweka hata viraka. Kwa

suala la viatu hadi soli zimelika upande. Hivi kweli hata hili linashindikana? Ni matumaini yangu kuwa hili liko chini ya uwezo wa Serikali. Ninaomba utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba suala la nyumba za Maaskari Wizara husika imeliona, Kamati ya Bunge imeona na hata kambi ya Upinzani imeliona. Nyumba hizo ni chache na ndogo na hazina hadhi kwani hazikidhi mahitaji ya Maaskari wenye familia, nyingi zina chumba na sebule, kati ya hizo ‘full suit’ au ‘godown.’

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linawafanya hata Maaskari washindwe hata kuzaa kwa kuwaogopa watoto waliolala sehemu iliyotengwa kwa pazia. Ama ni kichocheo kwa watoto wengi wa Maaskari kusikia na kuona mambo ambayo hayalingani na umri wao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongea sana suala la vitendea kazi, lakini si vibaya hata mimi nikalikazia hili. Ninaiomba Serikali ipeleke vitendea kazi vya kisasa Wilayani na Mikoani. Mfano silaha, magari, vimulika mwendo, *radio* za mikononi hata gari la kubeba maiti kwa kitengo cha usalama wa barabarani. Upungufu huu uko Mkoa wa Singida, naamini hata Mkoa mingine ni taabu tupu!

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaipongeza Serikali kwa kuwateua Makamanda wa Polisi wa Mkoa Wanawake wawili yaani katika Mkoa Mtwara na Tanga. Naiomba Serikali basi idadi hii iongezwe kwani wapo wengine wenye uwezo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza *RPC* wa Singida, Maaskari wake uongozi wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa kwa kushirikiana na wananchi kwa kukamata silaha zaidi ya 400 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Juhudi hizi ni kubwa, naomba Serikali itambue jitihada zao.

Mheshimiwa Spika, nizungumze juu ya Idara ya Zimamoto. Kwa ufahamu wangu nadhani, Idara hii ofisi zake zipo Halmashauri za Miji, Manispaa na Jiji, kwani ndio maeneo yenye nyumba nyingi, Taasisi za Serikali, Vituo vya Mafuta na kadhalika ambavyo vikishika moto na ikashindikana kuzima Taifa hupata hasara kubwa.

Mfano, stendi ya basi Singida Mjini, iliteketea hivi hivi na Maaskari walikuwa wakizima kwa matawi na michanga. Uliona wapi jitihada kama hizo zikazaa matunda? Naomba Maaskari wa kitengo hiki wapewe mafunzo na kila Mkoa upate gari la zimamoto kwa tahadhari ili waweze kukabiliana na ajali za moto.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Jeshi la Magereza. Naomba niipongeze Magereza ya Singida na Dodoma ambazo nimewahi kuzitembelea kwa kweli wanajitahidi sana kwa usafi wa mazingira, upandaji wa miti, kilimo cha mazao ya chakula, mboga na matunda kiasi kwamba wameweza kujitosheleza kwa chakula na kuipunguzia Serikali mzigo wa kuwalisha. Vilevile hawako mbali na suala la uzalishaji

mali kama vile useremala, uwashi, ususi na ushonaji ambayo pia ni mafunzo tosha kwa wafungwa pindi wanaporudi makwao. Hivyo waongezewe maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie kwa kuzungumzia Idara ya Uhamiaji. Kwa niaba ya wapiga kura wangu Idara hii ni kero, kwani ukiritimba wa hali ya juu katika zoezi zima la utoaji wa vyeti vya kuzaliwa, visa na *passsport* kwa wananchi. Hii inasababisha mizunguko isiyokuwa ya lazima na kusababisha kuwepo mianya ya rushwa, watu kuchelewa kwenda kusoma nje, matibabu, ama shughuli mbalimbali zinazofanyika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naomba nitamke rasmi kuwa naunga mkono bajeti hii na kuwashukuru walioiandaa Bajeti hii.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda sana kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kwa Taifa hili. Nchi hii inaishi kwa amani na utulivu kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na vyombo vyetu vya dola Polisi, Magereza na Jeshi.

Pili, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Omar Ramadhani Mapuri, Naibu Waziri Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Katibu Mkuu na wataalam mbalimbali wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Tatu, maombi ya Korogwe. Kwanza, kwa muda mrefu nimekuwa nikiomba nyumba za magereza Korogwe zilizoanzishwa mwaka 1980 kukamilishwa. Hivi ni kwa sababu gani hadi leo hii hakuna dalili zozote za kumaliza nyumba hizo na hali kila mwaka ninapewa ahadi tu. Hali ni mbaya sana ninaomba katika bajeti ya safari hii ifikiriwe Korogwe.

Pili, jengo la magereza la Korogwe limechakaa sana na linavunja. Ninaomba sana likarabatiwe hali ni mbaya sana.

Tatu, vifaa vya wafungwa, vilago, mavazi yamechakaa wapatiwe mapya.

Nne, Gereza la Kwamngumi kwa muda mrefu wameomba umeme ninaomba lipatiwe umeme. Meneja wa *TANESCO Korogwe* yupo tayari kufanya kazi hiyo. Gereza lile ni la uzalishaji linahitaji msaada huo muhimu.

Tano, madawa kwa wafungwa hayatoshelezi yaongezwe. Sita, Askari wa magereza wanafanya kazi nzito waongezewe maslahi.

Saba, kwa muda mrefu nimekuwa nikiomba kituo cha Mashana kupatiwa gari na pikipiki kutokana na unyeti wake kipo karibu na machimbo ya vito Kalalani ni mbali sana na mji wa Korogwe! Ninaomba sana kipatiwe usafiri. Korogwe ni katikati ni vyema tukawa na usafiri wa uhakika. Pia suala la upelelezi wa kesi kuchukua muda mrefu litazamwe wapo mahabusu wengi sana katika magereza ya Korogwe kwa sababu ya upelelezi kuchukua muda mrefu.

Mfano, Mheshimiwa Waziri ninaomba utupate jibu ni kwa nini hadi leo hii mzee mmoja wa kijiji cha Indurui ambaye inasemekana ameuua mwenzake shambani kesi yake hasikilizwi. Mzee huyu inasemekana aliyeuua ni mtu mwingine wa kijiji cha Mgobe lakini ameshikiliwa yeye hadi leo ni miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala hili ulifanyie kazi. Familia yake inateseka. Ni bora kesi ikaanza ikionekana ana hatia au vinginevyo. Suala la utekelezaji kuchukua muda mrefu ni donda ndugu kwa polisi. Ninashauri sana lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Serikali yafuatayo:- Moja uingiaji wa watu wengi nchini mwetu, huingia sana kiholela hilo lichunguzwe. Pili, zipo silaha nyingi sana zinazolingia kiholela nchini mwetu hili lichunguzwe. Suala la kuwa na majambazi wanaishi kwenye baa peke yake hilo siyo sahihi. Majambazi wengi wapo kwenye *guest house* kwa hiyo kuwe na uchunguzi wa dharura kwenye *guest houses*.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na team nzima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kazi nzuri na hotuba ya bajeti yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi kwenye Wizara hii ambao kwa wadhifa zao au ubinafsi na utu wao ningependa kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa kushirikiana na famili yangu wakati wa majonzi makubwa yaliyotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa mpenzi mke wangu Ekaeli Mbise kwa ajali ya gari tarehe 6 Aprili, 2003.

Napenda kuwataja wafuatao *RPC* Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Kombe, *Senior Assistant Commissioner* Augustino Nanyaro wa Magereza Makao Makuu Dar es Salaam na *OCD* Wilaya ya Arumeru *Usa River* Mheshimiwa Urassa.

Mheshimiwa Spika, tuna mengi ya kulishukuru Jeshi la Polisi kwanza kabisa tunapenda kumshukuru *Regional Police Commander* wa Mkoa wa Arusha kwa kututafutia mfadhili wa Kituo cha Polisi kwenye kata ya Kikatiti, Arumeru Mashariki.

Eneo la barabara ya Arusha-Moshi kuanzia Maji ya Chai, mpaka njia panda *Kilimanjaro International Airport* limekuwa likihifadhi majambazi kwa muda mrefu. Wezi hutegea wasafirishaji wa madini ya Tanzanite kutoka Mererani kwenda Mjini Arusha. Kwa hiyo, ujenzi wa Kituo cha Polisi Kikatiti utakapomalizika na kituo kuanza kazi wakazi wa Maji ya Chai Kikatiti na Kingori (Malula na Kolila) watalala usingizi!

Mheshimiwa Spika, kazi ya kujenga Kituo cha Polisi cha Kikatiti bado kumalizika. Lengo letu ni kwamba kituo hicho kianze kazi ifikapo mwezi Desemba, 2003. Kufikia lengo hili tunahitaji msaada au mchango wa Wizara, ikiwa ni pamoja na

kuwaomba *RPC* wa Arusha Mheshimiwa Kombe aone uwekezano wa kuwaona *AFGEM* (Mereani wasaidie kwenye kumalizia ujenzi wa hicho Kituo.

Mheshimiwa Spika, kitakapomalizika Kituo cha Kikatiti kitahitaji watendaji na vitendea kazi. Tunaomba Wizara ianze kutufikiria kuhusu hilo. Vitendea kazi ni pamoja na gari la Kituo ambalo litakuwa muhimu sana kudhibiti usalama wa eneo linalozunguka Kikatiti mpaka Kingori.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Kituo cha Polisi Tengeru. Kwa miaka karibu mitatu sasa, nimekuwa nikizungumzia maatizo ya Kituo hiki. Kwanza nimeomba kihamishiwe penye watu Patandi kutoka chuoni Tengeru.

Pili, nimeomba kipatiwe gari la kuwezesha Kituo kiutendaji. Hatujafanikiwa bado yanaendelea kuwa matatizo na mahitaji yanayotia kero. Kituo kiko ndani ya Chuo cha Tengeru. Kilometa 2 kutoka Patandi kwa upande wa Kaskazini penye barabara ya Moshi-Arusha.

Shida siyo huo urefu tu, bali giza lililopo kati ya Patandi na Tengeru kuna eneo la kahawa na miti iliyosongana, majambazi na vibaka hutumia mazingira haya kubaka, kunyang'anya na kuibia wanaotumia barabara ya Patandi- Tengeru. Kwa hiyo wengi wanaotaka kwenda Kituoni huogopa kufanya hivyo iwe mchana au giza!

Mheshimiwa Spika, Wizara ihamishe Kituo cha Polisi Tengeru kutoka Chuo cha Tengeru kwenda Patandi sisi wananchi tuko tayari kuchangia ujenzi utakaohitajika.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Arumeru Mashariki lina Tarafa tatu, Poli, King'ori na Mbuguni. Tarafa ya Poli ina kata nane, kati ya 17 zilizopo Jimboni. Kati ya hizo kata 8, kata 7 zina idadi ya watu wanaofikia karibu 109,00 kwa sensa ya mwaka 2002. Hii ni karibu nusu ya wakazi wa Arumeru yote. Kata ya 8 ni *Usa River*.

Hii ni idadi ya wakazi wa tarafa ya Poli kwenye hizo kata 7 husafiri takriban wastani wa kilomita 9 kupata huduma ya Kituo cha Polisi Tengeru au *Usa River*. Kwa hiyo, gharama ya huduma ni kilomita 18 kwa siku za kutembea. Kwa hali hii ni rahisi kuona ni wangapi wanaoweza kudai haki zao kupitia njia ya polisi na ni wangapi hushindwa na kukata tamaa!

Mheshimiwa Spika, ombi letu ni kupatiwa Kituo cha Polisi katikati ya hizo kata 7 kwenye eneo la Poli Mringaringa. Nimeishazungumzia na Washili (viongozi wa mila) kuhusu eneo la kujengea Kituo cha Polisi wako tayari kutoa eneo. Tunaomba Wizara itufikirie kutupa hicho Kituo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ombi la Kituo cha Polisi, Poli Mringaringa, pia tunaomba Kituo kama hicho, Kingori sokoni kwenye kata ya Kingori, kijiji cha Kingori. Hicho kituo kitatoa huduma kwa kata 2 Leguruki na Kingori. Hizi kata kwa pamoja zina wakazi karibu 40,000 kwa sensa ya mwaka 2002. Kingori sokoni iko kilomita 18 kutoka barabara kuu ya Arusha- Moshi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida mjadala unapokwisha tunawapa watoa hoja nafasi ya kuandaa majibu ili waweze kuyatoa wakati wa Kikao cha jioni. Tutafanya hivyo hata leo.

Lakini nieleze kwamba baada ya msafara wa Spika kutoka nje ya Ukumbi huu wa Bunge, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ataingia na wataalamu wake ili waweze kutoa maelezo yale niliyoyatangaza. Kwa wale ambao wanataka kuyasikia watasubiri. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.25 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kuna makaratasi yamegawiwa mchana huu yana kurasa mbili, yanaitwa Marekebisho ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na ya pili Marekebisho ya Bajeti ya Maendeleo. Sasa mnaarifiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, hokusudii kuwasilisha marekebisho haya ya Matumizi ya Kawaida ule ukurasa wa kwanza, isipokuwa itakayowasilishwa ni ile ya Bajeti ya Maendeleo ukurasa wa pili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza, ningependa kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Manyoni Mashariki, nitoe pongezi kwa Wabunge wenzetu waliojiunga nasi hivi karibuni wa kutoka Chama Tawala na wenzetu kutoka kwenye Kambi ya Upinzani. Tunawapongeza sana, karibuni sana tushirikiane katika kufanya maamuzi ya kuendesha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nikiingia kwenye hoja yenyewe nataka niseme moja kwa moja kwamba, naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Katika kuchangia ningependa kujibu baadhi ya hoja za Wabunge hasa zile zilizohusu vitendea kazi katika Wizara ya Mambo ya Ndani na vyombo vyake vyote, ujenzi wa Ofisi na nyumba za Askari na upatikanaji wa vifaa mbalimbali. Hoja ni nyingi sana sidhani kama zote tutazijibu, lakini kwa zile ambazo hatutazigusa mtuwie radhi.

Sasa kabla sijaingia kwenye hoja, moja moja nitoe tu kwanza taarifa ya jumla kwamba, Bajeti ya Wizara yetu hasa katika kipengele cha maendeleo, ambacho ndicho kinachohusika na vitendea kazi na ujenzi wa Ofisi na nyumba za Askari na vifaa mbalimbali, ilionekana hesabu imeongezeka kutoka Sh. bilioni 5 za mwaka 2002 mpaka Sh. bilioni 8. Kwa maana kwamba, Jeshi la Polisi mwaka 2002 walikuwa na Sh. bilioni

3.3 sasa wana Sh. bilioni 5.2. Jeshi la Magereza mwaka 2002 walikuwa na Sh. bilioni 2.9 na mwaka huu wamepata zile zile Sh. bilioni 2.9. Fedha hizi tukizitamka na ongezeko hili tunaweza tukapata matumaini makubwa sana kwamba, kwenye Majimbo yetu miradi yote sasa itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, fedha hizi zinakwenda kupambana na matatizo mengi na makubwa na ambayo yamelimbikizwa kwa miaka mingi. Majeshi haya kwa karibu miaka 8 hayakupata hata senti moja ya fedha za maendeleo. Kwa hiyo, matatizo yao ni makubwa kweli. Kwa hiyo, hizi fedha zinakwenda kupunguza ule mlima mrefu wa matatizo lakini hautamaliza wala nusu hatutafika. Kwa hiyo, ningependa Waheshimiwa Wabunge, msiwe na matumaini makubwa mno na ongezeko hili la karibu asilimia 30. Hata hivyo, tutafanya yale ambayo tutaweza kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa jumla katika kutumia hizi Sh. bilioni 8 za fedha za maendeleo. Kwanza, zitakwenda kwenye kumalizia viporo. Tuna viporo vingi sana huko katika Wilaya zetu na Majimbo yetu. Viporo vya Ofisi ambazo zilijengwa zikafika kwenye *lintel* zikaachwa hapo kwa miaka 10, viporo vya nyumba za Askari ambazo zimeachwa nyingine usawa wa madirisha, nyingine usawa wa *lintel*, nyingine hazijapauliwa kwa miaka mingi. Viporo vya Mabweni ya Magereza, ambayo yalianza kujengwa takriban miaka 6 au 7 iliyopita halafu ujenzi ukasimama baada ya *Vote* ya Maendeleo kusimamia. Kwa hiyo, fedha za mwaka huu zitakwenda kwenye viporo hivyo. Hatutaanzisha mradi mpya wa ujenzi kwa fedha za mwaka huu isipokuwa tutakwenda kumalizia viporo. (*Makofi*)

Vile vile fedha hizi zitakwenda katika kuimarisha mawasiliano ya *Radio Calls*. Vituo vyetu vingi sana huko tuliko havina mawasiliano hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, mmesema hapa kwamba, Askari wanatumwa doria hawawezi wakawasiliana na Makao Makuu hata kama watapata matatizo huko. Kwa hiyo, kuna kiasi kikubwa kitakwenda katika *Radio Calls* na hili nataka niahidi kwamba, tutagusa maeneo mengi katika suala la usambazaji wa *Radio Calls* katika vituo vyetu na katika Magereza.

Vile vile vifaa vya kilimo na viwanda vitapewa umuhimu hasa katika Jeshi la Magereza ili wafungwa waweze kuzalisha. Kuhusu magari wengi sana mmeomba magari mapya. Kwa Bajeti ya safari hii hatutapata magari mengi ya kutosha mpaka mkaona *impact* katika Majimbo yetu. Tutaweza kununua machache na haya machache ndiyo tutakayoyagawa.

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa ni maelezo ya jumla, sasa niingie kwenye hoja zenyewe. Kwanza, Kamati ya Ulinzi na Usalama imetushauri kwamba, tufanye ukarabati katika majengo ya vyuo vyetu vya Polisi na Magereza. Bajeti ya safari hii itatuwezesha kukarabati vyuo vyetu kule Kiwira - Mbeya, tutakarabati, Chuo cha Moshi ambacho kimetajwa sana na kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama kitakarabatiwa na zimetengwa karibu Sh. milioni 75 kwa ajili ya kukarabati Chuo cha Polisi kule Moshi.

Mheshimiwa Mabina na Mheshimiwa Faustine Rwilomba, wao walizungumzia habari za Geita, Wilaya kubwa wanataka magari mapya. Sasa hili la magari siwezi

kuliahidi kwa sababu magari ambayo tutayapata ni machache na mahitaji ni makubwa kweli. Kuna Wilaya zingine hazina gari mpaka sasa hata moja. Sasa rafiki zangu kule kwenye Wilaya yangu ya zamani ya Geita walau wana magari mawili naomba msubiri kidogo ili wenzenu ambao hawana hata moja waweze kupata.

Mheshimiwa Shibiliti, yeye alikumbusha kwamba Misungwi hawana *OCD*. Sasa ni kweli karibu Wilaya 14 hazina *OCDs*, lakini tunawaambia kwamba, tufanye maandalizi kabla hatujapeleka *OCDs*. Tuwe na Vituo vya Polisi, siwezi kupeleka mahali ambapo hakuna Kituo cha Polisi, tuwe walau na nyumba za kuanzia kukaa Askari, tuwe na *armoury* na vifaa mbalimbali ambavyo hata *OCD* akifika pale anaweza akafanya kazi sawa sawa.

Mheshimiwa Profesa Maghembe, alizungumzia habari ya vituo vyake kule Mwanga na wengi wamezungumzia vituo ambavyo vinajengwa kwa nguvu za wananchi viko vingi. Hata kule Mpanda Mheshimiwa Margareth Bwana na Mheshimiwa Gembe, vile vile wana vituo karibu viwili kule katika Tarafa ya Kirema na mimi nimepata bahati ya kuvitembelea vituo hivyo. Sasa kwa jumla tunaweza kusema kwamba, tunazipongeza juhudi za wananchi waendeleo na ujenzi na sisi hali kadiri itakavyoruhusu, tunaweza kwenda kushirikiana nao, tukaunga mkono kwa kuchangia. Lakini juhudi za sasa ziendeleo na sisi tutawaunga mkono.

Mheshimiwa Profesa Mbawala, amezungumzia kule Namtumbo, naye vile vile hana *OCD*, ni kesi kama zile Wilaya ambazo hazina *OCDs*. Anataka na gari, *Inshallah* kama fedha zitaruhusu tukapata magari mengi basi tutaanza na zile Wilaya ambazo hazina magari kabisa kama Wilaya ya Namtumbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ndugai, yeye ametaka kumalizia Kituo cha Polisi kule Kibaigwa, ambacho kinajengwa kwa nguvu za wananchi. Tunasema kwamba, juhudi hizo ziendeleo Kibaigwa tulishawasaidia tayari tulishawachangia kama Wizara, lakini kile kituo hakijaisha na kiko mahali ambapo kuna *Highway* na kuna uhalifu mwingi hata sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa kweli tunatamani kile kituo kiishe haraka haraka kwa sababu kitatusaidia kudhibiti hali ya uhalifu pale pamoja na usalama wa *Highway*. Kwa hiyo, waendeleo na sisi tukipata uwezo tunaweza tukachangia tena kwa mara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Profesa Mwaga, amezungumzia Kituo cha Kibakwe kutaka *Radio Call* na gari. *Radio Call* atapata kwa sababu vituo vingi vitapata *Radio Call* mwaka huu kama nilivyosema, lakini gari hatuwezi kuahidi.

Mheshimiwa Lubeleje, yeye kule Mpwapwa anasema ana gari lakini haliwezi kupanda milima. Sasa ninachoweza kukuahidi ni kwamba, tutalitengeneza hilo hilo lipande milima wakati tunasubiri kupata gari jipya. Kwa sababu kuna Wilaya ambazo bado mpaka sasa hazina magari. Kwa hiyo, tutaahidi kwamba tutalitengeneza gari hilo mpaka lipande milima, liendeleo kuwahudumieni na mbele ya safari tukipata fedha ya kupata magari mapya tutakuja ku-replace.

Mheshimiwa Kahumbi, kuhusu Kituo cha Polisi kule Bukene, tumepokea taarifa yake na tutafika kule tuone jinsi ya kushirikiana naye na ule Mgod. Inaelekea Mgod umeanza kusaidia kujenga Kituo cha Polisi, tutazungumza nao vile vile wasaidie na kujenga nyumba za wafanyakazi.

Mheshimiwa Frank Mussati kule Kasulu kuna Kituo kiko Mpakani kabisa cha Herushingo anataka mawasiliano kwa sababu kiko mpakani anataka na gari. Mawasiliano tutajitahidi kupata *Radio Call* lakini gari hatuwezi kuahidi kwa sababu zile ambazo nimezisema.

Mheshimiwa Mwenegoha, ana vituo vyake anajenga kule Matombo kwa nguvu za wananchi. Kama hali yetu ikiruhusu tutafika kule tushirikiane nao.

Mheshimiwa Fatma Said Ali, yeye anataka kijengwe kituo Vikokotoni. Kimsingi tunakubali kwa sababu kama wananchi wanataka kujenga Kituo cha Polisi mahali, sisi kwa kweli tunakubali tutashirikiana nao, kwanza wao watafute kiwanja, sisi tutawapa ramani ya kujenga Kituo cha Polisi kinachofanana na Polisi halafu waanze kwa nguvu zao ujenzi. Pale Mjini kuna wafanyabiashara wengi, wakianza ujenzi na sisi tutaangalia jinsi ya kushirikiana nao ili kusogeza huduma ya ulinzi karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabisa na wengine wengi wamezungumzia habari ya *speed boats* kwamba, tuwe na *speed boats* katika Maziwa yetu. Suala hili limezungumzwa na Mheshimiwa Kabisa, Mheshimiwa Ndaboine, kule *Lake Tanganyika*, Mheshimiwa Margareth Bwana kule *Lake Tanganyika*, Mheshimiwa Mabina, Mheshimiwa Shibiliti. Kimsingi suala la *speed boats* sisi kila mwaka kama Wizara, tunaomba fedha ili tununue *speed boats*. Kwa sababu ulinzi wa majini ni muhimu kama ulinzi wa nchi kavu. Lakini *speed boats* ni ghali. *Speed boat* moja inakwenda Sh. bilioni 4. Kwa hiyo, kama tungetaka kununua *speed boat* kwa zile fedha za Polisi ambazo ni Sh. bilioni 5, kwa mwaka huu fedha za maendeleo zote zingeishia katika kununua *speed boat* moja tu.

Kwa hiyo, suala hili kwa mwaka huu katika Bajeti hii kusema kweli tumeshindwa kubajeti fedha za *speed boat*, lakini suala la *speed boat* liko katika mpango wetu wa miaka 10 katika kuboresha Majeshi yetu ndani ya Wizara yetu. Kuhusu mpango wa miaka 10, tumeanza kuzungumza na wahisani hata mwezi uliopita tarehe 4 Juni kule *Royal Palm* tulikutana na timu ya nchi wahisani tukazungumza nao masuala mbalimbali jinsi wanavyoweza kutusaidia na hili la *speed boat* vile vile tulizungumza nao sasa tunangoja *reaction* yao, tuone tutasaidiana vipi. Kwa hiyo, kwa Bajeti ya safari hii kusema kweli hatuna fedha za *speed boats*, lakini tutatafuta vianzio vingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge imetukumbusha habari ya kuharakisha ujenzi wa nyumba za kuishi Askari. Huo mpango umo katika ule mpango wetu wa miaka 10 niliousema kwa sababu ni suala ambalo litachukua muda mrefu. Tumeanza kuzungumza na Mashirika ya Fedha kama *NSSF*, *PPF*, ili tuone jinsi ya kusaidiana nao katika kuharakisha suala hili. Vile vile tumeanza kuimarisha vikosi vyetu vya ujenzi kwa mfano, Vikosi vya Polisi vya Ujenzi, Vikosi vya Magereza vya

Ujenzi, ili kama tukapata fedha na vifaa badala ya kutumia makandarasi basi tutumie vikosi vya ujenzi katika kuharakisha kazi hii.

Polisi au Askari kukopeshwa vifaa vya ujenzi. Hili limezungumzwa na wengi akiwemo Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Aisha Kigoda. Sasa hili utaratibu huo kusema kweli upo wa kuwakopesha Polisi, sio vifaa vya ujenzi tu, vifaa mbalimbali ambavyo wanataka na tunatumia kwa Zanzibar kuna wafanyabiashara binafsi ambao wanakopesha sisi tunawezesha kwa maana kwa sababu sisi ndio tuna mshahara wao basi yeye Askari anafanya mkataba na yule mwenye vifaa sisi anasema tumkate shilingi ngapi tunamkata na kumpelekea yule aliyemkopesha. Kwa Tanzania Bara kuna Kampuni ya TUNAKOPESHA, kuna Askari wanakopa kule. Benki ya Posta inakopesha Askari, *Azania Bancorp* inakopesha Askari, *Exim Bank* inakopesha, *NMB* na hata Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam vile vile inatoa mikopo ya aina hii. Kwa hiyo, sisi tunawaambia Askari wale ambao wanataka kukopa sisi tutawawezesha waweze kurejesha mikopo yao taratibu.

Kambi ya Upinzani imetoa pongezi kwa ujenzi wa nyumba 48 za *FFU* Ukonga na zile 53 za Chake Chake. Lakini wamesema nyumba hizi ziwe za kudumu. Nataka kuwahakikishia kwamba nyumba hizi ni za kudumu na wakati wa kuzifungua zile nyumba za Pemba, tutawaalika baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, ambapo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara yetu Mheshimiwa Magoba ni Mjumbe katika Kamati hiyo, nafikiri na yeye atahudhuria siku hiyo ili aone mwenyewe kwamba, hizi nyumba ni za kisasa na imara kabisa. (*Makofi*)

Vile vile nikiwa huko huko Pemba Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, amezungumzia suala hilo hilo la nyumba za Sinya. Yeye ametupongeza, tunashukuru kwa pongezi zake tumezipokea. Amezungumzia suala la umeme. Nataka kumhakikishia kwamba, suala la umeme tutajitahidi ili nyumba zile zipate umeme kwa sababu ni huduma muhimu.

Rafiki yangu Sheikh Ali, kwenye Kambi ya Upinzani, yeye aliulizia habari za fidia kwamba, mahali pale walikuwepo wenyewe tumewakuta pale. Anauliza je, hali ya fidia ikoje? Nataka tu kumhakikishia kwamba, suala la fidia tunalo. Bahati nzuri kulikuwa hakuna nyumba za kudumu pale ilikuwa ni mashamba tu. Tumeshafanya tathmini ya wale waliokuwa wanalima pale, tumeshapata majina yao na hesabu ya kufidia na fidia italipwa mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mulyambatte yeye, aliulizia habari ya gari kule kwake kwamba, *IGP* alimuahidi gari liko wapi? Ahadi hiyo ya gari Meatu ipo na hali ya fedha ikiruhusu basi tutakupatia. Tumechelewa tu kwa sababu ya hali yenyewe ilikuwa hairuhusu.

Mheshimiwa Spika, kengele ya kwanza imeshalia, naomba niwajibu wafuatao. Mheshimiwa Batenga, yeye ameulizia habari ya Gereza la Bukoba kwamba, ni chakavu. Ni kweli lakini tumeshaanza kulikarabati. Mwaka 2002 tulipeleka Sh. milioni 5

kukarabati gereza lile, hazikutosha lakini mwaka huu tutaongeza tena nyingine ili gereza liwe katika hali nzuri zaidi.

Mheshimiwa Leonard Derefa, aliulizia habari ya ujenzi wa gereza la akinamama kule Shinyanga. Nataka kumweleza kwamba ujenzi wa gereza lile umeanza mwaka wa fedha uliopita, mwaka huu tutaomalizia ule ujenzi wa gereza la akinamama na baada ya hapo tutaendelea kukarabati gereza zima lile la Shinyanga.

Mheshimiwa Kahumbi, ameulizia habari za Gereza la Igunga. Watapata gereza lini na ujenzi utanza lini? Kama nilivyosema kwamba, mwaka huu tunamalizia viporo. Tukimaliza viporo ndipo tutaanza ujenzi wa Magereza mapya. Kuna Wilaya 32 hazina Magereza pamoja na Igunga. Kwa hiyo, tukianza ile awamu ya kujenga Magereza mapya, Igunga itapata kipaumbele kwa sababu sasa hivi Mahabusu wanapelekwa Nzega na inawapa matatizo makubwa.

Mheshimiwa Seleli, ameuliza kwa nini Magereza wasitumie nguvu za wafungwa katika ujenzi. Nataka kukuhakikishia kwamba, tunatumia nguvu za wafungwa katika ujenzi. Mheshimiwa Rwilomba, ameulizia Butundwe kwamba ni gereza la kilimo lipewe matrekta angalau mawili ili kuboresha kilimo. Tumepokea ombi lake, mwaka huu wa fedha tutampelekea trekta lakini si mawili, walau moja litakuja kuimarisha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shellukindo, ameulizia habari za wazabuni wanaotuletea vifaa mbalimbali katika Magereza yetu kwamba hawajalipwa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, utaratibu wa kuwalipa wazabuni unaendelea na hata wao wa kule Bumbuli tutawafikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje, vile vile alikuwa na suala la Gereza la Mpwapwa kuhusu umeme. Sasa hivi tunalijenga lile gereza, tukikamilisha ujenzi ndipo tutalipa kwanza usafiri, simu halafu sasa umeme utafuata baadaye kwa sababu huko unakopatikana mpaka gerezani mbali, gharama ni kubwa. Kwa hiyo, hili hatuwezi kumuahidi leo, asubiri apate hicho kwanza kinachopatikana.

Mheshimiwa Nyaburi, amesema ramani zetu ni za kizamani sana, zinafanya watu wanabeba mitondoo, kinyesi. Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ramani za sasa hivi hazina habari za mitondoo, zina maji ya kuvutwa na hata yale Magereza ya zamani ambayo yanatumia mitondoo, tunao utaratibu awamu kwa awamu, kuondoa habari za mitondoo ili tuweke maji ya ku-*flash* ili Magereza yetu yafanane na karne ya 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ledian Mafuru Mng'ong'o, amezungumza habari za wafungwa katika sehemu za baridi. Hilo tatizo tunalo tumeshaanza kusema kweli kugawa mablanketi katika maeneo ya baridi, masweta katika maeneo ya baridi na kuanzia mwakani kama fedha zitaendelea kutoka namna hii, tunataka kubadilisha *uniform* badala ya kuvaa vikaptula wavae suruali wafungwa wote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kigwalilo, amezungumzia habari za Gereza la Kipule kule Liwale. Nataka kumhakikishia kwamba, gereza hilo limejengwa miaka ya nyuma halijakamilika ni kiporo tutashughulikia kiporo hicho kama tunavyoshughulikia viporo vingine. Isipokuwa ameomba vile vile habari ya gari hili, siwezi kuahidi moja kwa moja lakini Jeshi la Magereza lina utaratibu wa kugawa magari kwa awamu katika Magereza mbalimbali na *Inshallah* awamu yake itafika ili naye aweze kupata gari katika gereza lake.

Mheshimiwa Wejja, anasema kwamba, naye vile vile anatumiza kwamba wafungwa waweze kufanya kazi mbalimbali za kilimo. Tunafanya, kama kwenye hotuba tumesema tumenunua matrekta 10 kwa kuanzia na kama fedha zikipatikana tutanunua na mengine tutayasambaza katika Magereza mbalimbali ili kuharakisha kilimo. Hivyo hivyo tunafanya na kwa viwanda mbalimbali katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa Mheshimiwa Singo kwenye gereza lake kule Same. Tulikarabati na *sewerage* na sasa hivi kwanza tunachimba kisima cha maji maana yake hatuwezi kuweka *sewerage* wakati gereza lenyewe halina maji. Sasa hivi tunachofanya ni kuchimba kisima pale, tukishakamilisha ndipo tutarekebisha sasa ile mifereji ya *sewerage*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joel Bendera kule Kwamungumi vile vile ameomba ukarabati na umeme. *Inshallah* kama fedha zikipatikana tunaweza tukafika huko. Gereza la Korogwe kukarabatiwa linavuja hilo tutalikarabati.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi sana, wale ambao sikuwafikia wataniwia radhi, lakini zote tutaziandika vizuri, majibu yatatoka na kila Mheshimiwa Mbunge atapata ile nakala yenye hoja zote na majibu yote.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kujitahidi kufunga mjadala kwa kujibu hoja na kufanya majumuisho ya mjadala kwa kujibu hoja kadri nitakavyoweza. Kama inavyoonekana kwamba hoja ni nyingi sana na haitowezekana pengine kuzijibu zote. Lakini kimsingi ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tunazipokea zote. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, wachukulie mchango wa Mheshimiwa Naibu Waziri, kuwa ni sehemu ya majumuisho haya, kwa sababu yale aliyoyasema sitoyarudia na yale yachukuliwe ndiyo kauli ya Waziri mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kupata jumla ya wachangiaji 120, ambao kati yao 35 wamechangia kwa mdomo na 85 kimaandishi. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wote. Nitawataja ila wakati wa kufanya majumuisho nitawaomba wanivumilie wakati ule sitotaja majina isipokuwa labda kama ni lazima sana nitakuwa nikizungumzia *issues*.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa mdomo kwanza ni Mheshimiwa Benito Malangalila, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Frank Magoba, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhani, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ali Sheha Mussa, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Haroub Masoud.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Ali Said Salim na mwisho Mheshimiwa Kapteni John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofi*)

Napenda pia kuwatambua waliochangia kwa maandishi mabao ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Abdulkarim Hassan Shah, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Frank Michael Mussati, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Juma Salum Kidunda, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Elizabeth Batenga na Mheshimiwa Stephen Kahumbi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Janeth Edward Mashele, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga na Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Kapt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Frank Magoba, Mheshimiwa Mohamed Rajab

Soud, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Sharifa M. Khamis na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Tembe K. Nyaburi, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Mchande Salim Mchande, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Col. Feteah Saad Mgeni, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz na Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza na maelezo ya jumla. Katika nchi yetu hii, yaani Zanzibar na Tanzania kwa jumla, tupo katika jitihada za kujenga nchi yenye umoja na isiyokuwa na ubaguzi wa aina yoyote. Hayo ndiyo yalikuwa malengo ya uhuru wa nchi zetu mbili, Tanganyika na Zanzibar kwa ujumla wake, yaani uhuru wa Tanzania nzima. Pia, hayo ndiyo yalikuwa malengo ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na Katiba zetu za nchi zinakataza ubaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapotazamana na kuhukumiana kwa rangi za ngozi zetu, asili zetu, makabila yetu, jinsia, dini na kadhalika, ni kujirudisha nyuma katika jitihada zetu hizi. Kwa mantiki hiyo, Wabunge tuliomo humu ndani tunawakilisha Watanzania wote na tujione hivyo. Nadhani hatuna sababu ya kujiona Wazungu au Waarabu weusi au Waafrika weupe, maana rangi kila mtu na yake, sisi tumo humu ndani tunawakilisha Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, tulipoingia katika mfumo wa Vyama vingi tulikubaliana kuondoa Majeshi yetu kwenye Siasa na hilo tukalitilia mkazo katika Katiba zetu, ile ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Zanzibar. Kwa hiyo, ajira katika Majeshi haipaswi kuongozwa na mitazamo ya Kisiasa. Kanuni za uajiri katika Majeshi zilirekebisha kwa kufuata maelekezo hayo ya Katiba na katika kanuni hizo za ajira, Itikadi ya Kisiasa si miongoni mwa sifa za kuajiriwa katika Majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la uzalendo lina msingi wake na nimesikia Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili, wakizungumzia suala la umuhimu wa uzalendo na uzalendo haupaswi kuhusishwa na Itikadi za Kisiasa au na Chama fulani, Wanachama wa Vyama vyote wanatarajiwa wawe na uzalendo kwa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi, Mheshimiwa Ngombare-Mwiru na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tulishiriki kwenye mazungumzo ya Muafaka. Tulikwama kwa muda mrefu sana katika baadhi ya vipengele, mpaka tulipokubaliana kwamba, maslahi ya nchi yawe mbele, yaje mwanzo kuliko maslahi ya Vyama. Nadhani huo ulikuwa ni

uzalendo na tulipokubaliana hivyo, njia ikawa nyepesi kufikia kwenye makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa vigezo vya uzalendo kwa mujibu wa historia ya nchi yetu ni lazima kwanza tukubali kuuthamini na kuulinda uhuru kama kipimo cha uzalendo. Tuyatambue, tuyathamini na tuyalinde Mapinduzi ya Zanzibar, tuuthamini na kuulinda Muungano na tuvithamini vielelezo vingine vya jitihada za kujenga umoja katika nchi yetu. Miongoni mwa vielelezo hivyo ni muafaka, mbio za mwenge na mambo mengine ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaposikia watu wakibeza Mapinduzi au unapoonana wanafanya vitendo vya kudhoofisha Muungano, wanakejeli mwenge, wanakerwa na neno Mapinduzi, wanakerwa na Askari wenye asili ya Tanzania Bara kuwepo Zanzibar au Pemba, kwa kweli unapata wasiwasi kuhusu uzalendo. Hiyo ndiyo inatoa mwanya kwa hoja kama hizi ambazo tunazisikia. Jana tumezisikia hapa, si nzuri kabisa, mie sikubaliani nazo, kwani zinatoa mwanya kama huo. Napenda kutoa changamoto na wito kwamba, wote tujitahidi kwa makusudi kabisa kuhakikishiana na kuondoleana shaka juu ya uzalendo wetu. Kauli na vitendo vyetu vitasaidia sana katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la uzalendo, nitawajata Waheshimiwa wawili wa Upinzani, ambao wako kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, tunakutana huko na michango yao na hamasa zao, hainipi shaka yoyote juu ya uzalendo kwa nchi yao. Wabunge hao ni Mheshimiwa Frank Magoba na Mheshimiwa Major Jesse Makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tujitahidi katika suala hilo, tukishahakikishiana kwamba tunathamini hayo mambo ya msingi ya uzalendo, nadhani na hizi hoja nyingine zitakufa zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo tutaendelea kufuata kanuni zilizopo ambazo tutazirekebisha kadri inavyohitajika ili ziende sambamba na *spirit* ya Katiba ya nchi yetu na kanuni za ajira katika Jeshi la Polisi na Majeshi yetu. Kwa hiyo, hatutaajiri watu kwa mitazamo ya kisiasa, hatutaajiri watu kutoka Mkoa wa Mara peke yake, JKT tutazingatia wale ambao wanatimiza sifa za msingi kwanza za uajiri katika Jeshi la Polisi na maoni ya ngazi za chini ya Wilaya yataendelea kuombwa kwa ajili ya uchujaji kwa sababu huko ndiko wanajulikana hasa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, niliombwa nitoe takwimu za uajiri. Takwimu za walioko kambini hivi sasa kwenye mafunzo ya awali ya Jeshi la Polisi jumla wako 1,700 na 350 kati yao wanatoka Zanzibar, migao ya Mikoa itaendelea kuheshimiwa na kama kuna vitendo ambavyo vinaingilia ingilia migao ya Mikoa mingine tutavidhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masharti ya kazi za Polisi, yamezungumziwa sana. Jambo la msingi katika mkataba wa kazi katika kazi zetu karibu zote ni kuwa tayari kufanya kazi popote katika nchi yetu na hilo linafuatiwa na masuala ya uhamisho. Hapa Waheshimiwa

Wabunge wengi wamezungumzia umuhimu wa uhamisho hasa kwa Askari ambao wanakaa mahali muda mrefu.

Suala hili si kwa Askari tu, ni hata kwa wafanyakazi wengine, lakini pia uhamisho unaweza kufanywa katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa kazi. Kwa hiyo, suala la uhamisho halina mjadala, lakini suala la maombi kwamba pamefanyika uhamisho na mtu mmoja hakuridhika, maombi hayo huwa tunayapokea na yanapimwa kila moja kwa uzito wake.

Mheshimiwa Spika, lakini maombi mengi tunayopata mara nyingi ni uhamisho unaoambatana na ndoa. Nadhani mnajua Mheshimiwa Rais Mkapa, amekuwa akiteua ma-DC wengi na hata Wakuu wa Mikoa Wanawake na wote hawa wana waume zao na pengine hawawezi kuhama kwenda kuwafuata wake zao.

Sasa hapa tulikuwa tunajiuliza, Wanawake wataendelea kuzuiliwa kupandishwa vyeo mpaka lini, eti kwa sababu tu wameolewa wakae kwa waume? Hii ni haki ya mtu, mfanyakazi amefika mahali anatakiwa apandishwe cheo, ni lazima apandishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ulitajwa mfano wa uhamisho wa Afisa wetu mmoja wa Uhamiaji, alipelekwa Kilimanjaro kutoka Zanzibar. Huo siyo uhamisho wa kwanza, ameombewa hapa kwamba atafutiwe mahali ambapo atakuwa karibu na mkewe, ambaye ni Katibu Mkuu kule Zanzibar. Ombi hili tumelipokea na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mfano wa Afisa mwingine wa SMZ, ambaye aliazimwa kuja Bara, ana mke yuko Uhamiaji kule Zanzibar. Wenyewe mume na mke wakafanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba, mke anamfuata mume Dar es Salaam, uhamisho huo ukafanyika. Mwaka huu imefika wakati mume anarejeshwa Zanzibar kwenye sehemu yake ya kazi, sisi kule Uhamiaji tulipoona kwamba zile *pressure* tulizopata za kumhamisha huyu mama kumfuata mume tusizisubiri, maadam bwana ameshahama na mke aende haraka haraka. Sasa, *pressure* ikaja kinyume chake, mume na mke wote wakasema, aah mke abaki Dar es Salaam. Tunapambana na matatizo kama hayo, kwa hiyo, mtuhurumie tunapokutana nayo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia, niliulizwa kuhusu suala la *IGP* kwamba, ni mara ngapi amewahi kutoka Zanzibar. Nadhani hizi nyadhifa zinakwenda kwa *merit* na kwa uwezo, hapa tuulizane kama *IGP* ana uwezo au hana! Tanzania ni moja, maana ukianza kuuliza, vile vile utauliza na *Commissioner* wa Polisi Zanzibar amewahi kutoka Bara mara ngapi? Jawabu ni lile lile, hajawahi na hakuna sababu. Nadhani tumuachie Mheshimiwa Rais, kwa mujibu wa taratibu zetu yeye ndiyo mteuzi. Yale ya kisiasa ni sawa, kwamba Rais akitoka Bara, Makamu wake atoke Zanzibar na kinyume chake, lakini haya ya kiutendaji tukiyaingiza huko tutakuwa tunakwenda sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lilizungumziwa suala la Askari walioko Pemba waliotoka Bara. Wale walipelekwa kule kwa uhamisho na barua zao ziko wazi, wanapoonekana wapo ki-*operation* ni kwa sababu tu ya matatizo yetu ya uhaba wa

nyumba za Askari, ndiyo maana unawakuta kwenye mahema na wengi wanakuwa pamoja, tatizo ni hilo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, imezungumziwa sana hoja ya kufanya ajira ya Askari Polisi wote iwe ni *pensionable*. Utaratibu wa Majeshi na siyo Polisi tu na wala si Tanzania tu, ni nchi zote, ni lazima siku za mwanzo uwe na uhakika wa Askari ambaye anaweza kupatikana wakati wote, hana *complications* za kwenda ku-*attend families* na mwenye nguvu, kwa sababu kazi za *field* ni za nguvu.

Kwa hiyo, ndiyo maana siku za mwanzo wanatakiwa wawe wana-*renew* mikataba kwa miaka mitatu, mitatu, kwa Jeshi la Polisi, ili akichoka zile kazi za nguvu aamue kutoka na akitoka apate haki zake. Lakini akikaa kwenye *pensionable*, halafu aamue kutoka na hajatimiza masharti ya *pension*, ndiyo anapotoka bila ya kupata haki yoyote, kwa hiyo, inabidi apime. Hawa Askari wetu wanapewa sana ushauri kabla ya kufikia maamuzi na wanaamua kwa kujua wanachokifanya. Ni kweli yanatokea matatizo ya wawili, watatu na nadhani ndiyo hao wanaolalamika, pengine matarajio yake hayakutumia, lakini hiyo isiathiri mwenendo mzima wa Jeshi. Tunapozungumza na Maaskari katika mabaraza yao, hili suala si miongoni mwa malalamiko tunayoyapokea, hata kidogo, tunapokea mengine yote isipokuwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti za umri wa kustaafu vile vile ni utaratibu wa Majeshi, si Tanzania tu, ni kwa nchi zote. Hoja ni ile ile, kwamba, Askari wa ngazi za chini ni watu wa *field*, wanatakiwa wawe na nguvu na wepesi wa kwenda na zile ngazi za juu zinataka busara zaidi kuliko nguvu. Kwenye mahakama nadhani mara zote wanapendekeza wale Majaji waongezewe muda na hoja ni kwamba, jinsi Jaji anavyokuwa na umri mkubwa, ndiyo na busara inazidi. Kwa hiyo, kwenye Majeshi napo kuna hoja hiyo hiyo. Jeshi lote haliwezi kuwa ni la mabavu, mabavu wanatakiwa wawe nayo watu wa chini, lakini wanaotoa amri, wanaopanga *operations*, waongozwe na busara na hao labda watakuwa ni watu wenye umri mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ndoa kwa Maaskari, hoja ni hiyo hiyo kwamba, siku za mwanzo wanatakiwa wawe *available* wakati wote na ndiyo maana wanatakiwa wasioe au wasiolewe katika miaka ya mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani hoja ya UKIMWI haina uzito sana hapa, kwa sababu taarifa za utafiti tunazozipata zinatubadilisha kwamba, *actually* wanandoa ndiyo wanaathirika zaidi na UKIMWI kuliko wale ambao wako nje ya ndoa. Kwa hiyo, nadhani tungeacha utaratibu ukaendelea kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Serikali kuhudumia mke mmoja iwe ni kwa uhamisho na kadhalika. Kwanza mantiki yake ni kudhibiti matumizi ya Serikali, lakini pili ni usawa, yaani kutoa huduma sawa kwa Watumishi wa Serikali. Serikali imekuajiri wewe, mfano imeniajiri Mheshimiwa Mapuri, imemuajiri na Mheshimiwa Chiligati, ni lazima tutendewe sawa. Kama ni suala la wake, wana haki zao, basi iwe ni mke mmoja tu kwa wote. Mheshimiwa Chiligati kama ana wake wanne, akiongezewa atakuwa amepewa haki zaidi kuliko mie mwenye mke mmoja! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, dini inayoruhusu wake zaidi ya mmoja ninajua ni dini ya Kiislam, lakini msisitizo na wajibu ni mke mmoja eeh, ndiyo, ukitaka wa ziada ni *optional* na amewekewa masharti kwamba, mpaka uwe na uwezo wa kuwapa huduma sawa. Uamuzi wako usiwe mzigo kwa Serikali. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna suala la *housing allowances* kwa Askari. Ni kweli mwanzoni zilipowekwa ilikuwa ni 10% ya mshahara, lakini baadaye uamuzi huo ulibadilika Serikalini, kikaachwa kile kile kiwango kilichokuwepo wakati ule na kikawa ndiyo *housing allowance* ya Askari na ndiyo kinachoendelea. Kwa hiyo, kama kimepitwa na wakati, kitazamwe upya na hiyo hoja nadhani ni ya msingi itabidi tuichukue, lakini haitokuwa *pledged* tena na mshahara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuhudumia vizuka Askari anapofariki, nadhani wamelinganisha na utaratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba mtumishi wa Serikali anapofariki, mke au mume na watoto wanaendelea kulipwa ule mshahara wa mtumishi kwa miezi minne wakati *process* za *terminal benefit* zinafanyika. Hapa utaratibu huo haupo, ila kuna *survivors benefit*, ambazo zina utaratibu wake, zinaanza kuandaliwa pale mtumishi akishafariki, lakini nazo zikishakuwa tayari wahusika wanapewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya mishahara baada ya mafunzo, kupanda vyeo na posho mbalimbali mara marekebisho yanapofanyika. Huko nyuma kweli tulikuwa na tatizo la kuchelewa chelewa, lakini sasa hivi tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa. Hivyo, inapotokea wachache wamesahauliwa ni suala la kukumbushana tu watahughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika suala la kuchelewa kwa mafao. Hapa napenda nizungumzie ombi la Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, kuhusu *X-PC* Omar, ambaye anamshughulikia. Kwa utafiti wangu wa awali, nimegundua kwamba, tatizo lililosababisha kuchelewesha ni kwamba, haikupatikana *death certificate* yake, hiyo ndiyo iliyoleta kikwazo. Lakini pamoja na yote hayo, ninakubaliana na ombi la Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, tutakapoondoka hapa tufuatane, tukalishughulikie hili suala lipate ufumbuzi. Pale Wizarani tulikwishakubaliana na safari hii tulimalize *once and for all*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyongeza za mishahara na posho mbalimbali za Askari, wameombewa hapa ili maslahi yaongezwe. Tunatarajia katika Bajeti hii kutakuwa na nyongeza za mishahara na posho mbalimbali kwa Askari. Hatuzitangazi sasa hivi, lakini kwa uhakika ni zaidi ya zile Shilingi thelathili zilizotajwa hapa jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, kuna mapendekezo ya *hardship allowances* au *risk allowances* kwa Askari wanaopangiwa kazi katika mazingira magumu. Wazo hilo tunalichukua ili tukalifanyie kazi. Hali kadhalika suala la *bonuses* au zawadi kwa

wafanyakazi wanaofanya kazi nzuri katika mazingira fulani mahsusi nalo pia tunalichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la sare za Askari, nadhani jitihada tunazifanya na tutaendelea kuzifanya ili kuziboresha. Hali ilivyo sasa hivi ni tofauti na ilivyokuwa miaka mitatu, minne iliyopita. Pamoja na kwamba tunaona wengine wachache labda sare zao zina hitilafu ya hapa na pale, lakini kwa ujumla ni afadhali zaidi na hali hiyo itaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, pia, niliombwa nitoe ufafanuzi kuhusu Askari anapofariki katikati ya mwezi kwamba, mshahara wake unaishia wapi? Jibu ni kwamba, zinahesabiwa siku zake alizofanya kazi, huo ndiyo utaratibu. Vile vile, tumeelezwa hapa kwamba Askari akipewa uhamisho kupelekwa *FFU* ni adhabu! Hatutarajii hivyo na wala hatutaki iwe hivyo. Sasa, kama Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, aliyesema suala hili ana ushahidi na alisema anao, kwa kweli nitamwomba aninong'oneze ili kama jambo hilo lipo tulikomeshe mara moja lisiendele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mafunzo ya Jeshi la Polisi tuliombwa tuongeze muda badala ya miezi sita iwe ni muda mrefu zaidi. Tulipunguza muda wa mafunzo tukawa na utaratibu wa *crush programs*, kutokana na upungufu mkubwa wa Askari baada kutoajiri Askari wapya kwa kipindi kirefu. Kwa kuwa utaratibu wetu ni kwamba, Askari lazima apate mafunzo ya awali ndiyo aweze kuajiriwa, ndiyo maana tukaweka utaratibu huo wa miezi sita ili katika kila mwaka mmoja tuweze kutoa makundi mawili, hiyo ndiyo sababu hasa. Kwa hiyo, tutaendelea hivyo mpaka hali itakapokuwa nzuri zaidi katika Jeshi letu la Polisi ndipo tutaongeza muda wa mafunzo ya *field crafts*, *marshal arts* na mengine ya kuongeza uwezo wa kiakili yaliyotajwa. Sasa hivi yamo, lakini nadhani tutakapongeza muda nayo yatashughulikiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Polisi Zanzibar, kwa sasa tunaomba kiendeleo na madhumuni yake. Ni kweli huko nyuma tulisita kidogo kupeleka Maaskari kwa kozi za Ukoplo na hii ilitokana na matatizo ya ufinyu wa Bajeti, lakini sasa hivi Bajeti yetu imeshaanza kuruhusu, hivyo Chuo kile kitatumika kikamilifu kwa mafunzo ya Ukoplo. Tusipoyafanya mafunzo hayo, kwa kweli tutakuwa tunakaribisha matatizo kwa sababu huwezi ukawa na Askari wengi ambao ni *private* tu hawapandi daraja na kuingia Ukoplo ni lazima upate mafunzo na utaratibu huu tunataka tuendeleo nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tatizo la kesi ya Mbarali lilitajwa kwa mambo mawili, kwanza ni wale Askari. Kuna wazo hapa kwamba, pengine wamechukuliwa hatua ambazo hazistahili na pia kulikuwa na rai ya wale waathirika kulipwa fidia. Kwa utaratibu wetu, maadam hili suala liko Mahakamani hivi sasa, ni vyema tuache mkondo wa Mahakama umalizike, sasa ukishamalizika, haya yote tutayatazama kwa mujibu wa hali itakavyokuwa wakati huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumetajwa matatizo mengi yanayohusiana na utendaji kazi wa Askari ambayo ni masuala ya rushwa, kushirikiana na majambazi au kuwalinda majambazi, kupuuza taarifa za Wananchi, kutoa siri za wanaotoa taarifa na kadhalika.

Tunaomba na tunasisitiza kabisa kwamba, haya ni maeneo ambayo tunaendelea kuomba msaada kwa jamii yote, Wananchi pamoja na Viongozi wenzetu. Tunapoyaona matendo kama haya ni vizuri tuwe tunaarifiana ili yachukuliwe hatua. Katika suala hili, ninamwomba kwa dhiti kabisa Mheshimiwa Dr. Chiduo, anisaidie kuhusiana na hao anaowajua wanashirikiana na wanalinda majambazi. Sasa hivi tuko kwenye vita dhidi ya majambazi, halafu atokee tena Askari ashirikiane na jambazi, huyo ninamtaka! Ninamtaka kabisa kabisa iwe mimi au yeye. Pia, wale wengine wote wanaojua kuhusu hali hiyo tusaidiane. (*Makofi*)

Kuhusu *traffics* wanaovizia, nadhani ni mbinu ya kazi. Kule Zanzibar ninajua kwamba, kuna zile *road blocks*, Mheshimiwa mmoja alizitaja, pale ndiyo wanaenda kupekuliwa, abiria wanahesabiwa na kadhalika. Sasa, maadam wanajua kwamba kazi hiyo inafanywa kwenye kituo tu hata kama dreva amejaza abiria, akikaribia kwenye kituo hicho anawashusha, anakwenda pale na idadi yake sawa. Akipita kwenye kituo, anasogea mbele kidogo anasimama, anasubiri abiria wake wanaingia tena! Wakati mwingine hii kuvizia nayo inasaidia, ili madreva wasiwe na uhakika hasa ni mahali gani watakaguliwa. Hiyo ni pamoja na wingi wa abiria, kupima *speed* na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia, imelalamikiwa kuhusu suala la matumizi ya nguvu za ziada. Askari tunawasisitiza kwamba, waongozwe na taratibu zao na taratibu hizo ziko wazi namna nguvu gani itumike katika mazingira gani. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatutumii nguvu za ziada kiholela, tunawahimiza Askari wetu wajitahidi kufuata taratibu mpaka pale ambapo kwa kweli inabidi nguvu ya ziada itumike ndiyo itumike. Nadhani sasa hivi hali si kama ilivyokuwa huko nyuma. Kuna suala la kuruhusu *private investigation* na suala la upelelezi na uendeshaji wa mashaka kutenganishwa. Ni masuala ambayo yanafanyiwa kazi Serikalini katika vyombo vinavyohusika na hasa hili suala la uendeshaji wa mashtaka, Polisi wamekasimiwa yale madaraka na mwendesha mashtaka mkuu, kwa kweli wao hawana pingamizi hata kidogo kama mwendesha mashtaka mkuu ataamua kuzifanya mwenyewe zile kazi. Lakini kwa kweli kutokana na uzoefu wa muda mrefu si jambo la mara moja kuamua, inabidi na mwendesha mashtaka mkuu mwenyewe ajiandae kwa kazi hiyo na nadhani sasa hivi wako katika hatua ya kujiandaa. (*Makofi*)

Vile vile masuala ya ubambikizaji kesi, haya matatizo tutaendelea kupambana nayo kama nilivyosema na mengine tusaidiane kutoa taarifa tunapona mambo kama hayo yanatokea. Pia, motisha kwa *informers* zipo kwenye Bbajeti safari hii tumeweka. Wajibu wa kujenga mahusiano mazuri na jamii tunauhimiza. Kesi za madawa ya kulevyo ilitajwa kwamba kule Zanzibar kulikuwa na kesi 400 za madawa ya kulevyo, kesi hizo zimefutwa. Lakini tulipochunguza tumegundua kwamba katika kipindi cha miaka 8 iliyopita, kesi zilizofutwa ni 120 tu na zote ni kutokana kukosekana kwa ushahidi. Hatusemi kwamba hakuna kosoro kwa upande wa Askari wetu, lakini nalo vile vile nahimiza kwamba, tusaidiane tunapowapata hao watu. Lakini sisi tunapowapata wote wale ambao wanashiriki katika kuvuruga ushahidi, kwa kweli tunawachukulia hatua. Hivi karibuni wapo Maaskari Maofisa tumewafukuza kazi kwa sababu kama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu suala la *road blocks* zinazokera kule Zanzibar. Tutazungumza na wenzetu, lakini kwa sababu hili suala zaidi ni kule Zanzibar, nadhani Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhani, usisahau yale mazingira maalum ya kule Zanzibar, pamoja na hamu yake ya kutaka ziondoke hizi *road blocks*. (Makofi)

Vile vile kesi ya ajali ya Kaskazini Unguja, ambapo kuna waliopata ajali hawakuitwa hata mmoja kwenda kutoa ushahidi nimetakiwa nikaulizie kule Mahonda, nimekubali nitafanya hiyo kazi. (Makofi)

Kuna wazo kikosi cha *high way patrol* tumelichukua na suala la *speed governors* kuwa hazifanyi kazi nadhani tumekuwa tukijibu maswali kwamba tutaendelea kuongeza ukali wa kukagua *speed governor*. Lakini pia kutazama na *speed* zenyewe kama zile za km 80 kwa saa bado tuendele nayo au tuirekebishe. Lakini wakati tunalalamika kwamba *speed governors* zimefeli, kule Zanzibar wanazihitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Uhamiaji, kuna suala moja limezungumzwa kwa hamasa hasa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, suala la *vote* maalum ya Idara ya Uhamiaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Idara ya Uhamiaji kuwa na *vote* yake si suala la mjadala hata kidogo. Mimi nalikubali na Wizarani tumelikubali. Mara ya kwanza nilisikia kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama nilipoulizwa katika utekelezaji wa ahadi za nyuma. Kwa kweli nilishangaa kusikia kwamba, Idara ya Uhamiaji hawana *vote*, wakati ule nilikuwa bado ni mgeni sijajua Wizara ya Mambo ya Ndani. Mimi ninajua Idara ya Uhamiaji ni miongoni mwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama mkubwa, ina uzito wake, nilitarajia kama wanayo *vote* yao. Lakini kumbe *historically* toka huko nyuma walikuwa hawana. Lakini nadhani kwa sasa hivi umefika wakati wa hiki chombo kuwa na *vote* yake. (Makofi)

Zaidi ya sababu alizozitoa Mheshimiwa Ponsiano Nyami, lakini ukweli katika utaratibu wa sasa, ambapo Idara ya Uhamiaji ipo ndani ya utawala, wote uhamiaji na utawala wanaumia. Idara ya Uhamiaji wanaumia kwa sababu unapojenga hoja bado utaonekana ni utawala haijitokezi kwamba ni chombo cha dola kama vile ambavyo tulivyoweza kujenga hoja kwa Polisi na Magereza, ambao walikuwa na *vote* zao ikaonekana. Lakini pia na utawala nao, ile *allocation* ikishaonekana pale imechanganywa na Idara ya Uhamiaji inaonekana kubwa kwa mtazamo wa utawala maana masuala ya utawala kidogo tunayabanabana ili kutoa *priorities* kwa maeneo mengine. Kwa hiyo, matokeo yake ikitazamwa *figure* ile kama sasa hivi ni shilingi bilioni 9, kwa kweli kujenga hoja unaambiwa utawala tunayo shilingi bilioni 9. Sasa pengine Uhamiaji wangekuwa *separate* ikaonekana wazi jinsi ambavyo *staff* unaweza ukajenga hoja kabisa kwamba na utawala waongezewe fedha ili waendeleze shughuli zao vizuri. (Makofi)

Kwa hiyo, nimesema nilisikia mara ya kwanza nilipokwenda Tume ya Ulinzi na Usalama, kwenye kikao cha mwanzo tulikuja kulifuatilia, sasa tulipokuja kulifuatilia tukagundua kwamba, utaratibu wa maandalizi ya Bajeti ulikwishafikia hatua kubwa, kiasi ambacho isingewezekana kuanzisha *vote* katika kipindi hiki. Niliporudi nikaenda

nikaripoti kwenye kikao cha pili sasa kwenye Kamati ya Tume ya Ulinzi na Usalama wakanielewa ndiyo maana nadhani Wajumbe wa Tume ya Ulinzi na Usalama hawakulizungumzia hilo, wamenipa *another chance*. Naomba na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, naye anipe hiyo nafasi. Namwomba asije akatoa ile shilingi, naihitaji sana kama motisha ya kuendelea kulifuatilia hilo, maana kama ataitoa kwenye mshahara wangu sasa nitakuwa mnyonge kwa kupungukiwa shilingi kwenye mshahara wangu. Kwa hiyo, namwomba kwa dhati kabisa, kwa hilo nataka nimhakikishe kwamba, sisi *at least* nina hakika na Waziri mwenzangu wa Utumishi, tuna hakika kabisa na tumepania kuhakikisha kwamba, mwaka ujao dosari hiyo tutakuwa tumeirekebisha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa tatizo kwamba kwa nini inakuwa vigumu kupata *passport* wakati ni haki ya kila raia? Ni kweli kabisa lakini tukumbuke pia Tanzania ni nchi maskini, tuna matatizo ya kiuchumi, bado tunahangaika kukuza uchumi wetu, kuchapisha hizi *passport* ni gharama kubwa. Nadhani nalo mmelizungumzia sana, tunahangaikia vitambulisho ambavyo ni rahisi zaidi, sembuse *passport* ambayo ni ghali zaidi. Kwa hiyo, tuendeleo kuvumiliana, tukuze uchumi wetu kadri ambavyo tunakwenda, *Inshallah* itafika siku ambapo anayezaliwa tu ataandaliwa *paspoti* yake. Lakini kwa sasa hivi hali yetu haijaturuhusu kufikia hatua hiyo. (*Makofi*)

Kuhusu vitambulisho kama nilivyoeleza kwamba tumeshaamua sasa tunafanya utaratibu mwingine, nimeeleza kwenye Hotuba yangu ya Bajeti, baada ya kuachana na yule ambaye alikuwa mzabuni wa mwanzo na hamu yetu kwa kweli tunataka kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005 tuwe na vitambulisho tayari. Hili tulifanya kwa ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu analisimamia kwa karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna suala la Sheria ya *Passport*, suala la wanaostahili *Diplomatic Passports*, tulipitisha sheria mwaka 2002. Nataka nikiri kwamba, kwa kiasi fulani tulipitiwa wote kwa sababu wakati wa kupitisha kile kifungu ile *schedule of amendment* haikuwepo na ilipokwenda kwa mwandishi wa sheria akatazama *strictly schedule of amendment* ikawa haipo kwa hiyo kukawa hakuna njia ya kuliingiza maana atakuja kulaumiwa yeye. Halafu kuna watu wengine ambao wanastahili hizi *Diplomatic Passport* wamesahauliwa, mmojawapo ni Mkaguzi na Mdhambi Mkuu wa Mahesabu ameachwa. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile tutalazimika tulizingatie upya kwa marekebisho ya kisheria kwa kadri ambavyo tutaona inafaa na tutajitahidi kuharakisha hayo marekebisho yaje yatakayozingatia yale ambayo tutakubaliana. (*Makofi*)

Kwa bahati mbaya ile sheria tumefunga mlango, maana wakati mwingine Mawaziri huwa tunaomba hapa jamani weka mwanya fulani ili Waziri aweze kucheza, lakini tunakuwa wagumu. Sasa hili limefunga kabisa mlango kwa hiyo, Waziri hana nafasi ya kuweza kufanya *administrative arrangement*, mpaka hapo tutakapofanya marekebisho.

Halafu tuliombwa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Bunda tumelipokea tutalifanyia kazi. Vilevile tuliulizwa hapa kama tumepeleka watu wangapi nje kwa ajili ya kuhukumiwa kwa ajili ya ugaidi. Hatuna hata mtu mmoja ambaye tumempeleka nje kwa ajili ya kuhukumiwa nje ya nchi kwa ugaidi wala si kwa kosa lingine lolote.

Tutakumbuka ni kweli kuna Mtanzania alihukumiwa kule Marekani baada ya matukio ya ugaidi Dar es Salaam na Nairobi, lakini tunakumbuka vile vile kwamba, Mtanzania yule alikamatiwa Afrika ya Kusini na akapelekwa kule kutokea Afrika Kusini siyo Tanzania. Wala hakuna raia wa kigeni ambaye tumempeleka nje kwa ajili ya kuhukumiwa hata mmoja. Kwa hiyo, hilo nataka niwahakikishie hakuna hata mmoja aliyepolekwa kuhukumiwa nje kwani niliambiwa nitoe idadi na idadi ni hiyo ni *zero* kwa wote wawili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la fomu ya *PF3* nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, waliozungumzia hasa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, ambaye analifuatilia sana suala hili kwamba hatua safari hii zimeshaanza kuchukuliwa. Kuna vikao vya Watendaji vimeshaka zaidi ya mara mbili na wameshaanza kuifanyia marekebisho ikiwa ni pamoja na kwamba, iendeleo fomu moja au ziwe mbili, yote hayo bado uamuzi haujafikiwa. Lakini kimsingi nataka kumwambia kwamba, limeshaanza kufanyiwa kazi na mimi nina *instruction* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba niitishie kikao cha Mawaziri wenzangu tunaoshughulikia hizi fomu. Kwa hiyo, tulikubaliana kwanza kuwatuma Watendaji wetu walifanyie kazi ili likija kwa Mawaziri lije kwa ajili ya maamuzi halafu tutoe taarifa. (Makofi)

Vile vile nilitakiwa kufafanua kuhusu kujamiiana na kubaka. Mheshimiwa Mbunge aliona kwenye ile *table* vimetajwa vitendo vya kujamiiana. Lakini yeye anajua kwamba, kosa linalompeleka mtu Mahakamani ni kubaka. Sheria inazungumzia makosa ya kujamiiana, kubaka ni miongoni mwa makosa hayo na anaweza kwenda mwanamke Mahakamani kwa kosa hilo hilo la kubaka kama atakuwa ameshiriki katika kitendo cha kusaidia kubaka anaweza kutiwa hatiani kwa hilo. Naambiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hata kubaka na yeye mwenyewe. Kwa hiyo, kujamiiana ndiyo sheria inavyosema, ndiyo maana likatumika hilo neno lakini *otherwise* vyote ni sawa. (Makofi/Kicheko)

Halafu kuna suala la gereza kuwa shule ya sekondari, nilipata ombi la Gereza la Mgagalo Kilolo kutoka kwa Mheshimiwa Venance Mwamoto, pia nina barua ya Mheshimiwa Jackson Makwetta, wanaomba lile gereza kule ligeuzwe kuwa shule ya sekondari. Sasa hili tumelichukua na tunalifanyia kazi, lakini zaidi nitakwenda mwenyewe nikaone hali halisi kule halafu tuone la kufanya. Lakini kwa vyovyote vile shule ya sekondari maadam wanaitaka ni lazima watajenga. Sasa ama wajenge mahali gereza liachwe au kama watataka gereza ikifika huko basi itabidi wajenge gereza ambalo ni *standard*, ambalo wanatakiwa watukabidhi hilo, halafu wao wapate yale majengo. Kimsingi wataendelea kupata gharama, lakini jibu hasa nitatoa nitakapokwenda kuona kule tutabadilishana mawazo na Mkuu wa Mkoa na Wilaya na wadau wengine tutaona jinsi ya kufanya. (Makofi)

Vile vile masuala ya msongamano magerezani, suala la wafungwa watoto kuchanganywa na watu wazima, wafungwa wanawake, wenye watoto kuwekewa fursa ya kulea watoto, tumepata maombi hayo, wafungwa wajawazito na mengineyo. Juhudi zetu katika kuondoa msongamano ni pamoja na suala zima la kushughulikia *facilities* za wafungwa watoto na wanawake wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, hayo ni miongoni mwa

mambo ambayo katika uboreshaji wetu wa mazingira katika magereza tunayazingatia wakati tunakwenda. Hivi sasa hatujafika mahali pa kuleta *effects*, lakini tunaamini kwa mwenendo wa Bajeti tunavyokwenda sasa hivi, tunatarajia muda mfupi tutafikia mahali matokeo yataonekana. (*Makofi*)

Vile vile Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, alizungumzia tatizo la baiskeli kule Bukoba. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare aliniletea hili tatizo na ni kweli kabisa nimelifuatilia si mara moja, si mara mbili, kwa kuzungumza na Mkuu wa Mkoa mwenyewe na wadau wengine kuona hasa tatizo ni nini. Nataka nimwambie Mheshimiwa Lwakatare kwamba, Polisi kule wanafuata amri na ndiyo kazi yao. Amri zile zina nguvu za sheria na sheria inayokataza vyombo kama hivyo visivyokuwa vya moto kubeba abiria. Kwa hiyo, inapotoka amri kwenye *authority* ambayo inahusika Polisi ni wajibu wao kuitekeleza amri hiyo. Kwa hiyo, *solution* ya msingi ya tatizo ni kule kule Mkoani, wenyewe muamue kwa sababu Mheshimiwa Lwakatare, wewe ni sehemu ya Mkoa, mkae muelewane. Mimi taarifa ninayopewa ni kwamba, hizi baiskeli pale mjini zinasababisha ajali nyingi za mara kwa mara. Pengine sehemu nyingine hawana tatizo hilo na ndiyo maana unawaona Geita, Tanga hawana tatizo la ajali. Lakini ajali zinatokea mara kwa mara na uongozi hauwezi kunyamaza. Kwa hiyo, hilo hasa ndiyo la msingi pengine wenyewe Mkoani wakae walizingatie wapime athari za ajali na faida za biashara na kama sheria zinaruhusu. Sisi askari wetu tumewakataza maana alinipa picha kama Askari wetu kidogo ni *harsh* au *brutal* au *ruthless* katika kufuata sheria, sisi tumewahimiza kufuata ubinadamu katika kufanya kazi na ndiyo maana naambiwa rusha roho zimepungua.

Halafu kuna suala la baiskeli zinazorundikana, wale wenye baiskeli nao wanachangia kwa sababu hutakiwa waende wakazichukue, lakini hawaendi sasa sijui wanaogopa nini? Labda nimwombe hapa Mheshimiwa Lwakatare, atusaidie kuwahimiza wenye baiskeli zao kwenda kuzichukua. Baiskeli na vyombo vingine kama vinapokamatwa baada ya muda fulani vinakuwa *gazetted* kwa ajili ya kuuzwa. Vikishakuwa *gazetted* vinatangazwa kwamba vyombo hivi vinauzwa kama hawakutokea wenyewe kweli vitauzwa na ndiyo hivyo vilivyouzwa ni kwa misingi hiyo. Sasa hivi vilivyopo kabla havijafikia hatua ya kuuzwa nimwombe Mheshimiwa Lwakatare, akawahimiza wenyewe wakachukue baiskeli zao na sisi tumeshawaambia Polisi kwamba, wanapokuja wenye baiskeli zao wapewe na sisi tunakereka kuona marundo yale.

Mimi niliona kwenye picha siku moja baada ya kuniletea baadaye niliona na kwenye gazeti, hata kule wenzangu tulipowapelekea zile picha kila mmoja alishtuka baiskeli hizi namna gani! Kwa hiyo hata sisi hatupendi kuona namna ile.

Halafu kuhusu kesi ya yule mtu aliyemtaja, suala hili tumeshalifuatilia, tumeshatuma watu kutoka Makao Makuu waende wakapate ukweli wa ndani kama kuna kesi ya kufunguliwa basi ifunguliwe. Halafu Mheshimiwa Lwakatare, alisema kuhusu maneno ya kwenye kampeni, tunapokuwa kwenye kampeni tunasema maneno mengi! Mimi nadhani wewe umeniambia waliosema CCM, tukija tukiwauliza na uliyosema wewe pengine na wao watakuwa na mengi ya kusema. Kwa hiyo, hayo yasisitishughulishie

katika kazi zetu ndani ya Bunge, hayo ni ya *field* za kisiasa, tukabiliane nayo huko huko. *(Makofi)*

Kuhusu suala la wakimbizi ilielezwa kwamba wamekuwa tishio hasa baada ya kupungua kwa chakula katika makambi. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, hali ya chakula sasa hivi imeanza kuwa afadhali kidogo kwa hiyo kwa upande wa chakula baada ya kutoa wito kwa wahisani tukapata *response* nzuri, sasa hivi hali ya chakula imeanza kuwa bora zaidi. Sisi tutaweza kuwarejesha makwao kama mlivyoomba na mimi nimekwishasema kwenye hotuba kwamba tunaendelea na juhudi hizo na karibu tutakaa kikao cha *Tripartite Commission* na wenzetu wa Burundi ili kuzungumza utaratibu wa kuharakisha urejeshaji wa wakimbizi Burundi. Lakini ingawa wakati huo huo tukubali vile vile kwamba matatizo bado yapo.

Nimalizie kwa kuongezea kidogo alipozungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri, ametaja maeneo mengi na kutoa ahadi za hapa na pale kuwahakikishia Wabunge yale ambayo Bajeti ime-*cover* kwamba, hili litashughulikiwa na lile ambalo Bajeti yetu ya mwaka huu kidogo haitaweza ku-*cover* tumewaambia. Labda niongezee kwa kule Pemba kuna Ofisi ya *RPC* Mkoa wa Kusini Pemba na Nyumba ya *RPC* na *RCO* hizo zimo kwenye makisio ya mwaka huu, kukamilisha Ziwani Majengo ya Polisi imo kwenye makisio. Kwa hiyo, nalo lipo. Ila suala la Mji Mkongwe ile ya Malindi kidogo atatuvumilia, sasa hivi tunafanya makisio ili pengine kwenye Bajeti ya mwakani tutakuja kulishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulikwishaeleza kwamba tutakapokuwa kwenye Kamati tunakusudia kuomba marekebisho kwenye sehemu fulani.

Baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri kabisa na kuichangamsha Wizara yetu na kwa ujumla wamekuwa wenye kutusaidia na kwa mara ya kwanza tumepokea pongezi nyingi, tunazipokea na tunaamini mwakani tutapokea nyingi zaidi kwa sababu tutajitahidi kuyatekeleza tuliyoahidi pamoja na yale ambayo wametupa mawazo tutakayoyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoieleza siku za nyuma kwamba, Katibu atataja fungu halafu Mheshimiwa Mbunge, yeyote anayetaka ufafanuzi

katika mojawapo ya programu za fungu hilo anaweza akasimama. Tunaendelea na utaratibu huo.

Fungu - 28 Idara ya Polisi Sh. 64,486,361,200/=

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *vote* 28, programu ya 20, *subvote* 2001 *item* 310200 *acquisition of buldings* ukurasa wa 32, nimemwandikia Mheshimiwa Waziri, kutokana na matatizo ya Kituo cha *Mbamba Bay*, pamoja na nyumba za Askari, majengo yake yako katika hali mbaya sana. Majengo yalijengwa miaka karibu 37 iliyopita na toka yamejengwa hakuna ukarabati wowote uliofanyika. Kwa hiyo, niliomba ingefaa sana kwa kulinda haki ya wafanyakazi wa Polisi, walau ukarabati wa jengo la Kituo cha Polisi, pamoja na nyumba za Askari. Lakini katika majumuisho Mheshimiwa Waziri hakuweza kuelezea chochote kile. Ahsante.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maelezo yake. Suala la ukarabati wa Vituo vya Polisi, nadhani kila Mheshimiwa Mbunge, akipewa nafasi atazungumzia hilo hilo kwamba wana vituo ambavyo vina uchakavu na vinatakiwa kufanyiwa marekebisho. (*Makofi*)

Sasa kwenye programu yetu ya *Maintenance* kwenye *Recurrent* na kwenye *Capital*, tutapeleka baadhi ya fedha zinazokwenda kukarabati Vituo ambavyo viko katika hali mbaya sana na Kituo cha Mheshimiwa Luoga cha *Mbamba Bay* ni miongoni mwa vituo ambavyo vinahitaji ukarabati kweli kwa sababu nacho kiko katika hali mbaya sana.

Kwa hiyo, tutazingatia katika Bajeti hii hii ya mwaka huu kutokana na programu hizi. (*Makofi*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 28, *Sub-Vote* 2001, kifungu kidogo cha 270300 - *Vehicle and Mobile Equipment*. Mimi nimechangia kwa maandishi na Mheshimiwa Naibu Waziri, alijaribu kujibu kidogo juu ya Igunga kuwe na mahabusu na gereza. Inavyotokea pale Igunga hawana mahabusu wala hawana magereza. Kwa hiyo, wanapowakamata wahalifu kuwaleta kwenye Gereza la Nzega na wanapowaleta pale kwenye Gereza la Nzega huwasahau mpaka wale ndugu wa wahalifu wawatolee nauli kuwalipia kwenda kuhudhuria kesi.

Sasa kwa kifungu hiki kwa sababu kuna *mobile vehicle* haoni ingekuwepo gari maalum kwa sababu Naibu Waziri alisema kwamba hakuna mpango wowote wa kujenga gereza au mahabusu pale Igunga, iwepo gari maalum itakayowaleta mpaka mahabusu ya Nzega ili waweze kuchukuliwa tena kurudishwa Igunga kwa ajili ya kuhudhuria kesi zao ili kulipa nafasi Gereza la Nzega ambalo kila wakati linakuwa limejaa au kama haiwezekani hivyo basi wawapeleke Uyui kwa sababu Gereza la Uyui ni kubwa zaidi kuliko Gereza la Nzega?

Kwanza Gereza la Nzega ni la wafungwa 52 tu, lakini mara zote huwa limejaa. Kwa hiyo, naomba gari au wawe wanapelekwa Uyui.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango wa Maendeleo wa Magereza, tunao mradi wa ununuzi wa magari na tunakusudia kununua zaidi makarandinga haya ya kuchukulia wafungwa na mahabusu. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Mbunge, tuzungumze zaidi tutakapotoka. *(Kicheko/Makofi)*

Anielewe kwa sababu tukianza kuahidi hapa itakuwa kila mmoja atataka hivyo. Tunakusudia kupeleka kwenye matatizo ya aina hiyo ambayo ameelezea Mheshimiwa Selelii. Matatizo kama ya Mbarali na mengine ambapo inabidi tuhamishe mahabusu. Kwa hiyo, bila shaka ni eneo ambalo litakuwa la aina hiyo, ndiyo maana nikasema tutazungumza zaidi kwa sababu ya kupata undani zaidi na atanipa *data* zaidi. Wakati wa ugavi wa magari haya au ugawaji wa magari haya tutazingatia hilo.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Ahsante sana Mwenyekiti. *Vote* 28, Kifungu namba 270100.

MWENYEKITI: Mwenyekiti amesikia, endelea.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Sawa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunilinda. Nyumba za mbao ambazo ni za Maaskari wa Mgumu zimezeeka vibaya sana na Maaskari wana hali mbaya sana kule. Ningeliomba Mheshimiwa Waziri, anihakikishie hapa kwamba, Kituo hicho nacho kitaangaliwa.

MWENYEKITI: Anazungumzia *maintenance of physical infrastructure* Musoma.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nyumba za mbao itabidi tuzione kwanza kama zinafaa kwa *maintenance* au ni ujenzi mpya. Ikibidi ujenzi mpya tutamwomba tushirikiane, kama ni *maintenance* kama nilivyosema, tunacho kifungu safari hii ambacho ni kwa ajili ya vituo kama hivyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Idara ya Magereza Sh. 38,060,371,900/=

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia katika hii *Vote* ya *Prison and Administration Services*, kuna Gereza la Kiteto ambalo limekwisha.

MWENYEKITI: Liko katika kifungu gani cha programu ya 10?

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Nahitaji na programu hiyo, nahitaji tu mshahara wa Kamishna huyo wa Magereza. *(Kicheko)*

Nadhani Mwenyekiti umenielewa. Nilikuwa nachangia kwamba kuna Gereza la Kiteto limekwisha kwa mahabusu na tunapeleka sasa hivi wafungwa mpaka Kondo na hatuna gari. Nilikuwa ninaomba maelezo kwamba ni lini mtafungua hilo gereza ambalo limekwisha badala ya mahabusu kuteseka? Naomba jibu. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwa kazi kama zile ambazo zilikaa muda mrefu na kazi nzuri kama zile tutahitaji tupate mtu mzito kidogo wa kuja kufungua lile gereza, ambaye pengine sitakuwa na uwezo hapa kumpangia ratiba na kujua hasa ni lini. Lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge, achukue *spirit* hiyo kwamba, tutajitahidi haraka iwezekanavyo tupate mtu mzito wa kuja kulifungua Gereza. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Sh. 9,668,005,900/=

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri katika suala nililolizungumzia kuhusiana na baiskeli, kwa kweli sikuridhika nalo kwamba yamekuwa ni majibu ya jumla jumla. Tatizo langu la msingi nililoeleza si suala la biashara ya baiskeli ndani ya mji ambalo ndiyo chanzo cha tatizo. Maelezo yangu niliyoyotoa hapa mbele ya Bunge lako, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nimeeleza kwamba zoezi linaloendelea linawahusisha hata watu ambao hawafanyi biashara hii, *which means* kwamba, kumekosekana maelekezo mahususi toka utawala, ambayo yanaweza yakatofautisha kati ya watu ambao wanafanya biashara ya baiskeli na wale ambao wanatumia baiskeli kwa matumizi yao binafsi.

Kwa hiyo, katika majibu yake anapozungumzia zaidi suala la biashara ya baiskeli. Sasa mimi ningetaka kujua ufafanuzi, atoe ufafanuzi mahususi ambao utaweza ku-*rescue* watu hawa ambao hata hawahusiani na hizo taratibu zilizozuiwa za kufanya biashara ya baiskeli na pia kwa mtu ambaye ana akili timamu, sidhani kama anaweza akakataa kwenda kuchukua baiskeli yake wakati ambapo ni mali yake ameipata kwa jasho lake.

Sasa chanzo cha tatizo ni kwamba, hata baiskeli zilizoko pale zimeshindwa kuchukuliwa na wahusika kwa sababu wakienda wanaambiwa hii baiskeli ina makosa matatu, manne, matano na kila kosa Sh. 10,000/=. Kwa hiyo, ulete Sh. 50,000/= na baiskeli haina thamani hiyo. Sasa kwa kuwa mamlaka mazima ya Serikali yako hapa ambayo hata huyo Mkuu wa Mkoa anayezungumzia bosi wake yuko hapa. Anaweza akatoa maelekezo. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari kutoa maelekezo kwamba hawa watu wahusika wote wenye baiskeli ambazo ni zaidi ya baiskeli 1,000 waende wakachukue hizo baiskeli zao? Utaratibu uwekwe ili wachukue baiskeli zao bila masharti yoyote ya hizo Sh.20,000/=, Sh. 30,000/= na Sh.50,000/=. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa matatizo kama haya ni ya bughudha kwa wapanda baiskeli

ambao hawafanyi biashara ya kubeba abiria. Kwa kweli nataka nimhakikishie kwamba nikitoka hapa miongoni mwa mambo yangu ya mwanzo kabisa ni kutoa agizo la kuhakikisha kwamba bughudha hizo zinaondoka, hazistahiki. *(Makofi)*

Nimesema vile vile kwamba, wenye baiskeli zao waende wakazichukue na nilikuwa na maana kwamba pasiwepo na bughudha ya kutokabidhiwa baiskeli zao. Mradi tu athibitishie baiskeli ni yake. *(Makofi)*

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia programu ya 10, *Sub-Vote* 1001, Kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri.

MWENYEKITI: Mshahara wa Waziri hauko hapa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: *Okay!*

MWENYEKITI: Unataka mshahara wa nani wa Kamishna wa *Prisons* siyo? *(Kicheko)*

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia, nilichangia mambo mawili. Nilitaka maelezo tu, sina tatizo na mshahara wa Waziri, atapata. La kwanza lilikuwa nipate maelezo kuhusu uanzishwaji wa Chuo cha Upelelezi. Sasa hili sikupata maelezo. Kwa sababu walikuwa na mpango wa kujenga Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma. Sasa nipate maelezo.

La pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati anajibu hoja alisema kwamba, Gereza la Mpwapwa linaendelea kujengwa, nakubali na tsubiri mpaka likamilike ndipo tupate umeme. Lakini gereza linafanya kazi kuna wafungwa, kuna maaskari hawa wote wanataka umeme. Sasa hao maaskari watasubiri mpaka gereza likamilike ndiyo wapate nao umeme? Kwa hiyo, nilikuwa napenda nipate maelezo.

Halafu vile vile jinsi Serikali inavyozidi kuchelewa kupeleka umeme kuna hatari gharama zitaongezeka halafu Serikali itabeba mzigo mkubwa sana. Ahsante Mwenyekiti.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Chuo cha *CID* nadhani tuliliruka kwa bahati mbaya. Lakini kwa Bajeti ya mwaka huu tutaanza maandalizi. Kiwanja tumeshapata, tunaanza na maandalizi ya ramani na upimaji ili ujenzi uweze kuanza kwenye Bajeti ya mwaka ujao. Ikiwa wakati huo tutakuwa hatujapata wahisani, kwani ni miongoni mwa mambo ambayo pia tunatafutia wahisani wa kutusaidia.

Kuhusu umeme kwenye gereza, maadam gereza limemalizika na umeme una wajibu kufika. Lakini pia ni ukweli kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, masafa kidogo ni marefu na gharama ni kubwa. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kila tukikaa gharama zitaongezeka. Kwenye Bajeti yetu ya mwaka huu, kwa bahati mbaya katika kupanga hicho kidogo tulichonacho kwa kweli

hali haituruhusu. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, atuvumilie mpaka Bajeti ya mwaka unaofuata. *(Makofi)*

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nataka ufafanuzi. Nilichangia kwa maandishi na nimechangia mengi sijasikia hata moja kwamba limejibiwa. Lakini labda niulize moja na lingine ambalo nimesikia alipokuwa akitoa majumuisho Mheshimiwa Waziri. Kwanza kuhusu *passport* za Wabunge. Tulipokuwa tunapitisha *passport* tulisema kwamba, Waheshimiwa Wabunge wapate *Diplomatic Passport*. Wewe ni shahidi, AG ni shahidi, Waziri Mkuu ni shahidi. Lakini nashangaa sasa hivi Waziri amesema kwamba, imesahaulika ile *Schedule of Amendment* kwa hiyo, haikuwekwa. Ndivyo alivyosema.

MWENYEKITI: Hatukukusikia vizuri, ni kwa wake za Wabunge au waume za Wabunge?

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Lingine, tuna huu wakati wa operesheni, Wasomali walipotoka Longido kule na Loliondo Serikali ilituambia kwamba, tujenge Kituo cha Polisi na walituambia tujenge tukifikisha kwenye *intel* watamalizia. Tumejenga kituo kimoja kule *Lake Natron* na hicho kituo kimefika kwenye *intel* lakini hatujaona nguvu ya Serikali. Sasa Waziri atatuambia nini kuhusu hicho kituo ambacho mimi na DC tuliamia kule kuchangisha ng'ombe ili kituo hicho kijengwe?

Sasa naomba nipate maelezo niende kuwaambia nini wananchi kwa sababu kila siku wananiambia Mheshimiwa Mbunge hiki kituo tumekimaliza, waite Serikali wamalizie. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira maalum aliyoeleza katika fungu letu ambalo tutasaidia nguvu za wananchi, hicho kituo chake kimojawapo, kwa maana ni vingi, tumwahidi kimoja kwa mwaka huu cha *Lake Natron*. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Fungu 28 - Idara ya Polisi... .. Sh.5,300,000,000/=

MWENYEKITI: Waziri alitaka kurekebisha Fungu la 28, Mheshimiwa Waziri, ni wapo ulipokusudia kufanya marekebisho?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tufanye marekebisho ukurasa wa 11, *project number 5736*, ambayo imeandikwa Ujenzi wa Nyumba za *FFU* Ukonga. Mradi huu umeshakamilika,

tulichokusudia mwaka huu kwa kweli ni ujenzi wa nyumba za makazi na Ofisi Tanzania Bara.

(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa)

Fungu 29 - Idara ya Magereza Sh. 2,900,000,000/=

MHE. ESTHERINA KILASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anatoa majumuisho alisema kwamba, hakutakuwa na kazi mpya ambazo zitafanyika kwa kipindi hiki, isipokuwa kumalizia viporo. Lakini kwenye hotuba yake katika ukurasa wa 26, Mheshimiwa Waziri amesema kutakuwa na ujenzi wa Magereza Wilaya ya Mbarali. Ukiangalia kwenye fungu la maendeleo sijaona kifungu ambacho kinazungumzia au kiasi cha pesa ambacho kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa Magereza Wilaya ya Mbarali.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli thabiti ni iliyomo kwenye hotuba yangu. Gereza la Mbarali tutajenga. Tutaanza ujenzi. *(Makofi)*

(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima, imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2003/2004, kifungu kwa kifungu na kupitisha pamoja mabadiliko niliyoyataja. Hivyo naomba Bunge lako sasa lipitishie Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalipitishwa na Bunge)

*(Saa 12.50 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu
Tarehe 14 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*